**21 MEI, 2025**

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 21 Mei, 2025**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na: -

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Timotheo Mnzava kwa niaba yake Mheshimiwa Shangazi.

Na. 364

**Kuanzisha Vijiji Vipya Korogwe Vijijini**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itaanzisha Vijiji vipya kwenye maeneo ya Songea, Mkamani, Kwaluma Masimba na Sekioga – Korogwe Vijijini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishaji wa maeneo ya utawala hutekelezwa kwa mujibu wa Sheria za Serikali za Mitaa Sura ya 287 na 288 pamoja na Mwongozo wa uanzishwaji wa maeneo ya utawala wa Mwaka 2014 ambao umeainisha utaratibu na vigezo vinavyopaswa kufuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miongozo na vigezo vya kuanzisha kijiji kipya kwa mujibu wa Mwongozo wa Uanzishaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa wa Mwaka 2014 ni idadi ya watu wasiopungua 5,000. Katika kijiji kipya na kijiji kinachobaki kinapaswa kuwa na watu 10,000, hivyo kufanya jumla ya watu 15,000. Kwa mujibu wa takwimu za sensa ya watu na makazi iliyofanyika mwaka 2022 vijiji

vya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe vina idadi pungufu ya watu 15,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imetoa kipaumbele katika kuboresha na kukamilisha miundombinu ya msingi kwenye maeneo yaliyoanzishwa ili yaweze kutoa huduma kwa jamii na baadaye kuendelea na maeneo mengine kwa kufuata taratibu na vigezo vilivyoainishwa, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa miongoni mwa vigezo ni kuandaa pamoja na maeneo ya kiutawala na vijiji hivi vya Songea, Mkamani, Kwaruma, Masimba na Sekioga vyote vina shule za msingi zaidi ya mbili na zahanati zaidi ya mbili. Kwa hiyo, kwa maana kwamba maeneo ya huduma yamekamilika. Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kutoa upendeleo maalum kwa maeneo hayo ili yaweze kupata huduma za kiutawala?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Katika Wilaya ya Lushoto Kata ya Manolo kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 ina idadi ya watu 25,000 na ndiyo iliyoongoza katika Wilaya nzima, lakini ina sekondari tatu, vijiji sita na shule za msingi tisa. Serikali haioni kwamba ni wakati mwafaka kugawa kata hii ili tuweze kuboresha upatikanaji wa huduma kwa wananchi kwa urahisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali inatambua kwamba kuna uhitaji wa kugawa baadhi ya vijiji ili kurahisisha huduma za kiutawala na huduma za kijamii lakini kwa vijiji hivi vya Songea, Mkamani, Kwaruma, Masimba na Sekioga katika Halmashauri ya Korogwe Vijijini, bado havijakidhi vigezo vya idadi ya watu kwa maana ya

kwamba lazima kijiji ambacho kinazaliwa kiwe na idadi ya watu wasiopungua 5,000 na kile kijiji mama kiwe na watu wasiopungua 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sensa ya watu na makazi ya 2022 bado vijiji mama havijakidhi idadi ya watu 15,000 ili kuwezesha vijiji vingine hivi kuweza kugawika. Kwa hiyo, naomba nitumie nafasi hii nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe Vijijini kwamba Serikali itaendelea kufuatilia kwa karibu idadi ya watu na vigezo vingine ili ikiwezekana muda ukifika viweze kupata hadhi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, kuhusiana na Kata ya Manolo katika Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, tunafahamu kwamba ni kata kubwa ina watu wapatao 25,000 kwa taarifa za sensa na makazi 2022; na vijiji sita na shule za sekondari tatu, lakini bado haijafikisha idadi ya watu angalau 30,000 ili tukigawa kata ile, kata mama ipate angalau watu 20,000 na kata mpya ipate watu angalau 10,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Shangazi kwamba tunatambua umuhimu wa kugawa kata hiyo, lakini namwomba tuendelee kufuatilia vigezo hivyo vya idadi ya watu na baadaye Serikali itaona utaratibu mzuri wa kugawa kata hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, eneo la Sirari na Nyamongo, wana sekondari za kutosha, shule za msingi, Mahakama, idadi ya watu, eneo la kiutawala, vigezo vyote vilikamilika maeneo yote mawili, lakini majibu yaliyopita alisema kwamba hawajaanzisha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, uliza swali.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo swali, kwamba maeneo mapya yatasubiri maeneo mengine ya mwanzo...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, uliza swali. Swali la nyongeza lina utaratibu wake.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa majibu haya, Naibu Waziri yupo tayari akanisaidie kutoa maelezo Sirari na Nyamongo ili kuondoa mkanganyiko? Kwa sababu waliwaambia wasubiri maeneo mengine yaimarike ndiyo yaanzishwe mapya, leo anasema vigezo na idadi ya watu. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, kaa, ameshakuelewa.

**MHE. MWITA M. WAITARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Mheshimiwa Mwita Waitara, nafikiri hakunielewa wakati najibu swali la msingi. Taarifa na kauli ya Serikali ni moja, haijawahi kubadilika kwamba tunafahamu kuna uhitaji wa kugawa maeneo ya kiutawala, lakini tumeweka kipaumbele namba moja katika kuboresha kwanza miundombinu katika maeneo ya utawala yaliyopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunafahamu tunazo kata ambazo hazina Ofisi za Watendaji wa Kata, tunavyo vijiji ambavyo havina Ofisi za Serikali za Vijiji, hakuna Ofisi za Watendaji, tunazo halmashauri hazina majengo ya halmashauri, Ofisi za Wakuu wa Wilaya na Mikoa vivyo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kipaumbele namba moja ni kuhakikisha kwanza miundombinu muhimu ya kutoa huduma kwenye mamlaka zilizopo inaboreshwa, lakini tunafahamu yapo maeneo kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge, Sirari, Nyamongo ambayo tayari yamekidhi vigezo, na ni kipaumbele tunasubiri sasa tukikamilisha kipaumbele cha kwanza tutakwenda kuona namna ambavyo tunaanza kuchukua hatua kwa ajili ya kupandisha hadhi maeneo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chaurembo.

**MHE. ABDALLAH J. CHAUREMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kata ya Chamazi ina wakazi wapatao 226,000. Je, Serikali ina mpango gani wa kukata kata hiyo huku ikiwa imetimiza vigezo vyote vya shule, hospitali, ofisi za mitaa na ofisi za kata? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Kata ya Chamazi imekidhi vigezo vyote kwa idadi ya watu pamoja na miundombinu na huduma mbalimbali. Pia, ni moja ya kata ambazo tayari Ofisi ya Rais, TAMISEMI tumeiainisha kwenye kata za kipaumbele ambazo mara baada ya kukamilisha kipaumbele namba moja cha kuboresha miundombinu, tutahakikisha Kata ya Chamazi inagawika na kupata kata nyingine ili kusogeza zaidi huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Chaurembo na wananchi wa Kata ya Chamazi waendelee kuwa wavumilivu, Serikali hii sikivu tayari imeshalichukua jambo hilo, inaendelea kulifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Stella Fiyao.

Na. 365

**Kukamilisha Maboma Yaliyojengwa na Wananchi Songwe**

**MHE. STELLA S. FIYAO** aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kukamilisha maboma yaliyojengwa na Wananchi katika Mkoa wa Songwe?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 hadi 2023/2024, Serikali imepeleka jumla ya shilingi bilioni 156.5 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya elimu na zahanati kote nchini ambapo kwa kipindi hicho, jumla ya shilingi bilioni 4.68 zimetumika kukamilisha maboma 51 ya zahanati na maboma 211 ya elimu katika Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali imetenga shilingi bilioni 9.54 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya madarasa 734 ya shule za sekondari na msingi, matundu 114 ya vyoo, nyumba za walimu sita na bweni moja. Aidha, Serikali imetenga shilingi bilioni 30.38 kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma ya zahanati 346 kote nchini, ambapo Mkoa wa Songwe umetengewa shilingi milioni 752.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imetenga shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya kukamilisha maboma ya madarasa 209 ya shule za sekondari na msingi, matundu 66 ya vyoo, mabweni mawili na maabara 12 za shule za sekondari katika Mkoa wa Songwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi kote nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Stella.

**MHE. STELLA S. FIYAO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, lakini nataka kujua, wananchi wa Mkoa wa Songwe wamekuwa na mwamko mkubwa sana kuhakikisha wanajenga maboma yaliyo katika elimu na afya. Mwamko huo umepelekea Serikali kutoyakamilisha kwa wakati na kutokana na changamoto ya mvua ambazo zinaendelea kunyesha ndani ya mkoa wetu wa Songwe, maboma mengine mpaka yanaanguka na mvua. Sasa nataka kujua, mkakati wa Serikali ni upi kuhakikisha mnaongeza kasi ili kutowakatisha tamaa wananchi ambao wamejitoa kwa moyo kabisa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu namba mbili. Nilitaka kujua mkakati wa Serikali ni upi kuhakikisha mnakarabati Shule ya Msingi Ileya iliyoko ndani ya Wilaya ya Ileje Kata ya Ndola? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Katika kipindi cha miaka hii minne ya Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote wa Tanzania ni mashahidi, kazi kubwa sana imefanyika ya kujenga na kukamilisha maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kwa Sekta ya Afya, maboma zaidi ya 1,000 ya zahanati yamekamilishwa na zahanati zimeanza kutoa huduma. Pia katika Sekta ya Elimu maboma mengi yamekamilishwa ya maabara na madarasa na yanaendelea kutoa huduma. Tumeendelea pia kujenga vituo katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba Serikali ilisharatibu utaratibu wa kuainisha maboma yote kote nchini yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi na tuna idadi na tumendelea kuyatengea fedha kila bajeti kwa ajili ya kuhakikisha kwamba yanajengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la msingi, ili maboma yasikae muda mrefu na kuharibika, tulishatoa maelekezo kwa Makatibu Tawala wa Mikoa na Wakurugenzi kote nchini kuratibu ujenzi wa maboma kwa awamu badala ya kujenga maboma yote kwa wakati mmoja na mengine yakakaa muda mrefu kabla hayajakamilika. Basi tunaendelea kuyaratibu yanajengwa kwa awamu ili Serikali iendelee kutenga fedha na kukamilisha maboma hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kuhusiana na hiyo shule chakavu, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kukarabati shule kongwe na shule chakavu. Nikuhakikishie tu

kupitia mradi wa *boost* na miradi mingine tutaendelea kuhakikisha kwamba tunatenga fedha kwa ajili ya kukarabati shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ileje aweze kuwasilisha taarifa ya shule hiyo tuweze kuona mahitaji na Serikali iweze kutenga fedha kwa awamu kwa ajili ya ukarabati.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mchungahela.

**MHE. ISSA A. MCHUNGAHELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mwaka 2024 wakati tuna-*wind-up,* Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI aliniahidi shule tatu chakavu ambazo mpaka sasa hivi watoto wanasomea nje na Mheshimiwa Waziri alikuwepo akapewa maagizo hayo. Mpaka sasa hivi shule hizi chakavu sijazipata hata mojawapo. Wanasema nini kuhusiana na jambo hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Ni kweli kwamba Jimbo la Lulindi ni moja ya majimbo ambayo yana shule chakavu. Mheshimiwa Mbunge wa Jimbo hilo, Mheshimiwa Mchungahela alishawasilisha, na Waziri wa Nchi alishatoa maelekezo kupitia kwa Katibu Mkuu na tumeshaainisha shule hizo. Kilichobaki sasa tunatafuta fedha kwa ajili ya kwenda kukarabati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mchungahela kwamba zoezi hilo linaendelea, Serikali haijakaa kimya. Wakati wowote tukipata fedha hizo tutakuja kukarabati na kujenga shule hizo ili wananchi wa Lulindi wapate huduma za karibu katika Sekta ya Elimu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Getere.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika Jimbo la Bunda kuna Shule ya Masaba, Shule ya Chamtikiti, Shule ya Salagwa, na Nyasirori. Niliahidiwa kwamba

hizi shule zitajengwa kwa kutumia mradi wa *boost*. Je, ni lini pesa za *boost* zitaenda kwenye shule hizo kuzikamilisha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Utekelezaji wa mradi wa ukarabati wa shule na ujenzi wa shule kupitia programu mbalimbali ikiwemo *boost* na fedha nyingine za Serikali ni zoezi endelevu. Serikali inatambua kwamba katika Jimbo la Bunda Vijijini kwa Mheshimiwa Getere kuna uhitaji wa shule na yeye kama Mbunge alikwishawasilisha na Serikali inaendelea kufanya taratibu za kupata fedha kwa ajili ya kwenda kujenga na kukarabati shule hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Getere kwamba Serikali inaendelea kuyafanyia kazi maombi ya Halmashauri hiyo ya Bunda Vijijini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Suma.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa swali dogo la nyongeza. Je, ni lini Serikali itapeleka fedha za umaliziaji maboma mawili kwenye shule ya Sekondari ya Isongole iliyopo Wilayani Rungwe? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Serikali imekuwa ikiainisha maboma ambayo yanahitaji kukamilishwa katika shule mbalimbali za msingi na sekondari ikiwemo Shule ya Sekondari ya Isongole ambako Mheshimiwa Mbunge Fyandomo amesema.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge na nitumie nafasi hii nimwelekeze Mkurugenzi wa Halmashauri aweze kuainisha uwezo wa halmashauri yenyewe kukarabati na kukamilisha madarasa hayo kwa wakati, na ikiwa fedha za mapato ya ndani ya halmashauri

hazitatosha, atupe taarifa ya *gap* la fedha ambayo inahitajika ili Ofisi ya Rais, TAMISEMI ione uwezekano wa kupeleka fedha. Lengo ni kuhakikisha kwamba madarasa hayo yamekamilika na yanatoa huduma zinazostahili.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea. Mheshimiwa Kigua.

Na. 366

**Ujenzi wa Daraja Negero na Lukole – Kilindi**

**MHE. OMARI M. KIGUA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itajenga daraja linalounganisha Kijiji cha Negero – Kilindi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa daraja linalounganisha Kijiji cha Negero – Kilindi katika kuchochea shughuli za kiuchumi katika eneo hilo. Katika mwaka 2023/2024, Serikali ilitumia shilingi milioni 70 kufanya usanifu wa Daraja la Mto Negero ili kupata gharama halisi za ujenzi wa daraja hilo. Usanifu ulikamilika mwezi Machi, 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi inayoendelea sasa ni kupitia taarifa ya usanifu na baada ya kukamilika na kupata gharama halisi, daraja hili litaombewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa wananchi wa eneo hilo wanatumia kivuko cha chuma cha waenda kwa miguu *(Pedestrian Suspension Bridge)* chenye upana wa mita 100 kilichojengwa na kukamilika Desemba, 2021 kwa gharama ya shilingi milioni 66.68 ili kuwapunguzia adha katika eneo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kigua.

**MHE. OMARI M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naishukuru Serikali kwa kutoa fedha kiasi hicho kwa ajili ya kuweka daraja la muda, lakini ni ukweli kwamba eneo hilo lina uzalishaji mkubwa sana wa mahindi. Kwa hiyo, kwa kipindi chote hicho cha miaka mitatu mpaka sasa hivi ni kwamba ni pikipiki tu na wananchi ndiyo wanapita kwa miguu lakini magari hayapiti. Kwa hiyo, kwa kiasi kikubwa imeathiri uchumi wa wananchi wa maeneo hayo. Je, Serikali iko tayari kuongeza *speed* tupate fedha daraja hilo liweze kujengwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwenye Kata ya Pagwi, mkandarasi ambaye alipewa kazi hiyo kwenye Vijiji vya Lomotio na Makelele alipewa kazi ya kujenga vivuko, lakini mpaka sasa hivi amekimbia *site* na hajulikani alipo. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kumwelekeza Meneja wa *TARURA* Mkoa wa Tanga aweze kumrejesha mkandarasi huyo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Omari Kigua amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana wa kuhakikisha kwamba miundombinu ya barabara katika jimbo lake inaendelea kuimarika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali lake la kwanza, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuhakikisha inaendelea kuboresha miundombinu ya barabara hizi muhimu kabisa ambazo zinawawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kuweza kufikia maeneo yenye huduma za msingi kabisa za kijamii. Ndiyo maana utaona katika kipindi cha miaka minne, katika Wilaya ya Kilindi, shilingi bilioni 10.17 zimeletwa kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara hizi zinazosimamiwa na *TARURA*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa bajeti 2025/2026 tunatarajia kwamba, Wilaya ya Kilindi itakuwa ina bajeti ya shilingi bilioni 3.9, kwa ajili ya kuendelea kuimarisha miundombinu ya barabara katika Eneo la Kilindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutahakikisha daraja hili linapatiwa fedha na linajengwa haraka iwezekanavyo ili liweze kuwanufaisha wananchi wake, wasikwame kwenye shughuli zao za uzalishaji, kama alivyoainisha kwamba wanafanya uzalishaji mkubwa sana wa mahindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili, naomba nitumie nafasi hii, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, kumwagiza Meneja wa *TARURA* wa Mkoa aweze kuhakikisha anafuatilia kwa ukaribu sana, kuhakikisha mkandarasi huyu anafika *site* kwa ajili ya kuhakikisha kivuko alichokitaja Mheshimiwa Mbunge kinawanufaisha wananchi wake kiuchumi na kuwasaidia wananchi kufikia huduma za msingi kabisa za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Prof. Ndakidemi.

**MHE. PROF. PATRICK A. NDAKIDEMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Daraja linalojulikana kama Mohameid Mwita linalounganisha Vijiji vya Boro na Kindi katika Jimbo la Moshi Vijijini limekatika kutokana na mafuriko. Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu kulijenga na kuifungua barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Prof. Ndakidemi amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana wa Daraja hili la Mohameid Mwita, ambalo ni daraja lenye umuhimu sana katika jimbo lake. Daraja hili ni la chuma, lakini lina nguzo za mawe, nguzo moja imeharibika na tayari ma-*engineer* wetu wamefika kwenda kufanya tathmini ya kujua gharama, kwa ajili ya kurudishia nguzo hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Profesa Ndakidemi kwamba mkandarasi atapatikana na atakuja kujenga nguzo hiyo, kurekebisha daraja kwa utaratibu wa dharura, ili liweze kuwasaidia wananchi wake

kufanya shughuli zao mbalimbali za kiuchumi na kufikia huduma za kijamii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justin.

**MHE. JUSTIN L. NYAMOGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kijiji cha Idunda kilichopo Kata ya Kimala na Kijiji cha Kiwalamo kilichopo Kata ya Idete, vijiji hivi viwili havina mawasiliano kutokana na madaraja mawili yanayozunguka vijiji hivyo kubomoka toka mwaka 2024. Serikali inatoa kauli gani kwa sababu, hakuna mawasiliano kwenye maeneo haya na wananchi wanashindwa kusafiri wala kusafirisha mizigo yao?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kumpongeza Mheshimiwa Mbunge, kwa kweli, mara nyingi amekuwa akifanya ufuatiliaji wa karibu sana kuhakikisha kwamba, wananchi wake wa Kilolo wanaweza kupatiwa miundombinu bora zaidi ya barabara hizi ambazo zinasimamiwa na *TARURA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge kwamba, katika Bajeti hii ambayo tunaendelea nayo ya mwaka 2024/2025 zimetengwa shilingi bilioni 71 kwa ajili ya dharura ya kurudisha mawasiliano kwenye maeneo ambayo barabara zimekatika, ili wananchi waweze kupata barabara nzuri, kufanya shughuli zao za kiuchumi na pia kufikia huduma za kijamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikuhakikishie katika maeneo haya aliyoyataja tutafika na kuhakikisha kwamba, tunarejesha mawasiliano ili wananchi wake waweze kupata miundombinu bora kabisa, ambayo itawawezesha kufanya shughuli zao za kiuchumi na itawawezesha pia kufika katika huduma za msingi kabisa za kijamii. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Justin Nyamoga apate taarifa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, Mheshimiwa Dkt. Ishengoma.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi niulize swali la nyongeza. Je, Serikali ni lini itakarabati Daraja linalounganisha Kata ya Mwaya na Kata ya Mbuga, Ilonga na Ketaketa katika Halmashauri ya Ulanga, ambalo lilibomoka kwa sababu ya mafuriko?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mazingira ambayo kutokana na mvua nyingi zinazonyesha, na hasa Mkoa wa Morogoro ambao unaathirika sana na mvua hizi, kuna baadhi ya maeneo mawasiliano yanakatika. Ndiyo maana utaona dhamira ya dhati ya Serikali ya Awamu ya Sita ni kuendelea kurudisha mawasiliano kwenye maeneo ambayo mawasiliano yamekatika, kwa maana ya miundombinu hii ya barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Christine Ishengoma kwamba, kupitia bajeti ya shilingi bilioni 71 ya dharura ya *TARURA*, Serikali itafika katika daraja alilolitaja katika maeneo hayo aliyoyataja, kwa ajili ya kuhakikisha inarudisha mawasiliano, ili wananchi waweze kupata barabara ambazo zitawawezesha kufanya shughuli zao za kiuchumi na zitawawezesha kufikia huduma za msingi za kijamii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara hiyo, Mheshimiwa Monni.

Na. 367

**Uhaba wa Walimu wa Kike, Chemba**

**MHE. MOHAMED L. MONNI** aliuliza: -

Je, lini Serikali itapeleka walimu wa kike katika shule ambazo hazina walimu wa kike Wilayani Chemba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA)** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Chemba ina shule za msingi 113 na shule za sekondari 29. Aidha, shule zisizo na walimu wanawake ni shule za msingi 11 na shule za sekondari zote zina walimu wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo Februari na Machi, 2025, Serikali imeajiri walimu 15,925 ambapo Halmashauri ya Chemba imepokea walimu 93 wa (awali na msingi 40 na sekondari 53) wakiwemo walimu 32 wanawake na walimu 61 wanaume. Shule tatu za msingi ambazo ni miongoni mwa shule ambazo hazikuwa na walimu wanawake zimepangiwa walimu hao.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kuajiri walimu, wakiwemo walimu wanawake, kadiri ya upatikanaji wa fedha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Monni.

**MHE. MOHAMED L. MONNI:** Mheshimiwa Naibu Spika, miaka minne hii mmeongeza idadi kubwa sana ya shule za msingi na sekondari, lakini pia, tumejenga madarasa mengi sana. Hii inatafsiri kwamba, idadi ya walimu imekuwa ndogo sana. Nataka kujua mkakati wa haraka wa kuendana na kasi hii ya ujenzi wa shule za msingi na sekondari ambazo zimejengwa? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kutokana na utaratibu wa Elimu Bila Malipo, wazazi wengi wamehamasika kuwapeleka watoto wao shule, na kwa hakika udahili umeongezeka mara dufu. Ndiyo maana utaona kwamba, uhitaji wa madarasa umeongezeka na ndiyo maana Serikali imetumia, katika kipindi cha miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Sita, shilingi trilioni 5.1 kufanya uwekezaji katika sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi, kujenga madarasa na imefanya maendeleo mbalimbali katika miundombinu, kwa ajili ya kuwezesha kupokea wanafunzi hao wengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyosema Mheshimiwa Mohamed Monni, ongezeko la udahili huu pia limesababisha uhitaji wa walimu zaidi na utaona mikakati hii ya Serikali. Mkakati wa kwanza wa kuongeza walimu ni kuajiri. Serikali imekuwa ikiajiri waalimu kila mwaka wa fedha. Utaona kwamba, katika mwaka wa fedha tulionao, 2025/2026, walimu 15,925 wameajiriwa na tumepata taarifa kwamba, Serikali imetoa kibali cha kuongeza walimu wengine zaidi ya 10,000. Utaona kwamba, katika kipindi cha miaka minne walimu ambao wameajiriwa ni 45,742. Huu ni mkakati wa kwanza ambao ni kuajiri walimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkakati wa pili ni matumizi ya TEHAMA, ambapo sasa Serikali inatumia madarasa janja kufanya ufundishaji mubashara. Yaani mwalimu anakuwa yupo eneo moja anatumia TEHAMA kufundisha wanafunzi katika maeneo tofauti tofauti kwa utaratibu unaoitwa ufundishaji mubashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini mkakati mwingine ni kutumia walimu kwa utaratibu wa mkataba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu mwingine ni kutumia walimu wa kujitolea na pia, wale walimu ambao wapo katika mafunzo kwa vitendo. Kwa hiyo, Serikali itaendelea na mikakati hii, kuendelea kuongeza walimu ili wanafunzi wetu hawa waweze kupata walimu wa kutosha, waweze kuwapa elimu iliyo bora. Hiyo kazi inafanyika na Serikali ya Awamu ya Sita.

**MHE. HAWA M. CHAKOMA:** Mheshimiwa Hawa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ili niweze kuuliza swali. Ukosefu wa walimu wa kike katika Shule za Wilaya ya Chemba unafanana kabisa na Shule za Chalinze, Wilayani Bagamoyo. Je, ni lini Serikali itatupelekea walimu wa kike?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. ZAINAB A. KATIMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Mheshimiwa Hawa Mchafu, kwa kweli, amekuwa akifanya ufuatiliaji wa mara kwa mara na kuzungumzia sekta hii muhimu kabisa ya elimu msingi. Kuhusiana na swali lake, kuhusu walimu hawa wanawake, naomba nimhakikishie kwamba, Serikali inaendelea na utaratibu wa kuajiri walimu na tunazingatia pia, upatikanaji wa walimu wanawake, ambao tutawapanga katika vituo mbalimbali, ikiwemo katika mkoa ambao anatoka Mheshimiwa Hawa Mchafu.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Maji, Mheshimiwa Gambo.

Na. 368

**Kukamilisha Mfumo wa Maji Taka kutoka Kiwanda cha A – Z**

**MHE. MRISHO M. GAMBO** aliuliza: -

Je, lini Serikali itakamilisha mfumo wa maji taka Kiwanda cha A - Z ili kuondoa changamoto ya Wananchi wa Kata ya Olmot – Arusha?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Miundombinu ya Uondoshaji Majitaka wa Olmoti utakaonufaisha Kiwanda cha A to Z pamoja na wakazi zaidi ya 1,200 wa Kata ya Olmot – Arusha. Kazi zinazotekelezwa katika mradi huo ni pamoja na ulazaji wa mabomba umbali wa kilometa 9.206, ujenzi wa nguzo 15 za kushikilia bomba kwenye vivuko pamoja na ujenzi wa Chemba 188 za ukaguzi wa mfumo wa majitaka. Hadi sasa utekelezaji wa mradi huo umefikia wastani wa 78% na unatarajiwa kukamilika mwezi Juni, 2025.

**NAIBU:** Mheshimiwa Gambo.

**MHE. MRISHO M. GAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 26 mwezi wa sita mwaka 2024, wakati Mheshimiwa Naibu Waziri anajibu swali alisema kwamba, kufikia mwezi Disemba, mwaka 2024, mradi huu utakuwa umekamilika. Leo tena anajibu swali anasema hadi kufikia mwezi Juni, mwaka 2025 mradi utakuwa umekamilika. Sasa je, tuchukuwe majibu gani ya Serikali, ili tuweze kuwapelekea wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili. Sasa hivi anasema tumefika 78%, kwa hiyo, zimebakia kama 22%, kama kwa miaka isiyopungua mitatu wameweza kutekeleza kwa asilimia 78. Je, ana uhakika gani kwa muda uliobaki wa mwezi mmoja kuweza kumaliza 22%? Kama haijatekelezeka, yupo tayari kujiuzulu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gambo, mbona una maneno magumu?

Mheshimiwa Waziri hebu endelea.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninamshukuru sana kaka yangu, Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge mahiri kabisa wa Arusha na kazi anayoifanya ya kuwatetea wananchi wake. Sisi, Serikali tunaendelea kushirikiananaye kuhakikisha kwamba, tunaendelea kutatua changamoto za maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, maendeleo ni hatua kwa hatua na hatua hizo zinategemea na upatikanaji wa fedha. Mheshimiwa Mbunge anatambua hata katika jimbo lake, kila jambo amelipanga kwa wakati na kulingana na fedha zinavyopatikana. Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba, inachukua hatua stahiki kila inapopata fedha, ilimradi tu wananchi ambao wanahitaji kupatiwa huduma ya maji au kuondolewa majitaka kazi hiyo iwe imekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge nikutoe wasiwasi, majibu ya Serikali ni kwamba, mradi huu utakamilika kwa sababu, tunatambua kipindi cha hapo mwanzo kulikuwa na changamoto na mkandarasi, lakini tatizo hilo tumeshalimaliza.

Tumekaa na mkandarasi, tumeelekezana na ndiyo maana mradi huu ulikuwa 50% na kitu sasa upo 78%.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna uhakika kabisa kwamba, mpaka itakapofika muda wa mkataba wake, mradi huu unatakiwa uwe umekamilika. Kama mradi utakuwa haujakamilika, basi itabidi mkandarasi tumchukulie hatua stahiki kulingana na makubaliano katika mkataba.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mama Sitta.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Wananchi wa Urambo wamekuwa wakisubiri kwa muda mrefu sana upatikanaji wa maji kutoka *Lake Victoria* kutokana na shida kubwa ya maji tuliyonayo. Je, ni lini sasa mradi huu utakamilika?

**NAIBU:** Mheshimiwa Waziri, ni lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na ninapenda kujibu swali la mama yangu, Mheshimiwa  Margaret Sitta. Mradi wa Urambo, Kaliua pamoja na maeneo mengine unagharimu shilingi bilioni 143. Mradi huu umeshafikia 70%. Vilevile kuna maeneo ambayo tayari kulikuwa na *existing infrastructure,* tulitoa maelekezo na tayari sasa wameshaanza kufanya tathmini ya kuona kuna umbali gani kutoka kwenye matenki na kwenda kwenye *exiting infrastructure*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu kwamba tayari wataalamu wetu wapo *site* wanafanya kazi. Muda siyo mrefu mradi utakapokamilika wataanza kupata huduma ya maji safi na salama kutoka Ziwa Viktoria, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Mheshimiwa Ally Mlaghila.

Na. 369

**Miradi ya Maji Kyela**

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE** aliuliza: -

Je, lini Miradi ya Maji katika Wilaya ya Kyela itakamilika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/25, Serikali imekamilisha utekelezaji wa Mradi wa Maji Lema, ambapo unanufaisha wananchi 3,357 waishio kwenye Kijiji cha Lema, kilichopo Wilayani Kyela, Mkoa wa Mbeya. Vilevile, Serikali inaendelea na utekelezaji wa Miradi Minne ya Ngana, Sinyanga, Kyela - Kasumulu na Ipinda, wilayani humo, ambayo ipo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Miradi hiyo inatarajiwa kukamilika mwezi Disemba, 2025 na kunufaisha zaidi ya wananchi 110,000 waishio kwenye maeneo ya vijiji na Mitaa ya Wilayani Kyela.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ally.

**MHE. ALLY A. J. M. JUMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu ya Serikali na niipongeze Serikali kwa kuendelea kutekeleza miradi mingi sana pale Wilayani Kyela. Pamoja na miradi hiyo na juhudi za Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Mradi wa *Sinyanga Group*. Mradi huu mpaka sasa hivi una miaka miwili na umefikia 15% tu, bado Serikali haijapeleka vifaa. Je, ni mbinu na muujiza gani utatumika kuhakikisha mradi huu unakamilika Disemba, mwaka 2025?

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili. Mradi wa *Ngana Group* ambao utanufaisha wananchi wengi sana, zaidi ya 66,000 kwenye kata saba na wananchi hao wanategemea kupata maji, upo 50% tu. Ni nini Kauli ya Serikali kwenye mradi huo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na pia, namshukuru sana Mheshimiwa Mbunge wa Kyela, kaka yangu, Mheshimiwa Ally Jumbe Mlaghila. Ni kweli kabisa miradi hii amekuwa akiisemea sana na bahati nzuri ameshafika ofisini kuifuatilia, kuangalia utekelezaji unaendaje.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba, Mradi wa Sinyanga upo 15% na Mradi wa Ngana upo 50%, kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge. Tunatambua kabisa kwamba, wakati wa utekelezaji wake pale mwanzoni tulikuwa na changamoto, lakini pia, kulikuwa na mambo ya miundombinu, iliyokuwa inajengwa ilikuwa inapitia wakati mgumu kutokana na ushirikishwaji wa wananchi. Baada ya kugundua haya, tukaanza kufanya ushirikishwaji wa wananchi na baada ya hapo mradi ndiyo umeanza kukimbia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimtoe hofu. Disemba, 2025 mradi huu kwa sababu, fedha zipo na wataalamu wetu wameshapewa maelekezo na Serikali kuhakikisha kwamba unakamilika, ndiyo maana majibu yangu ya msingi ni kwamba, mradi utakamilika Disemba, 2025. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mabula.

**MHE. DKT. ANGELINE S. L. MABULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Ningependa kumwuliza Mheshimiwa Waziri, Mradi wa Kuunganisha Majitaka katika maeneo ya milima, eneo la Manispaa ya Ilemela, waliunganisha kaya 390 Eneo la Kilimahewa A na B na wakasema kutakuwa na Mradi wa Awamu ya Pili, ambayo itakwenda kuunganisha Nyamanoro, Kirumba na kumalizia Kilimahewa yote. Je, lini mradi huu utaanza ili kuunganisha miundombinu ya majitaka maeneo ya milima? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninapenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Angeline Mabula, Mbunge wa Ilemela, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa awamu ya kwanza ilienda Kilimahewa lakini ni kaya 390 ziliunganishwa, lakini pia kulikuwa na Ibungilo. Sambamba na hivyo, tuna awamu ya pili ambayo tayari tumeshatangaza *tender,* mkandarasi ameshapatikana na mwezi wa Saba tunaenda kusaini mkataba kwa ajili kuanza awamu ya pili ambayo itaenda Kirumba, Nyamanoro pamoja na Kilimahewa ambapo zaidi ya kaya 1,600 zitaunganishwa na mfumo huo wa majitaka ili kuyaondoa katika makazi ya watu. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Mwijage, kwa niaba Dkt. Kikoyo.

Na. 370

**Ujenzi wa Mradi wa Bonde la Mto Ngono**

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE** aliuliza: -

Je, nini mawanda ya Mradi wa Bonde la Mto Ngono lililofanyiwa upembuzi yakinifu ili liweze kuendelezwa na lini ujenzi wa Mradi huo utaanza?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Bonde la Mto Ngono ni miongoni mwa mabonde 22 ya kimkakati ambayo yamefanyiwa upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuendeleza kilimo cha umwagiliaji. Bonde hili linajumuisha maeneo ya umwagiliaji ya Wilaya za Bukoba, Misenyi na Muleba, zikiwemo Skimu za Kyabaramba, Katoro, Ngarama, Kyakakera, Kabaijuga, Kaibanja, Kishege, Minazi, Buterankuzi (Bukoba), Nkenge, kafunjo, Butulage, Buchurago, Bulembo Kusini (Misenyi), Ikondo, Buyaga, Buhangaza, Muhutwe, Katoke, Kagoma na

Kikuku (Muleba). Aidha, eneo linalofaa kwa kilimo cha umwagiliaji katika bonde hili ni zaidi ya hekta 16,000.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Kilimo kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na mchakato wa manunuzi kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ujenzi wa skimu katika bonde hili unaendelea. Ujenzi wa skimu za Mto Ngono unatarajiwa kuanza mwaka huu wa fedha baada ya hatua za manunuzi kukamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Kikoyo.

**MHE. DKT. OSCAR I. KIKOYO K.n.y. MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali. Tumekuwa tukianzisha miradi kama hii na wananchi wa maeneo hayo wakiondolewa: -

(a) Je, mradi huo utahakikisha kwamba wananchi wa maeneo hayo wanakuwa sehemu ya huo mradi?

(b) Je, Serikali imezingatia kuwa Mkoa wa Kagera kuna uzalishaji mzuri wa kahawa, kwamba kwenye huu mradi na zao la kahawa litazingatiwa na kupewa kipaumbele ili kuongeza tija na kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nimthibitishie tu Mheshimiwa Kikoyo kwamba, maeneo yote ambayo tunajenga miradi ya umwagiliaji kama Wizara, watu wa kwanza ambao tunawapa kipaumbele ni watu ambao wanamiliki maeneo ambayo mradi unapita. Kwa hiyo, awaondoe shaka wananchi wa Bukoba, katika maeneo ambayo nimeyaainisha hapa wao ndio watakaokuwa kipaumbele namba moja mradi huu utakapokuwa umekamilika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kulipa kipaumbele zao la kahawa, sehemu ya mradi inatekeleza hiyo, lakini vilevile nimthibitishie tu kwamba sisi Wizara ya Kilimo mpaka sasa hivi tumenunua magari 18 kwa ajili ya kuchimba visima ambavyo

vitakwenda kwenye hayo mashamba ya wakulima, hususan wakulima wa kahawa na mazao mengine kwa ajili ya kuongeza tija. Kwa hiyo, lipo katika mipango yetu na utekelezaji unaendelea. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mifugo. Mheshimiwa Sylvia, kwa niaba Mheshimiwa Felix.

Na. 371

**Kutokomeza Uvuvi Haramu Ziwa Tanganyika**

**MHE. KAVEJURU E. FELIX K.n.y. MHE. SYLVIA F. SIGULA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itatokomeza uvuvi haramu katika Ziwa Tanganyika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Wizara ya Mifugo na Uvuvi imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali ikiwemo TAMISEMI ili kuhakikisha rasilimali za uvuvi zinalindwa na kuvunwa kwa njia endelevu. Aidha, Wizara imeendelea kuimarisha vituo vyote vya ulinzi na usimamizi wa rasilimali za uvuvi vilivyopo katika ukanda wa Ziwa Tanganyika kwa kuvipatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hatua hiyo, Wizara imeendelea na mikakati ya matumizi ya teknolojia ya kisasa ya ndege nyuki katika kukabiliana na vitendo vya uvuvi haramu. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na asasi zisizokuwa za kiserikali inaendelea kutoa elimu kwa jamii za wavuvi na wadau wengine juu ya athari za uvuvi haramu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa wito kwa halmashauri kuendelea kushirikiana na Wizara katika kudhibiti vitendo vya uvuvi haramu. Pia, natoa wito kwa wavuvi wote nchini, wakiwemo wavuvi wa Ziwa Tanganyika kufanya shughuli zao kwa kuzingatia miongozo, taratibu, sheria na kanuni za uvuvi.

Kwa kufanya hivyo tutakuwa tumetokomeza uvuvi haramu hapa nchini ikiwemo Ziwa Tanganyika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Felix.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza, Serikali ina mikakati gani ya kuzuia nyavu haramu zinazoingizwa nchini kutoka nje ya nchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, uvuvi endelevu ni pamoja na uvuvi wa vizimba. Serikali ina mipango gani ya kupeleka vizimba katika ziwa Tanganyika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Jambo moja ambalo nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge na awe na uhakika, Serikali inakataza matumizi ya nyavu ambazo hazikubaliki ambazo ziko chini ya kile kiwango ambacho kinatakiwa. Moja ya mikakati tuliyonayo sasa hivi ni kwamba nyavu zote haramu zikitoka nje ya nchi haziruhusiwi kupita katika bandari zetu ama mipaka yetu hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, wale wote wanaohusika na biashara hiyo, endapo wakikamatwa cha kwanza wanafutiwa leseni, zile nyavu zinataifishwa na kuchomwa. Vilevile, tunafuatilia mpaka kule ambako wamekuwa wakichukulia. Wizara imekuwa ikisisitiza sasa, nyavu zianze kutengenezwa hapa nchini kwa kutumia viwanda vya ndani kwa kufuata ile miongozo na taratibu ambazo zinawekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu vizimba, Ziwa Tanganyika ni miongoni mwa maziwa ambayo yapo katika mikakati ambayo Wizara ya Mifugo na Uvuvi imeiweka, kwamba, kuna vizimba ambavyo tayari vitaletwa kwa ajili ya Ziwa Tanganyika kama ambavyo imefanyika katika Ziwa Victoria. Kwa hiyo, hilo lipo kwenye mipango ya Serikali. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ukienda katika Wilaya ya Karagwe na Kyerwa na hasa Kata za Kitwechenkura na Songambele utakutana na watu wengi ambao wamekatwa mikono wakisingiziwa kwamba wamevua samaki upande wa Rwanda kwenye Mto Kagere na pia Mto Kafunzo. Nataka nijue utaratibu ambao Serikali inaweza kuweka kwa ajili ya kuongea na Serikali ya Rwanda na kuwaelewesha wavuvi ili waweze kujua mipaka yao, wasivuke kwenye maji ya Rwanda na wakaishia kupata hizi adha ambazo wamekuwa wanazipata miaka yote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, unazo hizo taarifa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO K.n.y. WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nalifahamu, nimekuwa kule. Jambo moja ambalo nimthibitishie tu Mheshimiwa Mbunge, ni kwamba kwanza, kuna mahusiano kati ya hizi nchi wanachama wa Afrika Mashariki, na kuna ile taasisi yetu ambayo inahusika inayoitwa *Lake Victoria Foundation* kwa ajili ya nchi zote za *EAC*. Moja ya makubaliano tuliyokuwa tumeingia ni pamoja na kulinda wavuvi kutoka katika nchi wanachama, kwa maana ya Rwanda, Congo pamoja na Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa yanapotokea matatizo kama hayo, moja ya kazi ya Wizara ni kuhakikisha kuwa tunafikisha elimu, na pia tuna-*report* juu ya matukio hayo maovu. Vilevile, Wizara ikishirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani na Jeshi la Ulinzi wa Taifa, imekuwa na hiyo kazi mojawapo ya kuhakikisha usalama unapatikana katika maeneo hayo. Kwa hiyo, sisi tutaongeza kasi ili matendo haya yasiendelee kutokea. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Ujenzi. Mheshimiwa Paresso.

Na. 372

**Fidia Wananchi Waliopisha Upanuzi Uwanja wa Ndege Manyara**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza: -

Je, lini Serikali italipa fidia na riba kwa wananchi wa Manyara Kibaoni Wilayani Karatu waliopisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege Manyara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali bado inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kulipa riba ya fidia kwa wakazi waliopisha upanuzi wa Kiwanja cha Ndege cha Lake Manyara. Mara baada ya kupatikana fedha hizo, malipo ya riba kwa wananchi waliopisha upanuzi wa mradi huo yatafanyika. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru. Naomba kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza: -

(a) Je, Serikali sasa ipo tayari kwenda eneo husika kuwapa wananchi hao majibu haya? *(Makofi)*

(b) Je, ni lini sasa ujenzi wa uwanja huo kwa maana ya upanuzi utaanza rasmi kwa sababu ni muda mrefu pamekuwa kimya na hakuna kinachoendelea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, tuko tayari, lakini nina uhakika wananchi watakuwa bado wanatusikiliza kuhusu majibu haya, lakini kama Serikali kwenda pale, tutakwenda kwa ajili ya kuwajulisha namna ya kulipa hiyo riba ya fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ni lini tutaanza, ninataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, mradi huu upo kwenye mpango ambao tunasaidiana na wenzetu wa *World Bank*. Mkandarasi ameshapatikana, taratibu ziko tayari na tunategemea *kickoff*. Kumkabidhi mkandarasi haitachukua muda mrefu kwa sababu ni taratibu tu zile za kibenki. Mkandarasi akiwa tayari kukamilisha taratibu zake, basi ujenzi wa uwanja huo utaanza. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tecla Ungele.

**MHE. TECLA M. UNGELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Je, ni lini Serikali itawalipa fidia Wananchi wa Nachingwea waliopisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Nachingwea?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nitumie nafasi hii tu kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge kwamba, sasa hivi viwanja vingi ambavyo hasa tunatumia fedha ya Serikali kwa 100% ujenzi wake umehamia kwenye Wizara ya Uchukuzi chini ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, ikiwa ni pamoja na hiki Kiwanja cha Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru Mheshimiwa Mbunge. Ni kwamba, tutawasiliana na wenzetu wa uchukuzi ambao sasa hivi ndiyo uwanja huu uko chini yao tuone Serikali tumefikia wapi kuwalipa wananchi hao fidia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mnzava. Ajiandae Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. DKT. CHRISTINA C. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanja cha Ndege cha Ibadakuli kilichopo Shinyanga kiko karibuni kukamilika, lakini kuna baadhi ya wananchi walitoa

maeneo yao ili kuongeza eneo. Je, ni lini waliobaki watalipwa fidia?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kiwanja hicho alichokitaja cha Shinyanga kipo, kinaendelea. Tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama Wizara ya Ujenzi tulishapeleka mahitaji yale ya fedha ambayo ilikuwa imebaki kwa wenzetu wa Hazina na wanalifanyia kazi. Mara watakapokabidhiwa fedha, tutawalipa hawa wananchi ambao wamepisha mradi huo wa uwanja wa ndege, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Janejelly.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Napenda kujua, wananchi wa Rangi Tatu, Chamazi, Msongola na Mbande waliowekewa X na wakazuiwa kufanya maendeleo, ni lini watalipwa fidia ili wapishe ujenzi wa barabara?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sheria zetu za barabara baada ya kuongeza zile mita 60 tuliweka X ambazo tunatafuta fedha, lakini kama kuna wananchi ambao walikuwa ndani ya mita 45 kwa mujibu wa sheria yetu, maana yake walikuwa wako kwenye *reserved*. Itategemea, kama ni *X* nyekundu maana yake hayo wataondolewa bila fidia, lakini *X* ya kijani maana yake tumeshafanya tathmini na watatakiwa kulipwa fidia yao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Uchukuzi. Mheshimiwa Zedi.

Na. 373

**Ajira za Ujenzi wa *SGR* – kwa Vijana wa Bukene**

**MHE. SELEMANI J. ZEDI** aliuliza: -

Je, kwa nini Kampuni za *CCECC* na YAPI MARKEZI zinazojenga *SGR* Bukene zinatoa ajira zisizohitaji ujuzi kwa Vijana wanaotoka nje ya Bukene? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Reli *(TRC)* inaendela na ujenzi wa Reli ya Kisasa kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza (Km 1,219), Tabora – Kigoma (Km 506) na Uvinza – Msongati (Km 282) ambao ni chachu katika uchumi wa Taifa. Utekelezaji wa mradi huu umetoa fursa za ajira kwa wenye ujuzi *(skilled)* na wasio na ujuzi *(unskilled)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ajira za wasio na ujuzi, mradi huu umetoa kipaumbele kwa wazawa katika maeneo ambayo yamepitiwa na mradi kwa kupewa ajira hizo kwa lengo la kuongeza ushiriki wa wananchi katika uchumi *(local content)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchukua fursa hii kumtoa hofu Mheshimiwa Selemani Zedi, Mbunge wa Bukene kuwa Serikali imekuwa ikizingatia ajira kwa wazawa ambao wamepitiwa na mradi katika maeneo yote ikiwemo Bukene.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zedi.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Naibu Waziri, nina maswali ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ilivyo sasa hivi, Kampuni za *CCECC* na YAPI MARKEZI ambazo zinajenga Reli ya SGR na wana kambi pale Bukene, wana jumla ya vibarua (wafanyakazi wasio na ujuzi) kama 300; lakini kati ya hawa 300, wanaotoka katika Jimbo la Bukene hawazidi 12. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuongozana nami ili twende kwenye kambi hii ili akahakiki ukweli?

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ulivyo ni kwamba, hawa *CCECC* pamoja na YAPI MARKEZI hata kwa kazi za vibarua

wanaleta vijana kutoka Morogoro na Dar es Salaam na vijana wa eneo la pale wanakosa ajira.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru Mheshimiwa Zedi kwa jinsi anavyofuatilia Vijana wa Bukene waweze kupata ajira katika mradi ambao kimsingi unapita katika eneo ambalo yeye ni mwakilishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Zedi kwamba ni maelekezo ya Serikali, wakandarasi mbalimbali wanaotekeleza miradi mbalimbali katika maeneo mbalimbali katika nchi yetu, wahakikishe kwamba wanatoa kipaumbele kwa vijana wa eneo husika hususan wanapokuwa wanatekeleza miradi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, inaielekeza *TRC* iende katika eneo husika ikatazame, kama, ambavyo Mheshimiwa Mbunge amekuwa akizungumza, kwamba kuna watu wengi wametoka eneo lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, baada ya Bunge hili pengine tutapanga mimi na yeye twende tukajiridhishe; na ninawataka wakandarasi hao sasa waendelee kuhakikisha kwamba wanachukua vijana katika maeneo ambayo miradi hiyo inapita.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Hawa.

**MHE. HAWA S. MWAIFUNGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Changamoto ya vijana wa maeneo husika katika mradi huu siyo Bukene peke yake, hata katika Jimbo la Tabora Mjini, vijana wengi wanaoletwa pale hawatoki Tabora Mjini, wanakuja kutoka mikoa mingine mbalimbali. Nini changamoto hiyo ambayo hata vijana wetu wanaweza kufanya hizo shughuli ambazo wengine wanakuja kutoka mikoa mingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma takwimu za jumla ya ajira zote katika mradi wetu huu wa *SGR* kutoka Dar es Salaam mpaka Tabora kwenda mpaka Mwanza na kwenda mpaka Kigoma, tuna vijana au watu walioajiriwa takribani 1,730 na ajira za kati ni 5,659 wakati ajira za chini ni 5,694. Hawa wa ajira za chini wote kwa sehemu kubwa wanatoka nchini mwetu sehemu tofauti tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo basi, ninawaelekeza wakandarasi hao kuhakikisha kuwa wanapokuwa wanachagua vijana hao wa ajira za chini wahakikishe kwamba wanatoa msukumo zaidi au kipaumbele zaidi kwenye eneo ambalo mradi huo unapita.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa, tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Antipas Mgungusi.

Na. 374

**Hitaji la Magari kwa Jeshi la Polisi – Malinyi**

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI** aliuliza: -

Je, lini Serikali Itapeleka Magari kwa Jeshi la Polisi Malinyi ili liweze Kutoa Huduma Stahiki kwa Wananchi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba, mwaka 2023 Serikali kupitia Jeshi la Polisi iligawa gari moja jipya lenye namba za usajili *PT* 4851 *Toyota Land Cruiser Pickup* kwa Wilaya ya Malinyi, hivyo, kufanya wilaya hiyo kuwa na magari mawili ya Polisi yanayofanya kazi. Serikali inaendelea kutenga fedha kutoka kwenye bajeti yake kila mwaka wa fedha kwa ajili ya ununuzi vitendea kazi mbalimbali yakiwemo magari na kuyagawa kwenye mikoa na wilaya zote hapa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antipas.

**MHE. ANTIPAS Z. MGUNGUSI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini kwa ukubwa wa Wilaya ya Malinyi, huhitaji walau magari matatu kwa uchache sana lakini magari mawili ambayo Mheshimiwa Waziri ameyataja moja halipo kwenye hali nzuri. Je, Serikali iko tayari kutuongezea gari muda wowote mwaka huu? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni shukurani kwa Mheshimiwa Waziri na Kamanda *IGP* kwa kutupatia fedha kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Polisi kwa maana cha *OCD* katika eneo la Kipingo. Ahsante sana, nasubiri majibu ya swali la kwanza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Antipas Mgungusi kwa jitihada nzuri anazozifanya za maendeleo kwa ajili ya Jimbo lake la Malinyi, lakini pamoja na jitihada hizi amekuwa akifuatilia masuala ya vitendea kazi kwa upande wa Jeshi la Polisi jimboni kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la gari lingine kwa ajili ya kuimarisha usalama kule Malinyi, naomba nimwahidi Mheshimiwa Antipas, kwamba tutaongeza gari lingine la *OCCID* kwenye miezi ijayo ili kwenda kuimarisha ulinzi kwenye jimbo lake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitumie nafasi hii kuwaambia Waheshimiwa Wabunge, kuna magari ya *OCCID* (Wapelelezi wa Wilaya), kwamba kufikia mwezi Agosti, Mungu akijaalia tunapanga kuyasambaza nchi nzima kila wilaya ili kuimarisha ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Naibu Spika, natumia nafasi hii kuwahakikishia Watanzania kuwa tumejipanga ipasavyo kuhakikisha uchaguzi wa mwaka huu unafanyika kwa amani na usalama, na tumejipanga kwenye vitendea kazi pamoja na utimamu wa Jeshi la Polisi na vyombo vingine kuhakikisha kila atakayepanga kufanya fujo anashughulikiwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas.

**MHE. ATHUMAN A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Namwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani, katika Kijiji cha Ishihimulwa Kata ya Bukumbi, Mbunge na wananchi tumejenga kituo kizuri na cha kisasa lakini hatuna usafiri. Tunaomba atufikirie gari au pikipiki. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo nimesema kwanza, kwa Wilaya za Kipolisi ambazo zilikuwa hazijapata magari awamu ya kwanza, hivi sasa tayari tumeshapeleka magari mapya, *Land Cruiser* kwenye Wilaya zote za Kipolisi ikiwemo Wilaya za Mkoa wa Tabora.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama gari halijafika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Almas, mpango huu kama mlikuwa hamjapata gari ile awamu ya kwanza; awamu ya pili tumeshapeleka magari, nita-*check* kama halijafika basi nihakikishe linafika. Vilevile, hata kwenye mpango wa *OCCID* nchi nzima kupata magari *Land Cruiser* mapya kufika Agosti, pia na hili tutalizingatia. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wilaya ya Nyang'hwale pamekuwa na mwingiliano wa watu wengi kwa ajili ya kuja kuchimba madini na tuna Ofisi ya Uhamiaji pale na wako wawili hawana hata gari, je, Serikali iko tayari kutuongezea Watumishi wa Uhamiaji pamoja na kutupatia gari la ofisi? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Amar, kwa ufuatiliaji. Nimhakikishie, hivi ninavyozungumza, Chuo cha Idara ya Uhamiaji tuna vijana ambao wako kwenye mafunzo. Watakapotoka tutahakikisha tunapeleka Maafisa kwa ajili ya kuimarisha huduma za Idara ya Uhamiaji kule Nyang'hwale.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Kunti.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kituo cha Polisi Wilaya ya Chemba kinakabiliana na changamoto kubwa ya samani za ofisi. Kituo kimekamilika, kina zaidi ya miezi nane, lakini wanashindwa kuhamia kwa sababu tu ya ukosefu wa samani za ofisi. Serikali ina mkakati gani wa dharura wa kuwapatia Polisi wetu samani za ofisi ili waweze kulitumia lile jengo lao jipya? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Swali la msingi ilikuwa magari, wewe unaleta majengo. Mheshimiwa Waziri, majibu.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimesikia hoja ya Mheshimiwa Kunti, ninaomba niichukue tutaifanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Kanyasu, kwa niaba yake Mheshimiwa Amar.

Na. 375

**Kufufua Kiwanda cha Pamba na Mafuta Kasamwa**

**MHE. HUSSEIN N. AMAR K.n.y. MHE. CONSTANTINE J. KANYASU** aliuliza: -

Je, Serikali haioni haja ya kukifufua Kiwanda cha Pamba na Mafuta Kasamwa kwa kuwa hivi karibuni nchi ilikabiliwa na uhaba wa mafuta?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakushukuru. Serikali kupitia Bodi ya Pamba *(TCB)* mwaka 2020 ilifanya tathmini juu ya hali ya viwanda vya kuchambua pamba nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini hiyo iliwezesha Chama cha Ushirika Geita kufanya maamuzi ya kufufua Kiwanda cha Kuchambua Pamba cha Kasamwa kupitia mkutano wa tarehe 27 Machi, 2025 kwa kukopa fedha katika Benki ya Azania, mkopo wa kiasi cha shilingi bilioni 8.68. Aidha, chama kimepanga kuanza na kiwanda cha kuchambua pamba na kiwanda cha kukamua mafuta kitafuata baada ya hapo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amar.

**MHE. HUSSEIN N. AMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, kwa kuwa kiwanda kile kilikuwa kikitoa ajira kwa vijana wetu na upatikanaji wa mafuta kwa gharama nafuu, je, kiwanda hiki kitaanza lini matengenezo na kuanza kufanya kazi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa sababu Wilaya ya Nyang'hwale ni wakulima wazuri wa pamba, je, Serikali ina mpango gani wa kutafuta wawekezaji ili na sisi tuweze kujengewa kiwanda cha kuchambua pamba na kukamua mafuta Wilaya ya Nyang'hwale? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa maswali yake, lakini ufuatiliaji kuhusiana na viwanda hasa kwenye Wilaya ya Nyang'hwale na Jimboni kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, Serikali itavifufua viwanda karibu vyote vilivyobinafsishwa na vilivyokufa na hasa kwenye sekta hii ya pamba kupitia Ushirika. Vyama vya Ushirika tayari tumeshafanya tathmini na ndiyo maana tumewasaidia ili waweze kupata mikopo hii kwenye Benki zetu za Kilimo, lakini na hizi za Uwekezaji ikiwemo hii Azania.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, siyo tu Kiwanda hiki cha Kasamwa lakini pia na viwanda vingine ambavyo vilikuwa

vimefungwa, tunataka vifufuliwe vyote kwanza kama nilivyosema vya kuchambua pamba. Pili, mbegu zitakazopatikana kwenye kuchambuliwa pamba ndiyo zitakazopelekwa kuzalisha mafuta katika viwanda hivyo. Kwa hiyo, na viwanda hivi vingine vitafuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Wilaya yake ya Nyang'hwale, Serikali hasa itaendelea na utaratibu huu huu wa kuwasaidia, lakini na kuwahamasisha zaidi wakulima, kwa sababu changamoto tuliyonayo ni upatikanaji wa malighafi kwa ajili ya viwanda hivi. Kwa hiyo, nnawahakikishia Wananyang'hwale na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Wizara ya kilimo imepanga kuongeza uzalishaji wa mbegu ili mbegu hizo zitumike kwenye hivi viwanda kuzalisha mafuta ya kula. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Amandus.

**MHE. AMANDUS J. CHINGUILE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Serikali imefikia hatua gani kuhusu kufufua kiwanda cha kubangua korosho na kiwanda cha kuzalisha mafuta ya kula vilivyoko katika Jimbo langu la Nachingwea? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pia, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Amandus kwa ufuatiliaji kuhusiana na viwanda vya korosho. Kwa kuwa tunajua Serikali inategemea sana zao la korosho kuingiza mapato, lakini pia na wananchi kwa maana ya wakulima na hasa kwenye hiyo Mikoa ya Kusini ikiwemo kule Nachingwea.

Mheshimiwa Naibu Spika, viwanda hivi vya korosho na kile cha mafuta cha Ilulu ni moja ya viwanda ambavyo vilikuwa vimebinafsishwa, lakini kwa sababu vilikuwa havifanyi kazi vizuri, vilivirejeshwa Serikalini na kuviweka kwenye utaratibu wa usimamizi chini ya Mamlaka ya Uwekezaji na Mauzo ya Nje *(EPZA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshapata wawekezaji chini ya utaratibu huo, kile cha kubangua korosho tuna Mwekezaji mmoja *ANH & Raka Limited* ambao wako chini ya *EPZA*; lakini kile

Kiwanda cha Mafuta cha Ilulu nako pia tuna Mwekezaji mwingine mpya ambaye ameingia mkataba na *EPZ* ambaye anaitwa *MCL Agro Company Limited* nao hawa wanakwenda kuzalisha mafuta kupitia kukamua ufuta, karanga na mbegu nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, tutaendelea kuvifanyia kazi, kuvutia uwekezaji katika viwanda vya korosho Mikoa ya Kusini ikiwemo Nachingwea, ili tuhakikishe tunaongeza thamani badala ya kuuza malighafi hasa korosho ambayo tunaitegemea sana kama zao la biashara. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Pallangyo.

**MHE. DKT. JOHN D. PALLANGYO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa nafasi hii. Tunatambua kwamba, Serikali iko kwenye mpango wa kufufua zao la pareto Kisimiri Juu, ambako lilikuwa linalimwa kwa wingi miaka ya 1960 na 1970. Sasa, je, ni upi mpango wa Serikali kufufua kiwanda cha pareto kwa ajili ya kuchakata hilo zao, lakini pia kuhakikisha kwamba kunakuwa na soko na vijana wanapata ajira?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Nampongeza sana Mbunge Mheshimiwa Dkt. Pallangyo kwa ufuatiliaji kwenye hii sekta ya kilimo na mahsusi kwenye sekta ya pareto. Ni kweli zao hili miaka ya 1970 lilikuwa ni zao muhimu sana kwa ajili ya kuongeza kipato kwenye sekta ya kilimo na siyo tu kwake kule, lakini pia na kwa Mikoa ya Iringa, Mbeya, na maeneo yote ambayo yanalima pareto.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeshaanza kufanya juhudi kubwa za kufufua viwanda hivi ikiwemo kile kiwanda cha pareto pale Mafinga, ambacho nacho kinazalisha lakini bado hakipati malighafi ya kutosha. Pia na kwake kule, ambako tukishapata malighafi ya kutosha kwa maana ya pareto ikilimwa kwa wingi, tutahakikisha tunahamasisha wawekezaji ili waweze kuwekeza pale kwenye jimbo lake. Tayari tuna wengine ambao

wamewekeza kule Mbeya, kwa maana ya kuchakata na kuongeza thamani pareto na wanapeleka hata Nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutalifanyia kazi na hasa niwahakikishie wakulima kama watalima pareto ya kutosha ili viwanda hivi viweze kupata malighafi ya kuchakata kwenye jimbo lake na maeneo mengine.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya. Mheshimiwa Sekiboko. Kwa niaba ya Mheshimiwa Sekiboko, Mheshimiwa Shangazi.

Na. 376

**Chanzo cha Fedha za Kugharamia Huduma ya Afya kwa Mama Mjamzito na Mtoto Chini ya Miaka Mitano**

**MHE. RASHID A. SHANGAZI K.n.y. MHE. HUSNA J. SEKIBOKO** aliuliza: -

Je, kipi chanzo mahsusi cha fedha za kugharamia huduma ya afya kwa mama mjamzito na mtoto chini ya miaka mitano?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa vyanzo mahsusi vya ugharamiaji wa huduma za Afya kwa akina mama wajamzito na watoto wenye umri chini ya miaka mitano ni kupitia fedha za ndani pamoja na wadau wa maendeleo wanaochangia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Shangazi.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nina swali la nyongeza

Kwa kuwa Serikali kupitia Sera ya Afya ina utaratibu wa kuanzisha mifuko mahsusi kwa ajili ya kusaidia hasa katika haya maeneo ambayo yana uhitaji mkubwa, kwa mfano hili la mama mjamzito pamoja na watoto chini ya miaka mitano, Serikali haioni sasa kuna umuhimu ikaleta utaratibu wa kutengeneza mfuko mahsusi ambao utabeba jukumu hili? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Shangazi kwa swali lake hili la msingi hasa kwenye hili eneo ambalo kidogo utekelezaji wake unahitaji umakini wa hali ya juu. Wazo lake tunalichukua na kwenda kulifanyia kazi kama ambavyo amelipendekeza, tuone ni namna gani tunaweza tukashirikiana na wadau mbalimbali na kuunda huo mfumo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Gekul.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi. Mheshimiwa Naibu Waziri, ni vifaatiba vipi au dawa zipi mama mjamzito anayejifungua kwa *operation* anapaswa kulipia, kwa maana sasa wanachajiwa? Ni zipi hasa ambazo wanapaswa kulipia? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Sera ya Afya hakuna mama mjamzito anayetakiwa kupata huduma zote bure, lakini kama ambavyo nimekwishasema hapa Bungeni kwa sababu ya changamoto mbalimbali, imewezekana kuwalipia bure 65% ya akina mama, lakini 35% wamekuwa wakipata changamoto mbalimbali kutokana na masuala ya kibajeti, lakini pia na uzembe wa utendaji katika maeneo husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani siyo kwamba ni la kusema *specific* hiki na hiki kinatakiwa kilipiwe, na hiki hakitakiwi kulipiwa. Mama mjamzito kulingana na sera, anatakiwa kupata huduma. Tukishirikiana na hospitali zetu pamoja na Serikali za

maeneo husika kwa maana ya wilaya husika au mkoa husika, tunaweza tukapunguza hili tatizo kwa pamoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Salma Kikwete.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Huduma ya afya kwa mama mjamzito na watoto ni jambo muhimu na la msingi katika kunusuru changamoto zinazojitokeza kwa watoto hawa na mama yao. Sasa, je, ni lini Serikali itatupatia fedha ili kuweza kujenga Kituo cha Afya kule Nangaru, ili mama mjamzito na watoto hawa waweze kupata huduma hizo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge mama yetu Salma Kikwete, moja kwa kazi kubwa sana wakati akiwa *First Lady* aliyoifanya kwenye eneo la mtoto wa kike, amefanya kazi kubwa sana. Pia kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya kwenye jimbo lake. Nimwambie tu, nikitoka hapo tutafanya mawasiliano na *DMO* wake na uongozi wa wilaya ili tuweze kujua wameweka nini kwenye mpango kwa kushirikiana pamoja na TAMISEMI tuweke huu mkakati wa pamoja wa kuhakikisha hicho kituo kinaenda kujengwa na bajeti ya mwaka ujao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea. Wizara ya Mawasiliano, Mheshimiwa Sanga.

Na. 377

**Huduma ya *Internet* kwa *Satellite* Nchini**

**MHE. FESTO R. SANGA** aliuliza: -

Je, lini Serikali itafikia makubaliano na kampuni zinazotoa huduma ya *Internet* kwa *Satellite* duniani kutoa huduma hapa nchini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutoa huduma ya intaneti hapa nchini kwa kutumia *satellite*, kampuni inahitaji kuwa na leseni ya kutoa huduma hiyo kutoka Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*. Hadi sasa, *TCRA* imetoa leseni kwa mtoa huduma mmoja wa *satellite (Connect Broadband Tanzania Limited)* ambaye alipewa leseni mwaka 2021 baada ya kukikidhi vigezo vyote vinavyohitajika kwa mujibu wa sheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, maombi ya watoa huduma wote yamekuwa yanashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni, na pindi yanapokidhi vigezo wanapewa leseni. Aidha, utaratibu mzima wa upatikanaji wa leseni, aina ya leseni pamoja na masharti ya leseni vyote hivyo vinapatikana katika tovuti *(website)* ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* inakaribisha na inaendelea kupokea maombi kutoka kwa Kampuni mbalimbali zenye sifa ya kutoa huduma za *satellite* kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zinazosimamia sekta ya mawasiliano hapa Nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga.

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza, Mheshimiwa Waziri utakubalina nami kwamba, siyo maeneo yote ya nchi hii *network* inashika. Naweza nikasafiri kutoka Dodoma hadi nafika Makete kuna maeneo mengi *network* haishiki, lakini hiyo ni pamoja na maeneo mengine nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, moja kati ya maelekezo ya Rais ya tarehe 13 Mwezi Mei, 2023 yalikuwa siyo muhimu kuendelea kujenga minara kwenye nchi nzima, sasa twende kwenye *satellite*. Ni ipi kauli ya Serikali kuwa na *satellite* yake kwenye suala la *internet* kwenye Taifa letu la Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lingine, *internet* inakuja na mambo mema na inakuja na mambo mabaya. Siku ya jana na leo ...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sanga, subiri. Waheshimiwa Wabunge, naomba utulivu! Waheshimiwa Wabunge, tunaomba utulivu ndani ya Bunge!

**MHE. FESTO R. SANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, *internet* inakuja na mambo mema na mambo mabaya. Siku ya jana na leo tumeona *page* rasmi za taasisi mbalimbali za Serikali zimekuwa zikipata mtikisiko. Sasa kwa nafasi hii ya swali hili, ni ipi kauli ya Wizara ya Mawasiliano kwa Watanzania kuelekea tukio hili ambalo limekuwa likichafua taasisi na viongozi wetu wa Serikali kwa kipindi hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali la pili kwa kuwa ni uchunguzi usilijibu, jibu la kwanza. Mheshimiwa Waziri, una majibu?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri aliyoyatoa na ninaomba kwa ruhusa yako nimjibu Mheshimiwa Sanga kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, moja, ni dhahiri Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ameshatoa maelekezo ya nchi yetu kurusha *satellite* yake. Kwenye Hotuba yangu ya Bajeti hapa wiki iliyopita nilielezea ziko hatua ambazo tumeanza, kuzichukua ikiwemo kuanza mchakato wa uridhiaji wa mikataba miwili: Mkataba wa Sheria za Kanuni za Nchi za Utafiti wa Anga ya Juu wa Mwaka 1967, na Mkataba unaosimamia Usajili wa Vyombo vya Anga za Juu wa Mwaka 1975. Kwa hiyo, maelekezo ya Mheshimiwa Rais, yanatekelezwa, na ninalihakikishia Bunge lako kwamba, nchi yetu itarusha *satellite* yake yenyewe kusaidia mawasiliano ikiwemo mawasiliano ya *internet*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, ni suala la usalama wa mitandao yetu na mifumo yake. Naomba kulithibitishia Bunge

lako kwamba, Serikali kupitia *TCRA* inasimamia usalama wa mifumo yetu na mifumo yetu ipo salama salimini. Siku ya jana, *page* za Mitandao ya Kijamii chache, mbili za taasisi za Serikali ziliingiliwa, na tunaposema *account* ya mtandao wa kijamii siyo mfumo *perse* wa TEHAMA wa taasisi ya Serikali. Ni *account* ambayo hata mimi na wewe tunayo, ni *account* ambazo taasisi hizi kupitia Maafisa wake wengine wa ngazi za chini wanaweza kutumia hata simu ya mkononi ku-*login* kwa ajili ya kufanya habari mbalimbali za taasisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, zile taratibu zao za kiusalama zilikuwa siyo thabiti na ikasababisha kuingiliwa. Mitandao hiyo ama *account* hizo zimesharejeshwa, na Wizara yangu na taasisi nyingine za Kiserikali zinaendelea kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali za Serikali, kuhakikisha *accounts* za Mitandao ya Kijamii ziko salama, lakini kifumo yetu yote iko salama. Serikali itaendelea kusimamia jambo hili kwa kuhakikisha nchi yetu inaendelea kuwa salama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Waheshimiwa Wabunge, maswali yetu yamekwisha sasa ni kipindi cha wageni Bungeni.

Wageni wa Mheshimiwa Spika, Ndugu Nsolo Mlozi, Mkuu wa Kitengo cha Biashara na Kilimo, Benki ya NMB Makao Makuu. *(Makofi)*

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wageni wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, Waziri wa Kilimo, Ndugu Gerald Mweli, *ndc* – Katibu Mkuu, Dkt. Stephen Nindi - Naibu Katibu Mkuu, Mheshimiwa Mizengo Pinda - Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri wa Kilimo na Chakula nchini. *(Makofi)*

Ahsanteni, tunaye Dkt. Florens Turuka - Katibu wa Baraza la Ushauri wa Kilimo na Chakula nchini, Ndugu Andrew Massawe - Mjumbe wa Baraza la Ushauri wa Kilimo na Chakula nchini, Ndugu Geoffrey Kirenga - Mjumbe wa Baraza la Ushauri wa Kilimo na

Chakula nchini, Dkt. Mwatima Juma - Mjumbe wa Baraza la Ushauri wa Kilimo na Chakula nchini, Dkt. Leonard Akwilapo - Mwenyekiti wa Bodi, Chuo cha Sukari cha Taifa na Brigedia Jenerali (Mstaafu) Aloyce Damian Mwanjile, *ndc* - Mwenyekiti wa Bodi ya Korosho Tanzania (CBT). *(Makofi)*

Yupo pia Ndugu Filbert Mponzi - Mwenyekiti wa Bodi ya Sukari Tanzania *(SBT)* ambaye pia ni Afisa Mkuu wa Biashara wa Benki ya NMB, Ndugu Juma Kimori - Mwenyekiti wa Bodi ya Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika *(COASCO)* ambaye pia ni Afisa Mkuu wa Fedha wa Benki ya NMB, Mheshimiwa Balozi John Ulanga - Mwenyekiti wa Bodi, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula *(NFRA),* Dkt. Richard Masika - Mwenyekiti wa Bodi, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji *(NIRC)* na Kepteni (Mstaafu) John Chiligati - Mwenyekiti wa Bodi Kampuni *ITRACOM Fertilizers Limited,* ahsanteni. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge makofi kama hayo yatamtia moto wa kutaka kurudia. *(Kicheko)*

Wapo pia Ndugu Imani Kajula - Mjumbe wa Bodi ya Chai, Ndugu Frank Nyabundege - Mtendaji wa Benki ya Kilimo *(TADB),* Ndugu Godfrey Ng'urah - Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Ushirika Tanzania, Mheshimiwa Hajat Fatuma Mwasa - Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Mheshimiwa Kanali Patrick Sawala - Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Mheshimiwa Mwanahamis Munkunda - Mkuu wa Wilaya ya Mwanga, Ndugu Vianey Rweyendela - Mkurugenzi Mkaazi – *AGRA* na Ndugu Said Nkumba - Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Tabora, ahsanteni. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Gipson Magambo - Mwenyekiti wa Umoja wa Madhehebu ya Kikristu na Sheikh Zahoro Mrisho - Sheikh wa Wilaya ya Nzega, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wageni 65 wa Mheshimiwa David Ernest Silinde - Naibu Waziri wa Kilimo ambao ni Wenyeviti wa Serikali za Mitaa kutoka Tunduma, Mkoa wa Songwe. *(Makofi)*

Wapo pia wageni sita wa Mheshimiwa Deus Clement Sangu - Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambao ni wafanyabiashara kutoka Kariakoo, Jijini Dar es Salaam, karibuni. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Amina Daudi Hassan ambaye ni Ndugu Mwatima Mussa, mtoto wake kutoka Kusini Zanzibar. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Mohamed Suleimani Omar ambaye ni Ndugu Mahmoud Mohamed, mtoto wake kutoka Malindi, Zanzibar. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Balozi Liberata Rutageruka Mulamula ambaye ni Mwandishi wa Kitabu cha Uongozi wako, Historia yako kutoka Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Wageni wanne wa Mheshimiwa Robert Chacha Maboto ambao ni ndugu zake kutoka Bunda, Mkoa wa Mara. *(Makofi)*

Wapo wageni 54 wa Mheshimiwa Janeth Elias Mahawanga kutoka Taasisi ya Wanawake na Samia kutoka Jijini Dar es Salaam. *(Makofi)*

Wageni wengine 19 wa Mheshimiwa Munde Abdallah Tambwe ambao ni Baraza la Mawaziri wa Serikali ya Wanafunzi Chuo Kikuu Kishiriki cha Askofu Mihayo kutoka Mkoa wa Tabora. *(Makofi)*

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere ambao ni wakulima wa pamba na Ushirika kutoka Wilaya ya Bunda, Mkoani Mara. *(Makofi)*

Wageni 35 wa Mheshimiwa Edward Olelekaita ambao ni wanafunzi kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. *(Makofi)*

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wapo wageni wawili kutoka Chamwino, Mkoani Dodoma. *(makofi)*

Pia wapo wananchi watatu kutoka Mkoa wa Morogoro, wafanyakazi 21 wa Taasisi ya Kuboresha Hali ya Chakula na Lishe nchini kutoka Jijini Dar es Salaam, karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wanafunzi 100 na walimu watatu wa Shule ya Msingi St. Ann's kutoka Rujewa, Wilayani Mbarali Mkoa wa Mbeya. *(Makofi)*

Katibu.

**NDG. EMMANUEL MPANDA – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla sijamwita Mheshimiwa Waziri kuna Wenyeviti wa Serikali za Mitaa 71 kutoka Mji wa Tunduma, Wenyeviti Serikali za Mitaa, ahsanteni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa mwaka 2024/2025, tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa kipindi cha miaka minne na Mpango na Bajeti kwa mwaka 2025/2026 ambayo inagusa maisha ya wakulima kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee ninapenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza kwa kishindo Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020. Hakika utekelezaji huo umezingatia misingi ya mageuzi thabiti, ustahimilivu, kujali utu, uadilifu, upendo, usawa na maridhiano uliotokana na utashi wa kisiasa wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kufanya shughuli za maendeleo kwa ajili ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa unyenyekevu mkubwa, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025. Ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na ni matumaini yangu kuwa kutokana na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita, wananchi wataendelea kumuamini na kukiamini Chama Cha Mapinduzi kwa kumpa kura za ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa Mgombea Mwenza kwa nafasi ya Makamu wa Rais. Kutokana na umahiri na ushupavu wake, nina uhakika kuwa watakapopata ridhaa ya wananchi atamsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ili kufikia malengo ya kuwaletea maendeleo wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamfahamu na Wana-CCM tunamfahamu, uadilifu wake, umahiri wake, heshima yake kwa viongozi wake na wananchi na kwetu sisi ambao ni waumini wa misingi ya kijamaa inayoamini katika soko la haki. Tunaamini Mheshimiwa Rais amepata msaidizi sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee kabisa ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM kupitia

Wizara ya Kilimo. Ninamuahidi nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu mkubwa ili kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali na Chama chetu Cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika kusisitiza kilimo endelevu kinachozingatia utunzaji wa mazingira, kuimarisha usalama wa chakula na kupambana na umaskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa utumishi wake Serikalini umeendelea kuwa chachu katika kuchochea maendeleo nchini na wengi wetu ambao tumefanya naye kazi akiwa Waziri wa Fedha na Mipango na sasa Makamu wa Rais, ametupa somo muhimu sana katika uongozi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumshukuru yeye binafsi kwa kipindi chote cha uongozi wake. Vilevile, ninampongeza kwa kuwezesha kuidhinishwa bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo imetoa maelekezo ya msingi kwa Wizara ya Kilimo. Ninamhakikishia kuwa maelekezo yake yote yamezingatiwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2025/2026. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru ofisi yake kwa kuratibu mapitio ya Programu ya Kuendeleza Kilimo Awamu ya Pili *(ASDP II)* ambayo yamechochea Wizara ya Kilimo kuandaa Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo *(Tanzania Agriculture Master Plan 2050)*. Hivyo, kuanzia mwaka ujao 2025/2026 wa fedha, Wizara ya Kilimo inazingatia malengo hayo ambayo

yametafsiriwa kwenye mpango kabambe wa mageuzi ambayo yataendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na Azimio la Kampala *(CAADP 2026 – 2035)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Doto Mashaka Biteko (Mbunge), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati katika kuendelea kusimamia utekelezaji wa mipango ya kilimo kwa kuhimiza uwekezaji katika utafiti na kuboresha upatikanaji wa teknolojia za sasa ili kuongeza tija na uzalishaji katika kufikia malengo ya Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa weledi, ujuzi na ustadi mkubwa. Usimamizi wake umewezesha majadiliano ya Bunge kuwa na tija katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza kwa kutumia nafasi yake kuwatendea haki Waheshimiwa Wabunge pamoja na kuweka misingi imara wa majadiliano ndani ya Bunge ambayo inajenga uwajibikaji wa pamoja na kutoa haki kwa pande zote. Pia ninampongeza kwa kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini na kwa kuwa Jimbo hilo limegawanywa sehemu mbili na ninafahamu mapenzi yako ya kuwasaidia wakulima wengi wanaopatikana Jimbo la Uyole. Hivyo, sisi wakulima tunamuomba akagombee Jimbo la Uyole. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninakupongeza wewe mwenyewe pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mheshimiwa Deodatus Philip Mwanyika, Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; Mheshimiwa Dkt. Joseph Kizito Mhagama, Mbunge wa Jimbo la Madaba; na Mheshimiwa Najma Murtaza Giga, Mbunge wa Viti Maalum kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu Tukufu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano, maoni, usimamizi, ufuatiliaji na miongozo mbalimbali

kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Ninaiahidi Kamati kuwa maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 na maandalizi ya mpango wa mwaka 2025/2026. Hivyo, imekuwa sehemu ya maendeleo, mabadiliko na majadiliano juu ya kujenga msingi imara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawapongeza Waheshimiwa Wabunge wote kwa umahiri wenu mkubwa katika kuchangia mijadala inayoendelea katika Mkutano wa Kumi na Tisa wa Bunge hili la Bajeti. Tunafahamu kuwa huwezi kuongelea mabadiliko yoyote ya sekta ya kilimo katika nchi yetu bila kushukuru michango ya Wabunge wote, kwa hakika mmechangia kwa kiwango kikubwa sana kuishauri Serikali na kumtia moyo Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo. Pamoja na kuwa safari bado ni ndefu, lakini kuna matumaini makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee ninamshukuru Mheshimiwa David Ernest Silinde, Naibu Waziri wa Kilimo kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya kilimo. Kwangu binafsi Mheshimiwa Silinde ni Naibu Waziri, ni rafiki na ndugu yangu, nimhakikishie kama Waziri, rafiki na ndugu yake kuwa Tunduma tutakuwa wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo - Bwana Gerald Geofrey Mweli, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Hussein Mohamed Omar, Naibu Katibu Mkuu - Dkt. Stephen Justice Nindi pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana watumishi wa Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaotoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara, aidha watumishi hao kwangu binafsi wamekuwa wasaidizi na washauri wazuri, ninawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninawashukuru sana wakulima wote nchini kwa mchango wao mkubwa katika kuhakikisha nchi hii inakuwa na usalama wa chakula na kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, msingi wa usalama wa Taifa letu ni wakulima wa nchi hii na Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itaendelea kulinda maslahi yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa dhati kabisa ninaishukuru Wizara ya Fedha na wataalam wote kwa ushirikiano wanaonipatia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, ninawapongeza kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo zinalenga kuleta maendeleo katika Jimbo letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru sana viongozi wa Chama Cha Mapinduzi wa Wilaya ya Nzega, Mkuu wa Wilaya, Madiwani, Mkurugenzi na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020. Asanteni sana, tutakutana Julai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Profesa Mohamed Yakub Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani kwa Kanda ya Afrika. Tunafahamu uchapakazi na utendaji wake wa kazi tangu akiwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili na Mshauri wa Rais katika masuala ya afya. Hakika tumepata mrithi sahihi wa nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani kwa Kanda ya Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba wa aliyekuwa Makamu wa Kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ndugu Cleopa David

Msuya. Hayati Msuya alikuwa kiongozi anayetambua kuwa maendeleo ya kilimo ni msingi wa maendeleo ya Taifa na alihakikisha sekta ya kilimo inapewa kipaumbele ili kufikia malengo ya uchumi endelevu na kupunguza umaskini. Hakika kama Taifa tutamkumbuka kwa ujasiri wake na uongozi wake wenye busara na maono ya hali ya juu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya mzee wetu mahala pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninatoa pole kwa Mheshimiwa Rais, kwako wewe Mheshimiwa Naibu Spika na Spika, Waheshimiwa Wabunge na Watanzania wote na familia kwa kuondokewa na aliyekuwa Mheshimiwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani Kanda ya Afrika, Dkt. Faustine E. Ndugulile aliyekuwa mwananzengo na kijana wa Wilaya ya Nzega.

Mheshimiwa Naibu Spika, daima tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika sekta ya afya, utumishi wa umma na uongozi wa Kimataifa. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Mheshimiwa Dkt. Ndugulile mahala pema peponi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nitoe pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania kwa kuondokewa na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania, Dkt. Daniel Nyoki Mgori, Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele.

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba hii ninayoisoma leo mbele ya Bunge lako Tukufu ni hotuba yangu ya mwisho kama Waziri wa Wizara ya Kilimo katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita kabla ya kwenda kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Hotuba hii imetoa taswira kwa ufupi wa hali ilivyokuwa katika mwaka 2020/2021, tathmini ya maelekezo ya Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2020, hotuba na maelekezo mahsusi aliyoyatoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021 ambapo alitoa vipaumbele na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani, sekta ya kilimo ilikuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo: -

(i) Uwekezaji mdogo wa fedha za umma katika sekta ya kilimo, upatikanaji mdogo wa mikopo na kutokuwa na mfuko wa kuendeleza sekta ya kilimo;

(ii) Shughuli za kilimo kufanyika pasipo kutambuliwa katika mifumo rasmi;

(iii) Kupanda na kushuka kwa bei za mazao na pembejeo za kilimo kutokana na athari za kidunia na uhaba wa Maafisa Ugani na vitendea kazi;

(iv) Usafirishaji wa mazao nje ya nchi kupitia Bandari ya Dar es Salaam kuchukua muda mrefu ambayo baadhi huharibika haraka kwa kutokupewa kipaumbele wakati wa kupakia kwenye meli;

(v) Ushiriki mdogo wa vijana na wanawake katika sekta ya kilimo uliosababishwa na ukosefu wa mitaji na umiliki wa ardhi;

(vi) Uhaba wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo; ushirika dhaifu na mifumo ya masoko isiyoshindani;

(vii) Utegemezi wa baadhi ya mazao ya kilimo kutoka nje ya nchi ikiwemo ngano, sukari na mafuta ya kula uliotokana na uzalishaji mdogo wa ndani ya nchi na kutokuwepo kwa mpango wa kuondoa tatizo hilo;

(viii) Uwezo mdogo wa ndani wa kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mimea uliosababishwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa ikiwemo ndege maalum ya kukabiliana na milipuko hiyo na kutegemea ndege kutoka mataifa ya jirani;

(ix) Ukosefu wa maabara za kilimo zenye ithibati; upungufu wa viwanda vya mbolea; na upungufu wa wataalam wa umwagiliaji, vitendea kazi na ofisi;

(x) Ukosefu wa mwelekeo imara wa kisera katika kuendeleza kilimo; na

(xi) Mifumo dhaifu ya ugharamiaji wa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto hizo ambazo tumezitaja ziliathiri sana watu wetu kuendelea kubaki kwenye umaskini na kufanya sekta ya kilimo isiyovutia na kuwa isiwe rasmi. Pia changamoto hizo ziliathiri ukuaji wa sekta ya kilimo, mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi, kiwango cha usalama wa chakula nchini, upatikanaji wa mitaji na pembejeo za kilimo, tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Maeneo mengine yaliyoathirika ni pamoja na mtandao mdogo wa miundombinu ya umwagiliaji na uwekezaji mdogo katika uzalishaji wa mbegu bora nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi mpaka kufikia mwaka 2020/2021 sekta ya kilimo ilikuwa imebaki kama sekta inayokwenda kwa kudra za Mwenyezi Mungu na jitihada binafsi za wakulima, kutokana na uwekezaji hafifu sana na usio wa uhakika wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha utekelezaji wa Awamu ya Sita, Ilani ya CCM ya mwaka 2020 iliielekeza Wizara ya Kilimo kupitia Ibara ya 34 (a) - (j) ukurasa wa 32 - 33 na Ibara ya 37 (a) – (d) ukurasa wa 36 - 46 kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kusimamia dhana ya ushirika wa hiyari na kuwanufaisha wakulima na wanaushirika chini ya usimamizi wa Serikali na kulinda maslahi ya wakulima;

(ii) Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji;

(iii) Kuongeza tija na uzalishaji na kuimarisha utafiti, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani na zana za kilimo;

(iv) Kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao, upatikanaji wa masoko, kuwajengea uwezo vijana wa kujiajiri na upatikanaji wa mitaji; na

(v) Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa kitaasisi na uratibu wa shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa tarehe 22 Aprili, 2021 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliielekeza Wizara ya Kilimo kutatua changamoto ya tija ndogo, uzalishaji wa mazao, kuimarisha utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, miundombinu ya umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani, mitaji, uhifadhi wa mazao, kuboresha afya ya udongo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hatua na matokeo yaliyofikia hadi Aprili, 2025 kama ifuatavyo: -

(i) Bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 294 hadi shilingi trilioni 1.248 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la 324%.

(ii) Ukuaji wa sekta ya kilimo umeongezeka kutoka 2.6% mwaka 2021 hadi 4.2% mwaka 2023. Aidha, ukuaji wa sekta unatarajiwa kufika 5% mwaka 2025/2026 na 10% mwaka 2030;

(iii) Thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi imeongezeka kutoka dola bilioni 1.2 hadi dola bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 195%;

(iv) Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani milioni 17.14 mwaka 2021/2022 hadi tani milioni 22.8 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 33% na kufanya utoshelevu wa chakula nchini kufikia 128% dhidi ya lengo la 130%;

(v) Uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani milioni 6.4 mwaka 2021/2022 hadi tani milioni 12.26 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 91.06% na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili wa mahindi Afrika;

(vi) Uzalishaji wa mchele umeongezeka kutoka tani milioni 1.746 mwaka 2020/2021 hadi tani milioni 3.04 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 72%;

(vii) Uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 898,000 mwaka 2020/2021 hadi tani milioni 1.4 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la 61%;

(viii) Uzalishaji wa korosho umeongezeka kutoka tani 210,000 hadi kufika tani 528,000 sawa na ongezeko la 150.6%;

(ix) Uzalishaji wa tumbaku umeongezeka kutoka tani 58,000 mwaka 2021 hadi tani 160,000 sawa na ongezeko la 173% na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili Barani Afrika;

(x) Uzalishaji wa miwa umeongezeka kutoka tani milioni 3.8 ambazo zilizalisha sukari tani 367,000 hadi kufika tani milioni 4.7 zilizozalisha sukari tani 431,000 ambao ni sawa na ongezeko la 17.1% kwa ajili ya kufikia lengo la uzalishaji wa tani 700,000;

(xi) Uzalishaji wa mkonge umeongezeka kutoka tani 36,000 hadi tani 61,000 sawa na ongezeko la 69%;

(xii) Uzalishaji wa kahawa umeongezeka kutoka tani 59,000 hadi tani 81,000 sawa na ongezeko la 37%;

(xiii) Uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kutoka tani 30,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 63,000 mwaka 2024/2025, sawa na ongezeko la 110%. Uzalishaji huo umechangia kuongezeka kwa upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 44,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 79,000 sawa na ongezeko la 78%;

(xiv) Uzalishaji wa zao la parachichi umeongezeka kutoka tani 149,000 hadi tani 195,000. Aidha, mauzo ya mazao ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 26,000 hadi tani 35,000 mwaka 2023 yenye thamani ya shilingi bilioni 252;

(xv) Uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta ya kula umeongezeka kutoka tani milioni 1.7 hadi tani milioni 2.14 sawa na ongezeko la 25%. Aidha, uzalishaji wa alizeti umeongezeka kutoka tani 478,000 mpaka tani milioni 1.21sawa na ongezeko la 154%;

(xvi) Uzalishaji wa ndani wa mbolea umeongezeka kutoka tani 32,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 158,000 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la 394%. Uzalishaji huo umechangiwa na kiwanda kipya cha kutengeneza mbolea cha *ITRACOM* katika Mkoa wa Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha tani 1,000,000 kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha miaka mitatu Serikali imewezesha kutoa ruzuku ya mbolea tani milioni 1.45 yenye thamani ya shilingi bilioni 708 kwa mazao yote. Hatua hiyo, imewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka tani 363,590 mwaka 2021hadi tani 848,000 mwaka 2023/2024, sawa na ongezeko la 133%. Aidha, matumizi ya mbolea kwa hekta yameongezeka kutoka kilo 19 hadi kilo 24 sawa na ongezeko la 26%. Ongezeko la matumizi ya mbolea ni sawa na 48% ya lengo la *CAADP* la kilo 50 kwa hekta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kwa mara ya kwanza imewezesha kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo *(Agriculture Development Fund)* kupitia Sheria ya Fedha, Namba 344. Mfuko huo umeanza kazi Januari, 2025 kwa ajili ya kuendeleza kilimo kwa kuimarisha bei za mazao zinaposhuka, kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo, kuimarisha miundombinu ya uhifadhi, utafiti na kuongeza thamani na shughuli zote za kuendeleza kilimo. Vilevile Wizara imewekeza na kufufua kilimo anga kwa kununua ndege maalum kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao na ndege nyuki 41 kwa ajili ya uchunguzi na udhibiti wa visumbufu kwa mimea na mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara imeongeza uwezo wa miundombinu ya kuhifadhi ya chakula kutoka tani 251,000 hadi tani 776,000 sawa na ongezeko la 209%.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika kipindi cha miaka minne tumepata mafanikio kwa kuboresha miundombinu ya utafiti, uzalishaji wa mbegu na huduma za ugani; uongezaji wa thamani na matumizi ya zana za kilimo; uzalishaji wa ajira zilizotokana na utekelezaji wa miradi ya kilimo; usambazaji wa pembejeo za kilimo kwenye mazao ya kimkakati; kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi hii na kuimarika kwa ushirika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la miundombinu ya utafiti, tumekamilisha kazi ya ujenzi wa Kituo cha Udhibiti wa Visumbufu *(National Biological Control Unit)* Kibaha, Maabara ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania, Maabara ya Kuzalisha Miche kwa Njia ya *Tissue Culture*, Maabara ya Udongo ya *TARI* Mlingano na ununuzi wa mashine mbili za kukausha mbegu na mitambo miwili ya kuchakata mbegu kwa Wakala wa Mbegu na maabara ya udongo ya mimea ya *TRIT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumenunua na kusambaza vitendea kazi kwa maafisa ugani, magari 44, pikipiki 6,444, vipima afya ya udongo 143, vishikwambi 5,426, visanduku vya ugani 1,662 na kujenga nyumba za Maafisa Ugani 50. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la uongezaji thamani na matumizi ya zana za kilimo: -

(i) Tumenunua matrekta 500 na matrekta madogo *(power tillers)* 800 kwa ajili ya kutoa huduma za kilimo;

(ii) Tumekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusindika zabibu chenye uwezo wa kusindika tani 300; na

(iii) Tumekamilisha ujenzi wa kituo mahiri cha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna kilichopo Mtanana, Mkoani Dodoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la ajira zilizotokana na utekelezaji wa miradi ya kilimo, Wizara imezalisha ajira za kudumu na za muda mfupi 1,008,000 kupitia programu na miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo ikiwemo miradi ya uzalishaji

na utafiti; ujenzi, ukarabati, usanifu miradi ya umwagiliaji, programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora na Vyama vya Ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la usambazaji wa pembejeo za kilimo kwenye mazao ya kimkakati, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanya yafuatayo: -

(i) Imewezesha upatikanaji na usambazaji wa viuatilifu vya korosho vya unga tani 109,000 na vya maji lita milioni 8.8 na mabomba ya kunyunyuzia 6,000 yenye thamani ya shilingi bilioni 556.7 kwa mpango wa ruzuku;

(ii) Imewezesha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la tumbaku zikiwemo mbolea, viuatilifu vyenye thamani ya shilingi bilioni 607; na

(iii) Imewezesha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la pamba yenye thamani ya shilingi bilioni 325.36.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la miundombinu ya umwagiliaji, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imefanikisha yafuatayo:-

(i) Imeongeza miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa kutoka miradi 13 mwaka 2021 hadi miradi 780 mwaka 2024/2025. Miradi hiyo yenye ukubwa wa hekta 543,366 itagharamiwa kwa jumla ya shilingi 1,340,000,000,000;

(ii) Kukamilika kwa miradi 780 inayoendelea kutaongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni 1.27;

(iii) Imeongeza idadi ya vyama vya umwagiliaji kutoka 19 hadi 912; na

(iv) Imefungua ofisi 121 za Wilaya, imeajiri watumishi 344 na kununua vitendea kazi ikiwemo mitambo 30 na magari makubwa 17 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, imenunua mitambo 18 ya uchimbaji wa visima kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la maendeleo ya ushirika, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imeanzisha Benki ya Ushirika ya Tanzania kwa mtaji wa shilingi bilioni 58, kufungua matawi manne katika mikoa na kuanzisha mawakala 58;

(ii) Imeimarisha matumizi ya mashine za kidijiti yenye thamani zaidi ya shilingi bilioni 13;

(iii) Imeongeza ajira katika vyama vya ushirika kutoka 100,000 mpaka 155,000;

(iv) Imeongeza viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika kutoka 267 hadi 331;

(v) Imehamasisha wanachama kuongeza akiba katika *SACCOS* kutoka shilingi bilioni 576 hadi shilingi bilioni 966 na kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi trilioni 1.1; na

(vi) Imeimarisha usimamizi wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la maboresho ya muundo wa sheria, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza yafuatayo: -

(i) Imekamilisha kuandaa mpango kabambe wa mageuzi ya kilimo *(Tanzania Agricultural Master Plan)* ambayo inatoa dira ya kilimo katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu;

(ii) Imeanzisha shoroba nne za kuendeleza kilimo kulingana na ikolojia za kilimo ambazo zitaratibiwa na Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo;

(iii) Imefanya marekebisho ya sheria tano, Sheria ya Tasnia ya Sukari, Sheria ya Tasnia ya Korosho, Sheria ya Vyama vya Ushirika, Sheria ya ya Pamba, Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji;

(iv) Imeanzisha Mamlaka ya Afya ya Mimea kupitia Sheria Na. 4 ya mwaka 2020; na

(v) Imeanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko kupitia Sheria ya Usalama wa Chakula Sura Na. 249.

Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu kuu la msingi la *COPRA* ni kusimamia mazao yasiyo na bodi yakiwemo mazao ya nafaka, mazao ya mikundekunde na mazao ya bustani na mazao ya mizizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kuzitangazia rasmi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa, *COPRA* ina mamlaka kamili ya kisheria ya kusimamia maendeleo ya mazao hayo, kuratibu masoko ili kuhakikisha tunatimiza malengo ya kilimo biashara. Hivyo, miongozo na kanuni inayotolewa na *COPRA* ya kuendeleza mazao hayo ni ya kitaifa na inapaswa kuzingatiwa, kuheshimiwa na kufuatwa kuleta tija kwa wakulima wa Taifa hili kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wa mchango wa sekta ya kilimo unavyozidi kuongezeka kwenye Pato la Taifa ndivyo watu wengi wanavyozidi kuajiriwa kwenye sekta ya kilimo. Hali hiyo, si tafsiri nzuri ya ukuaji wa uchumi nchini na hii inatupa ulazima kama Taifa kuendelea kuwekeza kwa matumizi ya teknolojia bora ya kilimo kwa miaka 20 mfululizo ili kuwezesha watu wengi waweze kutoka mashambani na kuhamia kwenye sekta zingine ikiwemo viwanda na huduma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni kutokana na ukweli kwamba uchumi wowote imara duniani huhamia kwenye kuongeza thamani mazao yake na kuuza nje mazao yaliyoongezwa thamani na hivyo kutengeneza ajira nyingi viwandani na kwenye sekta za kutoa huduma. Kwa kipindi cha miaka minne Serikali ya Awamu ya Sita imeanza kujenga msingi huo unaoendana na Dira ya Taifa na Mpango wa Maendeleo wa *Agriculture Master Plan.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo sababu Wizara ya Kilimo tuliamua kwa makusudi kwa kipindi chote hiki kufanya

tathmini ya mikakati ya kilimo ikiwemo mkakati wa *ASDP I* na *ASDP II* na yote kufutwa na kuamua mpango wa kutekeleza kilimo kuongozwa na *Agriculture Master Plan* na hivyo kupelekea kupunguza ajira mashambani na kuongeza ajira viwanda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 sekta ya kilimo imekua kwa 4.1% ikilinganishwa na lengo la 6.1%, imechangia 26% katika Pato la Taifa ikilinganishwa na lengo la 23%. Imetoa ajira 61% ikilinganishwa na lengo la 60%. Sekta ya kilimo kwa upande wa mazao ilikua kwa 4% ikilinganishwa na lengo la 5.7%. Imechangia 16% kwenye Pato la Taifa ikilinganishwa na lengo la 12.3% na imeendelea kuchangia 100% ya upatikanaji wa chakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu hizo zinaashiria kuimarika kwa sekta ya kilimo kutokana na uboreshaji wa kuongeza kwa matumizi ya teknolojia za kisasa na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha ongezeko la upatikanaji wa malighafi kwenye sekta zinazohusika na usindikaji na uzalishaji wa bidhaa za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la chakula; uzalishaji wa mazao ya chakula umefika tani milioni 22 sawa na ongezeko la 11%. Utoshelevu wa chakula umekuwa na ziada ya jumla ya tani milioni tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaendelea kutekeleza miradi 780. Kati ya hiyo, miradi 125 yenye ukubwa wa hekta 237,000 ni ujenzi na ukarabati ambapo miradi 12 kati ya hiyo imekamilika. Miradi 114 ni ya upembuzi yakinifu na ujenzi wa mabwawa yenye takribani mita za ujazo bilioni 1.18 ambapo kati ya hayo, mabwawa 19 yanaendelea na ujenzi na mabwawa mawili yamekamilika. Aidha, mabwawa 28 yametangazwa kwa ajili ya ujenzi na mabwawa 65 yako katika hatua ya usanifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile miradi katika mabonde 22 yenye ukubwa wa hekta 306,000 ni ya upembuzi yakinifu na ujenzi. Upembuzi yakinifu wa mabonde 14 kati ya hayo

umekamilika na mabonde nane usanifu unaendelea. Aidha, ujenzi wa skimu umeanza katika mabonde matatu kati ya mabonde 14 yaliyokamilika. Usanifu wa miradi 11 umetangazwa kwa ajili ya kupata wakandarasi. Miradi hiyo ikikamilika itaongeza eneo la hekta 543,000 na kufanya eneo linalomwagiliwa kufikia hekta milioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya ushirika; hadi kufikia Aprili, 2025 Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa vimefika 7,820 ikilinganishwa na 7,522. Kati ya hivyo, vyama 76 ni Vyama vya Upili; 4,500 ni Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko *(AMCOS),* 2,100 chama kimoja ni Shirikisho la Vyama vya Ushirika; 1,075 ni vyama vinavyojishughulisha na umwagiliaji, mbogamboga, ufugaji, uvuvi, viwanda na madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mapato na Matumizi; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 7,000,000,000 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili 2025 kiasi cha shilingi 6,000,000,000 sawa na 86% ya makadirio kimekusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2024/2025 Wizara ilikadiria kukusanya shilingi bilioni 3.6 kwa Fungu 05 kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi kufikia Aprili Wizara imekusanya shilingi bilioni 2.4 sawa na 66.7%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara iliomba kuidhinishiwa shilingi 1,248,000,000,000 kwa mafungu yote. Kati ya fedha hizo shilingi 1,000,033,000,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi 215,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia Aprili, 2025 shilingi 664,000,000,000 sawa na 53% ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo shilingi 568,000,000,000 ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi 96,000,000,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 utekelezaji wake ilikuwa na vipaumbele sita na mikakati 27 na

mwaka wa fedha 2025/2026 nitakayoomba itakuwa na vipaumbele sita na mikakati 31. Msingi wa bajeti za miaka hii miwili ni kuendeleza miradi ambayo tumeanza kuitekeleza na kuanzisha katika maeneo ya kimkakati. Aidha, msingi wetu ni kufikia lengo la Serikali ya Awamu ya Sita kukua kwa 10% ifikapo mwaka 2030.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 vipaumbele ambavyo tulianza kuvitekeleza ni uzalishaji na tija, kuongeza ajira za staha kwa vijana na wanawake, kuimarisha usalama wa chakula, kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya nje, kuimarisha maendeleo ya ushirika na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA, vyote vimetekelezwa kwa kutekeleza mikakati 27. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kwa 11.8%; uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kwa 20.8% na uzalishaji unaendelea. Pia uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia 83.5% ya lengo, vilevile uzalishaji wa mazao ya mafuta umefikia 99.2% ya lengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la utafiti na mbegu, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ilitengewa shilingi bilioni 40.7 kwa ajili ya utafiti na ugunduzi wa teknolojia na kukarabati na kujenga miundombinu ya utafiti. Hadi Aprili, 2025 shilingi bilioni 16 sawa na 39% ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi mwezi Aprili Wizara kupitia *TARI* imetekeleza yafuatayo:-

(i) Imewezesha upatikanaji wa Ithibati ya Kimataifa ya Maabara ya Udongo na Mimea iliyopo Wilayani ya Mufindi. Ithibati hiyo itaiwezesha maabara hiyo kutambulika Kimataifa;

(ii) Usanifu umekamilika na zabuni ya kumpata mkandarasi imetangazwa kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha sayansi za kibiolojia *(bioscience lab)* katika Mkoa wa Morogoro;

(iii) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Benki ya Mbegu *(Gene Bank)* umekamilika na zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi imetangazwa; na

(iv) Ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya migomba kwa njia ya chupa na maabara ya patholojia umefikia 42%.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Bunge lako Tukufu liliidhinisha shilingi bilioni 44 kwa ajili ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu na miche bora kwa mpango wa ruzuku. Hadi kufikia Aprili, 2025 shilingi bilioni 18 sawa na 41% ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora umefikia tani 79,000 sawa na 99.6% ya lengo la kuzalisha na kuthibitisha tani 80,000 za mbegu dhidi ya mahitaji ya tani 128,000. Kati ya hizo, tani 63,000 zimezalishwa ndani ya nchi na tani 16,000 zimeingizwa kutoka nje. Tani 700 za mbegu bora za alizeti na tani 500 za mbegu bora za ngano zenye thamani ya shilingi 17,000,000,000 zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo mbalimbali kupitia mpango wa ruzuku; tani 9,600 za mbegu bora za mahindi zenye thamani ya ruzuku ya shilingi bilioni 10.47 zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa ruzuku; miche milioni 24.4 ya mazao mbalimbali imezalishwa na kusambazwa sawa na 51% ya lengo la kuzalisha miche 47,000, 000.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora yenye ukubwa wa hekta 580 umefikia 74%. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,000 umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la utoaji wa ruzuku, Serikali imeratibu upatikanaji wa mbolea na visaidizi vya mbolea tani milioni 1.2 sawa na 80.9% ya lengo ambapo tani 542,000 za

mbolea zenye thamani ya shilingi bilioni 182 zimesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea. *TFC* imeingia makubaliano na Kiwanda cha *Biotech Products* kwa ajili ya kusambaza mbolea zisizo na kemikali zitakazozalishwa na kiwanda hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili, 2025 Wizara imenunua ndege moja kwa ajili ya huduma za anga za udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao. Wizara kupitia Bodi za Mazao ya Pamba, Korosho na Tumbaku imeratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu ambavyo ugharamiaji wake unatokana na zao lenyewe na tozo zinazotokana na Serikali ambazo zinalipwa na wanunuzi. Aidha, imenunua viuatilifu vya pamba, korosho na tumbaku vyenye thamani ya shilingi bilioni 266 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la umwagiliaji; Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitengewa shilingi bilioni 393 kwa ajili ya miradi 788 yenye ukubwa wa hekta 543,000. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Tume imekamilisha yafuatayo: -

(i) Imekamilisha ujenzi wa skimu mpya tatu za Magurukenda, Sukuma na Tlawi zenye ukubwa wa hekta 850 na ujenzi katika skimu 60 umefikia wastani wa 52%;

(ii) Imekamilisha ukarabati wa skimu saba zenye ukubwa wa hekta 9000 na ukarabati wa skimu 41 na umefikia wastani wa 60%;

(iii) Imekamilisha ujenzi wa Bwawa la Tlawi na ukarabati wa Bwawa la Ulyanyama lenye mita za ujazo milioni 3.17. Aidha, ujenzi wa mabwawa 19 yenye mita za ujazo 326,000,000 umefikia wastani wa 57%;

(iv) Imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde 14 kati ya 22 ya kimkakati na upembuzi unaendelea wa mabonde nane. Aidha, ujenzi wa skimu 19 zenye ukubwa wa hekta 17,000 katika

mabonde matatu ya kimkakati ya Mkomazi, Lukuledi na Mtambo umeanza na umefikia wastani wa 10%;

(v) Imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 98 kati ya skimu 527, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa Bonde la Mto Rufiji lenye ukubwa wa hekta 68,000 umekamilika na wakandarasi wamepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mabwawa mawili ya Mbakiamtuli na Ngorongo;

(vi) Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa Mradi wa Bugwema (Mara) amepatikana na kandarasi ya ujenzi wa mradi katika Bonde la Mto Ngono imetangazwa; na

(vii) Zabuni ya kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa ajili ya shughuli za kilimo imetangazwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026; Wizara ya Kilimo inawasilisha mpango wa bajeti ya mwaka 2025/2026 wakati Taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu na uzinduzi wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka 25. Mpango huu wa bajeti wa mwaka 2025/2026 umezingatia Dira ya Maendeleo ya 2025; Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano wa 2021/2022 – 2025/2026; Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Kilimo ya mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya mwaka 2010; na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya mwaka 2002. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango umezingatia Mpango Kabambe wa mwaka 2050 *(Tanzania Agricultural Master Plan);* Mkakati wa Ukuzaji wa Sekta ya Kilimo (Ajenda 10/30); Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni 2023/2024 - 2027/2028; Maoni na Ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Usalama wa Chakula na Kilimo; wadau wa maendeleo na masuala mtambuka ya kijinsia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele sita kuendelea na utekelezaji wa miradi iliyoanza mwaka 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025 na kuanza miradi mipya. Miradi hiyo inajumuisha

miradi ya umwagiliaji, vituo vya zana za kilimo, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, uhifadhi, uongezaji thamani, uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja, uzalishaji, ujenzi wa masoko, utafiti, huduma za ugani, na utoaji wa ruzuku za pembejeo za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa miradi katika mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara inalenga kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo kufikia asilimia tano; kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati kutoka tani milioni 1.45 hadi tani milioni 2.2; utoshelevu wa chakula kufika 130%; thamani ya mauzo ya nje kufika bilioni nne; na kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta milioni 1.2. Malengo hayo yatafikiwa kwa kutekeleza vipaumbele sita na mikakati 30. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la kuongeza tija na uzalishaji, Wizara kupitia *TARI* imelenga kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha *Bioscience* katika Kituo cha *TARI* Ilonga;

(ii) Kujenga Benki ya Taifa ya Mbegu kutoka Kituo cha *TARI* cha Silian;

(iii) Kuendelea na ujenzi wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa;

(iv) Kuendelea na utafiti wa mbegu 56 za kuzalisha mbegu tani 566 za awali; na

(v) Kukusanya, kusafisha na kutunza mbegu 363 za mbegu za asili; na

(vi) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 2,120.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la usambazaji wa mbegu Wizara imepanga kutekeleza yafuatayo: -

(i) Kuongeza uzalishaji wa mbegu bora wa ndani ya nchi kufika tani 90,000 na kufanya upatikanaji wa mbegu kufika 105,000;

(ii) Kuendelea kuongeza kutoa ruzuku ya mbegu bora kwenye mazao ya kimkakati (alizeti na mahindi) tani 52,000;

(iii) Kuzalisha na kusambaza miche milioni 64 ya mazao mbalimbali kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; na

(iv) Kujenga, kukarabati na kusimika miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 4,063.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye maeneo ya utoaji wa ruzuku, Wizara imepanga kufanya yafuatayo: -

(i) *TFRA* itaratibu upatikanaji wa tani 1,500,000 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku;

(ii) Itanunua tani 200,000 za mbolea na tani 50,000 za chokaa mazao kutoka viwanda vya ndani.

Naomba nirudie; Serikali itanunua tani 200,000 za mbolea na tani 50,000 za chokaa mazao kutoka viwanda vya ndani na hili lengo ni kulinda viwanda vyetu vya ndani na kupunguza utegemezi wa uagizaji mbolea kutoka nje;

(iii) *TFC* itanunua tani 133,000 za mbolea na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku;

(iv) *TFC* itanunua ghala za *SHIRECU* na Bodi ya Pamba Tanzania zilizopo katika Bandari ya Dar es Salaam kwa ajili ya kuanzisha kiwanda cha kuchanganya na kufungasha mbolea nchini;

(v) *TFC* itaanzisha kiwanda cha kuchimba, kufungasha na kusambaza chokaa mazao kwa ajili ya wakulima katika eneo la Visiga mkoani Pwani;

(vi) Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na *Korosho Cooperative Joint Enterprise* itanunua na kusambaza viuatilifu vya korosho lita milioni 3.8 na *Sulphur* tani 30,000;

(vii) Kununua na kusambaza viuatilifu vya pamba *Hecker Park* milioni 12 na vinyunyizi 100,000;

(viii) Bodi ya tumbaku kupitia *TCJE* itaratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu vya tumbaku lita 183,000, pakiti milioni 1.4 na chupa milioni 2.2;

(ix) *TPHPA* itanunua na kusambaza lita 1,000 za viuatilifu vya parachichi aina ya *Copper sulphate* kwa mpango wa ruzuku; na

(x) *TPHPA* itanunua ndege moja na ndege nyuki 20 kwa ajili ya kunyunyizia viuatilifu, kuanzisha vituo vya kilimo anga katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Mbeya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la usajili wa wakulima na urasimishaji, Wizara itaendelea na urasimishaji wa shughuli za kilimo kwa kusajili wakulima, kuwapatia kadi za kielektroniki na hatimiliki wakulima 10,000 kwa njia ya ruzuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uwekezaji kwenye huduma za ugani; Serikali itanunua magari 100, vishikwambi 3,000 na mavazi maalum ya utambulisho 5,000 na kuwapatia maafisa ugani na kuwajengea nyumba 50 kwa ajili maafisa ugani; kuendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye viwanja vya Nanenane vya Dodoma na Mwakangale, Mbeya na kuanza ujenzi wa kiwanja cha Ipuli, Tabora; kujenga miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu ili kuwa na hadhi ya kimataifa; kuchukua  na kukarabati Vituo vyote vya Kata vya rasilimali za kilimo ambavyo Wizara ilivikabidhi kwenye halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara itashirikiana na *VETA* na *CAMARTEC* katika uhaulishaji wa matumizi ya vituo vya rasilimali za kilimo vya kata katika kuhaulisha teknolojia za kilimo na kutoa mafunzo kwa wakulima na kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Wakala wa Huduma za Ugani wa Taifa na kuwa na afisa kilimo mratibu wa kata. Pia Wizara itaanzisha mfumo wa huduma za ugani wa kidijiti ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa sekta binafsi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kupitia Bunge lako Tukufu, ninaomba kuzitaarifu halmashauri zote nchini zilizokabidhiwa *Ward Resource Centres* na kushindwa kuzitumia kwa malengo yaliyowekwa ya kutoa mafunzo ya ugani kwa wakulima na kuzifanya kuwa Ofisi za Maafisa Watendaji, waanze kuandaa ofisi hizo kwa ajili ya matumizi ya kilimo na kuzikabidhi Wizara ya Kilimo na bajeti kwa ajili ya ukarabati imeshatengwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la upimaji wa afya ya udongo, Wizara itaendelea na upimaji wa afya ya udongo na kuchora ramani za kidijiti katika maeneo ya vijiji; kununua *mobile soil laboratory van* kwa ajili ya kupima afya ya udongo na kununua na kusambaza *soil scanner* 43.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la umwagiliaji Wizara imepanga kufanya fafuatayo: -

(i) Ujenzi wa mabwawa ya Mbakiamtuli na Ngorongo katika Bonde la Rufiji yenye mita za ujazo 57,000,000 zitakazomwagilia skimu yenye ukubwa wa hekta 64,000;

(ii) Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Mabonde ya Mto Ngono na Bugwema yenye ukubwa wa hekta 22,000;

(iii) Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa Mradi wa Ziwa Victoria na Tanganyika. Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano na ukikamilika utaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta

3,000,000 na mabwawa 52 ya umwagiliaji ambapo utanufaisha mikoa 12, Wilaya 69, Kata 192 na Vijiji 943;

(iv) Ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 101 zenye ukubwa wa hekta 209,000;

(v) Ujenzi wa mabwawa 46 yenye ukubwa wa mita za ujazo milioni 813;

(vi) Ujenzi wa skimu katika mabonde 14 ya kimkakati na kukamilisha upembuzi yakinifu wa mabonde nane;

(vii) Kuendelea na ujenzi wa mabwawa 46 na kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya mabwawa 65; na

(viii) Kuanzisha mfumo wa usimamizi wa mashamba ya Membe, Bugwema, Madibila na Lumpungu na kuhakikisha mashamba hayo yana hati na Serikali inakuwa na uwezo wa kurudisha gharama za uwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara pia itanunua Shamba la *Mbarali Estates* lenye ukubwa wa ekari 6,437 na kuwapa fursa wakulima wadogo kutumia mashamba hayo kwa utaratibu utakaowekwa na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kumshukuru kwa dhati mwekezaji wa *Highland Estate Limited* kukubali kuachia shamba hilo kwa makubaliano maalum na Serikali na wakulima ambapo kuanzia msimu ujao wa kilimo Serikali itatoa utaratibu wa kutumia mashamba hayo. Vilevile Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itajenga mabwawa mawili ya Dudumizi na Mambi katika Wilaya ya Mbarali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye eneo la zana za kilimo; Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi na umiliki wa zana za kilimo za kisasa kwa wakulima wadogo ambao wengi wao wana uwezo mdogo wa kumiliki zana hizo kutokana na gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kutangaza rasmi kuwa Wizara katika mwaka wa fedha 2025/2026 itatoa huduma za zana za kilimo ambapo wakulima watalipia gharama za huduma hiyo kwa bei ya ruzuku *(subsidized mechanization services)*. Katika kutekeleza hilo tutafanya yafuatayo: -

(i) Kuanzisha vituo 1,000 vya kutoa huduma ya zana za kilimo;

(ii) Kununua matrekta 10,000 na zana zote za msingi zinazohitajika kwa ajili ya kufanya kazi za shambani, *power tiller* 10,000 na mashine za kuvunia na kukaushia na vifaa vyote muhimu vya zana za kilimo;

(iii) Kuanzisha kituo kimoja cha kitaifa *(National Mechanisation Centre)* ambacho kitakuwa na zana zote za msingi, kwa ajili ya kusafisha na kusawazisha mashamba ya wakulima, uchimbaji wa visima na mabwawa na kutoa huduma za mafunzo; na

(iv) Kutoa mafunzo kuhusu uendeshaji na usimamizi wa zana za kilimo kwa waendesha mitambo na wasimamizi wa vituo 500 (mradi huu utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu).

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuendeleza ushoroba wa uzalishaji, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kuimarisha shoroba nne za kuendeleza kilimo kulingana na ikolojia za kilimo. Shoroba hizo zitaendelea kuratibiwa na Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo *(ATO)* kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kilimo, ikiwemo kusimamia matokeo ya afya ya udongo, kufanya tathmini ya kiuchumi na kujenga msingi wa utaalamu kwenye shoroba hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara itaendelea kutambua juhudi zilizofanywa na *SAGCOT Centre* katika kutekeleza miradi ya kilimo. Hivyo, *SAGCOT* itakuwa sehemu ya *AGCOT* chini ya usimamizi wa *ATO*. Nitoe rai kwa wadau wa maendeleo kuendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika utekelezaji wa

miradi ya kilimo kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika miongozo ya Serikali, hususan *Agricultural Master Plan* ya Mwaka 2050.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la uzalishaji wa mazao ya kibiashara, Wizara imelenga kuongeza uzalishaji wa mazao ya asilia kutoka tani milioni 1.4 hadi tani milioni 2.2, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, katika zao la pamba tumejiwekea lengo kufika tani laki nne, kahawa kufika tani 85,000, korosho kufika tani 700,000 na tumbaku kufika tani 200,000. Katika kufikia malengo hayo, kwenye zao la pamba Wizara itajenga kongani ya pamba katika Mkoa wa Simiyu kwenye eneo la ukubwa wa ekari 1,000, kuanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi, kwa ajili ya kufungia tumbaku katika Mkoa wa Simiyu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua hiyo itaipunguzia nchi gharama za kiasi cha dola za Kimarekani milioni 19.5 za kuagiza pamba za hospitali na nyuzi, kwa ajili ya zao la tumbaku. Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Nishati kuanzisha ruzuku ya bei ya umeme kwa kongani ya pamba ili kupunguza gharama za uzalishaji. Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na wadau wa pamba kutengeneza mfumo wa kikodi *(tax regime)* kwa ajili ya kulinda viwanda vya nguo zitokanazo na pamba iliyozalishwa ndani ya nchi ili kuweka vivutio vya kikodi na kuwapa motisha wazalishaji wa ndani inayolenga kupunguza gharama za uzalishaji, kuimarisha bei ya pamba na kuwalinda wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaratibu ufufuaji wa *ginnery* mbili zinazomilikiwa na *SHIRECU* zilizopo Mhunze na Uzogole, kuimarisha Kituo cha Mafunzo ya Wakulima cha Nyakabindi ili kukiwezesha kutoa huduma za zana za kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la chai; Serikali itabadili mfumo wa uuzaji wa chai wa wakulima wadogo kutoka kuuza chai ya majani mabichi na kuanza kuuza chai nyeusi. Bodi ya Chai Tanzania kwa kushirikiana na wawekezaji kutoka China,

itafufua Kiwanda cha Chai cha Kilolo kwa ajili ya kuanza uzalishaji wa chai maalum *(orthodox tea)* na kununua mashine mbili za kuchakata na kuchanganya chai ambazo zitasimikwa katika ghala la Kipawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Wizara kupitia Bodi ya Chai itaanzisha viwanda viwili vitakavyomilikiwa na wakulima wadogo na viwanda vinne vitajengwa na wawekezaji, kuendelea na majadiliano na wamiliki wa Kiwanda cha Mvyulu, kwa ajili ya kulipa fidia ya kiwanda hicho. Majadiliano hayo yakishindikana Bodi iatajenga kiwanda kipya na fedha zimetengwa kwa ajili ya mradi huo na kuwezesha upatikanaji wa Hati ya Kimataifa kwa wakulima wadogo wa chai, kwa ajili ya uendeshaji katika Mashamba ya Halmashauri ya Kilololo na Busokelo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaanza kufanya tathmini kwa wawekezaji waliobinafsishiwa viwanda vya kusindika chai na kushindwa kuviendesha ili kuona namna ya kuvirejesha kwa wakulima kwa kuzingatia sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye zao la kahawa; kuweka mfumo wa kusimamia uandaaji, usambazaji na utunzaji wa miche, kuwezesha uanzishwaji wa mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000 katika maeneo yanayozalisha kahawa, kwa maana ya Mkoa wa Kagera, kuchimba visima katika *block farm* iliyopo Kagera ili wakulima wapate maji ya uhakika, kwa ajili ya umwagiliaji, kujenga maabara ya *tissue culture* katika vituo vya *TaCRI* vya Maruku na Mbozi ili kuzalisha...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, omba fedha.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kueleza mpango wa bajeti wa mwaka 2025/2026, ninaomba sasa nitoe muhtasari wa maeneo yatakayotekelezwa na kuomba fedha kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti hii inatazama uongezaji wa thamani ya zao la pamba kwa kujenga kiwanda cha vifaa tiba kitakachotumia pamba na kujenga kongani ya *Industrial Park* katika Mkoa wa Simiyu. Ujenzi wa Kituo cha Sayansi cha

*Bioscience,* ujenzi wa Benki ya Mbegu, ujenzi wa Maabara ya *Tissue Culture,* ujenzi wa vituo 1,000 vya kutoa huduma za zana za kilimo, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika Bonde la Bugwema, Ngono na Rufiji, Mradi wa Ziwa Victoria na Tanganyika utakaokuwa na mabwawa 52 na kuhudumia vijiji 943. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uanzishwaji wa kiwanda cha kuongeza thamani cha vyama vya ushirika, ujenzi wa kiwanda cha tumbaku katika Mkoa wa Tabora, ujenzi wa Kongani ya Korosho, kununua ndege, uanzishwaji wa dirisha maalum kwa ajili ya *Equity Fund* na *guarantee scheme* katika Benki ya Ushirika. Majadiliano na Wizara ya Fedha kuanzisha mfumo wa kodi nafuu uatakaolinda mazao ya kilimo hasa mafuta ya kula, kununua mbolea kutoka viwanda vya ndani, kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati, kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula, kuanzisha sera ya fedha, kwa ajili ya upatikanaji wa mtaji na kuongeza thamani ya mazao ya kilimo, kuuza nje kufikia shilingi bilioni nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye hitimisho; ninaomba nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu na Watanzania wenzangu kuwa hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ndani ya sekta ya kilimo zinajenga msingi imara wa ukuaji wa sekta hii kwa muda mrefu ambapo utaleta uimara wa uchumi, kupunguza umaskini na kuongeza thamani. Hatua hizo zitafikiwa tu kama Taifa tutaamua kuwekeza kwa muda mrefu kwenye sekta ya kilimo ambayo imeajiri watu wengi kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi mingi tunayoitekeleza chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ni miradi itakayochukua muda mrefu, siyo chini ya miaka mitano hadi kumi. Tutaendelea kuchukua hatua hii ili kuweza kuijengea sekta hii uimara dhidi ya mitikisiko mbalimbali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania tumepata mtikisiko wa *Covid-19* na uzalishaji wetu haukuathirika. Tanzania tulipata mtikisiko wa vita inayoendelea katika nchi za Ulaya, lakini tumeendelea kuwa wahimilivu kwa sababu sekta ya kilimo imeendelea kuwa imara ambapo hatukupata upungufu wa

chakula. Serikali imetekeleza miradi mbalimbali ya kutoa ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba Bunge lako Tukufu litambue kuwa Taifa hili ni Taifa la wakulima wadogo wanaohitaji kulindwa na kupewa nyenzo mbalimbali na Serikali. Ruzuku zozote zinazotolewa na Serikali siyo gharama, bali ni sehemu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwani taasisi za kimataifa zimekuwa zikitazama mipango yetu ya ruzuku kama ni matumizi yasiyo muhimu, jambo ambalo siyo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ruzuku ya mbolea, ruzuku ya mbegu, ruzuku ya zana za kilimo, ruzuku ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ni muhimu sana, kwa ajili ya kuendelea kuongeza tija. Hatuwezi kupunguza umaskini kama hatutowekeza kwa wakulima wetu wadogo. Dhana ya *commercial farming* kwa Tanzania siyo ukubwa wa shamba, bali ni kiwango cha uzalishaji cha mkulima mdogo, anachokipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kwenye Uchaguzi Mkuu mwezi wa kumi, mwaka 2025 sisi wakulima tutakapoenda kupiga kura, tunapigia kura ruzuku ya mbolea, tunapigia kura ruzuku ya mbegu, tunapigia kura ruzuku ya matrekta, tunapigia kura viuatilifu, mikopo yenye riba nafuu, kupitia benki zetu, bei nzuri ya mazao, upatikanaji wa huduma za ugani na huduma za upimaji wa afya ya udongo. Hivyo, sisi wakulima tunafahamu kinachotupeleka kwenye Uchaguzi Mkuu, mwezi Oktoba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taifa hili msingi wake ni ujamaa na kujitegemea na linajengwa zaidi na wakulima wadogo, mpango wowote wa maendeleo utakaowaacha wakulima wadogo nje itakuwa ni sawa na kuisaliti Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa mujibu wa Ibara ya 9, kukisaliti Chama Cha Mapinduzi na kuwasaliti Watanzania wengi walioajiriwa katika sekta ya kilimo. Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itaendelea kuwalinda wakulima wadogo kwa wivu mkubwa na kuwawezesha kuwa *commercial farmers* na kuwa wakulima wanaozalisha kwa tija, ili tuweze kuondokana na umaskini. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, fanya maombi ya pesa. Maombi ya fedha za matumizi kwa mwaka 2025/2026.

**WAZIRI WA KILIMO:** Mheshimiwa Naibu Spika, makadirio katika mwaka wa fedha 2025/2026; Serikali inatarajia kukusanya shilingi 12,265,370,000 Kifungu 43 na Fungu 05. Kati ya fedha hizo shilingi 8,665,370,000 zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za zabuni kupitia Fungu 43 na kiasi cha shilingi 3,600,000,000 kutokana na ada za umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu iidhinishiwe jumla ya shilingi 1,242,975,075,000 Kifungu 43, Fungu 05 na Fungu 24 kwa mchanganuo ufuatao: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 43, kiasi cha shilingi 838,259,822,000 zinaombwa; kati ya fedha hizo shilingi 702,275,933,000 ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, ambapo kiasi cha shilingi 424,328,013,000 ni fedha za ndani na kiasi cha shilingi 277,947,920,000 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 135,983,889,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo shilingi bilioni 81,447,048,000 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 54,536,841,000 ni, kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 05 katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali inaomba jumla ya shilingi 382,138,408,000; kati ya fedha hizo shilingi 308,721,961,000 ni fedha za maendeleo na shilingi 73,416,447,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa kiasi cha shilingi 259,617,801,000 ni fedha za ndani na kiasi cha shilingi 49,104,160,000 ni fedha za nje. Aidha, shilingi 73,416,447,000 ni fedha za matumizi ya kawaida zinazoombwa. Kiasi cha shilingi 65,148,830,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na kiasi cha shilingi 8,267,617,000 ni kwa ajili ya mishahara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Fungu 24 - Wizara inaomba shilingi 22,576,845,000; kati ya fedha hizo shilingi 21,879,669,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 12,000,000,000 ni matumizi mengineyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia, hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA WAZIRI WA KILIMO, MHESHIMIWA HUSSEIN MOHAMED BASHE (MB), KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**1 UTANGULIZI**

1. ***Mheshimiwa Spika,*** kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, ninaomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa lipokee, kujadili na kupitisha taarifa ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka 2025/2026.

2. ***Mheshimiwa Spika,*** awali ya yote ninamshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutuwezesha kukutana hapa siku ya leo tukiwa na afya njema ili tuweze kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mwaka 2024/2025, tathmini ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 kwa kipindi cha miaka minne na Mpango na Bajeti kwa Mwaka 2025/2026 ya Wizara ya Kilimo ambayo inagusa maisha ya wakulima kwa ajili ya maendeleo ya Taifa letu.

3. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya pekee ninapenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kutekeleza kwa kishindo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020. Hakika, utekelezaji huo umezingatia misingi ya mageuzi thabiti, ustahimilivu, kujali utu, uadilifu, upendo, usawa na maridhiano uliotokana na utashi wa kisiasa wa Serikali ya Awamu ya Sita wa kufanya shughuli za maendeleo kwa ajili ya wananchi.

4. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa unyenyekevu mkubwa, nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuteuliwa na Chama cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais katika

Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 2025. Ninamuombea kwa Mwenyezi Mungu afya njema na nimatumaini yangu kuwa, kutokana na mafanikio makubwa ya utekelezaji wa Serikali ya Awamu ya Sita, wananchi wataendelea kumuamini na kukiamini Chama Cha Mapinduzi kwa kumpa kura za ushindi wa kishindo katika Uchaguzi Mkuu ujao.

5. ***Mheshimiwa Spika,*** ninampongeza Mheshimiwa Balozi Dkt. Emmanuel John Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi kwa kuaminiwa na kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea mwenza kwa nafasi ya Makamu wa Rais. Kutokana na umahiri na ushupavu wake, nina uhakika kuwa watakapopata ridhaa ya wananchi atamsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa majukumu yake ili kufikia malengo ya kuwaletea maendeleo wananchi. ***Ninamfahamu na wana CCM tunamfahamu,*** uadilifu wake, umahiri wake, heshima yake kwa viongozi wake na wananchi na kwetu sisi ambao ni **waumini wa misingi ya kijamaa inayoamini katika soko la haki.** Tunaamini Mheshimiwa Rais amepata msaidizi sahihi.

6. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee kabisa, ninamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniamini katika kusimamia utekelezaji wa Ilani ya CCM kupitia Wizara ya Kilimo. Ninamuahidi nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa uadilifu mkubwa ili kufikia malengo yaliyowekwa na Serikali na Chama cha Mapinduzi.

7. ***Mheshimiwa Spika***, ninampongeza na kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Philip Isdor Mpango, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuwa mstari wa mbele katika kusisitiza kilimo endelevu kinachozingatia utunzaji wa mazingira, kuimarisha usalama wa chakula na kupambana na umasikini. Ni dhahiri kuwa, utumishi wake Serikalini umeendelea kuwa chachu katika kuchochea maendeleo nchini na wengi wetu ambao tumefanya naye kazi akiwa Waziri wa Fedha na Mipango na sasa Makamu wa Rais, ametupa somo muhimu sana katika uongozi.

8. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuwa mgombea wa nafasi ya Urais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba, 2025.

9. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninapenda kutumia fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kumshukuru yeye binafsi kwa kipindi chote cha uongozi wake. Vilevile, ninampongeza kwa kuwezesha kuidhinishwa Bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo imetoa maelekezo ya msingi kwa Wizara ya Kilimo. Ninamhakikishia kuwa maelekezo yake yote yamezingatiwa katika Mpango na Bajeti ya Wizara ya Kilimo katika mwaka 2025/2026.

10. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru Ofisi yake kwa kuratibu mapitio ya Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II) ambayo yamechochea Wizara ya Kilimo kuandaa Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo wenye malengo ya muda mrefu hadi mwaka 2050 (Tanzania Agriculture Master Plan 2050). Hivyo, kuanzia mwaka ujao wa fedha, bajeti ya Wizara ya Kilimo inazingatia malengo hayo ambayo yametafsiriwa kwenye Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Sekta ya Kilimo 2050 ambayo yataendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 pamoja na Azimio la Kampala kuhusu Programu ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (CAADP 2026 – 2035).

11. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Dotto Mashaka Biteko (Mb.), Naibu Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Waziri wa Nishati kwa kuendelea kusimamia utekelezaji wa mipango ya kilimo kwa kuhimiza uwekezaji katika utafiti na kuboresha upatikanaji wa teknolojia za kisasa za kilimo ili kuongeza tija na uzalishaji na kuchangia katika kufikia malengo ya Serikali.

12. ***Mheshimiwa Spika,*** nikupongeze wewe binafsi, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa

weledi, ujuzi na ustadi mkubwa. Usimamizi wako umewezesha majadiliano ya Bunge kuwa na tija katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi.

13. ***Mheshimiwa Spika,*** ninakupongeza kwa kutumia nafasi yako kuwatendea haki Wabunge pamoja na kuweka msingi imara wa majadiliano ndani ya Bunge unaojenga uwajibikaji wa pamoja na kutoa haki kwa pande zote.

14. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, ninakupongeza kwa kuwatumikia wananchi wa Jimbo la Mbeya Mjini na kwa kuwa Jimbo hilo limegawanywa sehemu mbili na ninafahamu mapenzi yako ya kuwasaidia wakulima na wakulima wengi wanapatikana Jimbo la Uyole. Hivyo, sisi wakulima tunakuomba ukagombee Jimbo la Uyole.

15. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninampongeza Naibu Spika Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mb.) pamoja na Wenyeviti wa Bunge Mhe. Deodatus Philip Mwanyika Mbunge wa Jimbo la Njombe Mjini; Mhe. Dkt. Joseph Kizito Mhagama Mbunge wa Jimbo la Madaba; na Mhe. Najma Murtaza Giga Mbunge wa Viti Maalum kwa jinsi mnavyoliongoza Bunge letu tukufu katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ya nchi.

16. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaishukuru kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano, maoni, usimamizi, ufuatiliaji na miongozo mbalimbali kwa ajili ya kuendeleza sekta ya kilimo. Ninaiahidi Kamati kuwa maoni na ushauri wao umezingatiwa katika kipindi chote cha utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2024/2025 na maandalizi ya mpango wa mwaka 2025/2026. Kamati hiyo, imekuwa sehemu ya maendeleo, mabadiliko na majadiliano juu ya kujenga msingi imara wa kilimo katika Taifa letu.

17. ***Mheshimiwa Spika***, ninawapongeza wabunge wote kwa umahiri wenu mkubwa katika kuchangia mijadala inayoendelea katika Mkutano wa 19 wa Bunge hili la Bajeti. ***Tunafahamu kuwa***, huwezi kuongelea mabadiliko yoyote ya sekta ya kilimo katika nchi yetu bila kushukuru michango ya wabunge wote, kwa hakika mmechangia kwa kiwango kikubwa sana kuishauri Serikali na

kumtia moyo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika kutafuta rasilimali kwa ajili ya kuwekeza kwenye sekta ya kilimo. Pamoja na kuwa safari bado ni ndefu lakini kuna matumaini makubwa.

18. ***Mheshimiwa Spika,*** kipekee ninamshukuru Mhe. David Ernest Silinde (Mb.), Naibu Waziri wa Kilimo kwa ushirikiano anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Kilimo. Kwangu binafsi Mhe. Silinde ni Naibu Waziri, ni rafiki na ndugu. **Nimhakikishie kama Waziri, rafiki na ndugu yake kuwa Tunduma tutakuwa wote**.

19. ***Mheshimiwa Spika,*** ninamshukuru Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Bw. Gerald Geofrey Mweli, Naibu Katibu Mkuu, Dkt. Hussein Mohamed Omar (Maendeleo ya Mazao na Usalama wa Chakula) na Dkt. Stephen Justice Nindi (Ushirika na Umwagiliaji), pamoja na Wakurugenzi, Wakuu wa Taasisi, Bodi na Wakala zilizo chini ya Wizara kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu.

20. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri na ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Aidha, watumishi hao, kwangu binafsi wamekuwa wasaidizi na washauri wazuri, ninawashukuru sana.

21. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa namna ya kipekee ninawashukuru sana wakulima wote nchini kwa mchango wao mkubwa katika kuhakikisha nchi inakuwa na usalama wa chakula na kuongeza uuzaji wa mazao nje ya nchi. Kwa mantiki hiyo, msingi wa usalama wa Taifa letu ni wakulima wa nchi hii, na Serikali ya Chama cha Mapinduzi itaendelea kulinda maslahi yao.

22. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa dhati kabisa ninaishukuru Wizara ya Fedha inayoongozwa na Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba (Mb.), Waziri wa Fedha; Mhe. Hamad H. Chande (Mb.), Naibu Waziri wa Fedha; Dkt. Natu E. Mwamba, Katibu Mkuu Wizara ya Fedha; Bi. Jenifer C. Omolo, Naibu Katibu Mkuu Huduma za Hazina, Bi. Amina K. Shaaban, Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Fedha za Umma na Elijah G. Mwandumbya, Naibu Katibu Mkuu Usimamizi wa Uchumi kwa ushirikiano wanaoipatia Wizara ya Kilimo.

23. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ninawashukuru Bw. Meshack J. Anyingisye, Kamishna wa Bajeti; Bw. Japhet S. Justine, Kamishna wa Madeni na Bw. Rished M. Bade, Kamishna wa Fedha za Nje kwa kuendelea kuiwezesha Wizara ya Kilimo hata pale kwenye matatizo ya upatikanaji wa fedha wamekuwa msaada na wenye mchango mkubwa sana.

24. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa shukrani za pekee kwa wananchi wa Jimbo la Nzega Mjini kwa ushirikiano wanaoendelea kunipatia katika kipindi chote cha kuwawakilisha hapa Bungeni. Aidha, ninawapongeza kwa ushirikiano wao katika utekelezaji wa shughuli mbalimbali ambazo zinalenga kuleta maendeleo katika Jimbo letu. Pia, ninawashukuru sana Viongozi wa Chama cha Mapinduzi wa Wilaya ya Nzega, Mkuu wa Wilaya, Madiwani, Mkurugenzi na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Nzega kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020. **Asanteni sana!** Safari ya Jimbo letu tumetoka mbali ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa uaminifu mkubwa.

25. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kumpongeza Prof. Mohamed Yakub Janabi kwa kuchaguliwa kuwa Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani kwa Kanda ya Afrika. Tunamfahamu uchapakazi na utendaji wake wa kazi tangu akiwa Mkurugenzi wa Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na mshauri wa Rais katika masuala ya afya. Hakika tumepata mrithi sahihi wa nafasi ya Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani kwa Kanda ya Afrika.

26. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pole kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa msiba wa aliyekuwa Makamu wa kwanza wa Rais na Waziri Mkuu Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ndugu Cleopa David Msuya. Hayati Msuya alikuwa kiongozi anayetambua kuwa maendeleo ya kilimo ni msingi wa maendeleo ya Taifa na alihakikisha sekta ya kilimo inapewa kipaumbele ili kufikia malengo ya uchumi endelevu na kupunguza umaskini. Hakika kama Taifa tutamkumbuka kwa ujasiri wake na uongozi wake wenye busara na maono ya hali ya juu. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Mzee wetu Msuya mahala pema peponi.

27. ***Mheshimiwa Spika,*** ninatoa pole kwa Mheshimiwa Rais, kwako wewe Mhe. Spika, Wabunge na Watanzania wote na familia kwa kuondokewa na aliyekuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mkurugenzi Mteule wa Shirika la Afya Duniani kwa Kanda ya Afrika, Dkt. Faustine E. Ndugulile aliyekuwa *mwananzengo* na kijana wa Wilaya ya Nzega. Daima tutaendelea kumkumbuka kwa mchango wake mkubwa katika sekta ya afya, utumishi wa umma na uongozi wa kimataifa. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya Dkt. Ndugulile mahala pema peponi.

28. ***Mheshimiwa Spika,*** pia nitoe pole kwa ndugu, jamaa, marafiki na watumishi wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania kwa kuondokewa na aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania, Dkt. Daniel Nyoki Mgori. Mwenyezi Mungu ampe pumziko la milele.

29. ***Mheshimiwa Spika,*** Hotuba hii ninayoisoma leo mbele ya Bunge lako Tukufu, ni Hotuba yangu ya mwisho kama Waziri wa Wizara ya Kilimo katika kipindi cha kwanza cha Serikali ya Awamu ya Sita kabla ya kwenda kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2025. Hotuba hii imetoa taswira kwa ufupi ya hali ilivyokuwa katika mwaka 2020/2021, tathmini ya maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020 na Hotuba na maelekezo mahsusi aliyoyatoa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ndani ya Bunge lako Tukufu tarehe 22 Aprili, 2021 ambapo alitoa vipaumbele na mwelekeo wa Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya kilimo.

30. ***Mheshimiwa Spika,*** kipindi Serikali ya Awamu ya Sita inaingia madarakani, sekta ya kilimo ilikuwa inakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwemo:-

i. Uwekezaji mdogo wa fedha za umma katika sekta ya kilimo, upatikanaji mdogo wa mikopo na kutokuwa na mfuko wa kuendeleza sekta ya kilimo;

ii. Shughuli za kilimo kufanyika pasipo kutambuliwa katika mifumo rasmi;

iii. Kupanda na kushuka kwa bei za mazao na pembejeo za kilimo kutokana na athari za UVIKO-19; na uhaba wa Maafisa Ugani na vitendea kazi;

iv. Usafirishaji wa mazao nje ya nchi kupitia bandari ya Dar es Salaam kuchukua muda mrefu ambayo baadhi huharibika haraka kwa kutokupewa kipaumbele wakati wa kupakia kwenye meli;

v. Ushiriki mdogo wa vijana na wanawake katika kilimo uliosababishwa na ukosefu wa mitaji na umiliki wa ardhi;

vi. Uhaba wa miundombinu ya kuhifadhi mazao ya kilimo; ushirika dhaifu; na mifumo ya masoko isiyoshindani;

vii. Utegemezi wa baadhi ya mazao ya kilimo kutoka nje ya nchi ikiwemo ngano, sukari na mafuta ya kula uliotokana na uzalishaji mdogo wa ndani ya nchi na kutokuwepo kwa mpango wa kuondoa tatizo hilo;

viii. Uwezo mdogo wa ndani wa kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao uliosababishwa na ukosefu wa vifaa vya kisasa ikiwemo ndege maalum ya kukabiliana na milipuko hiyo na kutegemea ndege kutoka Mataifa ya jirani;

ix. Ukosefu wa maabara za kilimo zenye ithibati; upungufu wa viwanda vya mbolea; na upungufu wa wataalam wa umwagiliaji, vitendea kazi na ofisi;

x. Ukosefu wa mwelekeo imara wa kisera katika kuendeleza kilimo; na

xi. Mifumo dhaifu ya ugharamiaji wa shughuli za kilimo.

31. ***Mheshimiwa Spika,*** changamoto hizo ziliathiri watu wetu kuendelea kubaki kwenye umasikini mkubwa na kuifanya sekta ya kilimo kuwa isiyo rasmi na isiyovutia. Pia, changamoto hizo ziliathiri ukuaji wa sekta ya kilimo, mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi, kiwango cha usalama wa chakula, upatikanaji wa mitaji na

pembejeo za kilimo, tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo. Maeneo mengine yaliyoathirika ni pamoja na mtandao mdogo wa miundombinu ya umwagiliaji na uwekezaji mdogo katika uzalishaji wa mbegu bora nchini.

***Mheshimiwa Spika, kwa kifupi katika mwaka 2020/2021 sekta ya kilimo ilikuwa imebaki kama Sekta inayokwenda kwa kudra za Mwenyezi Mungu na jitihada binafsi za wakulima, kutokana na uwekezaji hafifu sana na usio wa uhakika wa Serikali***

32. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kipindi cha utekelezaji wa Awamu ya Sita, Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020 iliielekeza Wizara ya Kilimo kupitia Ibara ya 34 (a-j) Ukurasa Na. 32 - 33 na Ibara ya 37 (A-D) Ukurasa Na. 36 - 46 kutekeleza yafuatayo:-

i. Kusimamia dhana ya ushirika wa hiyari na kuwanufaisha wakulima na wanaushirika chini ya usimamizi wa Serikali na kulinda maslahi ya wakulima;

ii. Kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji;

iii. Kuongeza tija na uzalishaji kwa kuimarisha utafiti, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani na zana za kilimo;

iv. Kuimarisha miundombinu ya uhifadhi wa mazao, upatikanaji wa masoko, kuwajengea vijana uwezo wa kujiajiri na upatikanaji wa mitaji; na

v. Kuimarisha mfumo wa usimamizi wa kitaasisi na uratibu wa shughuli za kilimo.

33. ***Mheshimiwa Spika,*** ikumbukwe kuwa tarehe 22 Aprili, 2021 wakati Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akilihutubia Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliielekeza Wizara ya Kilimo kutatua changamoto ya tija ndogo katika uzalishaji wa mazao kwa kuimarisha utafiti, uzalishaji wa mbegu bora, miundombinu ya umwagiliaji, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani, mitaji, uhifadhi wa mazao, kuboresha afya ya udongo na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

34. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu hatua tulizofikia hadi Aprili, 2025 kama ifuatavyo:-

i. Bajeti ya Wizara ya Kilimo imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 1.248 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 324.49;

ii. Ukuaji wa sekta ya kilimo umeongezeka kutoka asilimia 2.6 mwaka 2021 hadi asilimia 4.2 mwaka 2023. Aidha, ukuaji wa sekta ya kilimo unatarajiwa kufikia asilimia 5 mwaka 2025 na asilimia 10 mwaka 2030;

iii. Thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi imeongezeka kutoka Dola za Marekani Bilioni 1.2 mwaka 2019/2020 hadi Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 195;

iv. Uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021/2022 hadi tani 22,803,316 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 33 na kufanya utoshelevu wa chakula nchini kufikia asilimia 128 dhidi ya lengo la asilimia 130; Mathalani:-

    a. Uzalishaji wa mahindi umeongezeka kutoka tani 6,417,356 msimu wa 2021/2022 hadi tani 12,261,162 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 91.06 na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili Afrika; na

    b. Uzalishaji wa mchele umeongezeka kutoka tani 1,768,369 msimu wa 2020/2021 hadi tani 3,046,285 msimu wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 72.27.

v. Uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 898,967 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,451,694.11 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 61.5. Mathalani:-

    a. Uzalishaji wa korosho umeongezeka kutoka tani 210,786 msimu wa 2020/2021 hadi tani 528,263.82 msimu wa 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 150.61;

b. Uzalishaji wa tumbaku umeongezeka kutoka tani 58,508 msimu wa 2020/ 2021 hadi tani 160,000 msimu wa 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 173.47 na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa pili Afrika;

c. Uzalishaji wa miwa umeongezeka kutoka tani **Milioni 3.88** ambazo zilizalisha sukari tani 367,718 mwaka 2020/2021 hadi tani **Milioni 4.71** za miwa zilizozalisha sukari tani 431,736.74 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 17.41 za sukari ambayo ni sawa na asilimia 61.68 ya lengo la kuzalisha sukari tani 700,000;

d. Uzalishaji wa mkonge umeongezeka kutoka tani 36,170 mwaka 2020/2021 hadi tani 61,215.55 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 69.24; na

e. Uzalishaji wa kahawa umeongezeka kutoka tani 59,318 hadi tani 81,366 msimu wa 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 37.17 na kuifanya kuwa ya nne (4) kwa uzalishaji barani Afrika.

vi. Uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kutoka tani 30,167.11 mwaka 2020/2021 hadi tani 63,526.54 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 110.58. Uzalishaji huo umechangia kuongezeka kwa upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 44,581.08 mwaka 2020/2021 hadi tani 79,700.62 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 78.78;

vii. Uzalishaji wa mazao ya bustani umeongezeka kutoka tani 7,304,723 mwaka 2020/2021 hadi tani 7,513,026.83 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 2.85. Mathalani, Uzalishaji wa parachichi umeongezeka kutoka tani 149,340 mwaka 2022/2023 hadi tani 195,162 mwaka 2024/2025. Aidha, mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 26,826 mwaka 2022/2023 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 117.5 hadi tani 35,627.02 mwaka 2023/2024 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 252.3;

viii. na kuifanya Tanzania kuwa mzalishaji wa tatu (3) barani Afrika;

ix. Uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta umeongezeka kutoka tani 1,713,178 mwaka 2020/2021 hadi tani 2,143,098.70 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 25.1. Aidha, uzalishaji wa alizeti umeongezeka kutoka tani 478,900 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,217,025.51 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 154.13;

x. Uzalishaji wa ndani wa mbolea umeongezeka kutoka tani 32,239 mwaka 2020/2021 hadi tani 158,628 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 392. Uzalishaji huo umechangiwa na kiwanda kipya cha kutengeneza mbolea cha ITRACOM katika Mkoa wa Dodoma chenye uwezo wa kuzalisha mbolea tani 1,000,000 kwa mwaka na upanuzi wa kiwanda cha Minjingu kutoka uwezo uliosimikwa wa tani 30,000 hadi tani 100,000 kwa mwaka. Uzalishaji huo umechangia upatikanaji wa mbolea kuongezeka kutoka tani 678,017 mwaka 2020/2021 hadi tani 1,213,729 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 79;

xi. Wizara katika kipindi cha miaka mitatu (3) imewezesha ruzuku ya mbolea tani 1,454,974.721 yenye thamani ya Shilingi 708,627,762,436 kwa mazao yote. Hatua hiyo, imewezesha kuongezeka kwa matumizi ya mbolea kutoka tani 363,599 mwaka 2021/2022 hadi tani 848,884 mwaka 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 133.47. Aidha, matumizi ya mbolea kwa hekta yameongezeka kutoka kilo 19 mwaka 2021/2022 hadi kilo 24 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 26. Ongezeko la matumizi ya mbolea ni sawa na asilimia 48 ya lengo la kilo 50 kwa hekta kulingana na azimio la CAADP;

xii. Wizara ya Kilimo kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kwa mara ya kwanza imewezesha kuanzishwa kwa Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo (Agriculture Development Fund - ADF) kupitia Sheria za Fedha za Umma, Sura ya 348. Mfuko huo umeanza kazi Januari 2025 kwa ajili ya kuendeleza kilimo kwa kuimarisha bei za mazao zinaposhuka, kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo, kuimarisha miundombinu ya uhifadhi, utafiti na uongezaji thamani;

xiii. Wizara imewekeza na kufufua kilimo anga kwa kununua ndege maalum kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao na ndege nyuki 41 kwa ajili ya uchunguzi na udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao; na

xiv. Wizara imeongeza uwezo wa miundombinu ya Hifadhi ya Taifa ya Chakula (NFRA) kutoka tani 251,000 mwaka 2020/2021 hadi tani 776,000 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 209.16.



*Miundombinu ya Uhifadhi ya Ghala na Vihenge katika Mkoa wa Manyara.*

35. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, katika kipindi cha miaka minne (4) tumepata mafanikio kwa kuboresha miundombinu ya utafiti, uzalishaji wa mbegu na huduma za ugani; uongezaji thamani na matumizi ya zana za kilimo; uzalishaji wa ajira zilizotokana na utekelezaji wa miradi ya kilimo; usambazaji wa pembejeo za kilimo kwenye mazao ya kimkakati; kuongezeka kwa utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji; na kuimarika kwa ushirika.

36. ***Mheshimiwa Spika,*** kwenye eneo la Miundombinu ya Utafiti, Uzalishaji wa Mbegu na Huduma za Ugani:-

i. Tumekamilisha ujenzi wa Kituo cha Udhibiti wa Visumbufu vya Mimea Kibailojia (National Biological Control Unit) - Kibaha, Maabara ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania - Dar es Salaam, Maabara ya kuzalisha miche kwa

njia ya chupa (Tissue Culture) na Maabara ya udongo - TARI Mlingano na ununuzi wa mashine mbili (2) za kukausha mbegu na mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu kwa Wakala wa Mbegu za Kilimo. Vilevile, kupata ithibati ya kimataifa kwa Maabara ya udongo na mimea ya TRIT; na

ii. Tumenunua na kusambaza vitendea kazi ikiwemo magari 44, pikipiki 6,444, vipima afya ya udongo 143, vishikwambi 5,426, visanduku vya ugani 1,662 na kujenga nyumba za Maafisa Ugani 50.



*Magari kwa ajili ya Maafisa Ugani ngazi ya Halmashauri na Mikoa*

37. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Uongezaji Thamani na Matumizi ya Zana za Kilimo:-

i. Tumenunua matrekta makubwa 500 na matrekta madogo (power tiller) 800 kwa ajili ya kutoa huduma za kilimo;

ii. Tumekamilisha ujenzi wa kiwanda cha kusindika zabibu chenye uwezo wa kusindika zabibu tani 300 kwa mwaka katika Mkoa wa Dodoma; na iii. Tumekamilisha ujenzi wa Kituo Mahiri cha Usimamizi wa Mazao baada ya Kuvuna kilichopo Mtanana katika Mkoa wa Dodoma.

38. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la ajira zilizotokana na utekelezaji wa miradi ya kilimo, Wizara imezalisha ajira za kudumu na za muda mfupi 1,084,481 kupitia programu na miradi mbalimbali ya maendeleo ya kilimo ikiwemo miradi ya uzalishaji na utafiti; ujenzi, ukarabati na usanifu wa miradi ya umwagiliaji, programu ya Jenga Kesho Iliyo Bora na Vyama vya Ushirika.

39. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la usambazaji wa pembejeo za kilimo kwenye mazao ya Kimkakati, Serikali ya awamu ya sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imefanikisha yafuatayo:-

i. Imewezesha upatikanaji na usambazaji wa viuatilifu vya korosho (salfa ya unga tani 109,083.695, viuatilifu vya maji lita 8,823,687.5 na mabomba ya kunyunyuzia viuatilifu 6,337) vyenye thamani ya Shilingi 556,719,057,804.95 kwa mpango wa ruzuku;

ii. Imewezesha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la tumbaku zikiwemo mbolea, viuatilifu na vifungashio vyenye thamani ya Shilingi 607,292,419,460.43; na iii. Imewezesha upatikanaji na usambazaji wa pembejeo za zao la pamba zikiwemo mbolea, mbegu na viuatilifu vyenye thamani ya Shilingi 325,361,502,000.

40. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Miundombinu ya Umwagiliaji, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imefanikisha yafuatayo:-

i. Imeongeza miradi ya umwagiliaji inayotekelezwa kutoka miradi 13 mwaka 2020/2021 hadi miradi 780 mwaka 2024/2025. Miradi hiyo yenye ukubwa wa hekta 543,366.46 utekelezaji wake unakadiriwa kugharimu Shilingi 1,345,813,904,141.73.
Kukamilika kwa miradi 780 inayoendelea kutaongeza eneo la umwagiliaji hadi kufikia hekta 1,270,647.06;

ii. Imeongeza idadi ya Vyama vya Umwagiliaji vilivyosajiliwa kutoka 19 mwaka 2020/2021 hadi 912 mwaka 2024/2025.

Kwa mujibu wa Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013. Vyama hivyo, vina jukumu la kuhakikisha uendelevu wa miundombinu ya umwagiliaji; na

iii. Imefungua ofisi 121 za wilaya, imeajiri watumishi 344 na kununua vitendea kazi vikiwemo mitambo 30 na magari makubwa 17 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, imenunua mitambo 18 ya uchimbaji wa visima na magari madogo 58 kwa ajili ya usimamizi na ufuatiliaji wa miradi ya umwagiliaji.

41. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Maendeleo ya Ushirika, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza yafuatayo:-

i. Imeanzisha Benki ya Ushirika Tanzania ambayo imeanza na mtaji wa Shilingi Bilioni 58, kufungua matawi manne (4) katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Mtwara na Kilimanjaro na kusajili Vyama Vikuu vya Ushirika 58 kuwa mawakala;

ii. Imeimarisha matumizi ya mizani ya kidijiti kwenye ununuzi wa mazao ya wakulima ambapo jumla ya mizani 3,760 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.3 imenunuliwa na kusambazwa kwa Vyama vya Ushirika 992;

iii. Imeongeza ajira katika Vyama vya Ushirika kutoka 100,100 mwaka 2020/2021 hadi 155,106 mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 55.1;

iv. Imeongeza viwanda vinavyomilikiwa na Vyama vya Ushirika kutoka 267 mwaka 2021/2022 hadi 331 mwaka 2024/2025. Viwanda hivyo vinahusisha viwanda vya uchambuaji wa pamba; ukoboaji wa mpunga, kahawa na mahindi; usindikaji wa maziwa; ukamuaji wa mafuta ya pamba, alizeti, karanga na ufuta; na ubanguaji wa korosho;

v. Imehamasisha wanachama kuongeza akiba katika SACCOS kutoka Shilingi Bilioni 576 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Bilioni 966.9 mwaka 2023/2024. Aidha, mikopo iliyotolewa kwa wanachama imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 798 mwaka 2021/2022 hadi Shilingi Trilioni 1.1 mwaka 2023/2024; na

vi. Imeimarisha usimamizi wa Vyama vya Ushirika na kuwezesha vyama vilivyopata hati safi kuongezeka kutoka vyama 339 mwaka 2021/2022 hadi vyama 631 mwaka 2023/2024. Aidha, vyama vilivyopata hati isiyoridhisha vimepungua kutoka vyama 1,198 mwaka 2021/2022 hadi vyama 263 mwaka 2023/2024 na hati chafu kutoka vyama 2,075 mwaka 2021/2022 hadi 995 mwaka 2023/2024.

42. ***Mheshimiwa Spika,*** katika eneo la Maboresho ya Muundo na Sheria, Serikali ya Awamu ya Sita imetekeleza yafuatayo:-

i. Imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa mwaka 2050 ambao unatoa dira ya kilimo kwa kipindi cha muda mfupi, kati na mrefu;

ii. Imeanzisha shoroba nne (4) za Kuendeleza Kilimo Tanzania kulingana na ikolojia za kilimo ambazo zitaratibiwa na Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo (ATO);

iii. Imefanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Sukari Na.6 ya mwaka 2001 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 na kuipa NFRA mamlaka ya kununua na kuhifadhi sukari ya dharura na kuziba pengo la uzalishaji;

iv. Imefanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2024 na kuwezesha asilimia 100 ya mapato yanayotokana na mauzo ya korosho ghafi (export levy) kwenda Bodi ya Korosho Tanzania;

v. Imefanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.11 la tarehe 14 Machi, 2025. Marekebisho hayo yamempa Mrajis mamlaka ya kuchukua hatua za haraka anapoona ubadhirifu mara baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi;

vi. Imefanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba Na. 2 ya mwaka 2001 ili kuimarisha usimamizi na usahihi katika takwimu za ununuzi wa pamba, ubora wa pamba inayouzwa

ndani na nje ya nchi na kuimarisha upatikanaji wa mbegu za pamba;

vii. Imeanzisha Mamlaka ya Afya ya Mimea na Viuatilifu kupitia Sheria ya Afya ya Mimea na Viuatilifu Na. 4 ya mwaka 2020 kwa ajili ya kuwezesha udhibiti wa visumbufu na ukaguzi wa mazao;

viii. Imefanya marekebisho ya Sheria ya Taifa ya Umwagiliaji Na. 4 ya mwaka 2013 ambapo ofisi za umwagiliaji za Wilaya zimetambuliwa rasmi kisheria. Aidha, Vyama vya Umwagiliaji vimepewa hadhi kisheria kuwa *corporate bodies* ambapo pamoja na mambo mengine vimepewa uwezo wa kumiliki mali, kununua na kuuza kisheria; na

ix. Imeanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko kupitia Sheria ya Usalama wa Chakula Sura Na. 249 na marekebisho yaliyofanyika kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko Sura Na. 274 kwa ajili ya kudhibiti mnyororo wa thamani wa nafaka na mazao mchanganyiko.

43. ***Mheshimiwa Spika,*** jukumu kuu la msingi la COPRA ni kusimamia mazao yote yasiyo na Bodi yakiwemo mazao ya nafaka, mazao ya mikunde, mbegu za mafuta, mazao ya bustani na mazao ya mizizi.

44. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kuzitangazia rasmi Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuwa, COPRA ina mamlaka kamili kisheria ya kusimamia maendeleo ya mazao hayo na kuratibu masoko ili kuhakikisha tunatimiza malengo ya kilimo biashara. Hivyo, miongozo na kanuni inayotolewa na COPRA ya kuendeleza mazao hayo ni ya Kitaifa na inapaswa kuzingatiwa ili kuleta tija kwa wakulima na Taifa kwa ujumla.

## 2 HALI YA KILIMO KATIKA MWAKA 2024
### 2.1 Mchango wa Kilimo katika Uchumi

45. ***Mheshimiwa Spika,*** mchango wa sekta ya kilimo unavyozidi kuongezeka kwenye Pato la Taifa ndivyo watu wengi wanavyozidi kuajiriwa kwenye sekta ya kilimo. Hali hiyo, si tafsiri nzuri ya ukuaji wa uchumi nchini na hii inatupa ulazima kama Taifa kuendelea kuwekeza katika matumizi ya teknolojia bora za kilimo kwa miaka 20 mfululizo ili kuwezesha watu wengi waweze kutoka mashambani na kuhamia kwenye Sekta zingine ikiwemo viwanda na huduma.

46. ***Mheshimiwa Spika,*** hii ni kutokana na ukweli kwamba uchumi wowote imara duniani huhamia kwenye kuongeza thamani mazao yake na kuuza nje mazao yaliyoongezwa thamani na hivyo kutengeneza ajira nyingi viwandani na kwenye Sekta za kutoa huduma. Kwa kipindi cha miaka minne Serikali ya Awamu ya Sita imeanza kujenga msingi huo unaoendana na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050 na Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo 2050 (Tanzania Agriculture Master Plan 2050).

47. ***Mheshimiwa Spika,*** hiyo ndiyo sababu Wizara ya Kilimo tuliamua makusudi kwa kipindi chote hiki kufanya tathmini ya Mikakati ya Kilimo ikiwemo mikakati katika ASDPI na ASDPII na yote kufutwa na kuamua mpango wa kutekeleza kilimo kuongozwa na Agriculture Masterplan na hivyo kupelekea kupunguza ajira mashambani na kuongeza ajira viwanda.

48. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024 sekta ya kilimo imekua kwa asilimia 4.1 ikilinganishwa na lengo la asilimia 6.1 mwaka 2025, imechangia asilimia 26.3 katika Pato la Taifa ikilinganishwa na lengo la asilimia 23.4 na imetoa ajira kwa wananchi kwa wastani wa asilimia 61.4 mwaka 2024 ikilinganishwa na lengo la asilimia 60. Aidha, sekta ya kilimo kwa upande wa mazao ilikua kwa asilimia 4.0 mwaka 2024 ikilinganishwa na lengo la asilimia 5.7; imechangia asilimia 16.1 kwenye Pato la Taifa mwaka 2024 ikilinganishwa na lengo la asilimia 12.3; na imeendelea kuchangia asilimia 100 ya upatikanaji wa chakula.

49. ***Mheshimiwa Spika,*** takwimu hizo zinaashiria kuimarika kwa sekta ya kilimo kutokana na uboreshaji na kuongezeka kwa matumizi ya teknolojia mpya na za kisasa katika shughuli za uzalishaji wa mazao ya kilimo. Wizara itaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kuhakikisha ongezeko la upatinaji wa malighafi kwenye sekta zinazohusika na usindikaji na uzalishaji wa bidhaa za kilimo.

## 2.2 Hali ya Chakula

50. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula katika msimu wa kilimo wa 2023/2024 ulifikia tani 22,803,316 ikilinganishwa na tani 20,402,014 katika msimu wa kilimo wa 2022/2023 sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Katika kipindi hicho, uzalishaji wa mazao ya nafaka ulikuwa tani 14,587,177 na mazao yasiyo ya nafaka tani 8,216,139 ikilinganishwa na tani 11,448,757 za mazao ya nafaka na tani 8,953,258 za mazao yasiyo ya nafaka zilizozalishwa katika msimu wa kilimo wa 2022/2023.

51. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula kwa msimu wa kilimo wa 2023/2024 ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 17,753,989 kwa mwaka 2024/2025 na kuwepo kwa ziada ya tani 5,049,327. Kutokana na hali hiyo, Taifa limejitosheleza kwa chakula kwa asilimia 128.

## 2.3 Hali ya Umwagiliaji

52. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imeendelea kutekeleza miradi 780. Kati ya hiyo, miradi 125 yenye ukubwa wa hekta 237,005.46 ni ujenzi na ukarabati ambapo miradi 12 kati ya hiyo imekamilika. Miradi 114 ni ya upembuzi yakinifu na ujenzi wa mabwawa yenye takriban mita za ujazo **Bilioni 1.18** ambapo kati ya hayo, mabwawa 19 yanaendelea na ujenzi na mabwawa mawili (2) umekamilika. Aidha, mabwawa 28 yametangazwa kwa ajili ya ujenzi na mabwawa 65 usanifu unaendelea.

53. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, miradi katika mabonde ya kimkakati 22 yenye ukubwa wa jumla ya hekta 306,362 ni ya upembuzi yakinifu na ujenzi. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina

katika mabonde 14 kati ya hayo umekamilika na katika mabonde nane (8) usanifu unaendelea. Aidha, ujenzi wa skimu umeanza katika mabonde matatu (3) kati ya mabonde 14 yaliyokamilisha usanifu na zabuni ya miradi katika mabonde 11 imetangazwa kwa ajili ya kupata wakandarasi wa ujenzi.

54. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hiyo ikikamilika itaongeza eneo la hekta 543,366.46 za umwagiliaji na kufanya eneo linalomwagiliwa kufikia hekta 1,270,647.06 sawa na asilimia 105.89 ya lengo la kufikisha hekta 1,200,000.

### 2.4 Hali ya Ushirika

55. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na Wizara za kisekta, Mamlaka za Serikali za Mitaa na wadau wa ushirika imeendelea na uhamasishaji na uanzishaji wa Vyama vya Ushirika katika sekta mbalimbali za kiuchumi ikiwemo kilimo, uvuvi, mifugo, fedha, viwanda na madini. Hadi Aprili 2025, Vyama vya Ushirika vilivyosajiliwa vimefikia 7,820 ikilinganishwa na vyama 7,522 mwaka 2024. Kati ya hivyo, 76 ni Vyama vya Upili, 4,533 ni Vyama vya Ushirika wa Kilimo na Masoko (AMCOS), 2,135 ni Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), kimoja (1) ni Shirikisho la Vyama vya Ushirika, 1,075 ni Vyama vinavyojishughulisha na umwagiliaji, mbogamboga, ufugaji, uvuvi, viwanda na madini.

## 3 MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2024/2025

### 3.1 Makusanyo ya Maduhuli

**Fungu 43**

56. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **7,000,254,000** kupitia Fungu 43, kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za mazao na uuzaji wa nyaraka za zabuni. Hadi Aprili 2025, kiasi cha Shilingi **6,022,070,746.93** sawa na asilimia 86.03 kimekusanywa. Inatarajiwa kuwa malengo yaliyowekwa yatafikiwa ifikapo mwisho wa mwaka 2024/2025. **Fungu 05**

57. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara ilikadiria kukusanya mapato ya Shilingi **3,600,000,000** kupitia Fungu 05, kutokana na vyanzo mbalimbali. Hadi Aprili 2025, Wizara

imekusanya Shilingi **2,401,552,515.48** sawa na asilimia 66.71 ya lengo.

### 3.2 Fedha Zilizoidhinishwa kwa Mafungu Yote (43, 24 na 05)

58. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Kilimo ilitengewa jumla ya Shilingi **1,248,961,680,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24. Kati ya fedha hizo, Shilingi **1,033,046,318,000** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **215,915,362,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

**Fedha zilizotolewa.**

59. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Shilingi **664,362,952,241.59** sawa na asilimia 53.19 ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **568,062,970,958.11** ni kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na Shilingi **96,299,981,283.48** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

## 4 MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025

60. ***Mheshimiwa Spika***, bajeti ya mwaka 2024/2025 ambayo nitaelezea utekelezaji wake ilikuwa na vipaumbele sita (6) na mikakati 27 na bajeti ya mwaka 2025/2026 nitakayoiomba itakuwa na vipaumbele sita (6) na mikakati 30. Msingi wa bajeti za miaka hiyo miwili (2) ni kuendeleza miradi ambayo tumeanza kuitekeleza na kuanzisha katika maeneo ya kimkakati. Aidha, msingi wetu ni kufikia lengo la Serikali ya Awamu ya Sita la sekta ya kilimo kukua kwa asilimia 10 ifikapo mwaka 2030.

61. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2024/2025, Wizara ya Kilimo imetekeleza vipaumbele sita (6) ambavyo ni kuongeza uzalishaji na tija; kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake katika kilimo; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi; kuimarisha maendeleo ya ushirika; na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa sekta ya kilimo. Vipaumbele hivyo, vimetekelezwa kupitia mikakati 27. Mafanikio ya utekelezaji wa bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

4.1 Kuongeza Uzalishaji na Tija

62. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya chakula umeongezeka kutoka tani 20,402,014 msimu wa kilimo wa 2022/2023 hadi tani 22,803,316 msimu wa kilimo wa 2023/2024 sawa na ongezeko la asilimia 11.8. Uzalishaji wa tani 22,803,316 za mazao ya chakula ulitosheleza mahitaji ya chakula ya tani 17,753,989 na hivyo kuwezesha utoshelevu wa chakula kwa mwaka 2024/2025 kufikia asilimia 128.

63. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao asilia ya biashara umeongezeka kutoka tani 1,201,832.65 mwaka 2023/2024 hadi tani 1,451,694.11 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 71.51 ya lengo la kuzalisha tani 2,030,000 na uzalishaji unaendelea. Ongezeko hilo limechangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao mbalimbali yakiwemo korosho ambapo uzalishaji ulifikia tani 528,263.82 ikilinganishwa na tani 254,500 zilizozalishwa msimu wa 2023/2024 sawa na asilimia 88.78 ya lengo la kuzalisha tani 595,000; na uzalishaji wa kahawa ulifikia tani 81,366 ikilinganishwa na tani 66,071 msimu wa 2023/2024 sawa na asilimia 95.72 ya lengo la kuzalisha tani 85,000.

64. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ongezeko hilo limechangiwa na uzalishaji wa chai ambao umefikia tani 22,772 ikilinganishwa na tani 13,525 mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 75.9 ya lengo la kuzalisha tani 30,000; uzalishaji wa mkonge ambao umefikia tani 61,215.55 ikilinganishwa na tani 56,732.7 mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 76.5 ya lengo la kuzalisha tani 80,000; uzalishaji wa kakao ambao umefikia tani 13,652 ikilinganishwa na tani 11,499.4 mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 91 ya lengo la kuzalisha tani 15,000; na uzalishaji wa sukari ambao umefikia tani 431,736.74 ikilinganishwa na tani 395,292.55 mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 83 ya lengo la kuzalisha tani 520,000 na uzalishaji wa mazao unaendelea. Mwenendo wa uzalishaji wa mazao hayo umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 1.**

**Jedwali Na. 1:** Mwenendo wa Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) Mwaka 2023/2024 hadi 2024/2025

| Na | MAZAO | Uzalishaji mwaka 2023/2024 | Uzalishaji mwaka 2024/2025 | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | Lengo | Uzalishaji | Asilimia |
| 1 | Korosho | 254,500 | 595,000 | 528,263.82* | 88.78 |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2 | Pamba | 282,510 | 500,000 | 149,361 | 29.87 |
| 3 | Pareto | 4,238 | 5,000 | 3,327* | 57.30 |
| 4 | Kahawa | 66,071 | 85,000 | 81,366* | 95.72 |
| 5 | Tumbaku | 117,464 | 200,000 | 160,000* | 80.00 |
| 6 | Chai | 13,525 | 30,000 | 22,772* | 75.91 |
| 7 | Mkonge | 56,732.7 | 80,000 | 61,215.55* | 76.52 |
| 8 | Sukari | 395,292.55 | 520,000 | 431,736.74* | 83.00 |
| 9 | Kakao | 11,499.4 | 15,000 | 13,652* | 91.01 |
| | **JUMLA** | **1,201,832.65** | **2,030,000** | **1,451,694.11** | **71.11** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo 2024*
**Uzalishaji/Ununuzi unaendelea*

65. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya bustani umefikia tani 7,518,560.84 mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 83.5 ya lengo la kuzalisha tani 9,000,000. Lengo la uzalishaji halikufikiwa kutokana na athari za mtawanyiko wa mvua usioridhisha katika baadhi ya maeneo ya uzalishaji. Aidha, uzalishaji wa mazao ya bustani umeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2**.

**Jedwali Na. 2:** Uzalishaji wa Mazao ya Bustani (Tani) Mwaka 2023/2024

| **Na.** | **MAZAO** | **2023/2024** |
|---|---|---|
| 1. | Matunda | 6,212,065.19 |
| 2. | Maua | 5,534 |
| 3. | Mboga | 1,232,525.57 |
| 4. | Viungo | 68,436.08 |
| | **JUMLA** | **7,518,560.84** |

***Chanzo:*** *Wizara ya Kilimo 2024*

66. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mazao ya mafuta umefikia tani 2,181,603.65 sawa na asilimia 99.2 ya lengo la tani 2,200,000. Uzalishaji wa mazao ya mafuta umeoneshwa kwenye **Jedwali. Na. 3.**

**Jedwali Na. 3:** Uzalishaji wa Mazao ya Mafuta (Tani) Mwaka 2023/2024

| **Na** | **MAZAO** | **2023/2024** |
|---|---|---|
| 1. | Alizeti | 1,217,025.51 |
| 2. | Ufuta | 240,010 |

| | | |
|---|---|---|
| 3. | Nazi | 52,130.79 |
| 4. | Chikichi | 51,834.42 |
| 5. | Karanga | 620,602.93 |
| | **JUMLA** | **2,181,603.65** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2024*

67. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kufikia mafanikio hayo Wizara imetekeleza mikakati ifuatayo:-

### 4.1.1 Kuimarisha Utafiti wa Mbegu

68. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/ 2025 jumla ya Shilingi Bilioni 40.73 zilitengwa kwa ajili ya utafiti na ugunduzi wa teknolojia; kuzalisha mbegu za awali; na kukarabati na kujenga miundombinu ya utafiti. Aidha, hadi Aprili 2025, Shilingi Bilioni 16.03 sawa na asilimia 39.4 ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

**a) Utafiti na Ugunduzi wa Teknolojia**

69. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI katika mwaka 2024/2025 ilipanga kufanya utafiti wa visumbufu vya mazao ya migomba, soya, chai, muhogo na korosho; kutafiti aina bora za mbegu za soya zenye viwango vya protini na mafuta na kuendelea na utafiti wa mbegu za ngano; kufanya utafiti wa ladha ya mvinyo wa zabibu; kuhaulisha teknolojia ya matumizi ya Rafiki Planter; kukamilisha upatikanaji wa Ithibati ya Kimataifa ya Maabara ya Afya ya Udongo na Mimea iliyopo katika Wilaya ya Mufindi; kuimarisha vituo nane (8) mahiri vya usambazaji wa teknolojia (AgriTech Hubs) katika viwanja vya maonesho ya kilimo Nanenane; na kuanzisha shamba la vinasaba na mashamba mawili (2) ya mbegu kwa ajili ya utafiti wa chai.

70. ***Mheshimiwa Spika***, TARI ilipanga kuendelea na utafiti wa viwango, aina na mbinu za matumizi ya chokaa mazao; kusafisha na kutunza aina 24 za mbegu za asili; kutafiti aina za kahawa zenye tija kubwa; kutafiti aina za wanga wa muhogo; kutafiti zao la pareto; kuhaulisha teknolojia zikiwemo mbegu bora za ngano; na teknolojia za mazao yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia.

71. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia TARI:-

i. Imetambua aina 12 za mbegu tarajali (Promising lines) za soya zenye ukinzani wa kutu jani na utafiti unaendelea. Utafiti huo ukikamilika utawezesha nchi kupata mbegu bora za soya na kuondoa adha ya visumbufu na uagizaji wa mbegu kutoka nje ya nchi;

ii. Imetafiti viuatilifu hai vya kudhibiti ugonjwa wa mnyauko fusari katika zao la korosho na kubaini kuwa kiuatilifu aina ya *biofungicides* kinadhibiti ugonjwa huo. Aidha, majaribio ya kiuatilifu hicho yanaendelea katika mashamba ya korosho. Kukamilika kwa utafiti huo kutapunguza gharama za uagizaji wa viuatilifu vya kemikali kutoka nje ya nchi;

iii. Imefanya utafiti wa kudhibiti magonjwa ya *Cashew Leaf* na *Nut Blight* na kugundua aina nane (8) za mbegu za korosho (TARICA-1, TARICA 2, TARICA 3, TARICA 4, TARICA 5, TARICA 6, TARICA 7 na TARICA 8) zenye ukinzani na magonjwa hayo. Aidha, TARI imezalisha miche 500,000 ya aina hizo za mbegu ambazo zitasambazwa kwa wakulima;

iv. Imewasilisha aina 10 za migomba zenye sifa ya ukinzani dhidi ya visumbufu vya mazao na mavuno mengi kwa ajili ya vipimo vya majaribio ya utambuzi wa mbegu mpya (DUS) na majaribio ya umahiri wa mbegu (NPT) katika Taasisi ya Uthibiti wa Ubora wa Mbegu Tanzania;

v. Inaendelea kufanya majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano katika mikoa ya Morogoro na Tanga ili kupata mbegu zinazostahimili hali ya joto kwa lengo la kuongeza uzalishaji ili kuwa na mbegu zitakazotumika katika maeneo yasiyokuwa na baridi na kuongeza eneo la uzalishaji wa zao la ngano;

vi. Imehaulisha mbegu bora za ngano zilizozalishwa na TARI aina ya TARIWheat1 (tani 4.5 - 6 kwa hekta), TARIWheat2 (tani 3.3 – 4 kwa hekta), Merina (tani 3 kwa hekta) na Shangwe (tani 3.5 kwa hekta) kupitia maonesho ya 21 ya Arusha Agribusiness Expo na mashamba darasa yaliyopo katika Wilaya za

Monduli, Karatu na Siha. Pia, mbegu hizo zina sifa ya ukinzani dhidi ya magonjwa na zinastahimili ukame;

vii. Inaendelea kufanya majaribio ya Rafiki Planter ili kuongeza wigo wa matumizi ya teknolojia hiyo katika upandaji wa mbegu za alizeti na mahindi. Majaribio hayo yamefanyika katika Wilaya za Mvomero, Chamwino, Ikungi, Bariadi na Misungwi na kubaini kuwa teknolojia hiyo inaweza kutumika kwa ajili ya kupandia mazao ya alizeti na mahindi;

viii. Imefanya utafiti kuhusu viwango vya matumizi ya chokaa mazao kwenye udongo ili kupunguza athari za tindikali katika udongo. Aidha, utafiti uliofanyika katika mikoa ya Geita na Songwe umebaini kuwa tani mbili (2) za chokaa mazao zinafaa kwenye hekta moja (1) kwa mazao ya mahindi na maharage ili kuongeza uzalishaji;

ix. Imezalisha na kuhaulisha teknolojia za mazao ya maharage yaliyoongezewa virutubishi kibaiolojia katika mikoa ya Mwanza, Mara, Kagera, Simiyu, Geita na Shinyanga;

x. Imetoa mafunzo ya muda mfupi kwa wataalam 11 wa maabara za udongo na kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika Kituo cha TARI Mlingano ili kuwawezesha kufanya utafiti wa udongo na kuzalisha miche bora ya mkonge kwa lengo la kukidhi mahitaji yaliyopo;

xi. Imesafisha na kutunza aina 46 za mbegu za asili kwa mazao ya mpunga, nyanya na bamia ili kuzilinda zisipotee;

xii. Inaendelea na utafiti wa ladha ya mvinyo wa zabibu ambapo TARI imepanda miche ya zabibu kwa ajili ya majaribio kwa kutumia mbolea za asili na viwandani;

xiii. Imefanya tathmini ya mahitaji na kiwango cha wanga kinachohitajika kwa ajili ya matumizi ya viwanda ikiwemo viwanda vya nguo, dawa za binadamu na uokaji wa mikate. Tathmini hiyo itawezesha kufanya tafiti za aina za mbegu za muhogo zinazokidhi viwango vinavyohitajika ili kuhakikisha upatikanaji wa soko la uhakika la muhogo ndani ya nchi;

xiv. Imefanya utafiti wa zao la pareto na kugundua aina nne (4) za pareto zenye sifa ya mavuno mengi (kuzalisha kilo 1,500 hadi kilo 2,300 kwa hekta), ubora wa maua (pyrethrum content 1.9 – 2.2) na ukinzani wa ugonjwa wa mizizi. Aina hizo za pareto zipo katika hatua ya urasimishaji;

xv. Imewezesha upatikanaji wa Ithibati ya Kimataifa (ISO/IEC 17025:2017 Accreditation) ya Maabara ya Afya ya Udongo na Mimea iliyopo Wilaya ya Mufindi. Ithibati hiyo itaiwezesha maabara hiyo kutambulika Kimataifa;

xvi. Imeanza uchimbaji wa visima 10 na kuweka miundombinu ya umwagiliaji wa matone katika eneo lenye jumla ya ekari 15 ili kuimarisha vituo mahiri vya kuhaulisha teknolojia (AgriTech Hubs) katika viwanja vya maonesho ya wakulima Nanenane Nzuguni (Dodoma), Mwalimu Nyerere (Morogoro), Ngongo (Lindi), Nyamhongolo (Mwanza) na Nyakabindi (Simiyu) na maboresho yanaendelea; na

xvii. Imefanya utafiti wa magonjwa ya virusi (cassava mosaic disease na cassava brown streak disease) katika zao la muhogo na kugundua aina mbili (2) za mbegu za muhogo zenye ukinzani na magonjwa hayo. Mbegu hizo zimepelekwa TOSCI kwa ajili ya Majaribio ya Umahiri Kitaifa.

**b) Uzalishaji wa Mbegu za Awali**

72. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI ilipanga kuzalisha tani 1,550 za mbegu za mazao; kuzalisha mbegu kilo 300 za tumbaku ya mvuke aina ya K326; kukusanya vinasaba 11,400 vya chikichi na vinasaba 240 vya kakao; kuanzisha mashamba ya kutunza vinasaba katika Mkoa wa Morogoro; na kuwajengea uwezo watafiti sita (6) wa TARI kuhusu kilimo bora cha zao la chikichi katika nchi ya Indonesia.

73. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia TARI : -

i. Imezalisha tani 543.3 sawa na asilimia 33.8 ya lengo la kuzalisha tani 1,518 za mbegu za mazao ya nafaka, jamii ya mikunde, mafuta na mbogamboga ambapo tani 43.94 ni

mbegu za awali, tani 0.88 ni mbegu mama, tani 258.4 ni mbegu za msingi na tani 240.07 ni mbegu zilizothibitishwa;

ii. Imekusanya, kusafisha na kuhifadhi jumla ya mbegu za asili 770 za mazao ya ulezi (512), mpunga (118), mtama (105), uwele (17), migomba (10), maharage (5) na papai (3) ili kulinda mbegu hizo. Vilevile, kwa kushirikiana na TOSCI imekamilisha utambuzi wa aina 10 za mbegu za asili za mahindi nne (4), mpunga nne (4) na maharage mbili (2) ili kuziingiza kwenye mfumo rasmi wa mbegu. Aina hizo za mbegu za asili zimeshawasilishwa TOSCI kwa ajili ya usajili;

iii. Imekusanya vinasaba 102 vya chikichi kwa lengo la kuhifadhi na utafiti katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Mbeya, Morogoro, Ruvuma, Pwani, Tanga, Lindi na Mtwara; iv. Imekusanya aina 35 za kakao katika Mkoa wa Morogoro ili kupanda katika mashamba ya majaribio ya kuzalisha mbegu kwa lengo la kupata vinasaba na ukusanyaji unaendelea;

v. Imepanda miche ya tumbaku katika mikoa ya Tabora na Mbeya kwenye mashamba yenye ukubwa wa ekari 15 kwa ajili ya uzalishaji wa mbegu aina ya K326. Matarajio ya uzalishaji wa mbegu ni tani 4.5 za tumbaku zitakazotosheleza kupandwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 607,041; na

vi. Imekamilisha taratibu kwa ajili ya kuwajengea uwezo watafiti watano (5) wa TARI kuhusu kilimo bora cha chikichi nchini Indonesia. Watafiti hao watasafiri kwenda Indonesia ifikapo Septemba, 2025.

**c) Ujenzi wa Miundombinu ya Utafiti**

74. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI ilipanga kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya utafiti wa mbegu; ujenzi wa uzio na ghala 11; ujenzi wa nyumba nne (4) za watumishi; kulipa fidia kwa wananchi wa Uyole ili kupisha ujenzi wa uzio; na kuchimba kisima katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe).

75. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa,

i. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ulioanza mwaka 2022/2023 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 874.9 umefikia wastani wa asilimia 40.2 (TARI Selian hekta 120 asilimia 83), (TARI Kihinga hekta 150 asilimia 25), (TARI Ilonga hekta 200 asilimia 46), (TARI Hombolo hekta 70 asilimia 47), (TARI Uyole hekta 60 asilimia 27), (TARI Kibaha hekta 20 asilimia 44), (TARI Maruku hekta 32 asilimia 28), (TARI Tengeru hekta 50 asilimia 22), (TARI Kifyulilo hekta 66.5 asilimia 26), (TARI Dakawa hekta 50 asilimia 24) na (TARI Ifakara hekta 36.4 asilimia 73);



*Miundombinu ya Umwagiliaji katika shamba la utafiti TARI Selian.*

ii. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ulioanza mwaka 2023/2024 katika eneo lenye ukubwa wa hekta 246 umefikia wastani wa asilimia 10 katika vituo vya TARI Tumbi hekta 60 (asilimia 10), TARI Naliendele hekta 37 (asilimia 20), TARI Mikocheni hekta 60 (asilimia 5), TARI Ukiriguru hekta 47 (asilimia 5), TARI Mlingano hekta 20 (asilimia 10) na TARI Uyole - Ismani hekta 22 (asilimia 10);

iii. Mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika eneo lenye ukubwa wa hekta 1,000 katika vituo vya TARI Ukiriguru hekta 200 na TARI Uyole hekta 800 amekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ujenzi;

iv. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika kituo cha TARI Ilonga (hekta 15) umekamilika;

v. Ujenzi wa ghala tano (5) za kuhifadhi mbegu katika vituo vitano (5) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,075 ulioanza mwaka 2022/2023 umefikia wastani wa asilimia 50 ambapo Dakawa (asilimia 25), Naliendele (asilimia 95), Selian (asilimia 50), na Hombolo (asilimia 25). Aidha, ujenzi wa ghala katika kituo cha TARI Tumbi umekamilika;

vi. Ujenzi wa ghala tano (5) za kuhifadhi mbegu zenye uwezo wa kuhifadhi tani 2,075 (tani 415 kila moja) ulioanza mwaka 2023/2024 umefikia wastani wa asilimia 15 katika vituo vya TARI Ukiriguru (asilimia 25), TARI Maruku (asilimia 25) na TARI Uyole yenye ghala 3 (asilimia 40);

vii. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ghala katika vituo vya TARI Uyole, Ilonga, Ifakara na Kihinga amepatikana na kukabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi;

viii. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Kituo cha Sayansi za Kibaolojia (Bioscience) katika Mkoa wa Morogoro umekamilika na zabuni za kumpata mkandarasi wa ujenzi imetangazwa. Ujenzi wa kituo hicho utawezesha utoaji wa huduma za kisasa za kisayansi katika utafiti wa mbegu, wadudu, magonjwa, uhimilivu wa tabianchi, udongo, uhandisi wa kibaiolojia na kanzidata za taarifa za kibaiolojia;

ix. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Benki ya Mbegu (Gene Bank) itakayotumika kutunza mbegu katika kituo cha TARI Selian umekamilika. Aidha, zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi imetangazwa;

x. Ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche ya migomba kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI – Maruku umefikia asilimia 30;

xi. Ujenzi wa maabara ya patholojia ya TARI – Naliendele kwa ajili ya utafiti wa kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao umefikia asilimia 55;

xii. Ujenzi wa ofisi ya TARI Makao Makuu - Njedengwa umefikia asilimia 75 na ujenzi wa ofisi na nyumba nne (4) za watumishi katika kituo cha TARI Kihinga umekamilika;

xiii. Ujenzi wa uzio katika shamba la utafiti la Uyole umefikia asilimia 40;

xiv. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI Tengeru amepatikana na kukabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi;

xv. Imefanya tathmini kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa uzio katika shamba la Uyole. Aidha, taratibu za malipo ya fidia zinaendelea;

xvi. Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti ya vituo vya TARI Mlingano, TARI Tumbi na TARI Ukiriguru amepatikana na kukabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ujenzi. Pia, ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti umefikia wastani wa asilimia 45 katika vituo vya TARI Kifyulilo (asilimia 30), Hombolo (asilimia 60), Maruku (asilimia 40), Kihinga (asilimia 30), Dakawa (asilimia 60) na Ifakara (asilimia 50); na

xvii. Mkandarasi wa ujenzi wa nyumba nne (4) za watumishi na kuchimba kisima katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe) amepatikana na kukabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza kazi.

### 4.1.2 Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu na Miche Bora kwa Mpango wa Ruzuku kwa baadhi ya Mazao

76. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025 Bunge lako Tukufu liliidhinisha matumizi ya Shilingi Bilioni 44.42 kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji na usambazaji wa mbegu na miche bora. Hadi Aprili 2025, Shilingi Bilioni 18.2 sawa na asilimia 41 ya fedha zilizoidhinishwa zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hizo.

77. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuongeza upatikanaji wa mbegu bora nchini kufikia tani 80,000; ASA kuipatia Sekta binafsi mashamba yenye ukubwa wa hekta 4,914; kufanya marekebisho

ya tindikali ya udongo kwa kuweka chokaa mazao katika mashamba matano ya mbegu; na kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 1,075

78. ***Mheshimiwa Spika,*** ASA ilipanga kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji (hekta 3,000); kujenga uzio katika mashamba ya mbegu na miundombinu ya kukausha na kuhifadhi mbegu, ghala, karakana, ofisi na kukarabati karakana; kujenga na kukarabati nyumba 49; na kununua matrekta, magari madogo, malori, pikipiki na mitambo ya kuchakata na kuvunia mbegu.

**a) Uzalishaji na Usambazaji wa Mbegu na Miche Bora**

79. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, hadi Aprili 2025:-

i. Upatikanaji na usambazaji wa mbegu bora umefikia tani 79,700.62 sawa na asilimia 99.6 ya lengo la kuzalisha na kuthibitisha tani 80,000 za mbegu dhidi ya mahitaji ya tani 127,650. Kati ya hizo, tani 63,526.54 zimezalishwa nchini na tani 16,174.08 zimeingizwa kutoka nje ya nchi. Kati ya mbegu zilizozalishwa nchini tani 4,510 zimezalishwa na ASA na tani 59,016.54 zimezalishwa na sekta binafsi. Upatikanaji na uzalishaji wa mbegu bora nchini umeoneshwa kwenye **Jedwali Na.4**;

ii. ASA imeipatia sekta binafsi mashamba yenye ukubwa wa hekta 5,038 sawa na asilimia 102 ya lengo la hekta 4,914 kwa ajili ya kuzalisha mbegu za mazao ya mahindi, mpunga, alizeti, ngano, maharage na ufuta;

iii. Marekebisho ya tindikali ya udongo yamefanyika ambapo jumla ya tani 1,100.2 za chokaa mazao zimenunuliwa na kutumika katika mashamba tisa (9) ya mbegu ya Mbozi (hekta 260), Dabaga (hekta 400), Kilimi (hekta 400), Msungura (hekta 100), Mwele (hekta 300), Bugaga (hekta 120), Arusha (hekta 450), Namtumbo (hekta 1,384) na Kilangali (hekta 400). Aidha, marekebisho ya tindikali ya

udongo yanaendelea katika shamba la mbegu la Luhafwe (hekta 150);

iv. Tani 700 za mbegu bora za alizeti na tani 500 za mbegu bora za ngano zenye thamani ya Shilingi 17,380,000,000 zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa ruzuku;

v. Tani 9,639.63 za mbegu bora za mahindi zenye thamani ya ruzuku ya Serikali ya Shilingi 10,473,750,000 zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji kupitia mpango wa ruzuku; na

vi. Mbegu bora za kahawa tani 9.9 zikiwemo tani 5 za arabika na tani 4.9 za robusta zimezalishwa. Kati ya hizo, tani 9.2 zimesambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji na usambazaji unaendelea.



*Uzalishaji wa mbegu bora za mahindi katika shamba la wakala wa mbegu za kilimo (ASA), Iringa.*

**Jedwali Na. 4:** Upatikanaji wa Mbegu Bora Nchini (Tani) mwaka 2024/2025

| Zao | Uagizaji Nje ya Nchi | Uzalishaji Ndani ya Nchi | Jumla Ndogo |
|---|---|---|---|
| Mahindi | 15,214.74 | 29,078.16 | 44,292.90 |
| Mpunga | 116.08 | 716.59 | 832.67 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Mtama | 18.01 | 174.52 | 192.53 |
| Alizeti | 121.54 | 1641.96 | 1,763.50 |
| Mboga | 696.33 | 136.811 | 833.14 |
| Njegere | 0.20 | 286.02 | 286.22 |
| Maharage | 2.62 | 448.99 | 451.61 |
| Pamba | - | 28,800.00 | 28,800.00 |
| Choroko | - | 15.78 | 15.78 |
| Mbaazi | - | 105.44 | 105.44 |
| Karanga | - | 72.89 | 72.89 |
| Ufuta | - | 23.48 | 23.48 |
| Ngano | 3.97 | 1670.03 | 1,674.00 |
| Kunde | - | 316.99 | 316.99 |
| Njugu mawe | - | 8.89 | 8.89 |
| Ulezi | - | 1.20 | 1.20 |
| Tumbaku | 0.59 | 0.04 | 0.63 |
| Maharage ya Soya | - | 28.74 | 28.74 |
| **Jumla Kuu** | **16,174.08** | **63,526.54** | **79,700.6 2** |

**Chanzo:** *Wizara ya Kilimo, 2025*

**b) Ujenzi wa Miundombinu kwenye Mashamba ya Mbegu**

i. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora yenye ukubwa wa hekta 580 kati ya hekta 805.5 ulioanza katika mwaka 2022/2023 umefikia wastani wa asilimia 74 katika mashamba ya Msimba - Morogoro (hekta 200 asilimia 70), Arusha (hekta 200 asilimia 82) na Kilimi - Tabora (hekta 180 asilimia 70). Kukamilika kwa ujenzi huo kutawezesha uzalishaji wa mbegu kwa mwaka mzima.



*Miundombinu ya umwagiliaji katika shamba la mbegu Arusha.*

ii. Mshauri elekezi ameanza kazi ya usanifu wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya uzalishaji wa mbegu bora uliopangwa kuanza mwaka 2023/2024 yenye ukubwa wa hekta 300 (Msimba - Morogoro hekta 100, Mbozi - Songwe hekta 100 na Arusha hekta 100);

iii. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina umekamilikakwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya mbegu yenye jumla ya hekta 3,000 katika mashamba ya Namtumbo - Ruvuma (hekta 1,000), Mbozi – Songwe (hekta 500), Msimba - Morogoro (hekta 200), Kilimi - Tabora (hekta 160), Arusha (hekta 240), Msungura – Pwani (hekta 100) na Luhafwe - Katavi (hekta 800);

iv. Mkandarasi wa ujenzi wa uzio katika shamba la mbegu la Mwele - Tanga (hekta 874) amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi na mkandarasi wa ujenzi wa uzio katika shamba la mbegu la Kilangali – Morogoro (hekta 1,200) amepatikana. Aidha, tathmini ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa uzio katika mashamba ya mbegu ya Arusha (hekta 618.5) na Namtumbo – Ruvuma (hekta 3,580.4) imekamilika;

v. Ujenzi wa miundombinu ya kukausha na karakana katika shamba la Kilimi umekamilika. Aidha, ujenzi wa ghala umefikia asilimia 8;

vi. Ukarabati wa nyumba tano (5) za watumishi katika shamba la Msimba umefikia wastani wa asilimia 70 na mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi na nyumba nne (4) za watumishi katika shamba la Kilimi amepatikana;

vii. Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za watumishi katika mashamba ya mbegu ya Mwele (4) na Msungura (3) wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ujenzi;

viii. Wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa nyumba katika mashamba ya mbegu ya Arusha (10), Mbozi (6), Namtumbo (3) na Luhafwe (2) wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ukarabati; na

ix. ASA imenunua malori matatu (3) ya tani kumi kila moja na mawili (2) ya tani 30 kila moja kwa ajili ya kusambaza mbegu, matrekta matatu (3), pikipiki tatu (3), mitambo miwili (2) ya kuchakata mbegu, mtambo mmoja (1) wa kuvunia mbegu na mitambo miwili (2) ya kukausha mbegu. Upatikanaji wa magari na mitambo hiyo utasaidia usambazaji na kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora.



*Kiwanda cha kuchakata mbegu kinachomilikiwa na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA) Msimba Kilosa Mkoani Morogoro.*

80. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Bodi za mazao, Wakala na Taasisi zake kwa kushirikiana na sekta binafsi ilipanga kuzalisha na kusambaza jumla ya miche

47,500,000 ya mazao ikiwemo miche ya kahawa (20,000,000), korosho (1,000,000), zabibu (500,000), minazi (10,000,000), migomba (2,000,000), parachichi (6,000,000), chikichi (2,000,000), chai (3,000,000) na mkonge (3,000,000). Pia, kuzalisha na kusambaza pingili za muhogo 6,290,000 na vipando vya viazi vitamu 450,000 katika maeneo ya uzalishaji wa mazao hayo.

81. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jumla ya miche 24,426,895 ya mazao mbalimbali imezalishwa sawa na asilimia 51 ya lengo la kuzalisha miche 47,500,000 na uzalishaji unaendelea. Miche iliyozalishwa ni kahawa (19,881,703), korosho (1,300,000), zabibu (318,283), minazi (300,000), migomba (121,000), parachichi (569,500), chikichi (636,415) na mkonge (1,300,000). Aidha, miche iliyozalishwa imesambazwa kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku katika maeneo ya Zanzibar, Kagera, Kigoma, Iringa, Njombe, Manyara, Arusha, Dodoma, Ruvuma, Kilimanjaro, Morogoro, Tanga, Manyara, Songwe, Pwani, Dar es Salaam, Lindi, Mtwara na Mbeya.

82. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, pingili za muhogo 5,012,442 aina ya TARICASS4 sawa na asilimia 79.7 ya lengo la kuzalisha pingili 6,290,000 zimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika mikoa ya Kigoma, Tabora, Katavi, Singida, Mwanza na Mara. Pia, vipando vya viazi vitamu 55,800 vimezalishwa na kusambazwa kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji.

**c) Uthibiti wa Ubora wa Mbegu**

83. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TOSCI ilipanga kukagua mashamba ya mbegu yenye jumla ya hekta 55,285; kuchukua sampuli 4,185 za mbegu; kukagua maduka ya mbegu 2,420 na ghala 130 za kuhifadhi mbegu; kusajili kampuni 30 na wafanyabiashara 500; kutoa lebo 32,000,000 za mbegu bora; na kutoa mafunzo kwa wakaguzi 90 wa mbegu.

84. ***Mheshimiwa Spika,*** TOSCI ilipanga kufanya majaribio ya utambuzi wa aina mpya za mbegu (DUS tests) kwa aina 150 za mbegu na Majaribio ya Kitaifa ya Umahiri wa aina mpya za mbegu (NPT) kwa aina 50 za mbegu; majaribio ya uhalisia wa mbegu zilizopo katika uzalishaji (Control plot testing) kwa sampuli

za mazao 250; na kuweka utaratibu wa kikanuni wa kusimamia bei ya mbegu na kutangaza bei elekezi tarehe 01 Septemba ya kila mwaka.

85. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, TOSCI imekagua mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 45,652.3 sawa na asilimia 82.6 ya lengo la kukagua hekta 55,285 na kubaini kuwa mashamba hayo yamekidhi vigezo vya kuzalisha mbegu bora. Vilevile, maduka ya mbegu 3,155 sawa na asilimia 130.4 ya lengo la kukagua maduka 2,420 na ghala 135 sawa na asilimia 104 ya lengo la kukagua ghala 130 za kuhifadhi mbegu yamekaguliwa kwa ajili ya uthibiti wa mbegu.

86. ***Mheshimiwa Spika,*** maduka ya mbegu 3,155 yaliyokaguliwa, maduka 234 sawa na asilimia 7.41 hayakukidhi vigezo. Hivyo, wamiliki walipewa amri ya kusitisha mauzo (stop sale order) na kupatiwa mafunzo kuhusu biashara ya mbegu pamoja na kukamilisha taratibu za usajili. Aidha, Kampuni 35 na wafanyabiashara 704 wa mbegu wamesajiliwa kwenye mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusambaza mbegu za mahindi kupitia mpango wa ruzuku.


87. ***Mheshimiwa Spika,*** kadhalika, lebo 15,094,169 sawa na asilimia 47.2 ya lengo la kutoa lebo 32,000,000 za mbegu bora zimetolewa. Vilevile, mafunzo kuhusu ukaguzi wa mbegu kwa wakaguzi 55 wa mbegu bora katika mikoa 11 ya Tanzania Bara yametolewa ili kuimarisha uwezo wa ukaguzi. Aidha, majaribio ya utambuzi wa aina 69 za mbegu mpya (DUS tests) yamekamilika na kufaulu na majaribio ya kitaifa ya umahiri wa aina mpya 28 za mbegu (NPT) yanaendelea. Pia, sampuli za mbegu 2,642 za mazao jamii ya nafaka, mikunde na mboga zimechukuliwa na kuthibitishwa ubora.

88. ***Mheshimiwa Spika,*** majaribio ya uhalisia wa mbegu za mazao kwa sampuli 250 zilizopo katika uzalishaji (Control plot testing) yanaendelea kwa lengo la kuhakikisha mbegu husika zinaendelea kutunza uhalisia wake. Aidha, utaratibu wa kikanuni wa kusimamia bei ya mbegu umewekwa na bei elekezi za mbegu kwa msimu wa kilimo 2024/2025 zimetangazwa tarehe 01 Septemba 2024.


**d) Ushiriki wa Sekta Binafsi katika Kuimarisha Upatikanaji wa Mbegu Bora**

89. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI kwa kushirikiana na World Vegetable Center imetoa mafunzo kuhusu ukusanyaji wa taarifa kwa njia ya kidijiti kwa kutumia vishikwambi kwa wakulima 784 na Maafisa Ugani 31 katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Lindi na Mtwara. Vilevile, TARI imefanya majaribio ya aina mpya za mchicha, mgagani na nyanya chungu katika mikoa ya Lindi na Mtwara kwa lengo la kujenga uwezo wa muda mrefu katika uhifadhi wa mbegu na matumizi ya mazao ya mboga za asili ya Afrika.

90. ***Mheshimiwa Spika,*** sekta binafsi imeendelea kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora nchini ambapo katika mwaka 2024/2025 imezalisha mbegu tani 59,016.54 ikilinganishwa na mbegu tani 25,555.04 zilizozalishwa katika mwaka 2023/2024 kama inavyooneshwa kwenye **Kielelezo Na. 1 na 2.**




**Kielelezo Na. 1**: Mchango wa kampuni za ndani katika uzalishaji wa mbegu bora mwaka 2023/2024




**Kielelezo Na. 2**: Mchango wa kampuni za nje katika uzalishaji wa mbegu bora mwaka 2023/2024

**4.1.3 Uwekezaji kwenye Utoaji wa Ruzuku ya Mbolea na Viuatilifu**
**a) Upatikanaji wa Mbolea**

91. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuratibu upatikanaji wa tani 1,500,000 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; kukamilisha vigezo muhimu katika mfumo mfumo wa ruzuku ya pembejeo za kilimo; kusajili wakulima, waagizaji na wasambazaji wa mbolea katika mfumo wa kielektroniki; TFC kununua tani 100,000 za mbolea na kusambaza kwa wakulima; kujenga kiwanda cha kuchanganya mbolea; kununua magari kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa mbolea na kukarabati ghala saba (7) kwa ajili ya kuhifadhi mbolea.

92. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC ilipanga kuingia makubaliano na kiwanda cha *Tanzania Biotech Products Limited* (TBPL) kwa ajili ya kuanza kuzalisha na kusambaza mbolea zisizo na kemikali; kuunda na kufunga mfumo wa kidijiti katika ghala/vituo vya mauzo ya mbolea kwa ajili kusimamia na kuhakiki mauzo ya mbolea na viuatilifu katika vituo vya mauzo na mawakala; na TFC kununua *Point of Sale Machines* (POS) 40.

93. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia TFRA imeratibu upatikanaji wa mbolea na visaidizi vya mbolea tani 1,213,729 sawa na asilimia 80.9 ya lengo la tani 1,500,000 ambapo tani 542,096 zenye thamani ya ruzuku ya Shilingi 182,125,280,724 zimesambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea. Aidha, kati ya kiasi cha mbolea kilichozalishwa, tani 158,628 zimezalishwa nchini.

94. ***Mheshimiwa Spika***. vilevile, ili kuimarisha upatikanaji wa mbolea TFC imenunua mbolea tani 59,127 (tani 10,075.75 - CAN, tani 2,041.25 - UREA na tani 47,010 – NPK) na kusambaza kwa wakulima wa tumbaku kupitia mpango wa ruzuku. Pia, imenunua mbolea tani 15,000 aina ya DAP kwa ajili ya kusambaza kwa wakulima wa mazao mengine.

95. ***Mheshimiwa Spika***, ukarabati wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi mbolea tani 15,000 katika Mkoa wa Ruvuma umekamilika. Ghala hilo litaongeza uwezo wa TFC kuhifadhi mbolea na kusambaza kwa wakulima. Aidha, taratibu za kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa ghala tano (5) katika mikoa ya Mwanza, Tabora, Rukwa, Njombe na Mbeya zinaendelea.

96. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa mbolea ndani ya nchi, usimikaji wa mitambo ya kiwanda cha mbolea cha TFC chenye uwezo wa kuchanganya mbolea tani 120 kwa saa umefikia asilimia 30 katika eneo la Kurasini Mkoa wa Dar es Salaam. Aidha, TFC imenunua malori matano (5) yenye uwezo wa kubeba tani 15 kila gari kwa ajili ya kuwezesha usambazaji wa mbolea. Pia, uundaji wa mfumo wa kidijiti kwa ajili ya kusimamia na kuhakiki mauzo ya mbolea na viuatilifu katika vituo vya mauzo na mawakala umefikia asilimia 80. Mfumo huo utafungwa katika ghala na vituo vyote vya mauzo ya mbolea vya TFC.

97. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC imeingia makubaliano na kiwanda cha *Tanzania Biotech Products Limited* (TBPL) kwa ajili ya kusambaza mbolea zisizo na kemikali (Bio - fertilizers)

zitakazozalishwa na kiwanda hicho. Aidha, TFC imepokea POS 42 ili kurahisisha ukusanyaji wa mapato na maduhuli.

**b) Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya Mazao na Mimea**

98. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA ilipanga kununua na kusambaza lita 95,000 za viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti nzige, viwavijeshi vamizi, panya, kweleakwelea, nzi wa matunda na visumbufu vya parachichi; kununua magari saba (7) na ndege moja (1); kuzalisha wadudu rafiki na kusajili viuatilifu hai; kununua vifaa vya maabara ya karantini ya Taifa ya mimea na maabara ya uchambuzi wa viuatilifu; kukarabati ofisi mbili (2) za kanda; kununua maeneo matatu (3) kwa ajili ya kujenga ofisi; na kujenga ofisi na maabara ndogo 12 kwenye vituo vya ukaguzi mipakani.

99. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, TPHPA imenunua ndege moja (1) kwa ajili ya huduma za anga za udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao, magari 10 na pikipiki 19 kwa ajili ya kuimarisha ukaguzi na shughuli za udhibiti wa visumbufu. Pia, wadudu rafiki wamezalishwa na aina 20 za viuatilifu hai vimesajiliwa kwa ajili ya udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao kama njia mbadala ya matumizi ya viuatilifu vya viwandani na hatua za kutangazwa kwenye gazeti la Serikali zinaendelea.

100. ***Mheshimiwa Spika***, TPHPA imenunua vifaa vya maabara ya karantini ya Taifa ya mimea na maabara ya uchambuzi wa viuatilifu zilizopo katika Mkoa wa Arusha ikiwemo mashine za kisasa tano (5) (GC intuvo - 1, GC Ms/Ms - 2, LC Ms/Ms - 2 na jenereta 2 za kuzalishia hewa ya oxygen).

101. ***Mheshimiwa Spika***, wakandarasi kwa ajili ya ukarabati wa ofisi mbili (2) za kanda (Kurasini na Tengeru) wamepatikana na wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza kazi. Aidha, maeneo mawili (2) kwa ajili ya kujenga maabara katika Mkoa wa Njombe (hekta 0.82) na ofisi katika Mkoa wa Tabora (hekta 0.17) yamenunuliwa na hati za maeneo hayo zimepatikana. Vilevile, upatikanaji wa eneo kwa ajili ya ujenzi wa ofisi ya Mtwara unaendelea na wakandarasi kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ofisi pamoja na maabara ndogo 16 kwenye vituo vya ukaguzi

mipakani wamepatikana na wamekabidhiwa maeneo kwa ajili ya kuanza ujenzi. Kukamilika kwa ujenzi wa vituo hivyo kutaimarisha biashara ya mazao ya kilimo mipakani.

102. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA ilipanga kukagua vifaa vya kunyunyizia viuatilifu; kuimarisha usajili wa miundo mipya ya vifaa vya kunyunyizia viuatilifu na ufuatiliaji wa athari za viuatilifu kwa binadamu na mazingira; kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi na utumiaji wa rasilimali za kijenetiki za mimea; kuimarisha usimamizi na uratibu wa kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea; kuimarisha kituo cha ufuatiliaji wa magonjwa; kupima masalia ya mabaki ya viuatilifu katika mazao ya bustani na nafaka. Vilevile, TPHPA ilipanga kutoa mafunzo ya matumizi sahihi ya viuatilifu na afya ya mimea kwa wakulima 4,000 na wafanyabiashara 500.

103. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, ukaguzi wa vifaa vya kunyunyizia viuatilifu katika maduka 155 ya pembejeo za kilimo umefanyika katika mikoa ya Ruvuma na Dodoma na kubaini kuwa vifaa vilivyokaguliwa kwa ajili ya kunyunyizia viuatilifu vinafaa kwa matumizi. Aidha, usimamizi na uratibu wa kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea umeimarishwa ambapo takriban ekari 438,271 zimeokolewa na kuwezesha kuokoa takriban tani 1,000,000 za nafaka katika mikoa ya Morogoro, Dodoma na Manyara.

104. ***Mheshimiwa Spika,*** mifumo ya GIS na *Remote Sensing* kwa ajili ya ukusanyaji na uhifadhi wa takwimu imefungwa katika kituo cha ufuatiliaji wa magonjwa (BBTD observatory system) ili kudhibiti visumbufu vya mimea na mazao kwa wakati. Aidha, ufuatiliaji wa athari za viuatilifu kwa binadamu na mazingira umefanyika katika mikoa ya Arusha, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma na Mbeya na kubaini baadhi ya wakulima kutozingatia matumizi sahihi ya viuatilifu. Katika kukabiliana na changamoto hiyo, mafunzo kuhusu matumizi sahihi na salama ya viuatilifu na afya ya mimea yametolewa kwa wakulima 253 na wafanyabiashara 310 ili kupunguza athari za viuatilifu kwenye afya ya binadamu na mazingira na kuongeza tija katika kilimo.

105. ***Mheshimiwa Spika,*** TPHPA imesajili miundo mipya 17 ya vifaa vya kunyunyizia viuatilifu ili kuimarisha shughuli za udhibiti wa visumbufu. Pia, ukusanyaji, uhifadhi na utumiaji wa rasilimali za kijenetiki za mimea umeimarishwa kwa kutengeneza kanzidata za kijenetiki kwa ajili ya utafiti wa mimea na mazao.

106. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA ilipanga kukagua maduka 4,000 ya viuatilifu nchini. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, maduka 819 ya viuatilifu katika mikoa ya Morogoro, Mbeya, Dodoma, Ruvuma na Tabora yamekaguliwa na kubaini baadhi ya wafanyabiashara wa viuatilifu wanafanya biashara hiyo bila vibali ambapo ni kinyume cha Sheria Na. 4 ya Afya ya Mimea ya mwaka 2020. Kutokana na ukaguzi huo, TPHPA imetoa mafunzo kuhusu biashara ya viuatilifu kwa wauzaji wa maduka hayo ili kukidhi vigezo vya kuendesha biashara ya viuatilifu. Vilevile, jumla ya maduka 364 katika mikoa ya Mbeya (105), Dodoma (126), Ruvuma (133) yamesajiliwa kwa ajili ya biashara ya viuatilifu.

### 4.1.4 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Umwagiliaji

107. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilitengewa jumla ya Shilingi Bilioni 393.435 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya umwagiliaji 780 yenye jumla ya hekta 543,366.46 iliyoanza kutekelezwa mwaka 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025 kama ifuatavyo:-

i. Kujenga skimu mpya 63 zenye jumla ya hekta 148,283.46;

ii. Kukarabati skimu 48 zenye jumla ya hekta 81,972;

iii. Kufanya upembuzi yakinifu na kujenga mabwawa 114 yenye takriban mita za ujazo 1,180,570,701;

iv. Kufanya upembuzi yakinifu na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya kimkakati 22 yenye takriban hekta 306,361;

v. Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu pamoja na kujenga mashamba ya pamoja (Block farms) sita (6) yenye jumla ya hekta 79,518.46;


iii. Kufanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 527 zenye takriban hekta 290,095 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati;

iv. Kununua magari 13 na pikipiki kwa ajili ya ofisi za umwagiliaji za wilaya;

v. Kununua mitambo 30 ya kuchimba visima na mitambo mitatu (3) kwa ajili ya uchimbaji wa mabwawa ya umwagiliaji;

vi. Kuanza ujenzi wa ofisi 19 na ukarabati wa ofisi sita (6) za umwagiliaji za mikoa; na

vii. Kutoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa watumishi na wakulima katika skimu.



*Skimu ya Umwagiliaji ya Madibira*

108. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imetekeleza yafuatayo:-

i. Imekamilisha ujenzi wa skimu mpya tatu (3) za Magurukenda yenye ukubwa wa hekta 150, Sukuma hekta 350 (Buchosa) na Tlawi hekta 350 (Mbulu). Ujenzi unaendelea katika skimu mpya 55 na umefikia wastani wa asilimia 52. Aidha, taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa skimu tano (5) za Kalupale (Sikonge), Igwisi,

Mwamabondo (Uyui), Iloba (Mpanda) na Nyamgongwa (Nyang'wale) zinaendelea kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 1**;

iii. Imekamilisha ukarabati wa skimu saba (7) za Madibira hekta 3,200 (Mbarali), Mgambalenga awamu ya kwanza hekta 3,000 (Kilolo), Myamba hekta 1,470 (Same), Muhukuru hekta 300 (Songea), Idudumo awamu ya kwanza hekta 400 (Nzega), Mbaka hekta 600 (Busokelo) na Mtula hekta 75 (Mufindi). Ukarabati unaendelea katika skimu 41 na umefikia wastani wa asilimia 60 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 2**;

iv. Imekamilisha ujenzi wa bwawa la Tlawi (Mbulu) lenye mita za ujazo 1,100,000 na ukarabati wa bwawa la Ulyanyama (Sikonge) lenye mita za ujazo 2,070,000. Ujenzi wa mabwawa 19 yenye mita za ujazo 326,449,973.00 unaendelea na umefikia wastani wa asilimia 57.2. Aidha, taratibu za ununuzi wa kuwapata wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa 28 zinaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa 65 unaendelea kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 3**;

v. Imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde 14 kati ya 22 ya kimkakati na upembuzi unaendelea katika mabonde nane (8). Aidha, ujenzi wa skimu 19 zenye jumla ya hekta 17,848 katika mabonde matatu (3) ya kimkakati ya Mkomazi, Lukuledi na Mtambo umeanza na umefikia wastani wa asilimia 10. Taratibu za ununuzi kwa ajili ya kuwapata wakandarasi wa ujenzi wa skimu katika mabonde 10 ya kimkakati zinaendelea kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 4**;

vi. Imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mashamba matatu (3) ya pamoja na kuanza ujenzi katika mashamba hayo ambayo ni Membe, Ndogowe na Chinangali kati ya mashamba sita (6) ambapo ujenzi umefikia wastani wa asilimia 60 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 5**;

vii. Imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 98 kati ya skimu 527 kwa ajili ya ujenzi wa skimu mpya na ukarabati wa skimu. Kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu inaendelea katika skimu 429 kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 6**;

iv. Tume imenunua magari 10 na pikipiki 23 kwa ajili ya kuimarisha shughuli za umwagiliaji katika mikoa ya Dodoma, Morogoro, Njombe, Tanga, Arusha, Tabora, Mwanza, Mbeya na Singida. Kadhalika, zabuni kwa ajili ya ununuzi wa pikipiki 100 imetangazwa;

viii. Imenunua mitambo 18 ya kuchimba visima vya kati na virefu kwa ajili ya shughuli za umwagiliaji;

ix. Wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi 13 za wilaya na ofisi tatu (3) za mikoa ya Kilimanjaro, Iringa na Ruvuma wamepatikana na wamekabidhiwa maeneo ili kuanza ujenzi. Aidha, ujenzi wa ofisi ya Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji umefikia asilimia 85; na

x. Tume imesajili Vyama vya Umwagiliaji 120 hivyo kufanya vyama vilivyosajiliwa kuwa 902. Aidha, Tume imetoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa watumishi 152, wakulima viongozi 506 na wakulima 3,735 ili kuhakikisha uendelevu wa miundombinu ya umwagiliaji.

109. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Tume ilipanga kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la mto Rufiji; kuanza ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya Mbakiamtuli na Ngorongo; kufanya upembuzi yakinifu wa kutumia maji ya ziwa Victoria na Tanganyika kwa ajili ya umwagiliaji.

110. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imekamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa bonde la mto Rufiji lenye ukubwa wa hekta 64,800 na wakandarasi wamepatikana kwa ajili ya kuanza ujenzi wa mabwawa mawili (2) ya Mbakiamtuli na Ngorongo. Aidha, Mkandarasi kwa ajili ya

ujenzi wa mradi wa Bugwema (Mara) amepatikana na kandarasi ya ujenzi wa mradi katika bonde la mto Ngono (Kagera) imetangazwa.
Vilevile, zabuni ya kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya upembuzi yakinifu wa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa ajili ya shughuli za kilimo imetangazwa.

**4.1.5 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo**
111. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi ilipanga kuanza kupima ardhi ya wakulima wadogo 10,000 katika mikoa yote nchini na kuhakikisha wanapatiwa hati za hakimiliki bila gharama yoyote ikiwa ni sehemu ya urasimishaji. Aidha, ilipanga kusajili wafanyabiashara wa mazao ya kilimo na watoa huduma za ugani, ghala na pembejeo za kilimo.

112. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi imepima ardhi kwa wakulima 9,117 na kuwapatia hati za hakimiliki katika Halmashauri ya Iramba (Singida), Mbinga (Ruvuma), Songwe (Songwe) pamoja na Chamwino (Dodoma) na upimaji unaendelea.

113. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, ukamilishaji wa vigezo muhimu kwenye mfumo wa ruzuku ya pembejeo za kilimo umefanyika na kuwezesha kusajili wakulima 677,842 na kufanya idadi ya wakulima waliosajiliwa kufikia 4,522,011. Aidha, mfumo huo umetumika kusajili waagizaji 64, wasambazaji wa mbolea 7,147 na Vyama vya Ushirika 720 kwa lengo la kuimarisha usambazaji wa mbolea nchini tangu kazi ya usajili ianze mwaka 2023/2024. Pia, ghala 1,738 na wafanyabiashara 518 wamesajiliwa kupitia mfumo wa *Crop Stock Dynamics System* - CSDS ili kurasimisha biashara ya mazao ya kilimo na usajili unaendelea.



*Afisa Ugani akichukua taarifa za Mkulima kwa ajili ya Usajili.*

**4.1.6 Kuwekeza kwenye Ujuzi kwa Wataalam wa Ndani**

114. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara ilipanga kuwawezesha wataalam 485 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi. Kati ya hao, Shahada ya Uzamivu ni 33, Shahada ya Uzamili 124, Shahada 52, Stashahada mmoja (1) na mafunzo ya ujuzi maalum 275. Lengo la mafunzo hayo ni kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ikiwemo kuhaulisha teknolojia na kutoa mafunzo kwa wakulima.

115. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jumla ya wataalam 258 wamewezeshwa kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na ufanisi katika utendaji kazi. Kati ya hao 208 mafunzo ya muda mrefu (shahada ya Uzamivu 41, Shahada ya Uzamili 113, Shahada 51 na Stashahada 03) na mafunzo ya muda mfupi 50.

**4.1.7 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani**

116. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2024/2025, ilipanga kununua na kusambaza magari 50, pikipiki 600 na vipima afya ya udongo 43; kujenga nyumba 50 za Maafisa Ugani; kujenga na kukarabati vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata; kujenga miundombinu kwenye viwanja vya maonesho ya wakulima Nanenane katika mikoa ya Dodoma na Mbeya;

kuendelea kuimarisha mfumo wa ufuatiliaji wa vitendea kazi; na kuunganisha mfumo wa M-Kilimo na mfumo wa usajili wa wakulima.

117. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imenunua na kusambaza pikipiki 555 kwa Maafisa Ugani na kufanya pikipiki zote zilizonunuliwa na kusambazwa kuanzia mwaka 2022/2023 kufikia 6,444. Vilevile, imenunua na kusambaza magari 44 kwa Maafisa Ugani ngazi ya Mkoa 15, Halmashauri 14 na magari 15 katika Vituo vya Uhaulishaji wa Teknolojia za Kilimo (MATI). Lengo la kununua vitendea kazi hivyo ni kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima nchini.

118. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, magari 14 yapo kwenye hatua ya ukaguzi kwa ajili ya kusambazwa na taratibu za ununuzi wa magari mengine 50 na vipima afya ya udongo 43 zinaendelea. Pia, ujenzi wa nyumba 50 za Maafisa Ugani umefikia wastani wa asilimia 80 na ukarabati wa vituo vitano (5) vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward Resource Centres - WARCs) katika mikoa ya Singida, Kilimanjaro, Kigoma, Dodoma na Iringa umefikia wastani wa asilimia 35.



*Nyumba ya Afisa Ugani*

119. ***Mheshimiwa Spika***, ujenzi wa miundombinu kwenye viwanja cha maonesho ya wakulima Nanenane Nzuguni (Dodoma)

umefikia asilimia 75 ya awamu ya kwanza. Aidha, wakandarasi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu kwenye kiwanja cha maonesho ya wakulima Nanenane John Mwakangale (Mbeya) wamepatikana na wamekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza ujenzi. Pia, uunganishaji wa mfumo wa M-Kilimo na mfumo wa usajili wa wakulima umefanyika na umeanza kutumika kwa ajili ya usajili wa Maafisa Ugani ambapo jumla ya Maafisa Ugani 6,063 wamesajiliwa na usajili unaendelea. Kati ya hao, Maafisa Ugani kilimo wa Serikali ni 5,796 na Maafisa Ugani kilimo wa sekta binafsi ni 267.

120. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kufanya mabadiliko ya mfumo wa utoaji wa mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATIs); kuandaa mkakati wa mafunzo kwa wakulima na kutekeleza programu za uhaulishaji wa teknolojia zinazogunduliwa na watafiti kwa kuwanufaisha wakulima 5,000; na kukarabati miundombinu ya vituo 12 vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo.

121. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara imeanza kufanya mabadiliko ya mfumo wa utoaji wa mafunzo katika Vyuo vya Mafunzo ya Kilimo (MATIs) ambapo vituo hivyo kwa sasa vinatoa mafunzo ya uhaulishaji wa teknolojia zinazotokana na tafiti za kilimo, kuwajengea uwezo Maafisa Ugani na baadhi ya vituo kuvifanya kuwa vituo mahiri kwa aina mahsusi za mazao. Jumla ya wakulima 11,874 wamepatiwa mafunzo kuhusu kilimobiashara na Maafisa Ugani 1,701 kupatiwa mafunzo kuhusu kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya TEHAMA katika kutoa huduma za ugani. Aidha, Wizara inaendelea kuboresha miundombinu katika Vituo vya kuhaulisha teknolojia za kilimo vya Mkindo, Bihawana, MATI Igurusi, MATI Mlingano na MATI Mtwara ambapo wakandarasi wamepatikana kwa ajili ya kuanza ukarabati.

**4.1.8 Kupima Afya ya Udongo kwa Wakulima**

122. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kupima afya ya udongo kwa kutumia *soil scanners* zilizosambazwa katika Halmashauri; kubuni na kuhamasisha matumizi ya teknolojia sahihi za utunzaji wa maji na udongo mashambani; kununua *mobile soil laboratory van* kwa ajili ya kupima afya ya udongo; na kukamilisha upimaji wa afya ya udongo katika mikoa ya Tanzania Bara.

123. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, wakulima 54,188 katika Halmashauri 141 wenye jumla ya eneo la ukubwa wa hekta 328,659 wamepimiwa afya ya udongo kwa kutumia *soil scanners* na kupatiwa matokeo ya vipimo vya afya ya udongo. Matokeo hayo yanawezesha wakulima kupanda mazao na kutumia aina na kiwango sahihi cha mbolea.

124. ***Mheshimiwa Spika,*** upimaji wa afya ya udongo umefanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekta 8,869,026.81 katika mikoa ya Ruvuma (hekta 3,815,075), Arusha (hekta 958,096.74), Kilimanjaro (hekta 864,276.57), Simiyu (hekta 206,843.5) na Manyara (hekta 3,024,735). Mchanganuo wa ukubwa wa maeneo yaliyopiwa afya ya udongo ni kama inavyoonekana kwenye **Kiambatisho Na. 7**. Aidha, kazi ya kupima afya ya udongo inaendelea nchini kwa ajili ya kuandaa ramani ya awali itakayoonesha afya ya udongo kwa kila Mkoa itakayosaidia matumizi sahihi ya teknolojia za uzalishaji wa mazao. Pia, Wizara imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia sahihi za utunzaji wa maji na udongo mashambani kwa wakulima 5,429 katika mikoa ya Morogoro, Dodoma, Simiyu na Mbeya.

### 4.1.9 Uanzishaji wa Vituo vya Kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo

125. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuanzisha vituo 10 vya kuhifadhi na kutoa huduma za zana za kilimo na ununuzi wa matrekta makubwa 553 na matrekta madogo (power tiller) 800. Hadi Aprili 2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa zao la pamba imenunua matrekta makubwa 500 na matrekta madogo (power tiller) 800 na inaendelea na taratibu za ukamilishaji wa vituo jumuishi 45 vya kutoa huduma za zana za kilimo katika mikoa ya Tanga, Tabora, Mwanza, Morogoro, Mtwara, Njombe, Lindi, Simiyu, Dodoma, Mbeya, Geita, Kilimanjaro, Arusha, Kagera na Kigoma. Pia, taratibu za usambazaji wa matrekta 500 na zana zake katika vituo hivyo unaendelea ili kuwawezesha wakulima wadogo kupata huduma za zana za kilimo kwa bei ya ruzuku.

126. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kushirikiana na sekta binafsi ambayo imeingiza nchini jumla ya matrekta makubwa 3,055 na matrekta madogo (power tiller) 4,401 kwa ajili ya kilimo.

Uingizaji huo, umeongeza idadi ya matrekta makubwa na madogo kufikia 28,693 na 23,315 mtawalia. Hatua hiyo, imechangia ongezeko la matumizi ya matrekta nchini kutoka asilimia 25 mwaka 2023/2024 hadi asilimia 26 mwaka 2024/2025 sawa na wastani wa matumizi ya trekta moja kwa hekta 500.



*Zana za kilimo zilizozinduliwa siku ya kufunga maonesho ya kilimo Nanenane Jijini Dodoma*

**Mikakati ya Kuongeza Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo**

**Zao la Pamba**

127. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania katika msimu wa kilimo wa 2024/2025 ilipanga kununua, kuchakata na kusambaza mbegu bora za pamba tani 28,000; chupa (acrepacks) 10,000,000 na vinyunyizi 100,000 kwa wakulima wa pamba; kununua ndege nyuki 40; mitambo mikubwa ya kunyunyizia viuatilifu 3,000; mitambo mitano (5) ya kuchimba mabwawa ya umwagiliaji; na mitambo 10 ya kuongeza thamani katika zao la pamba.

128. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi kwa kushirikiana na wadau ilipanga kujenga kiwanda cha vifaa tiba vinavyotumia pamba kama malighafi katika Wilaya ya Maswa; kujenga kiwanda kikubwa cha kusindika mafuta ya pamba katika Wilaya ya Bariadi; na kuendelea na mpango wa kujenga *serviced industrial park* kwa ajili ya uwekezaji na uongezaji thamani wa zao la pamba.

129. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania hadi kufikia Aprili 2025, imenunua, kuchakata na kusambaza kwa

wakulima mbegu bora za pamba tani 28,800, chupa (acrepacks) 10,000,000 na vinyunyizi 100,000 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 50.11 katika maeneo ya uzalishaji, ndege nyuki 60 na mitambo mikubwa 216 ya kunyunyizia viuatilifu (high presure boom sprayers) kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la pamba na kunyunyizia (Self propelled boom sprayers) kwenye mashamba makubwa ya pamba katika mikoa ya Simiyu, Shinyanga na Tabora.



*Ndege nyuki kwa ajili ya kunyunyizia Viuatilifu vya mazao.*

130. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi kwa kushirikiana na sekta binafsi imezalisha na kusambaza mbolea hai lita 408,000 kwa wakulima wa pamba kwa mpango wa ruzuku katika Wilaya ya Meatu ili kuongeza tija na uzalishaji. Vilevile, katika kuimarisha huduma za ugani katika zao la pamba, Bodi imewapatia wakulima wawezeshaji baiskeli 2,500 katika Kata na Vijiji ili kuwawezesha kuwafikia wakulima na kutoa elimu ya kilimo bora cha zao la pamba.

131. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi imesaini mkataba na Mkandarasi kwa ajili ya ununuzi wa mitambo mitatu (3) ya kuchimba mabwawa ya umwagiliaji kwa wakulima wa pamba kwa lengo la kuwawezesha wakulima wa zao la pamba kuongeza uzalishaji kupitia kilimo cha umwagiliaji. Vilevile, ujenzi wa kiwanda cha kusindika mafuta ya pamba chenye uwezo wa kusindika tani 600 kwa saa katika Wilaya ya Bariadi umekamilika na kimeanza uzalishaji. Aidha, Bodi imeainisha maeneo yanayopatikana katika Mkoa wa Shinyanga, Mwanza na Simiyu kwa ajili ya ujenzi wa *serviced industrial park* na uongezaji thamani wa zao la pamba. Pia, inaendelea kufanya tathmini ya ardhi kwa ajili ya kulipa fidia kwa wananchi watakaopisha ujenzi wa kongani hiyo. Pia, Serikali imelipa Shilingi 24,791,570,661 ya madeni ya wanunuzi wa pamba

ya mwaka 2019/2020 na kufanya jumla ya madeni yaliyolipwa hadi Aprili, 2025 kufikia Shilingi 60,280,109,504.40 dhidi ya deni lililohakikiwa la Shilingi 93,097,976,640.20. Aidha, deni liliobaki litaendelea kulipwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**Zao la Mkonge**

132. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania ilipanga kununua mashine ya kuchakata mkonge; kukarabati miundombinu ya shamba la Kibaranga - Tanga; kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 6,000; kuratibu usambazaji wa miche ya mkonge 3,000,000; na kutoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge kwa wadau 100,000 na Maafisa Ugani 500.

133. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge kwa kushirikiana na Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (NM – AIST) ilipanga kujenga kituo cha uzalishaji wa nzi chuma kwa kutumia mabaki ya mkonge ili kutengeneza protini; na kwa kushirikiana na watafiti kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), TARI, NM – AIST na Kampuni ya Carbonovia UK ya Oxford Uingereza kuzalisha protini kutokana na hewa ukaa.

134. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania hadi Aprili 2025, imenunua mashine ya kuchakata mkonge yenye uwezo wa kuchakata tani tatu (3) kwa siku itakayosimikwa katika kijiji cha Taula Wilaya ya Handeni. Vilevile, ukarabati wa mashine za kuchakata mkonge (dikotiketa) katika shamba la Kibaranga umefikia asilimia 70. Aidha, umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 3,000 umewezeshwa kwa wawekezaji 12 kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja katika Mkoa wa Morogoro.

135. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi imesambaza miche ya mkonge 84,000 katika maeneo ya uzalishaji na usambazaji unaendelea; imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la mkonge na fursa zitokanazo na zao hilo kwa wadau 6,067 na Maafisa Ugani 359 kutoka katika mikoa ya Tanga, Kilimanjaro, Pwani, Dodoma, Singida, Arusha, Shinyanga, Mara na Manyara.

136. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza thamani ya zao la mkonge, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa nzi chuma (Blacksoldier flies) kwa kutumia mabaki ya mkonge amepatikana na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na watafiti kutoka UDSM, TARI Mlingano, NM – AIST inaendelea kutafiti ili kuangalia uwezekano wa kuzalisha protini kutokana na mabaki ya mkonge itakayotumika katika kutengeneza chakula cha mifugo.

**Zao la Kahawa**

137. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania katika mwaka 2024/2025 ilipanga kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 48,000 na Maafisa Ugani 511; kuzalisha na kusambaza miche 20,000,000 ya kahawa; kuboresha mfumo wa ununuzi wa kahawa kuwa wa kidigiti; kushirikiana na wadau kuratibu na kushiriki Mkutano wa Tatu wa Kahawa Afrika (Third African Coffee Summitt); na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000.

138. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uzalishaji wa zao la kahawa, Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania hadi Aprili 2025, imezalisha na kusambaza miche 19,881,703 sawa na asilimia 99.4 ya lengo la kuzalisha miche 20,000,000 kwa wakulima katika mikoa ya Kagera, Kigoma, Iringa, Njombe, Ruvuma, Kilimanjaro, Tanga, Manyara, Songwe na Mbeya. Aidha, Bodi imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 5,831 na Maafisa Ugani 219. Vilevile, Bodi imeboresha mfumo wa ununuzi wa kahawa kuwa wa kidijiti ili kupunguza gharama kwa wanunuzi na kurahisisha malipo kwa wakulima wa kahawa. Pia, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 46.53 katika Wilaya ya Muleba Mkoa wa Kagera umefikia asilimia 35.

139. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi imeratibu Mkutano wa Tatu wa Kahawa Afrika uliofanyika Februari, 2025 Jijini Dar es Salaam ambapo wanachama waliridhia na kupitisha Azimio la Dar es Salaam ambalo linasisitiza uongezaji thamani wa zao la kahawa

barani Afrika. Vilevile, Shirika la *Inter African Coffee Organisation* - IACO limeahidi kujenga Kituo cha Umahiri cha Maendeleo ya Kahawa Jijini Dodoma na Kituo cha Utafiti wa Kahawa barani Afrika nchini Tanzania.




*Mkutano wa nchi 25 zinazozalisha zao la kahawa Barani Afrika (G25 COFFEE SUMMIT)*

**Zao la Chai**

140. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuwezesha upatikanaji wa hati ya Kimataifa kwa ajili ya uendeshaji wa mashamba ya Kilolo na Lupembe; kutoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha chai kwa wakulima wadogo wa chai 32,000; kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya chai ya wakulima wadogo; kuanzisha maeneo mapya kwa ajili ya uzalishaji wa mashamba ya chai; na kuanzisha viwanda viwili (2) vya kusindika chai.

141. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, katika kuimarisha Tasnia ya chai, kiwanda kilichoanzishwa wakati wa J. K. Nyerere na baadae kufa, kimepata mwekezaji (Kampuni ya Hong Din Xin Investment Limited) kwa ajili ya kuendeleza kiwanda hicho cha kuchakata chai maalum (Othodox Tea) chenye uwezo wa kuchakata tani 20 kwa siku kilichopo katika Wilaya ya Kilolo. Vilevile, Bodi imenunua mashine mbili (2) za kuchanganya chai zenye uwezo wa kuchanganya tani moja (1) za chai kwa saa kila moja. Mashine hizo, zitasimikwa kwenye ghala la Kipawa Jijini Dar es Salaam na Halmashauri ya Korogwe (Tanga) kwa ajili ya wakulima wadogo wa zao la chai.

142. ***Mheshimiwa Spika,*** zabuni kwa ajili kumpata mkandarasi wa ujenzi wa viwanda viwili (2) vya kusindika chai kati ya lengo la kuanzisha viwanda saba (7) nchini imetangazwa. Pia, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vidogo viwili (2) vya kuchanganya chai nchini amepatikana. Pia, Serikali imeanza kubadili mfumo wa wakulima wadogo kuuza chai ya majani mabichi na kuanza kuuza chai nyeusi.

143. ***Mheshimiwa Spika,*** zabuni kwa ajili ya kumpata mkandarasi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya chai ya wakulima wadogo katika Mkoa wa Njombe yenye ukubwa wa hekta 1,000 imetangazwa. Vilevile, maeneo mapya matatu (3) yaliyopo katika Halmashauri za Kilolo, Korogwe na Lushoto yameanzishwa kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya chai ambapo miche 1,500,000, 1,000,000 na 500,000 imezalishwa katika maeneo hayo mtawalia.

144. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi imeendelea kutoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha zao la chai kwa wakulima wadogo wa chai 17,041 na kuwezesha upatikanaji wa hati ya Kimataifa (Ithibati) ya *Rain Forest Alliance* kwa ajili ya uendeshaji wa mashamba ya chai yaliyopo Lupembe kwa wakulima 4,041. Aidha, mzabuni kwa ajili ya kusambaza mashine ya kuchakata chai nyeusi amepatikana na zabuni ipo katika hatua ya kusaini mkataba kati ya Bodi ya Chai Tanzania na Kampuni ya *Colmat General Supplies Co. Ltd*.

**Zao la Tumbaku**

145. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuhamasisha wakulima kujenga na kuboresha mabani ya kukaushia tumbaku; kuanzisha mashamba mawili (2) ya mfano; kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa Maafisa Ugani, kukamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa katika ofisi ya Bodi iliyopo Tabora na kuanza ujenzi wa ofisi mpya za Bodi katika Wilaya za Urambo, Kaliua, Sikonge na Songea; na kuratibu upatikanaji wa tani 127,316 za mbolea, viuatilifu lita 236,329 na pakiti 1,664,286, vifungashio belo 11,709 na nyuzi kilo 166,429 kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa tumbaku.

146. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania hadi kufikia Aprili 2025, imeendelea kuratibu uzalishaji wa zao la tumbaku kwa kutoa mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku, kujenga na kuboresha mabani ya kukaushia tumbaku kwa wakulima 88,762. Vilevile, imeanzisha shamba la mfano lenye ukubwa wa hekta 40 katika Wilaya ya Mvomero kwa ajili ya wakulima kujifunza kukausha tumbaku kwa kutumia jua. Pia, imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa Maafisa Ugani 500 katika maeneo ya uzalishaji.

147. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuongeza uzalishaji wa tumbaku Bodi ya Tumbaku imesambaza kwa wakulima tani 124,771.05 za mbolea, viuatilifu lita 72,418, chupa 1,627,839, pakiti 772,913 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 7.69, vifungashio (magunia 1,242,126 na Jute Twine kilo 383,220) na nyuzi kilo 84,301.5 vyenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.3 kwa mpango wa ruzuku. Vilevile, katika kupunguza matumizi ya kuni na kutunza mazingira mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa mabani ya kisasa 573 katika Halmashauri 25 amesaini mkataba wa ujenzi. Pia, ujenzi wa ofisi mpya ya Bodi katika Wilaya ya Urambo umekamilika na ujenzi wa Ofisi ya Bodi iliyopo katika Manispaa ya Tabora umefikia asilimia 95.

**Zao la Korosho**

148. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania katika mwaka 2024/2025, ilipanga kununua na kusambaza viuatilifu vya korosho tani 30,000 za *sulphur* na lita 3,800,000 za viuatilifu vya maji; kuzalisha miche 1,000,000; kuanzisha kitalu cha Taifa cha uzalishaji wa miche ya korosho; kuzalisha mbegu tani 100; kusajili wakulima na kutambua mashamba yao; kubadili mfumo wa kuuza korosho; kutoa mafunzo kwa wakulima 1,300 na Maafisa Ugani 300; kuandaa mashamba darasa 15 ya korosho; kuendelea na ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho pamoja na kuongeza thamani na viwanda vingine vya mazao ya mafuta; na kukamilisha ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000 za korosho.

149. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania imenunua viuatilifu vya korosho tani 29,408.03 za *Sulphur* na lita

2,689,581 za viuatilifu vya maji vyenye jumla ya thamani ya Shilingi 208,902,762,216.95 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la korosho. Aidha, tani 41,263 za *Sulphur* ya unga na lita 2,689,581 za viuatilifu vya maji vimesambazwa kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na usambazaji unaendelea.

150. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi kwa kushirikiana na TARI imezalisha miche 1,300,000 ya korosho na mbegu za korosho tani 11.51 na kusambaza kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, katika kuimarisha uzalishaji wa miche ya korosho TARI imeanzisha kitalu cha Taifa cha uzalishaji wa miche hiyo katika kituo cha TARI Naliendele. Pia, Bodi imesajili wakulima 598,246 na kutambua mashamba yao ili kurahisisha utoaji wa huduma za ugani.

151. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha mfumo wa uuzaji wa zao la korosho, Wizara kwa kushirikiana na wadau imeratibu matumizi ya mfumo wa Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) katika msimu wa mauzo kwa mwaka 2024/2025 kupitia Vyama vya Ushirika na Stakabadhi ya Ghala na kuwezesha bei ya juu kufikia Shilingi 4,195 na bei ya chini Shilingi 1,110. Hatua hiyo, imewezesha kuongeza uwazi, mapato na faida kwa wakulima ambapo tani 406,362 zimeuzwa zenye thamani ya Shilingi 1,461,679,068,453.50.

152. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha korosho inayozalishwa inabanguliwa nchini, Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania imelipia fidia ya Shilingi 635,211,217.70 ya eneo lenye ukubwa wa ekari 1,572 kwa wakulima 387 kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa kongani ya korosho. Vilevile, Bodi imeendelea kuratibu ujenzi awamu ya kwanza wa kongani la viwanda vya kubangua na kuongeza thamani mazao ya korosho katika eneo la ekari 354 Maranje katika Halmashauri ya Nanyamba ambapo ujenzi umefikia asilimia 50. Aidha, mwekezaji (Kampuni ya Mateak Holdings Ltd) atakayejenga kiwanda chenye uwezo wa kubangua korosho ghafi tani 100,000 kwa mwaka amepatikana.

153. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha ujenzi wa viwanda vya kubangua na kuongeza thamani mazao ya korosho, Bodi imechimba kisima kimoja (1); inajenga ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 10,000 kila moja; na imekamilisha ujenzi wa miundombinu ya umeme. Vilevile, ujenzi wa barabara na uzio

unaendelea. Aidha, katika kuimarisha uhifadhi wa korosho, Bodi imekamilisha ujenzi wa ghala lenye uwezo wa kuhifadhi tani 3,000 za korosho katika Wilaya ya Manyoni katika Mkoa wa Singida.



*Shughuli za ubanguaji wa korosho cha Chama Kikuu cha Ushirika cha Tandahimba na Newala (TANECU) zikiendelea katika kiwanda cha kubangua korosho kilichopo Mtwara*

**Zao la Pareto**

154. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA katika mwaka 2024/2025, ilipanga kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima 10,500 na wakaguzi wa pareto 25; kuratibu usambazaji wa mbegu bora kilo 5,300; kujenga makaushio 100 katika maeneo ya uzalishaji; na kuratibu vituo 450 vya ukaguzi wa pareto.

155. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto yametolewa kwa wakulima 16,000 na wakaguzi wa pareto 25 katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Manyara na Arusha. Vilevile, mbegu bora kilo 900 zimesambazwa kwa wakulima 3,500 katika mikoa ya Manyara, Arusha, Mbeya na Songwe na usambazaji unaendelea.

156. ***Mheshimiwa Spika***, ukaguzi umefanyika katika vituo 200 vya pareto katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Njombe, Iringa, Manyara na Arusha na kubaini kuwa vituo 40 havijakidhi vigezo vya kununua maua ya pareto na hivyo kupatiwa mafunzo kuhusu vigezo muhimu kwa ajili ya ununuzi wa maua ya pareto. Pia, ujenzi wa makaushio 100 katika Wilaya za Mbeya (25), Makete (20),

Ludewa (10), Ileje (20), Arusha (10) na Mbulu (15) umefikia wastani wa asilimia 80.

**Zao la Kakao**

157. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2024/2025, Wizara kwa kushirikiana na wadau wa kakao ilipanga kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima na Maafisa Ugani; Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa kushirikiana na wadau kuendelea kufanya maboresho ya mfumo wa uendeshaji wa minada; na kuendelea kutoa elimu ya masoko na fedha kwa wanachama na wakulima 100,000 wa kakao.

158. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia COPRA imetoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha kakao kwa wakulima 274 na Maafisa Ugani 30 katika Halmashauri za Kyela, Rungwe, Busokelo, Mlimba na Mvomero. Vilevile, kwa kushirikiana na wadau, maboresho ya mfumo wa uendeshaji wa minada umefanyika na kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa kufanya minada ya kidijiti kupitia Soko la Bidhaa Tanzania (TMX).

159. ***Mheshimiwa Spika***, hatua hiyo imewezesha jumla ya tani 11,362.40 za kakao zenye thamani ya Shilingi 213,330,436,629.10 kuuzwa kupitia mfumo huo kwa wastani wa bei ya Shilingi 18,775.12 kwa kilo ikilinganishwa na wastani wa bei ya Shilingi 4,869.27 kwa kilo mwaka 2022/2023. Pia, Tume ya Maendeleo ya Ushirika imetoa elimu ya masoko na fedha kwa wanachama na wakulima 88,951 wa kakao sawa na asilimia 88.95 ya lengo la wakulima 100,000 ili kuwawezesha wakulima hao kupata mikopo kwenye taasisi za fedha nchini.

**Mazao ya Bustani**

160. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia COPRA kwa kushirikiana na wadau imewezesha wakulima kuzalisha tani 7,518,560.84 za mazao ya bustani katika mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 83.54 ya lengo la kuzalisha tani 9,000,000. Uzalishaji huo umefikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kilimo bora cha mazao ya bustani kwa Maafisa Ugani 250 na wakulima 1,200 katika maeneo ya uzalishaji.

161. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara imefanya tathmini ya awali kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa hekta 949 kwa ajili ya kilimo cha biashara cha migomba katika Wilaya ya Rombo. Aidha, taratibu za kuanzisha mashamba hayo zinaendelea.

**Zao la Parachichi**

162. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia COPRA kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuratibu uzalishaji wa parachichi nchini, ambapo mauzo ya parachichi nje ya nchi yameongezeka kutoka tani 26,826.3 kwa mwaka 2022/2023 hadi tani 35,627.02 kwa mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 118.76 ya lengo la kuzalisha tani 30,000. Kadhalika, katika kuimarisha upatikanaji wa miche ya parachichi, Wizara kupitia TARI imezalisha na kusambaza miche 569,500 ya parachichi kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku.

163. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ubora, uzalishaji na uwezo wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika zao la parachichi, Wizara inaendelea na uwekezaji wa miundombinu ya umwagiliaji ikiwemo uchimbaji wa visima kwa wakulima wa parachichi katika Mkoa wa Njombe. Pia, vifaa viwili (2) vya kupima ubora wa parachichi (dry matter machine) zimenunuliwa ili kupima ubora wa parachichi zinazozalishwa na wakulima kabla ya kuuza kwa ajili ya kulinda soko la zao hilo ndani na nje ya nchi. Aidha, katika kuhakikisha uzalishaji wenye tija wa zao la parachichi, TARI kwa kushirikiana na kiwanda cha ITRACOM inaendelea na utafiti wa mbolea zinazofaa kwa uzalishaji wa zao hilo.

**Mazao yenye mahitaji makubwa**

164. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa mazao yenye mahitaji makubwa ambayo ni ngano, miwa na mazao ya mafuta yanayoagizwa kutoka nje ya nchi.

**Zao la Ngano**

165. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025, ilipanga kuzalisha ngano tani 150,000; kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za ngano tani 18,000; kuzalisha tani 864 za mbegu za Msingi; kuwezesha uwekezaji katika mashamba ya West Kilimanjaro na

Hanang; na TARI kutoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500.

166. ***Mheshimiwa Spika***, ilipanga kukamilisha taratibu za kuchukua mashamba yaliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina na kuyakabidhi kwa wazalishaji; kutambua na kupima maeneo yenye ukubwa wa hekta 20,000 yanayofaa kwa kilimo cha ngano nchini; kujenga miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu za ngano; na kutafiti mbegu za ngano zenye kukidhi sifa za mahitaji ya soko na tija katika uzalishaji.

167. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeendelea kuimarisha uzalishaji wa ngano nchini kwa kuongeza upatikanaji wa mbegu bora za ngano kufikia tani 1,274.4 na TARI imezalisha mbegu za msingi tani 100.3 kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora. Vilevile, Wizara kupitia COPRA imeingia makubaliano ya hakikisho la ununuzi wa ngano na kampuni sita (6) zinazohusika na usambazaji, usindikaji na uchakataji wa zao la ngano nchini ili kununua ngano yote itakayozalishwa na wakulima kabla ya kuagiza kutoka nje ya nchi.

168. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI imeendelea na utafiti wa mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko na tija katika uzalishaji. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye mashamba ya utafiti na uzalishaji wa mbegu za ngano yenye ukubwa wa hekta 120 umefikia asilimia 30. Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu hiyo kutaiwezesha TARI kutafiti na kuzalisha mbegu za ngano bila kusubiri mvua za masika na hivyo kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora.

169. ***Mheshimiwa Spika,*** katika jitihada za kuongeza eneo kwa ajili ya uzalishaji wa ngano, Wizara imeomba mashamba yaliyo chini ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ili iweze kuyakabidhi kwa wazalishaji.

**Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari**

170. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 kupitia Bodi ya Sukari Tanzania, ililenga kuhakikisha uzalishaji wa zao la miwa unafikia tani 5,200,000 zitakazozalisha sukari tani 520,000;

kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya Dakawa; kusimamia upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera; kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero; kuzalisha miche ya miwa 2,520 kwenye mashamba yenye ukubwa wa hekta 56; na kuanzisha vitalu vya mbegu za miwa katika eneo la ekari 20 katika bonde la Kilombero.

171. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa zao la miwa ambapo uzalishaji wa miwa umeongezeka kutoka tani 4,215,555.27 zilizozalisha sukari tani 395,292.55 mwaka 2023/2024 hadi kufikia takriban tani 4,713,907.89 mwaka 2024/2025 iliyozalisha sukari tani 431,736.74 sawa na ongezeko la asilimia 9.22.

172. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali imeendelea kuhamasisha uwekezaji katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari ambapo viwanda vya sukari vya Mkulazi na Bagamoyo vimeanza uzalishaji. Hadi kufikia Aprili 2025, uzalishaji katika viwanda vya Mkulazi na Bagamoyo umefikia tani 19,124 sawa na asilimia 95.6 ya lengo la tani 20,000 na tani 16,556 sawa na asilimia 47.3 ya lengo la tani 35,000 mtawalia.

173. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania imeendelea kutengeneza mtambo wa kutibu mbegu za miwa (hot water treatment plant) na ujenzi wa kiwanda kidogo cha sukari ambapo hadi Aprili 2025, utekelezaji umefikia asimilia 99 na 80 mtawalia. Aidha, ili kuongeza eneo linalolimwa miwa, Bodi imeratibu upanuzi wa mashamba ya miwa ya *Mtibwa Sugar Estate* katika eneo lenye ukubwa wa hekta 4,900 sawa na asilimia 40.8 ya lengo la hekta 12,000 zinazofaa kwa kilimo cha miwa na upanuzi unaendelea.

174. ***Mheshimiwa Spika***, upanuzi wa mashamba ya miwa ya Dakawa yaliyochini ya Kiwanda cha Mtibwa umefanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekta 4,700 na upanuzi unaendelea. Aidha, upanuzi wa mashamba ya miwa ya kiwanda cha sukari Kagera umefanyika katika eneo lenye ukubwa wa hekta 9,592 sawa na asilimia 73.7 ya lengo la hekta 13,000 na upanuzi

unaendelea; upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero umefikia asilimia 92.9; na usimikaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba lenye ukubwa wa hekta 100 kwenye mashamba ya pamoja ya wakulima wadogo Kilombero umefikia asilimia 42.

175. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI kwa kushirikiana na wakulima imepanda miche ya miwa katika shamba lenye ukubwa wa hekta 22.7 katika mikoa ya Kagera (hekta 12.3) na Morogoro (hekta 10.4) inayotarajiwa kuzalisha tani 2,240 za mbegu bora za miwa.

176. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, TARI imepanda miche ya miwa katika eneo lenye ukubwa wa hekta 8.1 (Kilombero hekta 4.05 na Mkulazi hekta 4.05), eneo hilo linatosha kuzalisha mbegu tani 800 ambazo zinatosha kupanda hekta 64.8 za mashamba ya wakulima wadogo. Pia, mafunzo ya kanuni za kilimo bora cha miwa yametolewa kwa wakulima 150 kupitia maonesho na makongamano mbalimbali kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa miwa.

**Mazao ya Mafuta**

177. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kutoka tani 2,143,098.70 mwaka 2022/2023 hadi kufikia tani 2,200,000 kwa kuwezesha upatikanaji wa mbegu bora za alizeti tani 5,000 na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku; kuzalisha na kusambaza mbegu bora za karanga tani 150 na mbegu za ufuta tani 150; kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 2,000,000 kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji; kuzalisha mbegu za ufuta tani 108; kutoa mafunzo ya kilimo bora cha zao la ufuta kwa wakulima 2,000 na Maafisa Ugani 500; na kuandaa mashamba ya mfano 105.

178. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara imeendelea kuratibu uzalishaji wa mazao ya mafuta nchini ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka tani 2,143,098.70 mwaka 2022/2023 hadi tani 2,181,747.65 mwaka 2023/2024 sawa na asilimia 99 ya lengo la kuzalisha tani 2,200,000. Vilevile, Wizara imesambaza mbegu bora za alizeti tani 700 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Mbegu bora za karanga tani 72.89 na ufuta tani 23.48 zimezalishwa na kusambazwa kwa

wakulima katika maeneo ya uzalishaji ili kuimarisha upatikanaji wa mbegu na kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula.

179. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeratibu uzalishaji na usambazaji wa miche ya chikichi 636,415 kwa wakulima katika mikoa ya Kigoma, Rukwa, Mtwara, Kagera, Pwani, Geita, Morogoro na Tanga ili kuimarisha uzalishaji wa chikichi na kuongeza uzalishaji wa mafuta ya kula nchini. Pia, TARI imeandaa mashamba yenye ukubwa wa hekta 80.9 yenye uwezo wa kuzalisha mbegu za ufuta tani 50 kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu za zao hilo.

**4.1.10 Kuendeleza Kanda za Kilimo na Uzalishaji**

180. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 imeanzisha Kanda nne (4) za Kuendeleza Kilimo Tanzania kupitia shoroba za Kilimo (Agriculture Growth Corridor of Tanzania - AGCOT), zilizozinduliwa na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb.), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 27 Aprili, 2025. Kanda hizo, zitasimamiwa na Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo (Agriculture Transformation Office - ATO) na Serikali itatenga fedha ili kuwezesha shoroba hiyo. Pia, zitaimarisha uzalishaji na tija, masoko ya mazao ndani na nje ya nchi, mitaji, kuongeza thamani ya mazao ya kilimo na upatikanaji wa pembejeo. Kanda hizo ni Kanda ya Kati, Kanda ya Kusini, Kanda ya Mtwara na Kanda ya Kaskazini.




*Shoroba nne (4) za Kilimo Tanzania.*

**4.2 Kuongeza Ajira zenye Staha na Ushiriki wa Vijana na Wanawake kwenye Kilimo**

181. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika kuhakikisha upatikanaji wa ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo imeendelea na utekelezaji wa Programu ya Jenga Kesho

Iliyobora (Building a Better Tommorrow – BBT) inayotekelezwa kupitia miradi mitano (5) ambayo ni Mashamba Makubwa ya Pamoja; Upatikanaji wa mitaji kwa vijana na wanawake; Huduma za Ugani; Uongezaji thamani ya mazao ya kilimo; na kuwezesha upatikanaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo.

**Mashamba Makubwa ya Pamoja (Block Farms) Shamba la Chinangali**

182. ***Mheshimiwa Spika,*** katika Utekelezaji wa Mradi wa Mashamba Makubwa ya Pamoja, Wizara imeendelea na Uwekezaji katika shamba la pamoja ya Chinangali lenye ukubwa wa ekari 1,772 ambalo lina jumla ya vijana 261 (Ke 105, Me 156). Vijana hawa wamekabidhiwa kila mmoja ekari 5 na wanaendelea na shughuli za uzalishaji chini ya Chama chao cha Ushirika cha BBT Chinangali AMCOS LTD chenye usajili Na. PRI-DOM-CHM-DC-2023-6213.

183. ***Mheshimiwa Spika,*** katika msimu wa pili (2024/2025) vijana wa BBT Chinangali wanafanya uzalishaji kama ifuatavyo: Uzalishaji wa mbegu ya Alizeti aina ya RECORD katika eneo la ekari 550 kwa makubaliano na Wakala wa mbegu za Kilimo (ASA); Uzalishaji wa pilipili aina ya Loleza katika eneo la ekari 20; Uzalishaji wa mbegu ya Mtama (Masia) katika eneo la ekari 20; na Uzalishaji wa mazao ya bustani ikiwemo matango na hoho za rangi kwa kutumia vitalu nyumba vitano (5).

184. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa awamu ya kwanza, kazi ya uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone unaendelea katika eneo la ekari 220 kati ya ekari 1,772 na umefikia asilimia 80 ambapo visima vitano (discharge 8,000 – 30,000/ saa) vimechimbwa; ujenzi wa bwawa lenye ujazo wa lita 27,000,000 limekamilika; na *pump house* 1 imejengwa. Pia, ujenzi wa vitalu nyumba vitano (5) kwa ajili ya kuzalisha mazao ya bustani na miche ya mbogamboga umekamilika.

185. ***Mheshimiwa Spika,*** awamu ya pili inayohusisha ufungaji wa miundombinu ya umwagiliaji (center pivot) katika eneo la ekari 1,552 unaendelea; visima vinne (4) kati ya 29 vimechimbwa; ujenzi wa bwawa 1 kati ya 2 umefanyika; na ujenzi wa uzio katika

shamba umefikia asilimia 89. Pia, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa kutoa maji katika bwawa la Hombolo kwa ajili ya umwagiliaji katika mashamba ya Chinangali unaendelea.

**Shamba la Mlazo/Ndogowe**

186. ***Mheshimiwa Spika,*** Shamba la Mlazo/Ndogowe lina jumla ya ekari 11,453 ambapo jumla ya ekari 5,700 zimeandaliwa kwa awamu ya kwanza na vijana 342 wameanza uzalishaji katika msimu wa kilimo 2024/2025. Aidha, kila kijana amepewa shamba lenye ukubwa wa ekari 10 kwa ajili ya uzalishaji chini ya Chama chao cha Ushirika cha BBT Ndogowe AMCOS LTD chenye usajili Na. PRI-DOM-CHM-DC-2025-6983.

187. ***Mheshimiwa Spika,*** uwekezaji wa miundombinu ikiwemo ya umwagiliaji katika shamba hili unaendelea. Ujenzi wa nyumba 53 umekamilika na nyumba saba (7) umefikia wastani wa asilimia 92. Aidha, kati ya ekari 11,453, ekari 5,700 tayari zimesafishwa ambapo ekari 4,200 kati ya hizo ni za vijana na inahusisha miundombinu ya shamba ikiwemo ghala na barabara za shambani. Vilevile, ekari 1,000 zimekabidhiwa kwa Serikali ya Vijiji vya Mlazo na Ndogowe ikiwa ni mpango wa kuhakikisha wananchi wanafaidika na miradi inayotekelezwa katika maeneo yao. Ekari 2,500 amepewa Mwekezaji (Kampuni ya Longping Agriscience Tanzania Ltd) ambaye tayari ameanza uwekezaji, na atakuwa na jukumu la kutoa huduma ya teknolojia na soko kwa vijana na wakulima katika shamba hilo.

188. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha miundombinu ya umwagiliaji, uchimbaji wa visima 11 umefanyika na ufungaji wa pampu kwa ajili ya kupeleka maji kwenye mabwawa (reseviour) umefikia asilimia 89. Kazi ya ujenzi wa mabwawa 8 (reservoir) zipo katika hatua ya kuweka *damliner* na umefikia asilimia 93. Usimikaji na utandazaji wa mfumo wa umwagiliaji umefikia asilimia 65 na mtandao wa barabara za mashambani zenye urefu wa kilomita 18.6 zinaendelea kujengwa ambapo ujenzi wa *calvate* na *drainage system* unaendelea. Pia, usimikaji wa miundombinu ya umeme na minara ya mawasiliano umekamilika.

**Shamba la Mapogoro (Chunya - Mbeya)**

189. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kutekeleza programu ya mashamba makubwa ya pamoja katika Mkoa wa Mbeya, Serikali imesaini makubaliano ya kupokea fedha kiasi cha Dola za Marekani Milioni 129 kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika kwa ajili ya kuanza kutekeleza mradi wa Mapogoro kwa kuanzia na hekta 20,000. Hadi Aprili 2025, Wizara imekamilisha upimaji wa afya ya udongo na kufanya utafiti wa maji chini ya ardhi katika shamba hilo. Pia, imefanya tathmini ya athari za mazingira na kijamii katika mradi na kupata hati za umiliki wa shamba.

**Mashamba ya pamoja ngazi ya Halmashauri**

190. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya BBT katika ngazi ya Halmashauri ambapo utekelezaji umehusisha upimaji wa afya ya udongo; upatikanaji wa hati za umiliki; usafishaji wa mashamba; na ekari 148,563.91 zimetengwa katika mikoa tisa (9) ya Kagera, Mbeya, Dodoma, Njombe, Kigoma, Singida, Mara, Tabora na Pwani.

**Upatikanaji wa mitaji kwa vijana na** *wanawake*

191. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia AGITF katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuongeza mikopo yenye riba nafuu kufikia Shilingi Bilioni 10; kusimamia AGITF na TADB kukamilisha makubaliano ya mashirikiano (MoU) ili kutumia mifumo ya dhamana kuzisaidia taasisi za fedha ziweze kuwakopesha vijana kwa kutumia dhamana zitakazosimamiwa na TADB; na kukamilisha majadiliano na IFAD kwa ajili ya kuanzisha mradi wa upatikanaji wa mitaji wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 40.

192. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa kupitia AGITF mikopo yenye riba nafuu isiyozidi asilimia 4.5 kwa vijana na wanawake waliopo kwenye shughuli za kilimo na uongezaji thamani mazao imeongezeka kutoka Shilingi Bilioni 2 mwaka 2023/2024 hadi Shilingi Bilioni 5.7 mwaka 2024/2025 sawa na asilimia 57 ya lengo la Shilingi Bilioni 10. Aidha, mikopo yenye thamani ya Shilingi Milioni 503.5 imetolewa kwa wanufaika 49 (vijana na wanawake).

193. ***Mheshimiwa Spika,*** AGITF na TADB zimesaini hati ya makubaliano (MoU) ya kutumia mifumo ya dhamana ili kuzisaidia taasisi za fedha ziweze kuwakopesha vijana kwa kutumia dhamana zitakazosimamiwa na TADB. Pia, maombi 1,546 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 21.3 kwa ajili ya mikopo kwa vijana na wanawake yamepokelewa na yapo kwenye hatua mbalimbali za kutolewa.

194. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha kupitia Mradi wa BBT project 1 unaofadhiliwa na AfDB inakamilisha majadiliano ya Dola za Marekani Milioni 35 kwa ajili ya dhamana na mikopo yenye riba nafuu kwa Vijana na Wanawake. Aidha, tathmini itafanyika kwa ajili ya kuona uwezekano wa AGITF kutoa huduma hiyo kupitia Benki ya Ushirika Tanzania.

**Mradi wa Huduma za Ugani (BBT – Ugani)**

195. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha utoaji wa huduma za ugani nchini, Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), sekta binafsi na bodi za mazao ilipanga kutekeleza mradi wa huduma za ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) kwa kuajiri vijana 300. Kupitia mradi huo, Serikali kwa kushirikiana na wadau inaajiri wahitimu wa ngazi ya stashahada na shahada katika fani za kilimo na kuwapatia mafunzo maalum ili waweze kutoa huduma za ugani kwa wakulima.

196. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, jumla ya wahitimu wa vyuo vya kilimo 1,261 wamepata ajira ya kutoa huduma za ugani kwa wakulima. Kati ya hao, vijana 761 wanatoa huduma za ugani katika zao la pamba na vijana 500 katika zao la korosho. Pia, kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania imeajiri vijana 108 kwa ajili ya kufundisha wakulima. Vilevile, Bodi ya Tumbaku Tanzania imeanzisha shamba darasa kwa vijana 20 katika eneo lenye ukubwa wa ekari 100 lililopo Dakawa katika Halmashauri ya Mvomero ili kutoa mafunzo kwa vitendo.



*Baadhi ya vijana walioajiriwa katika zao la Pamba.*

**Mradi wa Visima katika ngazi ya Halmashauri**

197. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 imeendelea kutekeleza mradi wa visima kwa wakulima wadogo kwa lengo la kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara imebainisha maeneo ya kuchimba visima 39 kwa ajili ya umwagiliaji vinavyotarajiwa kunufaisha wakulima wakiwemo vijana zaidi ya 1,100. Vilevile, imetangaza zabuni kwa ajili ya kununua unit 250 za pampu, jenereta na mipira kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwa wakulima waliopo kandokando ya Ziwa Victoria. Mradi huo unatarajiwa kunufaisha wakulima 10,000. Aidha, uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji katika shamba lenye ukubwa wa ekari 21 kwa wakulima 17 katika Kijiji cha Manchali kilichopo Halmashauri ya Chamwino umekamilika.

198. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imetangaza zabuni kwa ajili ya kununua unit 250 za pampu, jenereta na mipira kwa ajili kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yenye vyanzo vya maji. Aidha, mikataba ya ujenzi wa miradi midogo ya umwagiliaji (Community Irrigation) katika eneo lenye ukubwa wa ekari 4,000 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 12.68 inatekelezwa katika majimbo 62 na Halmashauri 58. Aidha, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imenunua mitambo 17 ya uchimbaji wa visima. Pia, Tume imeanza uchimbaji wa visima 127 kwa kutumia wachimbaji wa ndani katika mikoa 16 ya Lindi, Mtwara, Pwani, Tanga, Dodoma, Manyara, Singida,

Morogoro, Mara, Simiyu, Kagera, Geita, Kigoma, Ruvuma, Njombe na Songwe.

**Mradi wa Uongezaji Thamani ya Mazao**

199. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kutekeleza Programu ya BBT kupitia mradi wa uongezaji thamani ya mazao ambapo kupitia Bodi ya Mkonge imeanzisha Kituo Atamizi cha BBT Mkonge katika Mkoa wa Tanga ili kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye mahitaji maalum kuzalisha bidhaa mbalimbali kwa kutumia singa za mkonge. Mradi huo unahusisha pande mbili (2) za Muungano za Tanzania Bara na Zanzibar.

200. ***Mheshimiwa Spika,*** vijana 344 wanaendelea na mafunzo kwenye vituo atamizi katika Mkoa wa Tanga na Zanzibar kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa uongezaji thamani wa zao la mkonge. Aidha, tani 9 za singa zimetolewa kwa vijana hao ambapo tani 4 zimetumika kwa ajili ya kutengeneza bidhaa mbalimbali za utalii. Mradi huo, unasaidia Serikali kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira hasa kwa makundi ya wanawake na vijana, kuinua hali za kimaisha na kipato cha familia husika na kuongeza matumizi ya mkonge ndani ya nchi na hivyo kukuza soko la ndani la mkonge.

201. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, mashine 66 zenye uwezo wa kubangua korosho kilo 20 kwa siku kwa kila moja zimesambazwa katika vikundi 12 vya wakulima katika maeneo ya uzalishaji wa korosho. Pia, mikopo mitano (5) yenye thamani ya Shilingi 104,725,000 imetolewa na AGITF kwa vijana na wanawake kwa ajili ya usindikaji wa mazao ya mahindi, mpunga na alizeti.

**4.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe**

202. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ilipanga kuwekeza kwenye miundombinu ya uhifadhi wa chakula; kuiongezea NFRA uwezo wa kuhifadhi chakula; kuimarisha usimamizi wa mazao ya nafaka na mazao yasiyo ya nafaka; na kuhamasisha uzalishaji na matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

**4.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi**

203. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, ujenzi wa ghala 28 zenye uwezo wa

kuhifadhi tani 1,000 kila moja katika Mkoa wa Ruvuma umekamilika. Aidha, mkandarasi kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa miundombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 amepatikana. Vilevile, mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ghala 10 zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 95,000 amekabidhiwa eneo kwa ajili ya kuanza kazi katika mikoa ya Morogoro (ghala 3), Tabora (ghala 1), Shinyanga (ghala 1), Rukwa (ghala 3), Manyara (ghala 1) na Dodoma (ghala 1).

204. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi hiyo ikikamilika itaongeza uwezo wa NFRA wa kuhifadhi kufikia tani 1,036,000 ambayo ni sawa na asilimia 34.53 ya lengo la kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo 2030.

#### 4.3.2 Kuiongezea NFRA uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili kuongeza Hifadhi ya Chakula

205. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia NFRA ilipanga kununua tani 1,150,000 za nafaka kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula nchini; kuuza chakula kwa maombi maalum na kutoa chakula cha msaada pale itakapohitajika ndani na nje ya nchi; na kukamilisha majadiliano na Benki ya NBC kuanzisha Hati Fungani ya Usalama wa Chakula.

206. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, NFRA imenunua tani 444,440.95 za nafaka (mahindi tani 407,727.089, mpunga tani 28,511.394, dengu tani 2,018.579 na mbaazi tani 6,183.885) kwa lengo la kumhakikishia mkulima soko, kulinda uchumi na kuisaidia nchi kufanya biashara. Ununuzi huo, umewezesha kuongezeka kwa hifadhi ya chakula na kufikia jumla ya tani 776,000. Aidha, ili kumlinda mkulima NFRA ilinunua mpunga kwa bei ya wastani wa Shilingi 900 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya soko ya wastani wa Shilingi 600 kwa kilo na mahindi ilinunua kwa bei ya wastani wa Shilingi 700 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya soko ya wastani wa Shilingi 450 kwa kilo.

207. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia NFRA imeuza tani 195,000 za nafaka katika nchi ya Zambia; tani 10,904 nchini Malawi; na tani 35,000 kwa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (The World Food Programme - WFP) na kuipatia mapato ya Dola za Marekani 89,275,124. Aidha, NFRA na benki ya NBC itazindua hati Fungani ya Usalama wa Chakula (Food security bond) yenye thamani ya

Shilingi 463,823,435,500. Hati fungani hiyo itahusisha wadau wa ndani na nje ya nchi.

**4.3.3 Kuimarisha Usimamizi wa Mazao ya Nafaka na Yasiyo Nafaka**

208. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kutekeleza jukumu la msingi la kusimamia mazao ya nafaka na yasiyo nafaka, Wizara ilifanya marekebisho ya Sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka 1991 kupitia Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya Mwaka 2009. Marekebisho hayo yalianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA) na kuipa majukumu mbalimbali yakiwemo utoaji wa vibali vya kusafirisha mazao, kuandaa kanuni za kuwezesha biashara za mazao ya kilimo; kusajili ghala, masoko na wafanyabiashara, kutoa mafunzo kwa wadau na kushirikiana na WRRB na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kusimamia mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

209. ***Mheshimiwa Spika,*** COPRA imetoa vibali vya kusafirisha mazao ya kilimo yenye jumla ya tani 3,704,097 ambapo vibali 929 kwa ajili ya kusafirisha mchele tani 564,592, vibali 1,189 kwa ajili ya kusafirisha mahindi tani 3,026,623 na vibali 540 kwa ajili ya kusafirisha maharage tani 112,882.

210. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, jumla ya ghala 1,734, masoko 378 na vituo vya ukaguzi 155 vimesajiliwa kupitia mfumo wa *Crop Stock Dynamics Systems* katika mikoa yote na usajili unaendelea. Lengo la usajili huo ni kutambua idadi ya ghala za sekta ya umma na binafsi na kiasi cha mazao kilichohifadhiwa kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula na lishe. Vilevile, wafanyabiashara 616 wamesajiliwa katika mfumo huo ambapo kati ya hao, wafanyabiashara 239 walishiriki katika ununuzi wa mazao kupitia mfumo Stakabadhi za Ghala kwa njia ya minada ya kidijiti (TMX).

211. ***Mheshimiwa Spika***, Kanuni tatu (3) zinazohusu usimamizi wa nafaka na mazao mchanganyiko ambazo ni Udhibiti Ubora (Quality Control Regulation), Usajili na Utoaji wa Vibali (Registration and Permit Regulation) na Kilimo cha Mkataba (Contract Farming Regulation) zinaendelea kuandaliwa. Kanuni hizo zinatarajiwa

kukamilika ifikapo Juni, 2025. Pia, COPRA imetoa mafunzo kwa wadau 1,000 kuhusu shughuli inazozitekeleza ili kujenga uelewa kwa wadau kuhusu majukumu ya COPRA.

**4.3.4 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe nchini.**

212. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini na kuondoa utegemezi wa mazao yaliyoongezewa virutubishi kutoka nje ya nchi, Wizara kupitia TARI ilipanga kuzalisha mbegu mama 350,000 za viazi lishe zenye uwezo wa kuzalisha vipando 7,000,000 vilivyoongezewa virutubishi na kuvisambaza katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara; kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji na wazalishaji wa mbegu 150 katika wilaya za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba; na kuhaulisha na kusambaza mbegu za viazi lishe, mahindi na maharage zilizoongezewa viinilishe kibaiolojia.

213. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, mbegu mama 250,000 za viazi lishe zimezalishwa sawa na asilimia 71.4 ya lengo la kuzalisha mbegu 350,000 na kusambazwa katika mikoa ya Mwanza, Geita, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara na uzalishaji unaendelea. Vilevile, wakulima 2,577 wamehamasishwa kuzalisha mazao ya kilimo yenye virutubisho vya lishe yaliyofanyiwa utafiti na wataalam wa hapa nchini. Aidha, mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,525, maafisa ugani 280 na wazalishaji wa mbegu 52 yametolewa katika Wilaya za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba.

214. ***Mheshimiwa Spika,*** mbegu za viazi lishe 983,637 zilizoongezewa viinilishe kibaiolojia zimehaulishwa na kusambazwa katika mikoa ya uzalishaji ili kuboresha lishe kwa walaji. Vilevile, imezuia uingizaji wa vyakula vilivyoongezewa virutubishi kutoka nje ya nchi na kuhamasisha wadau wote kutumia mazao yaliyoongezewa virutubishi ndani ya nchi.

***Mheshimiwa Spika, ninapenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa, tunazo mbegu za maharage, mahindi na viazi zilizoongezewa virutubishi kibailojia na watafiti wetu wa ndani.***

***Hatutaruhusu zao lolote au chakula chochote ambacho kimeongezewa virutubishi nje ya nchi kuingia ndani ya nchi yetu. Hivyo, nitoe rai kwa wadau wote wanaotaka kutoa misaada ya vyakula vilivyoongezewa virutubishi nje ya nchi washirikiane na wazalishaji wa ndani kuongeza virutubishi hivyo ndani ya nchi yetu***

**4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao Nje ya Nchi**

215. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuendelea kuimarisha masoko ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi kwa kuongeza mauzo ya mazao; kuwekeza kwenye miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo; kuimarisha uongezaji thamani; kuimarisha upatikanaji wa mitaji na kuziwezesha maabara za Serikali na sekta binafsi ziweze kufikia viwango vya ubora vinavyotakiwa Kimataifa.

**4.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa Ajili ya Wakulima katika Halmashauri Mbalimbali;**
**Masoko ya kimkakati**

216. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati umefikia wastani wa asilimia 65 ambapo Kabanga Wilaya ya Ngara (asilimia 50), Nkwenda (asilimia 75) na Murongo (asilimia 55) yaliyopo Wilaya ya Kyerwa, Sirari (asilimia 80) lililopo Tarime na Busoka (asilimia 65) lililopo katika Manispaa ya Kahama. Ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi. **Ujenzi wa Masoko (Market sheds)**

217. ***Mheshimiwa Spika,*** mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa soko la Rombo (Mamsera) amepatikana na zabuni kwa ajili ya ujenzi wa soko la Hai (Mula) imetangazwa. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina katika soko la Kigoma (Kibondo) unaendelea. Ujenzi wa masoko hayo utawawezesha wakulima kuuza mazao ya kilimo katika masoko yanayotambuliwa.

### 4.4.2 Kuimarisha Uongezaji Thamani na Uhifadhi kwa Kushirikisha Sekta Binafsi

218. ***Mheshimiwa Spika,*** ujenzi wa kituo mahiri cha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna kilichopo Kongwa katika Mkoa wa Dodoma umekamilika na kukabidhiwa kwa NFRA kwa ajili ya uendeshaji. Vilevile, ujenzi wa vituo jumuishi vya kuhifadhi na kuchakata mazao ya bustani vya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe) umefikia wastani wa asilimia 15.

219. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeingia ubia na TAHA kwa ajili ya kuendesha kituo cha kufungasha na kuhifadhi mazao ya bustani cha Nundu kilichopo Halmashauri ya Njombe Mji Kata ya Yakobi Mkoa wa Njombe.Vilevile, TAHA wametafuta mwekezaji ambaye ni kampuni ya Avocado Avenue Tanzania Ltd ambaye amejenga kiwanda cha kufungasha na kukamua mafuta ya parachichi. Pia, TAHA imejenga vituo vitano (5) vya kukusanya na kuhifadhi parachichi katika Halmashauri za Wanging'ombe (2) na Njombe (3). Vituo hivyo vina uwezo wa kuhifadhi tani 25 – 30 za parachichi kila kimoja.

220. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeanza mchakato wa kuifumua na kuiunda upya CPB kutoka kuwa Bodi kwenda kuwa Kampuni ya Mazao ili kuweza kupunguza changamoto ya kufanya biashara katika muundo wa sasa. Katika muundo mpya, CPB itajikita katika uongezaji wa thamani wa mazao matano (5) ya kipaumbele ambayo ni mahindi, mpunga, mazao ya mafuta ya kula, muhogo na ngano. Uwekezaji huu utajumuisha ujenzi wa viwanda na ghala kwa ajili ya zao la muhogo katika Halmashauri za Kibondo na Kakonko.

### 4.4.3 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi

221. ***Mheshimiwa Spika,*** thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi imeongezeka kutoka takriban Dola za Marekani Bilioni 1.2 mwaka 2019/2020 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024. Ongezeko hilo limetokana na mauzo ya mazao mbalimbali ikiwemo korosho, parachichi, ufuta, mbaazi, pamba, kahawa na tumbaku. Pia, mwenendo wa thamani ya mauzo nje ya nchi ni kama inavyooneshwa kwenye **Kiambatisho Na. 8.**

222. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA kwa kushirikiana na wadau imeanza taratibu za kufungua masoko mapya kwa mazao (9) katika nchi 14 ambazo ni China (Vanilla na Nanasi), India (Vanila na Nanasi), Indonesia (Karafuu), Singapore (Karafuu), Israel (Parachichi), Malaysia (Parachichi), Canada (Pilipili Manga), Uturuki (Nanasi), Brazil (Nanasi), USA (Kakao), South Africa (Ndizi), Zambia (Viazi mviringo), Pakistan (Tumbaku) na Iraq (Tumbaku). Taratibu zikikamilika zitaongeza wigo wa mazao yetu kuuzwa nje ya nchi na kuchochea ukuaji wa pato la mkulima.

223. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa zuio la kibiashara kwa mazao ya kilimo lililokuwepo kati ya Tanzania na Malawi limeondolewa na kusaini tamko la pamoja la kibiashara na hivyo kuruhusu biashara kuendelea kama ilivyokuwa awali. Vilevile, Serikali inawahakikishia wananchi wote kuwa inaendelea na majadiliano na nchi ya Afrika Kusini ili kuondoa zuio la kibiashara.

***Mheshimiwa Spika, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kama Afrika Kusini haitatufungulia masoko ya mazao yetu kama ilivyoelezwa na Waziri wetu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki basi hatutaruhusu mazao yao kuingia nchini. Ninapenda kuwahakikishia wakulima na wafanyabiashara wa mazao kuwa tutalinda maslahi yao***

**4.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji**

224. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kufanya majadiliano na Taasisi mbalimbali za fedha kwa ajili ya kuongeza mikopo kwenye sekta ya kilimo; TADB kuongeza idadi ya taasisi zinazotumia mfuko wa dhamana kutoka 17 hadi 21; kuwezesha miradi mipya 34 katika mnyororo wa thamani; kutoa mikopo ya pembejeo kwenye miradi 24 ya kilimo; na kuwajengea uwezo wakulima wadogo 1,450 na vikundi 16 vya wanawake na vijana.

225. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha upatikanaji wa mikopo katika sekta ya kilimo unaongezeka. Hadi Aprili 2025, mikopo katika sekta ya kilimo imeongezeka kutoka Shilingi Trilioni 4.29 mwaka 2023/2024 hadi Shilingi Trilioni 5.18 mwaka 2024/2025. Aidha, Benki ya Maendeleo

ya Kilimo Tanzania (TADB) imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 265.052 katika sekta ya kilimo mazao kwa njia ya moja kwa moja (direct lending) na Shilingi Bilioni 137.494 kupitia mfuko wa dhamana ya mikopo wa wakulima wadogo (Smallholder Credit Guarantee Scheme).

226. ***Mheshimiwa Spika,*** Benki ya CRDB imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Trilioni 2.23 katika sekta ya kilimo; Benki ya NMB imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Trilioni 1.17 katika sekta ya kilimo; Benki ya Taifa ya Biashara (NBC) imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 314.8 katika sekta ya kilimo; na Benki ya Equity imetoa mikopo yenye thamani ya Shilingi Bilioni 15 katika sekta ya kilimo.

227. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya mikopo iliyotolewa na TADB kwa njia ya moja kwa moja, Shilingi Bilioni 59.806 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo; Shilingi Bilioni 41.773 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vya kuchakata mazao ya nafaka, mbegu za mafuta, zabibu, mkonge pamoja na utengenezaji wa vifungashio; na Shilingi Bilioni 13.555 zimetolewa kuwezesha shughuli za uendelezaji wa mazao na ununuzi wa malori ya usafirishaji wa mazao.

228. ***Mheshimiwa Spika,*** Shilingi Bilioni 6.470 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa ghala na vihenge kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna; Shilingi Bilioni 2.231 zimetolewa kwa ajili ya kuwezesha uwekaji wa mifumo ya umwagiliaji kwenye mashamba; Shilingi Bilioni 2.176 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo; na Shilingi Bilioni 139.041 imetolewa kwa Vyama vya Ushirika, kampuni na watu binafsi kwa ajili ya kufanikisha ununuzi wa mazao ya kahawa, pamba, korosho, miwa, parachichi, mahindi na mpunga katika mikoa ya Kagera, Mara, Katavi, Mwanza, Manyara, Ruvuma na Mbeya.

229. ***Mheshimiwa Spika,*** kati ya Shilingi Bilioni 137.494 zilizotolewa kupitia mfuko wa dhamana ya mikopo kwa wakulima wadogo, Shilingi Bilioni 50.396 zimetolewa kuwezesha ununuaji na uuzaji wa mazao; Shilingi Bilioni 34.207 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa pembejeo za kilimo na uendelezaji wa shughuli za kilimo; Shilingi Bilioni 28.169 zimetolewa kwa ajili ya ununuzi wa zana za kilimo; na

Shilingi Bilioni 11.655 zimetolewa kwa ajili ya miradi ya uchakataji wa mazao.

230. ***Mheshimiwa Spika,*** kiasi cha Shilingi Bilioni 11.191 zimetolewa kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa miundombinu mbalimbali katika mnyororo wa thamani wa kilimo; kiasi cha Shilingi Bilioni 1.774 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa ghala kwa lengo la kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna; na kiasi cha Shilingi Milioni 100 zimetolewa kufanikisha miradi midogo ya umwagiliaji.

231. ***Mheshimiwa Spika,*** taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) zimeongezeka kutoka taasisi 17 hadi 18. Hatua hiyo, imewanufaisha wakulima 577,609, biashara ndogo na za kati za kilimo (SMEs) 520, Vyama vya Msingi (AMCOS) na Vyama vya Ushirika 538.

232. ***Mheshimiwa Spika,*** miradi mipya 35 ya uchakataji, ghala sita (6), chumba cha ubaridi na miundombinu ya umwagiliaji 16 imewezeshwa na Benki ya TADB. Aidha, TADB imenunua matrekta 23 na *combine harvester* nne (4), imetoa mikopo ya pembejeo kwenye miradi 39 ya kilimo na kuwajengea uwezo kuhusu elimu ya fedha na mikopo wakulima wadogo 3,686 na vikundi 47 vya wanawake na vijana katika mikoa 13 ili kuwawezesha kuongeza uzalishaji na tija ya mazao.

**4.4.5 Kuziwezesha Maabara za Serikali na Sekta Binafsi kufikia Viwango vya Ubora Unaotakiwa Kimataifa**

233. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA ilipanga kuendelea kuimarisha maabara ya afya ya mimea; kukamilisha usimikaji wa mashine na kununua vitendanishi vya kituo cha udhibiti wa visumbufu vya mimea kibaiolojia (National Biological Control Unit). Vilevile, Wizara kupitia TOSCI ilipanga kufanya upanuzi wa maabara kuu ya mbegu ya Taifa; kujenga maabara katika ofisi za kanda; kukarabati maabara ya mbegu ya kanda ya kaskazini; na kukamilisha ujenzi wa maabara kuu ya kilimo Mtumba.

234. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufungua masoko ya kimataifa nchi lazima iwe na maabara zenye viwango vinavyotambulika

kimataifa. Wizara imewezesha upatikanaji wa cheti cha ithibati na ubora wa kimataifa wa maabara ya udongo na mimea ya TRIT yenye Na. ISO/ICE 17025:2017; ujenzi wa Maabara Kuu ya Kilimo iliyopo Mtumba katika Mkoa wa Dodoma umefikia asilimia 98. Kukamilika kwa maabara hizo kutasaidia kuimarisha ubora wa mbegu na mazao ya kilimo; na Wizara kupitia TPHPA imenunua mashine mpya tano (5) za kisasa za maabara (GC MS/MS -2, GC - 1 na HPLC – 2) kwa ajili ya kuthibitisha ubora wa viuatilifu ili kudhibiti na kuratibu biashara ya viuatilifu nchini.

235. ***Mheshimiwa Spika,*** ukarabati wa maabara kuu ya mbegu ya Taifa iliyopo Morogoro umefikia asilimia 20 upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ukarabati wa maabara ya mbegu ya TOSCI kanda ya kaskazini iliyopo katika Mkoa wa Arusha unaendelea. Pia, cheti cha tathmini ya athari ya mazingira (Environmental Impact Assessment - EIA) kwa ajili ya ujenzi wa maabara ya mbegu katika ofisi ya kanda ya TOSCI iliyopo katika Mkoa wa Mwanza kimepatikana na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea.

## 4.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika

236. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuwezesha uwekezaji katika mifumo ya kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika; kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuviwezesha kupata mitaji; na kuhamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum. Utekelezaji wa mikakati hiyo ni kama ifuatavyo:-

### 4.5.1 Kuwezesha Uwekezaji katika mifumo ya Kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi

237. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ilipanga kuimarisha matumizi ya mifumo ya Kidijiti kwa kununua na kusambaza kompyuta mpakato 129; na kuwezesha Vyama vya Ushirika kupata mikopo yenye riba nafuu kwa ajili ya ununuzi wa mizani ya kidijiti 1,500 katika Vyama vya Ushirika wa mazao.

238. ***Mheshimiwa,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Tume imeendelea kuimarisha

matumizi ya mifumo ya kidijiti katika kusimamia na kuendesha Vyama vya Ushirika ambapo imenunua na kusambaza kompyuta mpakato 64 kwa Maafisa Ushirika. Vilevile, Tume kwa kushirikiana na CRDB Foundation imewezesha Vyama vya Ushirika vya msingi 992 kupata mikopo yenye riba nafuu yenye thamani ya Shilingi Bilioni 13.268. Kiasi hicho, kimewezesha Vyama hivyo kununua mizani ya kidijiti 3,760. Aidha, Vyama hivyo vinajishughulisha na mazao ya korosho, ufuta, mbaazi, soya na kahawa kwenye mikoa ya Mtwara, Lindi, Pwani, Ruvuma na Kagera.

**4.5.2 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika**

239. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwa Vyama vya Ushirika 5,482; COASCO kukagua Vyama vya Ushirika 5,000; Tume kukagua sifa za watendaji kwenye Vyama Vikuu na SACCOS 118 nchini; na kuratibu na kusimamia taratibu zote za ajira katika Vyama vya Ushirika ili kuhakikisha vyama vinapata watendaji wenye sifa stahiki.

240. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Tume imekagua (Inspection) Vyama vya Ushirika 3,415 sawa na asilimia 62.3 ya lengo la kukagua vyama 5,482. Ukaguzi huo umebaini kuwa baadhi ya viongozi hawazingatii miongozo inayotolewa na Mrajis, hivyo Tume imetoa mafunzo kwa viongozi kuhusu uongozi bora.

241. Katika mwaka 2023/2024, COASCO imekagua (Audit) Vyama vya Ushirika 4,760 sawa na asilimia 95.2 ya lengo la kukagua Vyama 5,000. Kati ya vyama vilivyokaguliwa, vyama 631 vimepata hati safi, vyama 2,871 vimepata hati zenye shaka, vyama 263 vimepata hati isiyoridhisha na vyama 995 vimepata hati mbaya. Ukaguzi huo, umebaini vyama 1,258 kushindwa kuandika vitabu vya hesabu kwa usahihi. Hatua zilizochukuliwa baada ya ukaguzi huo ni kutoa mafunzo kuhusu uongozi, uandaaji wa hesabu na uandishi wa vitabu vya hesabu.

242. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imefanya ukaguzi katika Vyama Vikuu 44, miradi ya pamoja 15 na SACCOS Daraja B 113 ambapo jumla ya watendaji 118 walibainika kutokuwa na sifa stahiki. Kati ya hao, watendaji 62 ni kutoka SACCOS Daraja B na watendaji 56 ni kutoka Vyama Vikuu na miradi ya pamoja. Aidha, Tume imetoa

maelekezo kwa Vyama vyenye watumishi wasiokuwa na sifa kuchukua hatua kwa mujibu wa Sheria. Pia, Tume imeendelea kusimamia taratibu za ajira katika vyama ili kuhakikisha vyama vinaajiri watendaji wenye sifa ambapo watendaji 89 wameajiriwa.

**4.5.3 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuviwezesha kupata Mitaji**

243. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kukamilisha kuanzisha Benki ya Ushirika Tanzania; kufungua matawi matatu (3) ya Benki hiyo katika mikoa ya Dodoma, Mtwara na Kilimanjaro; kutoa elimu kwa vyama kuhusu umuhimu wa mfuko wa Kinga za Akiba na Amana za SACCOS; na kufungua akaunti maalum itakayotumika kukusanya fedha za Mfuko.

244. Ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara kupitia Tume imeanzisha Benki ya Ushirika Tanzania ambayo imezinduliwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 28 Aprili 2025. Benki hiyo imeanza na mtaji wa Shilingi Bilioni 58, kufungua matawi manne (4) katika mikoa ya Dodoma, Tabora, Mtwara na Kilimanjaro na kusajili Vyama Vikuu vya Ushirika 58 kuwa mawakala.

245. ***Mheshimiwa Spika***, Tume imehamasisha Vyama vya Ushirika kuongeza uwekezaji hadi kufikia Shilingi Bilioni 13.2 katika Benki hiyo sawa na asilimia 22.76. Pia, imeanzisha dirisha maalum la *guarantee Scheme* na *equity fund*. Vilevile, hati ya makubaliano kati ya Benki ya Ushirika Tanzania na AGITF imesainiwa na kuwezesha kufungua akaunti ya dhamana kwenye benki hiyo. Aidha, Tume imetoa mafunzo kuhusu umuhimu wa Mfuko wa Kinga za Akiba na Amana za SACCOS kwa viongozi 24 na watendaji 37.




*Jengo la Makao Makuu ya Benki ya Ushirika Tanzania lililopo katika Mkoa wa Dodoma.*



*Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua Benki ya Ushirika Tanzania katika Mkoa wa Dodoma.*

246. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, Tume ilipanga kuimarisha mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko kwa mazao; kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuwa Mawakala wa kusambaza mbolea kwa mpango wa ruzuku; kuratibu na kusimamia Vyama Vikuu kujenga viwanda vya kuchakata mazao ya kilimo; kufufua viwanda vya kuchambua pamba na kukamua mafuta vya Manawa na Mhunze; na kuratibu utambuzi na uthaminishaji wa mali za vyama vya ushirika na kutafuta wawekezaji wa kimkakati.

247. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tume kwa kushirikiana na wadau imeendelea kuratibu na kusimamia mauzo ya mazao ya wakulima kupitia mifumo rasmi na

jumuishi ya biashara na masoko. Hadi Aprili 2025, tani 2,225,397.56 za mazao zenye thamani ya Shilingi Trilioni 4.225 zimekusanywa kupitia Ushirika na kuuzwa kwa mfumo rasmi ikilinganishwa na tani 1,643,318.00 zilizouzwa kwa thamani ya Shilingi Trilioni 1.977 mwaka 2023/2024.

248. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhamasisha Vyama vya Ushirika kuuza mazao na bidhaa zinazozalishwa na Vyama hivyo nje ya nchi, Tume imewezesha Vyama vya Ushirika vya Kahawa kuuza nje ya nchi kahawa aina ya Arabika na Robusta tani 15,851.561 zenye thamani ya Dola za Marekani 73,678,065.68 katika nchi za Ufaransa, Ujerumani, Italia na Ubeligiji. Vilevile, Vyama vya Ushirika vya Pamba vimechakata na kuuza marobota ya pamba 29,161 yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.61 katika nchi za India na China. Vyama vilivyouza marobota hayo ni KACU Ltd, CCU Ltd, MBCU Ltd na SIMCU Ltd.

249. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume imeunganisha Vyama vya Ushirika 52 na wafanyabiashara kutoka nchi za India, Falme za Kiarabu, China na Ubeligiji ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa utafutaji wa masoko mapya kwa ajili ya kuuza mazao na bidhaa moja kwa moja. Vilevile, ili kurahisisha usambazaji wa mbolea, Vyama vya Ushirika 720 vimehamasishwa na kuwa mawakala wa usambazaji wa mbolea kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku.

250. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hiyo, imewezesha kununua na kusambaza mbolea ya ruzuku yenye thamani ya Shilingi Bilioni 4.3 kwa wakulima. Vyama vya Ushirika vilivyosambaza mbolea hiyo ni pamoja na IFCU Ltd, WAMCU Ltd, RIVACU Ltd, GCU Ltd, CCU Ltd, MBCU Ltd na TANCOOPs Ltd vilivyopo katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Singida, Manyara, Mara na Iringa.

251. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume imeratibu Vyama Vikuu vya Ushirika kujenga viwanda vitano (5) vya kuchakata mazao ya wakulima. Viwanda hivyo ni pamoja na kiwanda cha WAMACU Ltd kwa ajili ya kukoboa kahawa (Mara), kiwanda cha TANECU kwa ajili ya kubangua Korosho (Mtwara), kiwanda cha RUNALI kwa ajili ya kukamua mafuta ya alizeti na ufuta (Lindi), kiwanda cha CHUTCU Ltd kwa ajili ya kukoboa mahindi ya

wakulima (Mbeya) na kiwanda cha WETCU Ltd kwa ajili ya kukoboa na kusaga nafaka za wakulima (Tabora).

252. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, inaendelea kuratibu mpango wa ufufuaji wa Kiwanda cha kuchambua pamba na kukamua mafuta cha Manawa kinachomilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika Nyanza. Vilevile, Chama Kikuu cha Ushirika Chato (CCU) kinaendelea na taratibu za kufufua kiwanda cha kukamua mafuta ya pamba. Pia, Tume kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba Tanzania na Wizara ya Viwanda na Biashara inaendelea kufanya tathmini ya gharama za ufufuaji wa kiwanda cha kuchambua pamba kinachomilikiwa na Chama kikuu cha Ushirika SHIRECU Ltd**.**

253. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Tume imeratibu utambuzi na uthaminishaji wa mali 4,348 za Vyama vya Ushirika 673 zenye thamani ya soko ya Shilingi Trilioni 1.318 na kuingizwa kwenye Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU). Aidha, utambuzi na uthaminishaji wa mali za Vyama vya Ushirika unaendelea.

**4.5.4 Kuhamasisha Ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum**

254. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume ilipanga kuhamasisha vikundi 520 vinavyotekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi katika sekta za kilimo, mifugo, uvuvi, madini, viwanda na fedha pamoja na wanawake, vijana na watu wenye ulemavu 20,000 ili kujiunga na kuanzisha Vyama vya Ushirika. Vilevile, Tume kwa kushirikiana na wadau ilipanga kuunganisha vyama vipya vya ushirika wa mbogamboga na masoko na kuwajengea uwezo viongozi na wanachama wa Vyama hivyo kuhusu uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na kuendelea kuhamasisha uanzishaji wa Vyama vya Ushirika vya mazao ya bustani (Horticulture).

255. ***Mheshimiwa Spika***, ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Tume imehamasisha vikundi 415 vya makundi maalum na kuanzisha Vyama vya Ushirika 49 vyenye wanachama 4,177. Kati ya vyama vilivyoanzishwa, 32 ni vyama vya vijana na 17 ni vyama vya wanawake. Vilevile, Tume

kwa kushirikiana na wadau zikiwemo Bodi za Mazao, TMX, WRRB na Sekretarieti za Mikoa na Serikali za Mitaa, imeendelea kuratibu mauzo ya mazao ya wakulima kwa njia ya kidijiti kupitia Vyama vya Ushirika vikiwemo vya mazao ya bustani. Aidha, mafunzo rejea kuhusu taratibu za uendeshaji wa vyama yametolewa kwa watendaji wa vyama 1,256 katika mikoa ya Pwani (112), Lindi (475), Mtwara (457), Ruvuma (140) na Dodoma (72).

### 4.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

256. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 imeendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika Sekta ya Kilimo kwa kutekeleza mikakati ifuatayo:-

#### 4.6.1 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati

257. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuunganisha mifumo ya ndani ya Wizara na taasisi zake ili kuwa na mfumo mmoja ambao utaweza kusomana na mifumo ya nje ya Wizara ikiwemo mifumo ya NBS, Benki Kuu na TRA.

258. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara imeunda mfumo jumuishi (e – Kilimo) unaounganisha mifumo ya ndani na Taasisi zake katika maeneo mbalimbali yakiwemo, usajili wa wakulima, huduma za ugani, utoaji wa vibali na leseni za kilimo, usimamizi wa miradi, usimamizi wa mbolea na usimamizi wa Vyama vya Ushirika.

259. ***Mheshimiwa Spika***, mfumo huo umeunganishwa na mifumo mingine ya Serikali ambayo ina muingiliano katika kufanikisha huduma za kilimo ikiwemo *Government Electronic Payment Gateway* - GePG, *Business Registrations* and *Licensing Agency* - BRELA, *National Identification Authority* – NIDA, *Tanzania Revenue Authority* - TRA-TANCIS, *Human Capital Management Information Systems* – HCMIS (e – Watumishi) na *Government Mobile Platform* - mGOV. Aidha, uungasnishaji wa mfumo (e-Kilimo), TRA-TIN na *Tanzania Meteorological Authority* - TMA upo katika hatua ya kusaini mikataba ya kubadilishana taarifa.

### 4.6.2 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo

260. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kutoa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kidijiti kwa wadau wa kilimo; kujenga miundombinu ya kisasa ya kidijiti; kuwawezesha vijana na wanawake kutumia elimu ya uvumbuzi katika kilimo na kusaidia kukuza teknolojia mpya za kilimo; na kujenga kituo cha ubunifu wa teknolojia katika Mkoa wa Dodoma na kuweka teknolojia wezeshi.

261. ***Mheshimiwa Spika*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara imetoa mafunzo kuhusu matumizi ya mifumo ya kidijiti kwa watumishi 500 wa Wizara ya kilimo na Taasisi zake. Aidha, mafunzo hayo yanaendelea kutolewa kwa wadau wengine. Vilevile, ujenzi wa miundombinu ya kisasa ya kidijiti kwa ajili ya uendelezaji wa kilimo kwa kutumia teknolojia za *Internet of Things* (IoT), Akili Mnemba (AI), vitambuzi visivyotumia waya (Sensor) na uchambuzi wa taarifa umefikia asilimia 50. Pia, ujenzi na uwekaji wa teknolojia wezeshi katika kituo cha ubunifu wa teknolojia kilichopo Mkoa wa Dodoma umefikia asilimia 20.

### MAENEO MENGINE MUHIMU YALIYOTEKELEZWA NA WIZARA

i. **Kupitia Sera, Sheria za Kilimo, Makubaliano na Miongozo ya Uendeshaji wa Shughuli za Kilimo**

262. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025, ilipanga kuendelea na maboresho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013; kukamilisha uanzishaji wa Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo - 2050 (Agricultural Transformation Master Plan – 2050); kuhamasisha matumizi ya zana bora za kilimo; usimamizi wa kilimo cha mkataba; na kuanzisha *compact* ambayo itasainiwa na wadau wa maendeleo ambao watatakiwa kutekeleza miradi ya vipaumbele vya Wizara.

263. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara imekamilisha kuandaa Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa mwaka - 2050 ambao unatoa dira ya kilimo kwa kipindi cha muda mfupi, kati na mrefu; imefanya marekebisho ya Sheria ya Sukari Na.6 ya mwaka 2001 kupitia Sheria ya fedha ya mwaka 2024 na kuipa NFRA mamlaka

ya kununua na kuhifadhi sukari kisheria. Vilevile, imefanya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Korosho Na.18 ya mwaka 2009 kupitia sheria ya fedha ya mwaka 2024 na kuwezesha asilimia 100 ya mapato yanayotokana na mauzo ya korosho ghafi (export levy) kwenda Bodi ya Korosho Tanzania.

264. ***Mheshimiwa Spika***, vilevile, marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Ushirika Na.6 ya Mwaka 2013 yamekamilika na kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali Na.11 la tarehe 14 Machi, 2025. Marekebisho hayo yamempa Mrajis mamlaka ya kuchukua hatua za haraka anapoona ubadhilifu mara baada ya kupokea taarifa ya ukaguzi. Aidha, marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Pamba yamepitishwa na Bunge tarehe 29 Januari, 2025 ili kuimarisha usimamizi na usahihi katika takwimu za ununuzi wa pamba, ubora wa pamba inayouzwa ndani na nje ya nchi na kuimarisha upatikanaji wa mbegu za pamba.

265. ***Mheshimiwa Spika,*** pia, marekebisho ya Sheria ya Umwagiliaji yamefanyika ambapo ofisi za umwagiliaji za Wilaya zimetambuliwa rasmi kisheria. Aidha, Vyama vya Umwagiliaji vimepewa hadhi kisheria kuwa *corporate bodies* ambapo pamoja na mambo mengine vimepewa uwezo wa kumiliki mali, kununua na kuuza kisheria.

266. ***Mheshimiwa Spika,*** mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Tasnia ya Chai, Sura ya 275 kwa ajili ya kuunganisha Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai Tanzania na Bodi ya Chai Tanzania kuwa Taasisi moja (Bodi ya Chai Tanzania) yameidhinishwa na Baraza la Mawaziri. Aidha, uandishi wa marekebisho ya Sheria unakamilishwa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

267. ***Mheshimiwa Spika,*** taratibu za kuunganisha Taasisi za utafiti za kahawa, chai na tumbaku kuwa sehemu ya muundo wa TARI zinaendelea. Pia, taratibu za kufuta Bodi ya Pareto Tanzania na majukumu yake kuhamishiwa COPRA zinaendelea.

**ii. Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi na Uhifadhi wa Mazingira**

268. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025, ilipanga kuendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Mazingira katika Sekta ya Kilimo; kufanya tathmini ya athari za mazingira na jamii kwenye mashamba makubwa 10 yaliyo kwenye programu ya BBT; kuendelea na uhamasishaji wa kilimo chenye kutunza mazingira kwenye mashamba ya BBT; kusambaza Mkakati wa Kilimo Ikolojia Hai kwa njia ya mafunzo kwa Maafisa Ugani 120 katika Halmashauri 30; kupitia TARI kutafiti teknolojia za utunzaji wa mazingira: na tafiti ambazo zitazalisha teknolojia zinazostahimili mabadiliko ya tabianchi.

269. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, jumla ya miti 10,000 imepandwa kwenye shamba la BBT la Chinangali ili kuhifadhi mazingira katika mashamba ya programu ya BBT. Vilevile, mafunzo kuhusu matumizi ya teknolojia, mbinu za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi na uhifadhi wa mazingira yametolewa kwa wakulima na Maafisa Ugani 368 katika Halmashauri za Manyoni, Singida, Ikungi, Iramba, Uyui, Nzega na Igunga.

270. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, mpango wa udhibiti husishi wa visumbufu vya mazao (Intergrated Pest Management Plan) umeandaliwa kwa lengo la kudhibiti visumbufu vya mazao katika mnyororo wa thamani wa mazao ya alizeti, ngano na mpunga; na Mpango wa Utunzaji Mazingira na Jamii (Environmental and Social Management Plan) umeandaliwa ili kuhakikisha utekelezaji wa mradi wa TAISP unafuata sera, sheria, miongozo, taratibu na kanuni za utunzaji wa mazingira.

**iii. Jinsia**

271. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kilimo cha mazao kwa kuwezesha uandaaji wa Mpango Kazi wa Kijinsia (Gender Action Plan) ambao utatekelezwa na Mradi wa TAISP; kuhakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbegu na mbolea; kutoa mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa ya mradi; na kupitia

programu na miradi ya BBT, AFDP, TANIPAC na TFSRP ilipanga kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia masuala ya jinsia.

272. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa hadi Aprili 2025, Wizara kupitia Mradi wa TAISP imetathmini masuala ya kijinsia katika mikoa 14 na kuandaa Mpango Kazi wa Kijinsia (Gender Action Plan). Vilevile, utoaji wa ruzuku ya mbolea na mbegu umezingatia masuala ya jinsia ambapo wanaume 1,365,133 na wanawake 805,363 wamenufaika kupitia mpango huo. Pia, mafunzo kuhusu jinsia katika sekta ya kilimo (mazao) yametolewa kwa wakulima 748 (KE - 335, 413 - ME) katika mikoa ya Dodoma, Kagera na Singida.

### iv. VVU na UKIMWI

273. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2024/2025 ilipanga; kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi wanne (4) wanaoishi na VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza; kuratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika; Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya kuendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza; na kuweka vifaa kinga katika majengo yote ya Wizara na Taasisi zake.

274. ***Mheshimiwa Spika,*** hadi Aprili 2025, Wizara imetoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi tisa (9) wanaoishi na VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza. Vilevile, imeratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya imeendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa watumishi pamoja na vijana wa BBT.

275. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuweka vifaa kinga katika majengo yote ya Wizara na Taasisi zake; na imeendelea kuhamasisha watumishi kushiriki katika michezo mbalimbali.

## 5 MPANGO NA BAJETI YA MWAKA 2025/2026

276. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara ya Kilimo inawasilisha Mpango na Bajeti ya mwaka 2025/2026 wakati Taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu na uzinduzi wa Mpango wa Maendeleo wa Miaka 25. Mpango huu wa bajeti umezingatia Dira ya Maendeleo ya

Taifa (2025); Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano Awamu ya Tatu (2021/2022 – 2025/2026); Ilani ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020; Sera ya Taifa ya Kilimo ya Mwaka 2013; Sera ya Taifa ya Umwagiliaji ya Mwaka 2010; na Sera ya Maendeleo ya Ushirika ya Mwaka 2002.).

277. ***Mheshimiwa Spika,*** mpango umezingatia Malengo Endelevu ya Maendeleo (SDGs); Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa Mwaka 2050 (Tanzania Agriculture Master Plan 2050); Mkakati wa Ukuzaji wa Sekta ya Kilimo (Ajenda 10/30 Investment Roadmap); Mkakati wa Kuongeza Fedha za Kigeni 2023/2024 - 2027/2028; Azimio la Kampala kuhusu Programu ya Kuendeleza Kilimo Barani Afrika (CAADP 2026 – 2035); Mwongozo na Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2025/2026; Maoni na ushauri wa Kamati za Kudumu za Bunge; Maoni ya Baraza la Rais la Ushauri wa Usalama wa Chakula na Kilimo, wadau wa maendeleo na masuala mtambuka ya jinsia, mazingira, lishe, mabadiliko ya tabianchi, vijana, kutokomeza ajira kwa watoto katika Sekta ya Kilimo, VVU na UKIMWI.

278. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2025/2026 utazingatia Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa Mwaka 2050 (Tanzania Agriculture Master Plan 2050).

279. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara itaendelea kutekeleza vipaumbele sita (6) kwa kuendelea na utekelezaji wa miradi iliyoanza mwaka 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025 na kuanza miradi mipya. Miradi hiyo inajumuisha miradi ya umwagiliaji, vituo vya zana za kilimo, upatikanaji wa pembejeo za kilimo, uhifadhi, uongezaji thamani, uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja, uzalishaji, ujenzi wa masoko, utafiti, huduma za ugani na utoaji wa ruzuku ya pembejeo za kilimo.

280. ***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa miradi hiyo katika bajeti ya mwaka 2025/2026 unalenga kuongeza ukuaji wa sekta ya kilimo kwa upande wa mazao kufikia asilimia 5; kuongeza uzalishaji wa mazao ya kimkakati kutoka tani 1,451,694.11 hadi tani 2,275,000; utoshelevu wa chakula kwa asilimia 130; thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi kufikia takriban Dola za

Marekani Bilioni 4; na kuongeza eneo la umwagiliaji kufikia hekta 1,200,000.

281. ***Mheshimiwa Spika***, malengo hayo yatafikiwa kwa kutekeleza vipaumbele sita (6) na mikakati 30 kama ifuatavyo:-

**i. Kuongeza Tija na Uzalishaji; Mikakati:-**

a) Utafiti wa mbegu;
b) Uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora na miche na kutoa ruzuku ya mbegu bora na miche kwa baadhi ya mazao;
c) Uwekezaji kwenye utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu;
d) Usajili wa wakulima na urasimishaji wa shughuli za kilimo;
e) Kuwekeza kwenye ujuzi kwa wataalam wa ndani;
f) Uwekezaji kwenye huduma za ugani;
g) Kupima afya ya udongo kwa wakulima wadogo na wakubwa;
h) Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji;
i) Kuendeleza Kanda za kilimo na uzalishaji; na
j) Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo.

**ii. Kuchangia kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo (Contribute an increase on Decent Jobs and Enhancing Youth and Women Participation in Agriculture Sector) Mikakati:-**

a) Kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa ya pamoja;
b) Kuwezesha uendelezaji wa programu ya BBT ngazi ya Halmashauri;
c) Kuwezesha ujenzi wa miuondombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT visima);
d) Kuwezesha upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake (BBT mitaji);
e) Kuwezesha vijana na wanawake kuzalisha miche (BBT miche);
f) Kuwezesha vijana na wanawake kuongeza thamani ya mazao; na
g) Kuwezesha vijana na wanawake kutoa huduma za ugani (BBT Ugani).

**iii. Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe (To Improve Food and Nutrition Security); Mikakati:-**

a) Uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi kuweza kufikia uwezo wa kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo mwaka 2030;
b) Kuiongezea NFRA uwezo wa kununua mazao ya wakulima ili kuongeza hifadhi ya chakula; na
c) Kuhamasisha matumizi ya mazao yaliyoongezewa virutubishi ndani ya nchi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini.

**iv. Kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi (Strengthen access to market, agriculture financing and crop exports);**
**Mikakati:-**

a) Kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo kwa ajili ya wakulima katika Halmashauri mbalimbali;
b) Kuimarisha uongezaji thamani kwa kushirikisha Sekta Binafsi;
c) Kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi;
d) Kuimarisha upatikanaji wa mitaji; na
e) Kuziwezesha maabara za Serikali na Sekta Binafsi kufikia viwango vya ubora unaotakiwa kimataifa.

**v. Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika (Strengthening Cooperative Development) Mikakati:-**

a) Kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika;
b) Kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuvisaidia kupata mitaji; na
c) Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na makundi maalum.

**vi. Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo (Agriculture Digitalization) Mikakati:-**

a) Kuimarisha mifumo ya kidigiti itakayowezesha upatikanaji wa taarifa sahihi kwa wakati; na
b) Kuwekeza kwenye matumizi ya mifumo ya kidigiti katika Sekta ya Kilimo.

**KAZI ZITAKAZOTEKELEZWA KWA KUZINGATIA MIKAKATI YA VIPAUMBELE VYA MWAKA 2025/2026**

**5.1 Kuongeza Tija na Uzalishaji**

**5.1.1 Utafiti wa mbegu**

282. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuendeleza teknolojia za kilimo, Wizara kupitia TARI katika mwaka 2025/2026 itaendelea na utafiti wa mbegu aina 56 za mazao ya kimkakati ya nafaka, jamii ya mikunde na mafuta kwa lengo la kugundua mbegu mpya za mazao hayo. Vilevile, itatafiti teknolojia za afya ya udongo zinazohusu ufanisi wa kiasi na muda wa uwekaji wa mbolea ya Nitrojeni (mpunga), ubora wa udongo (tende), matumizi ya mbolea ya POLY4 (miwa), matumizi ya aina za mbolea katika zao la alizeti na kilimo mseto cha alizeti na karanga, matumizi ya mbolea mchanganyiko kwenye mazao ya maharage, mpunga, mahindi, mtama na ngano. Kukamilika kwa tafiti hizo kutawezesha mapendekezo ya matumizi sahihi ya mbolea.

283. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itatafiti kiwango sahihi cha uwekaji wa mbolea ya kupandia na kukuzia kwa tumbaku ya mvuke katika maeneo yanayolima tumbaku nchini. Aidha, itaendelea kufanya utafiti wa kutambua gharama za uzalishaji wa tumbaku zinazokaushwa kwa mvuke, moshi, hewa na jua. Aidha, TARI itatoa mafunzo kuhusu kurejesha afya ya udongo iliyoathirika na tindikali kwa wakulima 600 katika mikoa ya Songwe (Mbozi) na Iringa (Kilolo).

284. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na utafiti wa magonjwa ya fungashada – BBTV katika zao la migomba, *cashew leaf and nut blight*, ubwiri unga na mnyauko fusari katika zao la korosho ili kudhibiti magonjwa hayo. Aidha, itaendelea na utafiti wa funza wa vitumba na chawa jani katika zao la pamba; *thrips* kwenye zao la miwa; na tafiti za viuatilifu vya visumbufu vya mimea katika zao la mtama ili kuimarisha udhibiti wa visumbufu katika mazao hayo.

285. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha kilimo cha chai nchini, TARI itafanya utafiti wa miti ya kivuli kwa lengo la kupata aina bora ya miti ya kivuli na mfumo bora wa upandaji miti hiyo katika mashamba ya chai ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

286. ***Mheshimiwa Spika***, TARI imepanga kutafiti teknolojia saba (7) za kuongeza thamani ya mazao ya mtama, uwele, muhogo, soya na mazao jamii ya mikunde zitakazowezesha kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna na kuongeza ushindani wa mazao yanayozalishwa nchini katika soko la kimataifa. Vilevile, ili kuimarisha upatikanaji wa mbegu za asili, TARI itasafisha na kutunza aina 360 za mbegu za asili za mazao ya mpunga (62), ufuta (15), uwele (1), ulezi (6), choroko (10), kunde (15), migomba (91), korosho (85), viazi vitamu (48) pilipili manga (1), tango (1), mbaazi (15) na soya (10).

287. ***Mheshimiwa Spika***, TARI itakusanya na kutunza vinasaba 12,968 vya mazao ya mahindi (50), mpunga (474), ngano (4) maharage (17), pamba (604), viungo (6), alizeti (64), mtama (349), uwele (204), ulezi (243), choroko (43), kunde (2), miwa (150), mazao ya misitu (79), parachichi (6), chikichi (92), migomba (180), korosho (10,000), zabibu (26), viazi vitamu (87), viazi lishe (6), muhogo (134), karanga (16), kakao (25), matunda (47) na mkonge (60). Aidha, itazalisha mbegu za mazao ya kimkakati tani 1,500 zikiwemo mbegu mama (tani 20.01), awali (tani 256.42), msingi (tani 378.81) na zilizothibitishwa (tani 844.76).

288. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha uhifadhi wa mbegu za utafiti zinazozalishwa, TARI itaendelea na ujenzi wa ghala 11 zenye uwezo wa kuhifadhi tani 415 kila moja katika vituo vya TARI Tumbi - Tabora, TARI Selian - Arusha, TARI Hombolo - Dodoma, TARI Dakawa - Morogoro, TARI Naliendele - Mtwara, TARI Uyole - Mbeya, TARI Kifyulilo - Iringa, TARI Ifakara - Morogoro, TARI Ilonga - Morogoro, TARI Ukiriguru - Mwanza na TARI Maruku – Kagera, ili kuongeza uzalishaji wa miche, TARI itaendelea na ujenzi wa maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika vituo vya TARI Tengeru na TARI Maruku. Aidha, katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mimea, TARI itaendelea na ujenzi wa maabara ya kudhibiti visumbufu vya mimea katika kituo cha TARI Naliendele.

289. ***Mheshimiwa Spika***, katika kulinda mashamba ya utafiti wa mbegu dhidi ya uvamizi, TARI itaendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya utafiti wa mbegu katika vituo vya TARI Uyole, TARI Kifyulilo, TARI Dakawa, TARI Hombolo, TARI Maruku, TARI Ifakara, TARI Kihinga, TARI Mlingano, TARI Ukiriguru na TARI Tumbi. Vilevile,

italipa fidia kwa wananchi watakaohamishwa katika kituo cha TARI Uyole ili kupisha ujenzi wa uzio. Pia, itahakikisha upatikanaji wa hatimiliki katika vituo 17 na mashamba ya majaribio 18.

290. ***Mheshimiwa Spika***, TARI itaendelea na ujenzi wa kituo cha *Bioscience* katika kituo cha TARI Ilonga Mkoa wa Morogoro kwa ajili ya kutoa huduma za kisasa za kisayansi katika utafiti wa mbegu, wadudu, magonjwa, uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi, udongo, uhandisi wa kibaolojia (Bio - engineering) na kanzidata za taarifa za kibaolojia (Bioinformatics). Aidha, TARI itaendelea na ujenzi wa Benki ya mbegu katika kituo cha TARI Selian kwa ajili ya uhifadhi wa mbegu. Vilevile, TARI itaendelea na ujenzi wa Ofisi ya Makao Makuu (Njedengwa, Dodoma); kukamilisha ukarabati wa nyumba 49 za watumishi katika vituo vya TARI Ilonga (24), TARI Mlingano (15) na TARI Tumbi (10); na ukarabati wa ofisi nne (4) katika vituo vya TARI Ilonga (3) na Tumbi (1). Pia, TARI itajenga ofisi moja (1) katika kituo cha TARI Hombolo na kununua vifaa vya Ofisi ya TARI Kihinga.



*Mchoro unaonesha muonekano wa jengo la Benki ya Taifa ya Mbegu itakayojengwa katika Kituo cha TARI Selian – Arusha*

291. ***Mheshimiwa Spika***, TARI itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji yenye jumla ya hekta 1,120.9 katika vituo vya TARI Selian (hekta 120), TARI Kihinga (hekta 150), TARI Ilonga (hekta 200), TARI Hombolo (hekta 70), TARI Uyole (hekta 120), Isimani (hekta (22), TARI Kibaha (hekta 20), TARI Maruku

(hekta 32), TARI Tengeru (hekta 50), TARI Kifyulilo (hekta 26.5), TARI Dakawa (hekta 50), TARI Tumbi (hekta 60), TARI Naliendele (hekta 37), TARI Mikocheni (hekta 60), TARI Ifakara (hekta 36.4) TARI Ukiriguru (hekta 47) na TARI Mlingano (hekta 20).

292. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 1,000 katika vituo vya TARI Uyole (hekta 800) na TARI Ukiriguru (hekta 200). Kukamilika kwa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kutaiwezesha TARI kuendelea kuzalisha na kutafiti mbegu mwaka mzima. Pia, itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na uongezaji thamani wa mazao ya zabibu na korosho kwa wakulima 800 na Maafisa Ugani 180 katika maeneo ya uzalishaji.

293. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia TARI itaendelea na ujenzi wa nyumba tatu (3) za watumishi, jiko na hosteli katika Kituo cha Utafiti wa Kahawa cha Mwayaya (Buhigwe). Aidha, TARI itanunua mashine ya kukaanga kahawa yenye uwezo wa kukaanga kilo 60 kwa siku na kusimika kwenye maabara ya kutathmini ubora wa kahawa katika kituo hicho.

**5.1.2 Uzalishaji na usambazaji wa mbegu na miche bora na kutoa ruzuku ya mbegu na miche bora kwa baadhi ya mazao**

295. ***Mheshimiwa Spika***, mahitaji ya mbegu bora kwa mwaka ni tani 127,650. Katika mwaka 2025/2026, uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 63,526.54 hadi tani 90,000. Kati ya mbegu zitakazozalishwa, ASA itazalisha tani 15,000 na tani 75,000 zitazalishwa na sekta binafsi. Aidha, upatikanaji wa mbegu bora nchini unatarajiwa kuongezeka kutoka tani 79,700.62 hadi tani 105,000.

296. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2025/2026 imepanga kuendelea kutoa ruzuku ya mbegu bora kwenye mazao ya kimkakati ya alizeti tani 5,000 na mahindi tani 52,000. Aidha, katika kuimarisha uzalishaji wa mbegu bora, ASA itajenga na kusimika miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 3,000 ya Namtumbo (hekta 1,000), Mbozi (hekta 500), Msimba (hekta 200), Kilimi (hekta 160), Arusha (hekta 240), Msungura (hekta 100) na Luhafwe (hekta 800).

Vilevile, ASA itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 495 ya Kilimi (hekta 100), Mbozi (hekta 100), Arusha (hekta 100) na Msimba (hekta 195).

297. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itafunga miundombinu ya umwagiliaji kwa njia ya matone katika kituo cha mauzo ya mbegu Njombe (hekta 0.4) na kiwanja cha maonesho ya Nanenane Morogoro (hekta 2.4). Pia, itakarabati miundombinu ya umwagiliaji kwenye eneo la hekta 568 katika shamba la mbegu Kilangali.

298. ***Mheshimiwa Spika***, ili kulinda mashamba ya mbegu dhidi ya uvamizi, ASA itaendelea na ujenzi wa uzio katika mashamba ya kuzalisha mbegu ya Mwele (km 14), Namtumbo (km 33.3), Kilangali (km 23) na Arusha (km 17). Vilevile, ASA itajenga uzio katika mashamba ya Mbozi (km 40), Dabaga (km 22), Msungura (km 5), Bugaga (km 10) na Luhafwe (km 13). Aidha, itajenga nyumba 29 za watumishi katika mashamba ya mbegu ya Namtumbo (3), Arusha (3), Bugaga (3), Kilangali (3), Mbozi (3), Msimba (3), Dabaga (3), Mwele (3) na Kilimi (5). Pia, itajenga ofisi moja (1), karakana katika shamba la mbegu la Kilimi na Kukarabati ofisi mbili (2) katika mashamba ya mbegu ya Mwele na Mbozi.

299. ***Mheshimiwa Spika,*** ASA itajenga ghala mbili (2) zenye uwezo wa kuhifadhi mbegu jumla ya tani 2,500 katika shamba la BBT Ndogowe (tani 1,000) na shamba la mbegu la Arusha (tani 1,500). Vilevile, itanunua na kusimika mitambo minne (4) yenye uwezo wa kuchakata tani 16 za mbegu kwa saa katika mashamba ya mbegu ya Kilimi, Mwele, Arusha na Njombe na mashine moja (1) ya kukausha mbegu katika shamba la Kilimi.

300. ***Mheshimiwa Spika***, ASA itanunua magari matano (5) na lori moja (1) kwa ajili ya usimamizi wa mashamba na usambazaji wa mbegu na kukarabati nyumba za watumishi, karakana na jengo la kuanikia mbegu katika shamba la mbegu Msimba. Aidha, katika kuboresha afya ya udongo kwenye mashamba ya uzalishaji wa mbegu yaliyoathirika na tindikali, ASA itanunua chokaa mazao tani 1,000 na kutumia kwenye mashamba hayo.

301. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Bodi za Mazao na Taasisi, itazalisha na kusambaza kupitia mpango wa ruzuku miche 64,183,900 ya mazao ya mkonge (miche 4,000,000), kahawa (miche 30,000,000), parachichi (miche 2,100,000), karafuu (miche 250,000), korosho (miche 10,000,000), nazi (miche 2,000,000), miembe (miche 16,000), zabibu (miche 550,000), chai (miche 2,350,000), migomba (miche 1,917,900), kakao (miche 1,000,000), chikichi (miche 10,000,000) na pingili za muhogo 4,361,600. Aidha, katika kuhakikisha ufanisi wa usambazaji wa miche kwa wakulima, Wizara itaandaa mfumo wa kidijiti utakaosaidia kufanya ufuatiliaji wa usambazaji na maendeleo ya miche iliyosambazwa.

302. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuimarisha uthibiti wa ubora wa mbegu, TOSCI itakagua mashamba ya mbegu yenye ukubwa wa hekta 100 ili kuhakiki vigezo vinavyohitajika katika uzalishaji wa mbegu bora. Vilevile, itanunua mtambo wa kuchapisha lebo zinazotumika katika vifungashio vya mbegu na kutoa lebo 32,000,000 za mbegu bora.

303. ***Mheshimiwa Spika***, TOSCI itatoa mafunzo kwa wakaguzi wa mbegu 50 na wakaguzi wa mbegu walioidhinishwa (ASI's) 40 katika mikoa 25 ya Tanzania Bara. Pia, itaendelea na ukarabati wa ofisi za TOSCI Makao Makuu na ofisi za kanda kwa ajili ya kuongeza ufanisi, utendaji wa watumishi na kusogeza huduma kwa wadau wa mbegu.

### 5.1.3 Uwekezaji kwenye utoaji wa ruzuku ya mbolea na viuatilifu

#### a) Upatikanaji wa mbolea

304. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia TFRA itaratibu upatikanaji wa tani 1,500,000 za mbolea na kuzisambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Vilevile, TFC itanunua na kusambaza mbolea tani 200,000 kwa ajili ya mazao ya chakula na kuanza mchakato wa kujenga kiwanda cha kuzalisha mbolea aina ya (Triple SuperPhosphate – TSP) katika Mkoa wa Songwe. Aidha, TFC itanunua mbolea tani 133,000 kwa ajili ya zao la tumbaku na tani 500 kwa ajili ya zao la chai. Pia, Wizara itanunua tani 200,000 za mbolea na chokaa mazao tani 50,000 katika viwanda vya ndani.

305. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuwezesha usambazaji wa mbolea, Wizara kupitia TFC itanunua malori matano (5) yenye uwezo kubeba tani 15 kila lori. Vilevile, katika kuimarisha uhifadhi wa mbolea, TFC itakamilisha ukarabati wa ghala tatu (3) za kuhifadhi mbolea zilizopo katika mikoa ya Mbeya, Njombe na Ruvuma. Pia, TFC itajenga kiwanda cha kuchakata mbolea kwa kushirikiana na Bodi ya Pamba Tanzania na SHIRECU.

306. ***Mheshimiwa Spika,*** TFC itakamilisha usimikaji wa mitambo ya kuchanganya mbolea (Bulk Blending Facilities) yenye uwezo wa kuchanganya tani 120 kwa saa na kuanzisha mradi wa kuchimba, kufungasha na kusambaza chokaa mazao katika eneo la Visiga Mkoa wa Pwani. Wizara itawezesha ruzuku maalum ya uzalishaji wa mbolea kwa viwanda vya ndani ya nchi na kuviwezesha kuzalisha tani 200,000 na tani 50,000 za chokaa mazao.

**b) Upatikanaji wa Viuatilifu na Udhibiti wa Visumbufu vya mazao na mimea**

307. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TFC katika mwaka 2025/2026, itanunua na kusambaza viuatilifu vya pamba lita 1,000,000 na tumbaku lita 1,000,000 kwa ajili ya udhibiti wa visumbufu kwenye mazao hayo na kusambaza kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku. Vilevile, kupitia TPHPA itanunua na kusambaza lita 125,500 za viuatilifu kwa ajili ya kudhibiti milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao kwa mpango wa ruzuku. Viuatilifu hivyo vinahusisha lita 3,000 kudhibiti viuadudu, lita 100,000 kwa ajili ya kudhibiti vivutawadudu, lita 10,000 kwa ajili ya kudhibiti kwelea kwelea, lita 1,000 kwa ajili ya kudhibiti nzige, lita 9,000 kwa ajili ya kudhibiti viwavijeshi vamizi na lita 2,500 kwa ajili ya kudhibiti nzi wa matunda na kilo 7,500 kwa ajili ya kudhibiti panya.

308. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha udhibiti wa visumbufu vya mazao na mimea, Wizara itanunua ndege moja (1) na ndege nyuki 20 kwa ajili ya kunyunyizia viuatilifu. Vilevile, itaendelea kuimarisha matumizi ya njia za kibaolojia kwa kuzalisha wadudu rafiki na kusajili viuatilifu hai kwa ajili ya udhibiti wa wadudu waharibifu wa mazao. Aidha, itajenga Ofisi za TPHPA Makao Makuu ili kuongeza ufanisi kwa watumishi. Pia, TPHPA itakagua maduka 4,000 ya viuatilifu ili kukabiliana na uwepo wa viuatilifu

bandia na chakavu nchini. Kadhalika, TPHPA itaanzisha vituo vya kilimo anga katika mikoa ya Mwanza, Dodoma na Mbeya.

**5.1.4 Usajili wa Wakulima na Urasimishaji wa Shughuli za Kilimo**
309. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kurasimisha shughuli za kilimo kwa kusajili wakulima, wafanyabiashara wa mazao ya kilimo, watoa huduma za ugani, ghala na pembejeo za kilimo ili kuweka utaratibu utakaosimamia shughuli zote za wadau hao na kusajili wakulima wadogo watakaopimiwa afya ya udongo katika mashamba yao. Vilevile, Wizara kupitia TFRA itaendelea kutoa hatimiliki na kadi za kielektroniki (smart card) kwa wakulima 10,000 zitakazowawezesha kupata huduma mbalimbali ikiwemo kununua pembejeo za kilimo.

**5.1.5 Kuwekeza kwenye ujuzi kwa wataalam wa ndani**
310. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, kupitia mpango wake wa kuendeleza mafunzo itawawezesha watumishi 151 kupata mafunzo ya muda mrefu na mfupi katika vyuo vya ndani na nje ya nchi ili kuendana na mahitaji ya taaluma. Kati ya hao, Shahada ya uzamivu (22), Shahada ya uzamili (64), Shahada (37) na Stashahada (3) na mafunzo ya ujuzi maalum 25.

**5.1.6 Uwekezaji kwenye Huduma za Ugani**
311. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kununua na kusambaza vitendea kazi kwa Maafisa Ugani ikiwemo magari 100, vishikwambi 3,000 na mavazi maalum ya utambulisho 5,000. Vilevile, itaendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye viwanja vya maonesho ya wakulima ya Nanenane katika viwanja vya Nzuguni (Dodoma) na John Mwakangale (Mbeya) na kuanza ujenzi wa uzio katika viwanja vya Ipuli (Tabora).

312. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itakamilisha taratibu za uanzishaji wa Wakala wa Huduma za Ugani wa Taifa na kuwa na Maafisa Kilimo waratibu wa Kata. Pia, Wizara itaanzisha mfumo wa huduma za ugani wa kidijiti ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za ugani kwa sekta binafsi.

313. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TARI itaendelea kuimarisha vituo nane (8) mahiri vya usambazaji na uhaulishaji wa teknolojia katika viwanja vya maonesho ya kilimo Nanenane kwa kuweka miundombinu ya umwagiliaji ili kuwezesha shughuli za kilimo na mafunzo ya kilimo kwa wakulima kufanyika mwaka mzima.

314. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuwawezesha Maafisa Ugani kuwa karibu na wakulima, Wizara itajenga nyumba 50 za Maafisa Ugani. Vilevile, Wizara itachukua Vituo vyote vya Rasilimali za Kilimo vya Kata (Ward Resource Centres – WARC's) na kuanza kuvikarabati ili kuwezesha wakulima kupata mafunzo ya kilimo kupitia huduma za kilimo katika vituo hivyo. Pia, Wizara kwa kushirikiana na VETA na CAMARTEC itatoa mafunzo kuhusu uhaulishaji na matumizi ya teknolojia za zana za kilimo.

315. ***Mheshimiwa Spika,*** kupitia Bunge lako Tukufu ninaomba kuzitaarifu Halmashauri zote nchini zilizokabidhiwa WARCs na kushindwa kutumia kwa malengo yaliyowekwa ya kutoa mafunzo ya ugani kwa wakulima na kuzifanya kuwa ofisi za Maafisa Watendaji, waanze kuandaa ofisi hizo kwa ajili ya matumizi ya kilimo na tayari bajeti imetengwa kwa ajili ya kuanza ukarabati.

316. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia, Wizara itakarabati miundombinu ya vituo vya uhaulishaji wa teknolojia za kilimo vya KATRIN, Inyala, Igurusi, Mtwara, Mlingano, Tumbi, Mubondo, Bihawana FTC na Ichenga FTC. Vilevile, itajenga miundombinu ya Chuo cha Taifa cha Sukari Kidatu ili kuwa kituo mahiri cha tasnia ya sukari katika ukanda wa SADC na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia.



*Mchoro unaonesha muonekano wa jengo la Hostel itakayojengwa katika chuo cha Taifa cha Sukari – Morogoro*

317. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia vituo vya kuhaulisha teknolojia za kilimo itaendesha programu za uhaulishaji teknolojia za kilimo, mafunzo ya kanuni za kilimo bora na kilimo biashara kwa wakulima 20,000. Pia, itaendelea kutoa mafunzo rejea kwa Maafisa Ugani 7,000. Vilevile, Wizara kupitia vituo mahiri vya kuhaulisha teknolojia za kilimo ambavyo vimeteuliwa kwa ajili ya kuwajengea wanafunzi umahiri kwenye mnyororo wa uzalishaji na usimamizi wa mazao mahsusi, itagharamia mafunzo kwa vitendo wanafunzi 1,920 wa ngazi ya Stashahada.

**5.1.7 Kupima Afya ya Udongo kwa wakulima wadogo na wakubwa**

318. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika kuhakikisha matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo kwa wakulima, itaendelea na upimaji wa afya ya udongo na kuchora ramani za kidijiti zinazoonesha hali ya afya ya udongo na kutoa mapendekezo ya matumizi sahihi ya pembejeo za kilimo katika maeneo yote yaliyotengwa kwa ajili ya kilimo katika ngazi za vijiji. Vilevile, itanunua na kusambaza *soil scanner* 43 kwa ajili ya kupima afya ya udongo. Aidha, Wizara itajenga ofisi tatu (3) za usimamizi na mipango ya matumizi ya ardhi ya kilimo katika kanda ya Ziwa (Mwanza), Mashariki (Morogoro) na Mbeya kwa ajili ya kusogeza huduma kwa wakulima. Pia, Wizara itanunua *mobile soil laboratory van* kwa ajili ya kupima afya ya udongo.

**5.1.8 Uendelezaji wa kilimo cha umwagiliaji**

319. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji katika mwaka 2025/2026 itaendelea na utekelezaji wa miradi 768 kati ya 780 iliyoanza kutekelezwa mwaka 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025 kama ifuatavyo: -

i. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu mpya 60 zenye jumla ya hekta 147,433.46;

ii. Ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika skimu 41 zenye jumla ya hekta 72,175;

iii. Ujenzi wa mabwawa 19 yenye mita za ujazo 326,449,973.00 na kuanza ujenzi wa mabwawa 28 yenye mita za ujazo 487,361,277. Aidha, itaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabwawa 65;

iv. Ujenzi wa skimu katika mabonde 14 ya kimkakati na kukamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mabonde nane (8);

v. Ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba matatu (3) ya pamoja ya Membe, Ndogowe na Chinangali. Aidha, itaendelea na upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa mashamba matatu (3) makubwa katika mkoa wa Kagera, Njombe na Kigoma; na vi. Upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa skimu 429 na kuanza ujenzi/ukarabati wa skimu 98 ambazo upembuzi na usanifu umekamilika.

320. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea na ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde ya mto Ngono na Bugwema yenye jumla ya hekta 22,770. Vilevile, Tume itaendelea na ujenzi wa mabwawa ya Mbakiamtuli na Ngorongo katika bonde la Rufiji yenye jumla ya mita za ujazo 57,548,653 zitakazomwagilia skimu zenye jumla ya hekta 64,800. Pia, itajenga miundombinu ya umwagiliaji katika bustani ya mimea Chamwino (Dodoma).

321. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume itaanzisha mfumo wa usimamizi wa mashamba ya Mbarali Estate (ekari 6,437.5), Membe (ekari 2,500), Bugwema (ekari 7,500), Madibira (ekari 8,000) na Lumpungu (ekari 18,045) na kuhakikisha mashamba hayo yana hati na Serikali inakuwa na uwezo wa kurudisha gharama za uwekezaji. Vilevile, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itajenga mabwawa mawili (2) ya Dudumizi na Mambi katika shamba la Mbarali Estate.

322. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji kwenye maeneo yasiyopata mvua za kutosha, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itakamilisha upembuzi yakinifu na usanifu wa kina na kuanza ujenzi wa miradi ya umwagiliaji kwa ajili ya kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika kwa shughuli za kilimo. Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (5) na ukikamilika utaongeza eneo la umwagiliaji takriban hekta 3,000,000 na mabwawa 52 ya umwagiliaji ambapo utanufaisha wakulima wa mikoa 12 ikiwemo mikoa ya Simiyu, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Kigoma na Katavi, Wilaya 69, Kata 192 na Vijiji 943. Vilevile, itafanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa sita (6) ya Dabalo, Buigiri, Hombolo, Kimagae, Kidete na Ikowa. Mabwawa hayo yatatumika kuzuia mafuriko katika reli ya kati na kutumika katika shughuli za kilimo cha umwagiliaji.

323. ***Mheshimiwa Spika,*** kukamilika kwa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji iliyoanza mwaka 2022/2023, 2023/2024 na 2024/2025 kutaongeza eneo la umwagiliaji kwa hekta 543,366.46 na kufanya eneo linalomwagiliwa kufikia hekta 1,270,647.06 sawa na asilimia 105.89 ya lengo la kufikisha hekta 1,200,000. Aidha, kukamilika kwa miradi hiyo ikiwemo mabwawa kutawezesha upatikanaji wa maji ya uhakika kwa ajili ya kilimo na hivyo kuwezesha kilimo kufanyika zaidi ya mara mbili kwa mwaka katika maeneo mengi nchini.

324. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza ufanisi wa watumishi kwenye usimamizi wa shughuli mbalimbali za umwagiliaji nchini, Wizara kupitia Tume katika mwaka 2025/2026 itakamilisha ujenzi wa Ofisi ya Umwagiliaji ya Makao Makuu, itaendelea na ujenzi wa

Ofisi za mikoa 19 na Wilaya 13 na ukarabati wa ofisi nne (4) za mikoa. Vilevile, Tume itanunua pikipiki 100, magari 30 na mitambo mitatu (3) kwa ajili ya usimamizi, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji. Aidha, itajenga maabara moja (1) ya uhakiki wa ubora wa ujenzi katika Mkoa wa Dodoma.

325. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuhakikisha uendelevu wa miundombinu ya umwagiliaji nchini, Wizara kupitia Tume itaendelea kutoa mafunzo ya uendeshaji, usimamizi na matunzo ya miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima viongozi 3,000 na kusajili Vyama vya Umwagiliaji 300.

**5.1.9 Uanzishaji wa Vituo vya kutoa Huduma na Ununuzi wa Zana za Kilimo**

325. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara imeendelea kuhamasisha matumizi na umiliki wa zana za kilimo za kisasa kwa wakulima wadogo ambao wengi wao wana uwezo mdogo wa kumiliki zana hizo kutokana na gharama kubwa.

326. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kupitia Bunge lako Tukufu kutangaza rasmi kuwa, Wizara katika mwaka 2025/2026 itatoa huduma za zana za kilimo ambapo wakulima watalipia gharama za huduma hiyo kwa bei ya ruzuku (subsidized mechanization services). Katika kutekeleza azma hiyo, Wizara itaanzisha vituo 1,000 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima; kununua matrekta 10,000 na zana zote za msingi zinazohitajika kwa ajili ya kufanya kazi za shambani, *power tiller* 10,000 na mashine za kuvunia na kukaushia. Pia, kwa kushirikiana na CAMARTEC na VETA itatoa mafunzo kuhusu uendeshaji na usimamizi wa zana za kilimo kwa waendesha mitambo, wasimamizi wa vituo na watoa huduma 500.

327. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Wizara itanzisha kituo kimoja cha kitaifa (National mechanization centre) ambacho kitakuwa na zana zote za msingi kwa ajili ya kusafisha na kusawazisha mashamba, uchimbaji wa visima na mabwawa na kutoa mafunzo. Mradi huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu (3).

### 5.1.10 Kuendeleza Shoroba za Kilimo na Uzalishaji

328. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo itaendelea kuimarisha shoroba nne (4) za kuendeleza kilimo Tanzania (AGCOT) kulingana na ikolojia za kilimo. Shoroba hizo zitaendelea kuratibiwa na Ofisi ya Mageuzi ya Kilimo (ATO) kwa ajili utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kilimo ikiwemo kusimamia matokeo ya afya ya udongo na kufanya tathmini ya kiuchumi na kujenga msingi wa utaalamu kwenye shoroba hizo ili kuleta taswira halisi ya dhana ya biashara katika kilimo.

329. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara inaendelea kutambua juhudi zinazofanywa na SAGCOT Centre katika kutekeleza miradi ya kilimo. Hivyo, SAGCOT itakuwa sehemu ya AGCOT chini ya usimamizi wa ATO.

330. ***Mheshimiwa Spika,*** nitoe rai kwa wadau wa maendeleo kuendelea kushirikiana na Wizara ya Kilimo katika utekelezaji wa miradi ya kilimo kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika miongozo ya Serikali hususan Mpango Kabambe wa Mageuzi ya Kilimo wa mwaka 2050 katika shoroba hizo.

**Uzalishaji wa Mazao kwa Mwaka 2025/2026**

331. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa katika mwaka 2025/2026 Wizara itaendelea kusimamia mikakati ya uzalishaji wa mazao mbalimbali kulingana na mahitaji ya ndani na soko la kimataifa ili kuongeza tija katika uzalishaji. Mazao hayo yanahusisha Mazao Asilia ya Biashara, Mazao ya Bustani, Mazao ya Chakula, Mazao ya Mafuta na mazao yenye mahitaji makubwa yanayoagizwa nje ya nchi.

**Mazao Asilia ya Biashara**

332. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara ikiwemo pamba, kahawa, mkonge, korosho, tumbaku, pareto, kakao na chai kutoka jumla ya tani 1,451,694.11 mwaka 2024/2025 hadi tani 2,225,000 kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na.5.**

**Jedwali Na. 5**: Malengo ya Uzalishaji wa Mazao Asilia ya Biashara (Tani) Katika Mwaka 2025/2026

| Na. | MAZAO | 2024/2025 Uzalishaji | 2025/2026 Malengo |
|---|---|---|---|
| 1 | Korosho | 528,263.82 | 700,000 |
| 2 | Pamba | 149,361 | 400,000 |
| 3 | Pareto | 3,327 | 5,000 |
| 4 | Kahawa | 81,366 | 85,000 |
| 5 | Tumbaku | 160,000 | 200,000 |
| 6 | Chai | 22,772 | 40,000 |
| 7 | Mkonge | 61,215.55 | 80,000 |
| 8 | Sukari | 431,736.74 | 700,000 |
| 9 | Kakao | 13,652 | 15,000 |
| **JUMLA** | | **1,451,694.11** | **2,225,000** |

333. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kufikia malengo hayo, Mikakati ya uzalishaji wa kila zao ni kama ifuatavyo:-

**Zao la Pamba**

334. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Pamba Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pamba kutoka tani 149,361 mwaka 2024/2025 hadi tani 400,000 mwaka 2025/2026. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kusambaza mbegu bora za pamba tani 28,000, chupa (acrepacks) 12,000,000 na vinyunyizi 100,000 kwa wakulima wa pamba. Vilevile, ili kuimarisha udhibiti katika zao la pamba, Bodi itanunua mashine 20 za kupulizia viuatilifu (self propelled boom sprayer).

335. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi itaendelea kuimarisha utoaji wa huduma za ugani katika zao la pamba kwa kuajiri Maafisa kilimo 2,000 kupitia programu ya BBT. Vilevile, Bodi kwa kushirikiana na wadau itazalisha na kusambaza kwa wakulima mbolea hai lita 12,000,000 zenye uwezo wa kunyunyuzia hekta 800,000 na kununua na kusimika mtambo wa kuchakata mbegu wenye uwezo wa kuchakata tani 15,000 kwa mwaka. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaratibu ufufuaji wa *Ginnery* mbili (2) zinazomilikiwa na SHIRECU zilizopo Mhunze na Uzogole.

336. ***Mheshimiwa Spika,*** vilevile, Bodi kwa kushirikiana na MSD na Vyama vya Ushirika itaanzisha kiwanda cha kuchakata na kutengeneza pamba za hospitali na nyuzi kwa ajili ya kufungia tumbaku (cotton twine) katika Mkoa wa Simiyu. Hatua hiyo, itaipunguzia nchi matumizi ya fedha nyingi za kigeni kutokana na uagizaji wa vifaa tiba vinavyotokana na pamba kwa Dola za Marekani Milioni 19.5. Pia, Bodi itaanzisha kongani ya pamba (industrial park) kwenye eneo la ekari 1,000 katika Mkoa wa Simiyu.

337. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Nishati kuanzisha ruzuku ya umeme kwa kongani ya pamba ili kupunguza gharama za uzalishaji. Pia, Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Fedha, Wizara ya Viwanda na Biashara na wadau wa pamba kutengeneza mfumo wa kodi (tax regime) kwa ajili ya viwanda vya nguo zitokanazo na pamba inayozalishwa ndani ya nchi ili kuweka vivutio vya kodi na kuwapa motisha wazalishaji wa ndani zinazolenga kupunguza gharama za uzalishaji, kuimarisha bei ya pamba na kuwalinda wakulima.

338. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itanunua na kusimika mitambo miwili (2) ya kuzalisha nishati ya kupikia inayotokana na masalia ya miche ya pamba na mitambo nane (8) ya kusokota nyuzi za pamba na kuzalisha vikoi na mitandio. Pia, Bodi itaboresha kituo cha mafunzo ya wakulima cha Nyakabindi ili kukiwezesha kutoa huduma za zana za kilimo.

**Zao la Chai**

339. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha tasnia ya chai nchini, Wizara kupitia Bodi ya Chai Tanzania itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa chai kavu kutoka tani 22,772 mwaka 2024/2025 hadi tani 40,000 mwaka 2025/2026. Uzalishaji huo, utafikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la chai kwa wakulima wadogo wa chai 8,000 na kufufua mashamba ya chai yenye ukubwa wa hekta 56 katika Wilaya ya Kilolo.

Vilevile, ili kuimarisha upimaji wa chai inayovunwa, Bodi itajenga vituo sita (6) vya mizani kwenye maeneo mapya ya uzalishaji wa

chai katika Wilaya za Kilolo, Ludewa, Njombe, Lushoto, Korogwe na Tarime.

340. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha masoko na uongezaji thamani wa zao la chai, Serikali itabadili mfumo wa uuzaji wa chai wa wakulima wadogo kutoka kuuza chai majani mabichi na kuanza kuuza chai nyeusi. Bodi itaendelea kuwezesha shughuli za mnada wa chai Tanzania na kununua mashine mbili (2) za kuchakata na kuchanganya chai ambazo zitasimikwa katika ghala la Kipawa lililopo Wilaya ya Ilala ili kuwezesha wafanyabiashara kuuza chai iliyochanganywa kulingana na mahitaji ya soko. Kadhalika, kwa kushirikiana na wadau itaanzisha viwanda sita (6) vya kuchakata chai kavu nyeusi na chai ya kijani katika Wilaya za Kilolo, Mufindi na Korogwe. Kati ya hivyo, viwanda viwili (2) vitajengwa na Serikali na viwanda vinne (4) vitajengwa na sekta binafsi. Aidha, Bodi itaendelea na majadiliano na wamiliki wa kiwanda cha Mvyulu kwa ajili ya kulipa fidia ya kiwanda hicho chenye uwezo wa kuchakata tani 15 za majani mabichi kwa siku na shamba lenye ukubwa wa ekari 200 katika Mkoa wa Njombe. Majadiliano hayo yakishindikana Bodi itajenga kiwanda kipya na fedha zimetengwa kwa ajili ya mradi huo.

341. ***Mheshimiwa Spika,*** kiwanda kilichoanzishwa na iliyokuwa Mamlaka ya Chai Tanzania (TTA) kimepata mwekezaji Kampuni ya Hong Din Xin Investment Limited kwa ajili ya kuendeleza kiwanda hicho cha kuchakata chai maalum (Othodox Tea). Vilevile, Serikali itaanza kufanya tathmini kwa wawekezaji waliobinafshiwa viwanda vya kusindika chai na kushindwa kuviendesha ili kuona namna ya kuvirejesha kwa wakulima kwa kuzingatia sheria zilizopo;

342. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itawezesha upatikanaji wa hati ya kimataifa (ithibati) ya *Rain Forest Alliance* kwa wakulima wadogo wa chai kwa ajili ya uendeshaji wa mashamba katika Halmashauri za Kilolo, Rungwe, Busokelo na Lupembe. Aidha, Bodi itazalisha na kusambaza miche 2,350,000 kwa wakulima na kuanzisha maeneo mapya kwa ajili ya uzalishaji wa miche ya chai katika Wilaya za Bukoba, Kilolo na Mufindi. Pia, itajenga uzio katika ghala la kuhifadhia chai lililopo Kipawa ili kulinda eneo la ghala hilo.

**Zao la Kahawa**
343. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Kahawa Tanzania katika mwaka 2025/2026 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la kahawa kutoka tani 81,366 mwaka 2024/2025 hadi tani 85,000. Ili kufikia lengo hilo, Bodi kwa kushirikiana na TARI itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kahawa na mbinu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakulima 20,000 na Maafisa Ugani 500 kwenye maeneo ya uzalishaji.

344. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi kwa kushirikiana na TARI na sekta binafsi itazalisha na kusambaza miche 30,000,000 ya kahawa kwa mpango wa ruzuku kwa wakulima katika mikoa 17 inayozalisha kahawa nchini. Vilevile, Wizara itaweka mfumo wa kusimamia uaandaji, usambazaji na utunzaji wa miche hiyo. Aidha, Bodi itawezesha uanzishaji wa mashamba ya kahawa yenye ukubwa wa hekta 4,000 katika maeneo yanayozalisha kahawa. Pia, Bodi itachimba visima katika mashamba makubwa ya kahawa (block farm) katika Mkoa wa Kagera ili wakulima wapate maji ya uhakika kwa ajili ya umwagiliaji. Kadhalika, Bodi itajenga maabara za Tissue culture katika vituo vya TaCRI vya Maruku na Mbozi ili kuzalisha miche Milioni 50.

**Zao la Korosho**
345. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania katika mwaka 2025/2026 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 528,263.82 mwaka 2024/2025 hadi tani 700,000. Lengo hilo litafikiwa kwa Bodi ya Korosho Tanzania kwa kushirikiana na *Korosho Cooperative Joint Enterprise* (KCJE) kununua na kusambaza viuatilifu vya korosho tani 30,000 za *Sulphur* na lita 3,800,000 za viuatilifu vya maji kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao hilo. Vilevile, TARI itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la korosho kupitia mashamba darasa 30 kwa wakulima 1,000 na Maafisa Ugani 200 katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Songwe, Pwani, Manyara, Tanga, Kigoma na Dodoma.

346. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha upatikanaji wa miche ya korosho, Bodi kwa kushirikiana na TARI na sekta binafsi itazalisha na kusambaza mbegu za korosho tani 150 katika

Halmashauri zinazolima zao la korosho. Vilevile, Wizara kupitia Bodi itaweka mfumo wa kusimamia uaandaji, usambazaji na utunzaji wa mbegu hizo.

347. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara kupitia Bodi ya Korosho Tanzania itaendelea kuhamasisha uwekezaji, upatikanaji wa masoko na uongezaji thamani wa zao la korosho. Lengo hilo litafikiwa kwa kuendelea na ujenzi wa viwanda vya kubangua korosho pamoja na kuongeza thamani bidhaa nyingine zitokanazo na korosho kama vile mafuta ya ganda la korosho (Cashewnut Shell Liquid – CSL) na viwanda vingine vya mazao ya mafuta katika kongani ya viwanda iliyopo Maranje Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba. Aidha, mwekezaji ataanza kujenga kiwanda cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 100,000 kwa mwaka. Vilevile, Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Nishati kuanzisha ruzuku ya bei ya umeme kwa kongani ya korosho ili kupunguza gharama za uzalishaji. Pia, Bodi itatengeneza mfumo wa upatikanaji wa malighafi kwa wabanguaji wadogo kupitia ghala zinazojengwa katika kongani ya viwanda ya Maranje.

348. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuimarisha uhifadhi na ubora wa korosho, Bodi kwa kushirikiana na Vyama Vikuu vya korosho itajenga ghala tatu (3) zenye uwezo wa kuhifadhi jumla ya tani 15,000 katika vyama vya TANECU, MAMCU na CORECU.

**Zao la Mkonge**

349. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Mkonge Tanzania itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la mkonge kutoka tani 61,215.55 mwaka 2024/2025 hadi tani 80,000 mwaka 2025/2026. Ili kufikia lengo hilo, Bodi kwa kushirikiana na TARI itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mkonge na uongezaji thamani wa zao hilo kwa wadau 200 na Maafisa Ugani 50.

349. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi itaanzisha mashamba makubwa ya pamoja yenye ukubwa wa ekari 20,000 kwa ajili ya wakulima wadogo ili kuongeza uzalishaji wa mkonge katika mikoa ya Morogoro, Tanga, Tabora, Geita, Shinyanga, Singida, Kilimanjaro, Mara, Arusha na Manyara. Vilevile, Bodi itaendelea kuwezesha umiliki wa ardhi ya kilimo yenye ukubwa wa hekta 6,000 kwa ajili

ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja katika mikoa ya Tanga, Singida na Morogoro. Aidha, Bodi kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika itaanzisha Chama Kikuu cha Ushirika cha Mkonge ili kuimarisha ushirika na kufanya ufuatiliaji wa kurudisha mali zilizokuwa za Chama Kikuu cha Ushirika cha Tanga (TARECU).

351. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha masoko na uongezaji thamani wa mkonge, Bodi itanunua na kusimika mashine 10 za kuchakata mkonge (dikotiketa) zenye uwezo wa kuchakata tani mbili (2) kwa siku katika mikoa ya Tanga (6), Morogoro (2), Shinyanga (1) na Tabora (1). Vilevile, Bodi itanunua viwanda na mashamba yaliyokuwa chini ya kampuni ya Sisalana kwa ajili ya kuongeza uzalishaji na kuwezesha uchakataji wa mkonge. Pia, itaendelea na ujenzi wa kituo cha uzalishaji wa nzi chuma (Blacksoldier flies) kwa kutumia mabaki ya mkonge (Sisal waste) ili kutengeneza protini kwa matumizi ya binadamu na mifugo.

**Zao la Tumbaku**

352. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Tumbaku Tanzania itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la tumbaku kufikia tani 250,000 mwaka 2025/2026. Katika kufikia lengo hilo, Bodi itahamasisha na kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la tumbaku kwa wakulima 5,000 na Maafisa Ugani 200 katika maeneo ya uzalishaji.

353. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi ya Tumbaku Tanzania kwa kushirikiana na *Tumbaku Cooperative Joint Enterprise* (TCJE) itaratibu ununuzi na usambazaji wa viuatilifu aina ya Flumetralin lita 183,571, Imidacloprid (30g/pkt) pakiti 1,468,568 na Deltamethrin (20ml/chupa) chupa 2,202,852 kwa ajili ya kudhibiti visumbufu vya zao la tumbaku. Vilevile, itajenga mabani 2,500 ya kukaushia tumbaku na kuanza kutumia teknolojia ya jua na umeme kwa ajili ya ukaushaji wa tumbaku. Aidha, Bodi itaanza kufanya majaribio ya kukausha tumbaku kwa kutumia mitambo inayotumia nishati ya jua kwa lengo la kulinda mazingira na kupunguza ukataji wa miti.

354. ***Mheshimiwa Spika***, Bodi itanunua mitambo minne (4) ya kuchimba mabwawa na visima katika mashamba ya wakulima

wadogo wa tumbaku katika mikoa ya Tabora na Shinyanga ili kuimarisha kilimo cha umwagiliaji. Aidha, Bodi itakamilisha ujenzi wa ofisi katika Halmashauri za Kaliua na Mpanda na kuanza ujenzi wa ofisi mpya katika Manispaa ya Songea kwa lengo la kuimarisha ufanisi, utendaji na kusogeza huduma kwa wadau wa tumbaku. Vilevile, katika kuimarisha uongezaji thamani wa zao la tumbaku, Bodi itaratibu Kampuni ya Mkwawa Leaf kujenga kiwanda cha kuchakata tumbaku tani 28 kwa siku katika Mkoa wa Tabora na kuanzisha bandari kavu kwa ajili ya kupaki tumbaku.

**Zao la Pareto**

355. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa zao la pareto kutoka tani 3,327 mwaka 2024/2025 hadi tani 5,000 mwaka 2025/2026. Ili kufikia lengo hilo, COPRA na TARI kwa kushirikiana na wadau wa zao la pareto watatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la pareto kwa wakulima viongozi 19,000 na wakaguzi wa pareto 50 kupitia mashamba darasa 10 yatakayoanzishwa katika maeneo ya uzalishaji.

356. ***Mheshimiwa Spika***, TARI kwa kushirikiana COPRA itazalisha mbegu bora za pareto tani mbili (2) na kusambaza kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji. Vilevile, COPRA itajenga makaushio 150 katika Halmashauri za Makete, Ileje, Mbeya, Ludewa, Mbulu na Arusha. Aidha, COPRA itahamasisha sekta binafsi katika uongezaji thamani wa zao la pareto ili kuongeza thamani ya mauzo nje ya nchi. Pia, COPRA itaanzisha kilimo cha mkataba katika zao la pareto na kuzuia usafirishaji wa unga wa pareto kwenda nje ya nchi kwa lengo la kuongeza thamani na kulinda viwanda vya ndani.

**Zao la Kakao**

357. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA katika mwaka 2025/2026, itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa kakao kutoka tani 13,652 mwaka 2024/2025 hadi tani 15,000. Uzalishaji huo, utafikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la kakao kwa wakulima viongozi 500 na Maafisa Ugani 45 katika Halmashauri za Kyela, Rungwe, Busokelo, Mlimba na Mvomero. Vilevile, itajenga miundombinu ya usindikaji na

ukaushaji katika vituo saba (7) vya ukusanyaji wa kakao. Aidha, COPRA kwa kushirikiana na wadau itahamasisha uongezaji thamani wa zao la kakao ikiwemo utengenezaji wa *chocolate* kwa soko la ndani na nje ya nchi.

358. ***Mheshimiwa Spika***, ili kukidhi vigezo vya soko la kimataifa, COPRA itasajili wakulima 91,000 wa kakao na mashamba yao ya uzalishaji katika mikoa ya Mbeya, Morogoro na Tanga. Vilevile, COPRA itazalisha miche 1,000,000 na kuisambaza kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku katika mikoa ya Tanga, Kigoma, Kagera na Morogoro. Pia, Wizara itawekeza katika kituo cha TARI Ifakara ili kukifanya kuwa kituo mahiri cha utafiti wa zao la kakao.

**Mazao ya Bustani**

359. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA kwa kushirikiana na wadau katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuhamasisha na kusimamia utekelezaji wa mikakati ya kuendeleza mazao ya bustani itakayowezesha kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kutoka tani 7,518,560.83 mwaka 2023/2024 hadi tani 9,000,000. Uzalishaji huo utafikiwa kwa kutoa mafunzo rejea kuhusu kilimo bora cha mazao ya bustani kwa Maafisa Ugani 1,500 na wakulima 5,000 katika maeneo ya uzalishaji.

360. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itakamilisha ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) vya kuchambua, kufungasha na kuhifadhi mazao ya bustani katika Halmashauri za Mufindi (Iringa) na Rungwe (Mbeya) kwa ajili ya soko la ndani na nje ya nchi. Pia, COPRA kwa kushirikiana na TPHPA itafungua masoko mapya nje ya nchi hususan kwa nchi za Afrika.

**Zao la Parachichi**

361. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa parachichi zinazouzwa nje ya nchi kutoka tani 35,627.02 mwaka 2023/2024 hadi tani 40,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora cha zao la parachichi kwa wakulima 9,500 na Maafisa Ugani 200. Vilevile, Wizara kupitia TPHPA itanunua na kusambaza viuatilifu lita 3,000 za viuakuvu na lita 1,000 aina ya *Copper sulphate* kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku kwa ajili ya kudhibiti visumbufu katika zao la parachichi.

362. ***Mheshimiwa Spika***, ili kuongeza ushindani katika soko la parachichi na kuwezesha wakulima kuuza parachichi nje ya nchi, Tume ya Maendeleo ya Ushirika itahamasisha wakulima kujiunga na Vyama vya Ushirika wa parachichi katika maeneo ya uzalishaji. Aidha, COPRA itaandaa na kusambaza kwa wakulima mwongozo wa viwango vya uzalishaji wa parachichi na mazao ya viungo ili kuwawezesha wakulima kuzalisha kwa kuzingatia viwango vinavyohitajika na soko. Pia, Kutunga kanuni za kusimamia mnyororo wa thamani wa zao la parachichi kwa kutambua wanunuzi, mawakala, kusimamia bei elekezi na kuweka madaraja ya matunda.

363. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uongezaji thamani wa parachichi zinazozalishwa na wakulima wadogo na kuhakikisha hakuna daraja la parachichi litakalotupwa, Wizara itaviwezesha viwanda vya uchakataji na utengenezaji wa bidhaa zitokanazo na parachichi ikiwemo mafuta ya parachichi kwa ajili ya kusafirisha nje ya nchi. Aidha, ili kuhakikisha wakulima hawaibiwi parachichi wanapouza, kila kituo kitakuwa na Afisa atakayesimamia ununuzi wa parachichi. Vilevile, itajenga vituo 100 vya kukusanyia parachichi katika mikoa ya Njombe, Mbeya, Kilimanjaro na Iringa ili kuondoa madalali kwa na kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno. Pia, Wizara itajenga vituo vitatu (3) vya kupanga madaraja na kufungasha parachichi katika mikoa ya Njombe na Mbeya.

364. ***Mheshimiwa Spika***, katika kuhakikisha upatikanaji wa miche bora ya parachichi kwa wakulima wadogo, Wizara kupitia taasisi zake itazalisha na kusambaza miche ya parachichi 2,100,000 kwa mpango wa ruzuku na kuweka mfumo wa kusimamia uaandaji, usambazaji na utunzaji wa miche hiyo. Vilevile, Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itaendelea kuwawezesha wakulima wadogo kupata miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba ya parachichi.

**Zao la Viazi Mviringo**

365. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara katika mwaka 2025/2026, imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la viazi mviringo kutoka tani 2,251,687 mwaka 2023/2024 hadi tani 2,570,061. Ili kufikia lengo hilo, Wizara itaimarisha utafiti wa viazi mviringo kwa kukarabati

vitalu nyumba vinne (4) na kujenga vitalu nyumba vitatu (3) katika vituo vya utafiti vya Igeri (Njombe), Tengeru (Arusha), Uyole (Mbeya) na Nkundi (Rukwa) kwa ajili ya kuzalisha mbegu bora za viazi mviringo; itatoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora na himilivu cha zao la viazi mviringo kwa wakulima. Aidha, itatoa mafunzo kuhusu uzalishaji wa mbegu bora za viazi kwa wakulima wawezeshaji 500 katika mikoa ya Mbeya, Njombe, Morogoro, Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Manyara.
Vilevile, Wizara kupitia COPRA itaandaa na kusambaza mwongozo wa uzalishaji na uuzaji wa viazi mviringo.

**Mazao yenye Mahitaji Makubwa**
366. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mazao na bidhaa za ngano, sukari na mafuta ya kula kutoka nje ya nchi, Wizara itaendelea kuhamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao hayo kwa kuweka na kutekeleza mikakati mbalimbali ikiwemo kununua ardhi yenye ukubwa usiopungua hekta 200,000 kwa ajili ya kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja na kuwapatia wakulima wakubwa na wadogo. Aidha, mikakati mingine ni kama ifuatavyo:-

**Zao la Ngano**
367. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026, imepanga kuongeza uzalishaji wa zao la ngano kutoka tani 118,521 mwaka 2023/2024 hadi tani 300,000. Lengo hilo litafikiwa kwa kuendelea kusambaza mbegu za ngano tani 1,000 kwa wakulima kupitia mpango wa ruzuku na kuanzisha vituo maalum vya kuzalisha mbegu za ngano katika mashamba makubwa ya pamoja.

368. ***Mheshimiwa Spika,*** TARI itaendelea na majaribio ya aina 82 za mbegu mpya za ngano katika mikoa ya Morogoro na Tanga ili kupata mbegu zinazostahimili hali ya joto kwa lengo la kuongeza uzalishaji. Vilevile, Wizara kupitia COPRA itatoa utaratibu wa kiasi cha ngano (import quota) kitakachoingizwa nchini. Pia, Wizara itajadiliana na Wizara ya Fedha kutengeneza utaratibu wa kikodi ili kampuni zinazonunua ngano inayozalishwa nchini zinufaike na motisha hiyo.

369. ***Mheshimiwa Spika***, TOSCI itatoa mafunzo ya uzalishaji wa mbegu za kuazimia ubora (QDS) kwa wakulima 500 katika Wilaya za Nkasi, Babati, Hanang, Songwe, Mbinga, Siha na Makete. Vilevile, TARI itaendelea kufanya utafiti wa mbegu za ngano zenye kukidhi sifa ya mahitaji ya soko na tija katika uzalishaji. Aidha, Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itahamasisha Vyama vya Ushirika kuanzisha mashamba makubwa ya ngano na viwanda vidogo vya kuchakata ngano. Pia, itawezesha upatikanaji wa mitaji kwa wakulima watakaoendesha mashamba hayo kupitia dirisha za *equity* na *guarantee scheme* litakaloanzishwa katika Benki ya Ushirika Tanzania.

***Nitoe rai kwa wasindikaji wa ngano nchini, kuiunga mkono Serikali katika juhudi tulizozianzisha kwa kuhakikisha wakulima wa ngano wanapata soko la uhakika. Lengo hilo linaweza kufikiwa ikiwa wasindikaji watanunua ngano ya ndani ya nchi kwanza kabla ya kuagiza kutoka nje ya nchi kama tulivyokubaliana kwenye mikataba ambayo COPRA imeingia na wasindikaji*** **Zao la Miwa na Uzalishaji wa Sukari**

370. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania katika mwaka 2025/2026, itaongeza uzalishaji wa zao la miwa kutoka tani 4,713,907.89 zilizozalisha sukari tani 431,736.74 mwaka 2024/2025 hadi tani 7,000,000 za miwa zitakazozalisha sukari tani 700,000. Vilevile, kama nchi, tunaagiza sukari ya viwandani tani 250,000 na tumeanza kujitosheleza kwa sukari ya matumizi ya kawaida Uzalishaji huo utafikiwa kwa kusimamia upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Mtibwa na mashamba ya miwa ya kiwanda yaliyopo Dakawa yenye ukubwa wa hekta 12,000.

371. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itasimamia upanuzi wa mashamba yenye ukubwa wa hekta 13,000 ya kiwanda cha sukari Kagera na kusimamia utekelezaji wa mradi wa upanuzi wa kiwanda cha sukari cha Kilombero K4. Vilevile, itasimamia uanzishaji wa vitalu vya kuzalisha miche ya miwa kwenye eneo lenye ukubwa wa hekta 100 katika bonde la Kilombero kwa ajili ya wakulima wadogo wa miwa. Pia, Wizara kupitia Bodi ya Sukari Tanzania imeandaa maeneo kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo cha miwa nchini ikuhusisha eneo la Bonde la Mto Pangani (Korogwe, Muheza, Handeni na Pangani) lenye hekta 146,704.6 na Bonde la

Wembele (Tabora) lenye hekta 15,218 lililopo katika Wilaya za Uyui na Igunga kwa ajili ya uzalishaji wa sukari.

372. ***Mheshimiwa Spika,*** Bodi itaendelea kuratibu uanzishaji wa viwanda vya sukari vya Rai Group na Lake Agro. Halikadhalika, Bodi ya Sukari itaratibu uwekezaji wa kujenga viwanda vitatu katika Mkoa wa Tanga ambapo kimoja ni kwa ajili ya sukari ya viwandani na viwili kwa ajili ya sukari ya kawaida itakayotumika kama malighafi ya kuzalisha sukari ya viwandani. Pia, itakamilisha tathmini ya eneo la Bonde la Busega kwa ajili ya uzalishaji wa miwa na sukari kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Simiyu;

373. ***Mheshimiwa Spika***, TARI itaanzisha kitalu cha miche ya miwa kwenye eneo la ukubwa wa ekari 10 katika mashamba ya Mvomero (ekari 5) na Mkulazi (ekari 5) na kuzalisha mbegu za miwa tani 10 katika Mikoa ya Pwani, Kagera na Morogoro.

**Mazao ya Mafuta**

374. ***Mheshimiwa Spika,*** uzalishaji wa mafuta ya kula nchini umefikia tani 396,335 ikilinganishwa na mahitaji ya takriban tani 650,000 kwa mwaka. Uzalishaji huo unafanya Taifa kuwa na nakisi ya tani 253,665 za mafuta ya kula. Ili kujitosheleza kwa uzalishaji wa mafuta ya kula, Wizara kwa kushirikiana na sekta binafsi itawezesha uchakataji wa mafuta yanayotokana na alizeti na chikichi kwa kuviwezesha viwanda vidogo (backyard processing); kuwawezesha wakulima wakubwa wa alizeti kwa kuwapatia mashamba makubwa ya pamoja katika mikoa ya Singida, Manyara na Dodoma; na kuendelea kushauriana na Wizara ya Fedha kuweka sera za fedha ikiwemo kuongeza ushuru kwenye mafuta ya kula yanayotoka nje ya nchi ili kuvilinda viwanda vya ndani.

375. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itahamasisha wakulima kuongeza uzalishaji wa mazao ya mafuta kutoka tani 2,181,747.65 mwaka 2023/2024 hadi tani 2,200,000 mwaka 2025/2026. Lengo hilo litafikiwa kwa kutekeleza yafuatayo:-

i. Kusambaza mbegu bora za alizeti tani 2,150 kwa wakulima kwa mpango wa ruzuku;

ii. Kuzalisha na kusambaza miche ya chikichi 10,000,000 kwa wakulima katika maeneo ya uzalishaji;
iii. Kuzalisha na kusambaza mbegu bora za karanga tani 20.1 na mbegu za ufuta tani 40;
iv. Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika itahamasisha Vyama vya Ushirika kuanzisha mashamba makubwa ya pamoja na kununua mashine ndogo za kuchakata mafuta;
v. Wizara itaendelea kujadiliana na Wizara ya Fedha ili kuweka utaratibu wa kikodi kwa lengo la kuongeza kodi kwenye mafuta yote yanayotoka nje ya nchi na kutengeneza utaratibu wa usimamizi wa kiutawala ili kulinda viwanda vya ndani; na
vi. Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Nishati kuweka ruzuku ya umeme kwenye kongani za viwanda vya mafuta ya kula katika mikoa ya Singida na Kigoma.

***Mheshimiwa Spika,*** msimamo wa Wizara ya Kilimo ni kuendelea kujadiliana na Wizara ya Fedha kuhusu kufanya mabadiliko ya sera za kodi ikiwemo uongezaji wa tozo kwenye mafuta ya kula na ngano zinazotoka nje ya nchi ili kulinda wakulima na viwanda vya ndani

**5.2 Kuchangia kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo**

376. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza kipaumbele cha kuchangia kuongeza ajira zenye staha kwa vijana na wanawake kufikia 3,000,000 ifikapo mwaka 2030. Ajira hizo zitatokana na utekelezaji wa Programu za kuendeleza mashamba makubwa ya pamoja; na kuwezesha uendelezaji wa programu ya BBT ngazi ya Halmashauri.

377. ***Mheshimiwa Spika,*** Pia, Wizara itaendelea kuwezesha ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wadogo (BBT visima); upatikanaji wa mikopo kwa vijana na wanawake (BBT mitaji); na kuongeza thamani ya mazao na kutoa huduma za ugani (BBT Ugani).

**5.2.1 Kuwezesha Upatikanaji wa Ardhi ya Kilimo na Uanzishaji wa Mashamba Makubwa ya Pamoja (BBT – Mashamba)**

378. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itatambua, kupima na kutwaa mashamba yenye ukubwa wa hekta 80,000 kwa ajili ya uwekezaji wa kilimo biashara katika mikoa ya Singida, Njombe, Mara, Geita, Tabora, Mbeya, Songwe na Tanga.

379. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanza uwekezaji katika shamba la Mapogolo – Chunya (Mbeya) lenye ukubwa wa ekari 57,000 kwa kuanza na ekari 20,000 kwa fedha ya Mradi wa *BBT project 1* unaofadhiliwa na Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB) ambapo kazi mbalimbali zitafanyika ikiwemo usafishaji wa shamba; uchimbaji wa visima na mabwawa; uwekaji wa miundombinu ya umwagiliaji; na ujenzi wa nyumba kwa ajili ya vijana na ujenzi wa ghala.

380. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza programu ya BBT kwa kujenga ghala nane (8) zenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika mashamba ya pamoja ya vijana ya Chinangali (ghala 4) na Mlazo/Ndogowe (ghala 4); kujenga chumba cha baridi (cold room) chenye uwezo wa kuhifadhi tani 1,000 katika shamba la Chinangali; itajenga uzio wa umeme (km 27) kuzunguka shamba la Mlazo/Ndogowe; na kununua mitambo ya kuandaa mashamba ikiwemo, *Bulldozers, excuvators, water bowsers, planters, na harvesters* kwa ajili ya mashamba ya Chinangali, Ndogowe na Mapogolo.

**5.2.2 Kuwezesha Uendelezaji wa Programu ya BBT Ngazi ya Halmashauri**

381. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza mradi wa BBT katika Halmashauri 20 zitakazotenga maeneo yasiyopungua ukubwa wa hekta 200 kwa kila Halmashauri (**Jedwali Na. 6**). Wizara itasafisha, kupanga katika vitalu (blocks) na kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika mashamba hayo. Aidha, Wizara itatoa mafunzo ya kilimo biashara kwa vijana na wanawake watakaochaguliwa na Halmashauri zao kutekeleza mradi huo. Pia, katika kutekeleza programu ya BBT ngazi ya Halmashauri, Bodi ya Tumbaku Tanzania itaanzisha mashamba ya

tumbaku yenye ukubwa wa ekari 150 katika Halmashauri za Uyui (ekari 50) na Chunya (ekari 100).

**Jedwali Na. 6:** Idadi ya mashamba kwenye Halmashauri zilizotayari kutekeleza programu ya BBT Halmashauri

| Na. | MKOA | WILAYA | HALMASHAURI ZA WILAYA | JINA LA SHAMBA | IDADI YA EKARI |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kigoma | Kakonko | Kakonko | Kasanda | 200 |
| 2. | Singida | Manyoni | Itigi | Gurugu | 1,000 |
| | | Ikungi | Ikungi | Isuna | 20,000 |
| 3. | Dodoma | Bahi | Bahi | Ikumbulu | 3,600 |
| | | Chemba | Chemba | Gwandi | 3,424.54 |
| 4. | Mbeya | Chunya | Chunya | Nkung'ungu | 11,052.50 |
| | | | | Lualaje | 13,561.25 |
| 5. | Njombe | Njombe | Njombe Vijijini | Ikang'asi | 6,000 |
| | | | Njombe Mji | Utalingolo | 104 |
| 6. | Kagera | Misenyi | Misenyi | Kyakakera | 175.8 |
| | | | | Nkenge | 2,000 |
| | | Muleba | Muleba | Makongora | 296 |
| 7. | Tabora | Kaliua | Kaliua | Limbulakuzo bha/Luyembe | 6,000 |
| 8. | Iringa | Kilolo | Kilolo | Kilolo | 1,250 |
| 9. | Pwani | Kisarawe | Kisarawe | Palaka | 1,683 |
| 10. | Mara | Musoma | Musoma Vijijini | Bugwema | 6,525 |
| 11. | Geita | Nyang'whale | Nyang'whale | Nyamakara | 600 |
| | | | | Nyang'holongo | 800 |
| | | | | Ligembe | |
| | | Geita | Geita MC | Ibanda | 2,200 |
| | | | Geita DC | Saragulwa | 600 |
| 12 | Katavi | Katavi | Katavi MC | Mwamkulu | 3,200 |
| | **JUMLA** | **16** | **18** | **22** | **84,272.09** |

### 5.2.3 Kuwezesha Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji kwa Wakulima wadogo (BBT visima)

382. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji itachimba visima 500 vya umwagiliaji

vitakavyomwagilia eneo lenye ukubwa wa hekta 30,393.39 katika Halmashauri 178 nchini na kunufaisha wakulima 58,903.

**5.2.4 Kuwezesha Upatikanaji wa Mikopo kwa Vijana na Wanawake (BBT mitaji)**

383. ***Mheshimiwa Spika,*** AGITF kwa kushirikiana na benki ya Ushirika Tanzania itaanzisha dirisha maalum litakalotoa huduma za *guarantee scheme, direct lending* na *equity fund* kwa mikopo yenye riba nafuu na fedha za awali zitakazowekezwa ni kutoka AfDB kiasi cha Dola za Marekani **Milioni 35**. Pia, Wizara kupitia AGITF itaweka kiasi cha Shilingi **Bilioni 17** katika dirisha la guarantee scheme ili kutoa mikopo yenye riba nafuu ya thamani ya Shilingi **Bilioni 51** kwa wakulima kwa riba isiyozidi asilimia saba (7%).

384. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaanza majadiliano na Wizara ya Fedha kwa ajili ya kufungua akaunti ya Serikali kwenye Benki ya Ushirika Tanzania.

**5.2.5 Kuwezesha Vijana na Wanawake Kuongeza Thamani ya Mazao**

385. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kutekeleza mradi wa BBT kwa vijana na wanawake 200 kwa kuwapatia mafunzo ya kuongeza thamani ya zao la mkonge ili waweze kuzalisha bidhaa zitokanazo na zao hilo. Aidha, mradi huu utatatekelezwa visiwani Zanzibar na katika Mkoa wa Tanga. Vilevile, Bodi ya Korosho Tanzania itanunua mashine 100 za kubangua korosho na kuwapatia vijana na wanawake 5,000 ili kuongeza thamani ya zao la korosho.

**5.2.6 Kuwezesha Vijana na Wanawake kutoa Huduma za Ugani (BBT Ugani)**

386. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Bodi za mazao kwa kushirikiana na Chuo Kikuu Cha Kilimo cha Sokoine na sekta binafsi itaendelea kutekeleza Mpango wa Ugani (BBT – Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme) kwa ajili ya kuwatengenezea ajira vijana na wanawake 500, kuimarisha utoaji wa huduma za ugani na kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa kutoa huduma za ugani kwa wakulima. Vilevile, kupitia Bodi za mazao vijana na wanawake watahamasishwa

kushiriki katika uzalishaji wa miche ya mazao mbalimbali kulingana na mahitaji.

387. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itatekeleza Programu ya BBT – Miche kwa kuwawezesha vijana na wanawake kuzalisha miche ya mazao. Aidha, miche hiyo itazalishwa kwa kuingia mikataba na Bodi na Taasisi za Wizara.

***Nitoe rai kwa vijana na wanawake wa jamii ya kitanzania kuchangamkia fursa ya kuzalisha miche ambayo itasambazwa kwa wakulima ili kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo***

**5.3 Kuimarisha Usalama wa Chakula na Lishe**

388. ***Mheshimiwa Spika,*** pamoja na juhudi nyingine, Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha usalama wa chakula na lishe nchini kwa kuwekeza kwenye miundombinu ya uhifadhi wa chakula; kuhamasisha uzalishaji wa mazao yaliyoongezewa virutubishi ili kukabiliana na matatizo ya lishe nchini; na kuiongezea NFRA uwezo wa kuhifadhi chakula.

**5.3.1 Uwekezaji kwenye Miundombinu ya Uhifadhi ili kufikia Uwezo wa Kuhifadhi tani 3,000,000 ifikapo Mwaka 2030**

389. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuimarisha uhifadhi wa mazao nchini Wizara kupitia NFRA itakamilisha ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi yenye uwezo wa kuhifadhi tani 165,000 kupitia mradi wa kuongeza uhifadhi wa nafaka. Vilevile, NFRA itaanza ujenzi wa miumbombinu yenye uwezo wa kuhifadhi tani 300,000 katika Kanda za Songea, Makambako, Songwe, Shinyanga na Dodoma. Aidha, Wizara itakarabati ghala 46 katika mikoa ya Shinyanga, Geita, Kigoma, Tabora, Rukwa, Katavi, Mwanza, Manyara na Songwe; na itanunua vifaa kwa ajili ya ghala 28 zilizojengwa katika Mkoa wa Ruvuma. Vilevile, CPB itaanza ujenzi wa miundombinu ya uhifadhi wa mazao ya kilimo yenye uwezo wa kuhifadhi tani 30,000 katika Mkoa wa Ruvuma.

**5.3.2 Kuiongezea NFRA Uwezo wa Kununua Mazao ya Wakulima ili Kuongeza Hifadhi**

390. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha usalama wa chakula nchini Wizara kupitia NFRA katika mwaka 2025/2026 itanunua tani 1,140,000 za nafaka. Pia, NFRA itaendelea kuuza chakula ndani

na nje ya nchi pindi itakapohitajika. Vilevile, NFRA itaanzisha utaratibu wa hati fungani ya usalama wa chakula (Food Security Bond) ili kuongeza uwezo wa kujiendesha.

**5.3.3 Kuhamasisha Matumizi ya Mazao yaliyoongezewa Virutubishi ili Kukabiliana na Matatizo ya Lishe Nchini**

391. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara itaendelea kutekeleza Mpango Kazi wa Lishe katika Kilimo (Nutrition Sensitive Agriculture Action Plan – NSAAP) ili kukabiliana na matatizo ya lishe yanayohusisha udumavu, ukondefu na upungufu wa wekundu wa damu. Mpango kazi huo utaendelea kutekelezwa kwa TARI kuzalisha vipando vya viazi lishe 3,290,000 na kuvisambaza katika mikoa ya Mwanza, Geita, Tabora, Katavi, Kigoma, Shinyanga, Simiyu, Kagera na Mara. Vilevile, TARI itaendelea kutoa mafunzo kuhusu kanuni za kilimo bora kwa wakulima wawezeshaji 2,500 na wazalishaji wa mbegu za viazi lishe 100 katika Halmashauri za Bukombe, Geita, Misungwi, Misenyi na Bukoba.

**5.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Masoko, Mitaji na Mauzo ya Mazao nje ya Nchi**

392. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na wadau katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao kwa kutekeleza mikakati mbalimbali iliyojiwekea.

**5.4.1 Kujenga Miundombinu ya Masoko ya Mazao ya Kilimo kwa ajili ya Wakulima katika Halmashauri mbalimbali Nchini**

**Masoko ya Kimkakati**

393. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo, Wizara itaendelea na ujenzi wa masoko matano (5) ya kimkakati katika Halmashauri za Manispaa ya Kahama (Busoka), Ngara (Kabanga), Kyerwa (Nkwenda na Murongo) na Tarime (Sirari). Ujenzi wa masoko hayo utawezesha kuendeleza biashara ya mazao ya kilimo katika mipaka ya nchi za Uganda, Kenya, Rwanda na Burundi.

**Vituo vya Masoko (Market Sheds)**

394. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara itaendelea na ujenzi wa vituo saba (7) vya masoko (market sheds)

vya Endashangwet (Karatu), Kibakwe (Mpwapwa), Losirwa (Monduli), Ushirika (Nzega mji), Mamsera (Rombo), Mula (Hai) na Kigoma (Kibondo) vilivyoanza mwaka 2023/2024 na 2024/2025. Pia, itaanza ujenzi wa vituo vitatu (3) vya masoko (market sheds) katika Halmashauri ya Moshi (Himo), Singida DC (Merya) na Mpanda Manispaa (Mpanda hoteli). Ujenzi wa vituo hivyo, utawezesha wakulima kukusanya na kuuza mazao yao sehemu rasmi zinazotambulika na mamlaka husika. Vilevile, Wizara kupitia COPRA kwa kushirikiana na Halmashauri itaanzisha masoko manne (4) ya mazao ya kilimo kwenye mipaka ya Rusumo, Namanga, Kasumulo na Holili.

**5.4.2 Kuimarisha Uongezaji Thamani kwa Kushirikisha Sekta Binafsi**

395. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea na ujenzi wa vituo jumuishi viwili (2) katika mikoa ya Iringa (Mufindi) na Mbeya (Rungwe) ili kuwezesha kuchambua, kuhifadhi na kuchakata mazao ya bustani. Vilevile, itajenga miundombinu ya kukaushia, kuchakata na kuhifadhi muhogo katika Halmashauri za Kakonko na Kibondo na tangawizi katika Halmashauri ya Buhigwe. Pia, Wizara kupitia CPB italipa fidia ya viwanda na ghala katika maeneo ya Mzizima (Dar es Salaam) na Isaka (Shinyanga) kwa ajili ya kuchakata na kuhifadhi mazao. Kadhalika, CPB kununua tani 78,897 za nafaka na mazao mchanganyiko kwaajili ya uchakataji.

**5.4.3 Kuongeza Mauzo ya Mazao ya Kilimo Ndani na Nje ya Nchi**

396. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuongeza mauzo ya mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kushirikiana na sekta binafsi kuimarisha biashara ya mazao ya kilimo kwa kusimamia mikakati ya uzalishaji na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi kutoka Dola za Marekani Bilioni 3.54 mwaka 2023/2024 hadi takriban Dola za Marekani Bilioni 4. Vilevile, Wizara kupitia TPHPA, itakamilisha mchakato wa ufunguzi wa masoko mapya 15 kwa ajili ya mazao ya nafaka, bustani, mikunde na tumbaku.

397. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara kupitia COPRA itaandaa na kusambaza miongozo kuhusu uuzaji, ununuzi, usindikaji, uhifadhi, usafirishaji na uingizaji wa mazao ndani na nje ya nchi. Vilevile, COPRA kwa kushirikiana na Shirika la Viwango Tanzania (TBS)

itaandaa viwango vya uzalishaji wa mazao ya ufuta, mbaazi, dengu, viungo, kakao, parachichi, vitunguu na viazi mviringo. Aidha, itatoa mafunzo kuhusu viwango vya ubora wa mazao ya bustani kwa wakulima viongozi 4,500 katika mikoa ya Pwani, Iringa, Kilimanjaro, Manyara, Tanga, Mbeya, Morogoro na Arusha na kuwajengea uwezo wadau 5,350 kuhusu taratibu za usafirishaji wa mazao ya kilimo ndani na nje ya nchi na kanuni za kilimo cha mkataba, usajili na utoaji wa vibali na udhibiti ubora. Pia, itaendelea kuimarisha mifumo ya ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo ikiwemo TMX, minada na Stakabadhi za Ghala ili kuimarisha bei za mazao ya kilimo.

**5.4.4 Kuimarisha Upatikanaji wa Mitaji**

398. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 kupitia AGITF itaanzisha dirisha la dhamana na mitaji kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa mitaji yenye riba nafuu kwa wakulima katika Benki ya Ushirika Tanzania. Vilevile, itaendelea kushirikiana na taasisi za fedha katika kuimarisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu kwenye sekta ya kilimo. Aidha, TADB itaongeza idadi ya taasisi za fedha zinazotumia mfuko wa dhamana wa TADB kutoka taasisi 19 hadi 21 ili kurahisisha utoaji wa mikopo yenye riba nafuu katika shughuli za kilimo; na kuendelea na ujenzi wa ofisi ya AGITF Makao Makuu katika Mkoa wa Dodoma. Pia, Majadiliano ndani ya Serikali yameanza kwa ajili ya kuandaa sera ya ugharamiaji wa uwekezaji kwenye kilimo (Agriculture financing policy).

**5.4.5 Kuziwezesha Maabara za Serikali ziweze kufikia Viwango vya Ubora vinavyotakiwa Kimataifa**

399. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia TPHPA itaanza ujenzi wa maabara ya kisasa katika Mkoa wa Njombe kwa ajili ya kupima ubora wa mazao ili kusogeza huduma kwa wadau wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini na mikoa ya jirani. Vilevile, itaendelea kuimarisha maabara ya TPHPA Makao Makuu kwa kununua na kufunga vifaa vya kisasa vya maabara. Aidha, TOSCI itakamilisha ukarabati wa maabara ya Makao Makuu katika Mkoa wa Morogoro na maabara ya kupima ubora wa mbegu iliyopo katika Mkoa wa Arusha.

400. ***Mheshimiwa Spika***, TARI itakamilisha ujenzi na ununuzi wa vifaa vya maabara ya magonjwa ya mimea (Patholojia) katika

kituo cha TARI Naliendele na maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa katika kituo cha TARI Maruku. Vilevile, itaimarisha maabara za kuzalisha miche kwa njia ya chupa kwa kununua vifaa vya maabara katika vituo vya TARI Tengeru, TARI Mikocheni na TARI Mlingano. Pia, TARI itakamilisha upatikanaji wa ithibati ya maabara ya udongo katika kituo cha TARI Mlingano.

**5.5 Kuimarisha Maendeleo ya Ushirika**

401. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia Tume ya Maendeleo ya Ushirika katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha Vyama vya Ushirika, kwa kuimarisha mifumo ya kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa Vyama vya Ushirika; kuwezesha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuviwezesha kupata mitaji; na kuhamasisha ushirika kwenye sekta mbalimbali na makundi maalum. Ili kufikia malengo hayo, Wizara kupitia Tume itatekeleza yafuatayo:-

**5.5.1 Kuimarisha mifumo ya Kidijiti kwenye Vyama vya Ushirika na Mamlaka za Usimamizi**

402. ***Mheshimiwa Spika,*** ili kuimarisha ukusanyaji, utunzaji, usimamizi na uwezeshaji wa wadau kupata kwa urahisi na kwa wakati, taarifa na takwimu rasmi za maendeleo ya ushirika, Tume itatengeneza *dashboard* kwenye Mfumo wa MUVU na kuunganisha *Mfumo* wa MUVU na mifumo mingine ya TEHAMA inayotumiwa na Vyama vya Ushirika na Taasisi zingine za Serikali. Aidha, itakagua mifumo ya TEHAMA inayotumiwa na Vyama vya Ushirika kwa lengo la kutathimini ufanisi wake.

**5.5.2 Kuimarisha Usimamizi na Udhibiti wa Vyama vya Ushirika**

403. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itaendelea kuratibu na kusimamia utambuzi na uthaminishaji wa mali za Vyama vya Ushirika 5,973 na itaandaa Mpango wa Matumizi na Uendelezaji mali hizo. Aidha, Tume itaandaa kitabu kitakachoonesha fursa za uwekezaji zilizopo kwenye Vyama vya Ushirika. Pia, itafanya ufuatiliaji wa mali za Vyama vya Ushirika vilivyofutwa ikiwemo Chama Kikuu cha Ushirika cha Tanga (TARECU) na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC).

### 5.5.3 Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kujiendesha kibiashara na kuviwezesha kupata mitaji

404. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume kwa kushirikiana na Benki ya Ushirika Tanzania itaendelea kuwezesha Vyama vya Ushirika kuingia katika mfumo rasmi wa kifedha kwa kuhamasisha Vyama Vikuu kuwa mawakala wa Benki na kufungua matawi katika mikoa ya Kagera, Dar es Salaam, Mwanza, Mbeya, Katavi na Ruvuma. Vilevile, ili kuongeza thamani ya zao la korosho Tume itasimamia Chama Kikuu cha Tandahimba na Newala (TANECU) kujenga kiwanda kipya cha kubangua korosho chenye uwezo wa kubangua tani 3,500 kwa mwaka katika wilaya ya Tandahimba. Pia, itafufua kiwanda cha kuchakata pamba cha Manawa na kulipa fidia za hisa za Serikali ili kimilikiwe na ushirika; na kufufua viwanda vya kuchakata pamba vya Buyagu na Magu.

405. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itasimamia Chama Kikuu cha Ushirika cha Kahama (KACU) kujenga kiwanda cha kukamua mafuta ya kula ili kuongeza thamani na kukidhi mahitaji ya soko. Aidha, itaratibu ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza majora ya nguo kitakachojengwa katika Mkoa wa Simiyu. Pia, itasimamia Chama Kikuu cha Tabora (WETCU) kujenga kiwanda cha kutengeneza nyuzi za kusukia tumbaku katika kongani ya viwanda vya pamba itakayojengwa katika Mkoa wa Simiyu.

406. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume katika mwaka 2025/2026 kwa kushirikiana na WRRB, COPRA na TMX, itaendelea kuimarisha mifumo rasmi na jumuishi ya biashara na masoko ya mazao katika Vyama vya Ushirika. Vilevile, itahamasisha Vyama vya Ushirika kuendelea kuuza mazao ya kilimo kupitia mifumo rasmi ili kuongeza mauzo ya mazao ndani na nje ya nchi.

### 5.5.4 Kuhamasisha Ushirika kwenye Sekta mbalimbali na Makundi Maalum

407. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume katika mwaka 2025/2026 itahamasisha vikundi 105 vinavyotekeleza shughuli za kiuchumi katika Sekta ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi, Madini, Viwanda na Fedha ili kuunda Vyama vya Ushirika.

408. ***Mheshimiwa Spika***, Tume itaratibu uanzishwaji wa Kampuni ya Bima ya Ushirika itakayomilikiwa na wanaushirika wenyewe,

kwa lengo la kutoa huduma za kibima zitakazowakinga na vihatarishi vya aina mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei za mazao, majanga yanayotokana na mabadiliko ya tabia nchi na magonjwa ya mazao na binadamu. Aidha, Tume kwa kushirikiana na watoa huduma za Bima itahamasisha Vyama vya Ushirika kujiunga na Bima mbalimbali. Pia, itahamasisha wanaushirika kujiunga na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa lengo la kuwezeshwa kujikinga na majanga ikiwemo visumbufu vya mimea na mazao, mabadiliko ya tabianchi na moto.

409. ***Mheshimiwa Spika,*** Tume itaandaa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Ushirika utakaoonesha hali halisi ya ushirika katika sekta mbalimbali na fursa za uwekezaji zilizopo nchini. Vilevile, Tume itaanzisha SACCOS kwenye AMCOS zinazosimamiwa na Vyama Vikuu ili kurahisisha upatikanaji wa mikopo kwa wanachama.

**5.6 Kuimarisha Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA Katika Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo**

410. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kuendelea kuimarisha utendaji kazi, matumizi bora ya rasilimali za kilimo, ufuatiliaji, kutoa tahadhari ya mapema kuhusu udhibiti wa milipuko ya visumbufu vya mazao na mimea, kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kuongeza ufanisi wa utoaji wa huduma kwa wadau wa kilimo. Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika kilimo.

**5.6.1 Kuwekeza kwenye Matumizi ya Mifumo ya Kidijiti katika Sekta ya Kilimo**

411. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuimarisha mfumo wa *e – Kilimo* kwa kuendelea kujenga moduli ya taarifa za kilimo na kijiografia zitakazopatikana kwa lugha nyepesi ya ramani ikiwemo kuonesha mashamba, ghala, aina za udongo na maeneo ya umwagiliaji. Vilevile, itaboresha mawasiliano na njia ya kubadilishana taarifa za wadau wa kilimo (Agriculture data digitalization value chain) ili kuimarisha utendaji kazi, masoko, uwekezaji na matumizi bora ya rasilimali za kilimo.

412. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itaanzisha maktaba ya kidijiti (e-library) kwa ajili ya kutunza kumbukumbu za kilimo na itaendelea kutoa huduma za ugani kwa wakulima kidijiti. Aidha, kupitia TPHPA itaanzisha moduli ya kufuatilia mazao (crop traceability module) yanayosafirishwa nje ya nchi ili kulinda soko la mazao ya kilimo. Vilevile, itaanzisha *e-phyto* ili kuwezesha na kurahisisha biashara ya mazao kwa nchi 99 zinazotumia *e-phyto*.

413. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kupitia COPRA itaendelea kusajili ghala, masoko, vituo vya ukaguzi wa mazao na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo. Aidha, Wizara kupitia AGITF itaboresha mfumo wa kieletroniki kwa ajili ya usimamizi wa mikopo. Pia, Wizara itaendelea kununua vifaa vya TEHAMA kulingana na teknolojia mpya na za kisasa ili kuongeza ufanisi wa mifumo ya kidijiti katika utoaji wa huduma.

**5.6.2 Kuimarisha Mifumo ya Kidijiti itakayowezesha Upatikanaji wa Taarifa Sahihi kwa Wakati**

414. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) itaendelea kuboresha mfumo wa *e – Kilimo* wa Wizara kwa kuunganisha na mifumo mingine ya Serikali ili kuongeza ufanisi katika ubadilishanaji wa taarifa. Vilevile, itaanzisha kituo cha teknolojia za kilimo cha TEHAMA (AgriTech Hub) ambacho kitasaidia wakulima ikiwemo vijana kujifunza na kufanya ubunifu wa kutumia teknolojia za kidijiti.

**MAENEO MENGINE MUHIMU YATAKAYOTEKELEZWA NA WIZARA**

**Kuongeza Matumizi ya Teknolojia na Mbinu za Kilimo Kinachohimili Mabadiliko ya Tabianchi**

415. ***Mheshimiwa Spika,*** katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, hususan kwa wakullima wa nyanda kame, Wizara kupitia TARI itaendelea kujenga uwezo wa kituo cha TARI- Hombolo kuwa kituo mahiri cha tafiti za mazao ya nyanda kame na mabadiliko ya Tabianchi *(Centre for dryland crops and climate change research)*. Itaendelea kujenga Ofisi na miundombinu ya kisasa (Vitalu nyumba maalum – *Microclimate screenhouse,* umwagiliaji na maabara ndogo) vitakayowezesha kufanya tafiti za viwango vya mahitaji ya maji na hali ya hewa

kwa mazao tofautofauti katika maeneo kame. Hii itawezesha kupanua wigo wa mazao yanayolimwa katika nyanda kame. Aidha, TARI, itaendelea na utafiti wa zao la Tende nchini ambapo itaanzisha mashamba darasa ya zao hilo katika maeneo ya Hombolo, Mvumi na Chalinze Nyama.

416. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Sekta wa Usimamizi na Utunzaji wa Mazingira pamoja na Mpango wa Sekta wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi. Pia, itaendelea kufanya tathmini ya athari ya mazingira na jamii kwenye mashamba makubwa 10 yatakayoainishwa na Halmashauri kwa ajili ya programu ya BBT, maeneo ya miradi na Taasisi zilizo chini ya Wizara na kuandaa Mipango ya Usimamizi wa Mazingira katika maeneo hayo.

417. ***Mheshimiwa Spika***, Wizara itatoa mafunzo kuhusu utunzaji na usimamizi wa mazingira, mbinu na teknolojia za kilimo kinachohimili mabadiliko ya tabianchi ili kuwa na kilimo endelevu na himilivu kwa wakulima 800 katika mikoa ya Dodoma, Singida, Manyara na Tanga.

**Jinsia**

418. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kuhakikisha uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika kilimo cha mazao mbalimbali. Wizara kupitia Mradi wa TAISP itakamilisha mwongozo wa ujumuishaji wa masuala ya jinsia katika mnyororo wa thamani wa kilimo. Aidha, Mradi utaendelea kuhakikisha kuwa masuala ya kijinsia yanazingatiwa katika utoaji wa pembejeo za kilimo ikiwemo utoaji wa ruzuku ya mbegu na mbolea pamoja na utoaji wa mafunzo kupitia vikundi vya wakulima katika mashamba darasa ya Mradi. Pia, Wizara kupitia Programu na miradi ya BBT, AFDP na TFSRP itaendelea kutekeleza shughuli zake kwa kuzingatia usawa na jinsia.

**AFYA NA USTAWI WA WATUMISHI**

419. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 itaendelea kutoa huduma ya lishe na dawa kwa watumishi tisa (9) wanaoishi na VVU na UKIMWI. Vilevile, Wizara itaendelea kuhamisha watumishi kushiriki michezo mbalimbali ili kupunguza

athari za Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Pia, Wizara itaratibu vikao vinne (4) vya waelimisha rika kwa lengo la kubadilishana taarifa na kutathmini hali ya utekelezaji wa afua za VVU, UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza mahala pa kazi katika Utumishi wa Umma.

420. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya masuala ya afya itaendelea kutoa elimu ya VVU, UKIMWI, Afya ya Akili na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza.

421. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara itaendelea kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi kwa kuwapatia vitendea kazi, motisha na stahiki zao kwa mujibu wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu. Vilevile, Wizara itahakikisha watumishi wote wenye sifa wanapatiwa nafasi za kujiendeleza kitaaluma kwa kadri ya mahitaji ya Wizara kwenye maeneo mahsusi.

**Hitimisho na Shukrani**

422. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kulieleza Bunge lako Tukufu na kuwaambia watanzania wenzangu kuwa, hatua zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita katika sekta ya kilimo chini ya uongozi mahiri wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, zinajenga msingi imara wa ukuaji wa sekta hii kwa muda mrefu ambao utaleta uimara wa uchumi wetu, kupungua kwa umaskini na kuongeza thamani ya mazao ambayo itaongeza ajira kwenye eneo la sekta za huduma na kupunguza idadi ya watu kutoka kwenye sekta ya kilimo ambayo ndiyo alama muhimu sana kwenye kupunguza umaskini.

423. ***Mheshimiwa Spika,*** hatua hizo, zitafikiwa tu kama Taifa tutaamua kuwekeza kwa muda mrefu kwenye sekta ya kilimo ambayo imeajiri watu wengi kwa sasa. Miradi mingi tunayoitekeleza, chini ya Serikali ya Awamu ya Sita ni miradi itakayochukua muda mrefu kukamilika si chini ya miaka mitano (5) hadi miaka 10 na tutaendelea kuchukua hatua hii muhimu ili kuweza kuijengea sekta hii uimara dhidi ya mitikisiko mbalimbali.

424. ***Mheshimiwa Spika,*** Tanzania tumepitia mtikisiko wa COVID 19 na uzalishaji wetu haukuathirika. Tanzania tumepitia mtikisiko wa vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Tumeendelea kuwa himilivu kwa sababu sekta ya kilimo imeendelea kuwa imara, ambapo hatukupata upungufu wa chakula. Serikali imetekeleza miradi mbalimbali ya kutoa ruzuku kwenye pembejeo na kwenye ununuaji wa mazao ndio maana uchumi wetu umeendelea kuwa imara. Hii ni hatua muhimu sana.

425. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba Bunge lako Tukufu, litambue Taifa hili ni Taifa la wakulima wadogo wanaohitaji kulindwa na kupewa nyenzo mbalimbali na Serikali yao. Ruzuku zozote zinazotolewa na Serikali siyo gharama bali ni sehemu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, kwani Taasisi za kimataifa zimekuwa zikitizama mipango yetu ya ruzuku kama ni matumizi yasiyo ya muhimu jambo ambalo siyo sahihi. Ruzuku ya mbolea, ruzuku ya zana za kilimo, ruzuku ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji ni muhimu sana kwa ajili ya kuongeza tija na kupunguza umaskini.

426. ***Mheshimiwa Spika,*** hatuwezi kupunguza umaskini kama hatutawekeza kwa wakulima wetu wadogo. Dhana ya *commercial farming* kwa Tanzania siyo ukubwa wa shamba bali ni kiwango cha uzalishaji cha mkulima mdogo anachopata kwenye eneo la ekari moja dhidi ya gharama za uzalishaji na kumtengenezea faida. Tija ndiyo *commercial farming* kwetu na wala siyo ukubwa wa ardhi. Kama tukiweka nguvu kwenye dhana ya *commercial farming* kwa kuangalia ukubwa wa ardhi, tutakuwa tunawaonea na kuwaacha wakulima wadogo nje ya mipango yetu ya maendeleo.

427. ***Mheshimiwa Spika,*** nitumie nafasi hii kulishukuru Bunge lako Tukufu kwakuwa pamoja na wakulima wadogo wa nchi hii. Nitumie nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Rais ambaye ameendelea kuweka nguvu katika kusaidia sekta ya kilimo na wakulima wadogo.

428. ***Mheshimiwa Spika,*** tunaenda kwenye Uchaguzi Mkuu mwaka huu 2025 mwezi wa 10. Sisi wakulima tutakapoenda kupiga kura tunapigia kura ruzuku ya mbolea, ruzuku ya mbegu,

tunapigia kura ruzuku ya matrekta, viuatilifu, mikopo ya riba nafuu kupitia Benki ya ushirika Tanzania, bei nzuri ya mazao, upatikanaji wa huduma za ugani na huduma za upimaji wa afya ya udongo. Hivyo, sisi kama wakulima tunafahamu kinachotupeleka kwenye uchaguzi mwaka huu.

429. ***Mheshimiwa Spika,*** kwa kutambua kuwa Taifa hili msingi wake ni ujamaa na kujitegemea na linajengwa zaidi na wakulima wadogo, Mpango wowote wa maendeleo utakaowaacha wakulima wadogo nje itakuwa ni sawasawa na kusaliti Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa mujibu wa Ibara ya 9, kukisaliti Chama Cha Mapinduzi na kusaliti watanzania wengi walioajiriwa katika sekta ya kilimo.

430. ***Mheshimiwa Spika,*** Serikali ya Chama Cha Mapinduzi itaendelea kuwalinda wakulima wadogo kwa wivu mkubwa na kuwawezesha kuwa commercial farmers na kuwa wakulima wanaozalisha kwa tija ili waweze kuondokana na umaskini.

**Hatuwezi kuondoa umaskini kama hatuwezi kuwaondoa wakulima wadogo kwenye umaskini.**

431. ***Mheshimiwa Spika,*** mipango ya Serikali ya kuwalinda wakulima wadogo haiwezi kuwaacha wakulima wakubwa ambao wameanza kuingia katika sekta hii. Usalama wa wakulima wakubwa ni kuongezeka kwa tija na uzalishaji utakaoongeza kipato cha wakulima wadogo na kuwaondoa kwenye umaskini. Hii ndiyo itakayokuza sekta ya kilimo na kulinda Taifa letu.

432. ***Mheshimiwa Spika,*** ninaomba nitumie fursa hii kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa ambayo yamesaidia Wizara katika juhudi za kuendeleza kilimo. Baadhi yao kama ifuatavyo:- Serikali za Japan, Marekani, Uingereza, China, Indonesia, Korea ya Kusini, India, Italia, Misri, Kuwait, Israel, Ubelgiji, Ujerumani, Finland, Norway, Brazil, Uholanzi, Ireland, Malaysia, Vietnam, Canada, Poland pamoja na Umoja wa nchi za Afrika, Umoja wa Ulaya na Umoja wa Falme za Kiarabu. Vilevile, tunashukuru mashirika mbalimbali ya kimataifa na kitaifa ikiwemo AGRA, SAT, FAO, WFP, JICA, KOICA, Care International, World Vision, Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika, IMF, TAHA, World Vegetable Centre, SUGECO, SAGCOT,

Aspires Tanzania, USAID, CIAT, RIKOLTO, HELVATAS, IRRI, Agriedo, Mazao Hub, Global Community, TASTA, GAIN, NORAD, IITA, AATI, BMGF, AMDT, SNV, FSDT, ANSAF, MVIWATA, SWISS AID, TOAM, GIZ, ESRF, PASS, EFTA na TPSF.

433. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuzishukuru Taasis za Fedha ikiwemo CRDB, NMB, Benki ya Ushirika Tanzania, TADB, TIB, Azania Bank, NBC, PBZ, Commercial Bank of Tanzania, Equity Bank na Mwanga Hakika.

434. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda kuzishukuru Taasisi zote za elimu ya juu na Taasisi za utafiti. Vilevile, ninapenda kushukuru kampuni na wafanyabiashara wote wa mazao ya kilimo ambao tumekuwa tukishirikiana na nao katika kutoa soko la uhakika kwa wakulima. Ninawashukuru pia wafanyabiashara na wasambazaji wote wa pembejeo za kilimo kwa kuhakikisha pembejeo zinawafikia wakulima kwa wakati.

435. ***Mheshimiwa Spika,*** ninapenda pia kuzishukuru kampuni zote za mawasiliano nchini ikiwemo TTCL, Airtel, Vodacom, Yas na Halotel. Ninawashukuru pia kwa umuhimu wa kipekee wamiliki na wahariri wa vyombo vya habari vyote nchini pamoja na wanahabari wote wa vyombo vyote ikiwemo mitandao ya kijamii kwa kushirikiana nasi katika kuhabarisha umma na kutoa elimu kwa wakulima. Pia, ninawashukuru wasanii wote nchini kwa kuendelea kushirikiana nasi katika kutoa elimu kwa wakulima.

436. ***Mheshimiwa Spika,*** ninawashukuru sana Viongozi wa dini kwa kuendelea kutuombea na kutushauri katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yetu. Pia, nitumie fursa hii kuwashukuru viongozi wote wa kimila kwa kuendelea kutuunga mkono katika utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.

## 6 MAOMBI YA FEDHA MWAKA 2025/2026

### FUNGU 43, 24 na 05

### 6.1 Makadirio ya Makusanyo ya Maduhuli

437. ***Mheshimiwa Spika,*** Wizara katika mwaka 2025/2026 inatarajia kukusanya kiasi cha Shilingi **12,265,370,000** kupitia Fungu 43 na

Fungu 05. Kati ya fedha hizo, Shilingi **8,665,370,000** zitakusanywa kutokana na ukaguzi wa mazao, kodi za majengo na uuzaji wa nyaraka za zabuni kupitia Fungu 43 na kiasi cha Shilingi **3,600,000,000** kutokana na ada za umwagiliaji na ukodishaji wa mitambo kupitia Fungu 05.

### 6.2 Fedha za Matumizi kwa Mafungu yote

438. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026 Wizara ya Kilimo inaliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya kiasi cha Shilingi **1,242,975,075,000** kupitia Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24.

#### 6.2.1 Fedha kwa Fungu 43

439. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, kiasi cha Shilingi **838,259,822,000** zinaombwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **702,275,933,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya maendeleo ambapo kiasi cha Shilingi **424,328,013,000** ni fedha za ndani na kiasi cha Shilingi **277,947,920,000** ni fedha za nje. Aidha, Shilingi **135,983,889,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambapo kiasi cha Shilingi **81,447,048,000** ni kwa ajili ya mishahara na kiasi cha Shilingi **54,536,841,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo ya Wizara, Bodi na Taasisi.

#### 6.2.2 Fedha kwa Fungu 05

440. ***Mheshimiwa Spika***, katika mwaka 2025/2026, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **382,138,408,000**. Kati ya fedha hizo, Shilingi **308,721,961,000** ni fedha za Maendeleo na Shilingi **73,416,447,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kati ya fedha za maendeleo zinazoombwa, kiasi cha Shilingi **259,617,801,000** ni fedha za ndani na kiasi cha Shilingi **49,104,160,000** ni fedha za nje. Aidha, kati ya Shilingi **73,416,447,000** ya fedha za Matumizi ya Kawaida zinazoombwa, kiasi cha Shilingi **65,148,830,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) na kiasi cha Shilingi **8,267,617,000** ni kwa ajili ya Mishahara (PE) ya watumishi wa Tume.

#### 6.2.3 Fedha kwa Fungu 24

441. ***Mheshimiwa Spika,*** katika mwaka 2025/2026, Tume ya Maendeleo ya Ushirika inaomba kuidhinishiwa jumla ya Shilingi **22,576,845,000.** Kati ya fedha hizo, Shilingi **21,879,669,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambapo Shilingi **12,846,074,000** ni

mishahara (PE) ya watumishi na Shilingi **9,033,595,00** ni Matumizi Mengineyo (OC). Aidha, fedha za ndani kiasi cha Shilingi **697,176,000** zinaombwa kutekeleza miradi ya Maendeleo.

442. ***Mheshimiwa Spika,*** hotuba hii pia inapatikana katika tovuti ya Wizara: *www.kilimo.go.tz*

443. ***Mheshimiwa Spika,*** NINAOMBA KUTOA HOJA**.**

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaafiki.

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono. Mheshimiwa Waziri ahsante kwa kusoma vizuri. Hongereni sana.

Waheshimiwa Wabunge, kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri kuna maeneo ambayo kutokana na muda, taarifa yake yote imeingia kwenye *Hansard.* Kuna maneno hapa anasema, "Hatuwezi kuondoa umaskini, kama hatuwezi kuwaondoa wakulima wadogo kwenye umaskini." Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri hongera sana, Serikali ina mkakati maalum wa kuwanyanyua wakulima wadogo.

Mwenyekiti. *(Makofi)*

**MHE. DEODATUS P. MWANYIKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIAWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote ninapenda kutoa shukrani kwa niaba ya Kamati kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu ya Bunge, Toleo la Februari 2023. Kwa sababu ya muda, ninaomba taarifa yote iingie kwenye Kumbumbu Rasmi za Bunge, kama ilivyowasilishwa mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Februari 2023 ninaomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara

ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu makadirio na mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ina sehemu tatu; Sehemu ya Kwanza ni utangulizi; Sehemu ya Pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilivyotekelezwa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 na Sehemu ya Tatu inahusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati, pamoja na Hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, msingi wa uchambuzi; kifungu cha 6(1)(b) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023 kimeipa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo jukumu la kushughulikia bajeti ya Wizara ya Kilimo. Katika kutekeleza jukumu hili, tarehe 21 na 24 Machi, 2025 Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na kufanya ulinganisho kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 43 – Wizara ya Kilimo, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Ninaomba Bunge lijadili hoja ya Waziri wa Kilimo kwa pamoja na taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawanda ya uchambuzi; katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua Fungu 45 – Wizara ya Kilimo, Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika na Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kutembelea ili kujiridhisha kuhusu hali halisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mafungu yaliyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya uchambuzi na tathmini; kwa mujibu wa Kanuni ya 117(2), baada ya ziara ya

ukaguzi wa miradi ya maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa taarifa za utekelezaji wa mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025 na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, ili kuliwezesha Bunge kushauri ipasavyo kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya utekelezaji wa bajeti na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu kama nilivyoyataja. Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na ukusanyaji wa maduhuli, upatikanaji wa fedha za matumizi ya kugharamia miradi ya maendeleo na upatikanaji wa fedha, kwa ajili ya kugharamia matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli kwa Wizara ya Kilimo - Fungu 43; katika mwaka wa fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi 7,000,254,000, hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya shilingi bilioni 5.47 sawa na 78.17% ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Namba 01.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba: -

(a) Kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara na taasisi zake zilifikisha wastani wa 78% ya lengo;

(b) Ukusanyaji huu pia unaweza kumaanisha kuwa makadirio ya maduhuli siyo halisia; na

(c) Mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makusanyo ya maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya shilingi 3.6. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025

Wizara ilikuwa imekusanya shilingi 1.04 sawa na 28% ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali Namba 02.

Mheshimiwa Naibu Spika, makusanyo ya maduhuli kwa Fungu 05 yanaonesha kwamba: -

(a) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefika 28% tu ya lengo lake kwa kukusanya jumla ya shilingi 1.014 kati ya shilingi 3.6 zilizokusudiwa. Makusanyo haya hayaridhishi kwa kuwa hayaendani na matarajio na lengo la Wizara.

(b) Mwenendo huu wa makusanyo unaashiria kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa maduhuli na usimamizi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo lililokusudiwa. Changamoto zipo katika ukusanyaji wa maduhuli ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kutokufikia lengo lililotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117(1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Namba 4486 – Mradi wa Ujenzi wa *Mechanization Center* Itilima – Simiyu; Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma ya Zana Bora za Kilimo uliopo Itilima Mkoani Simiyu. Lengo la mradi huu ni kuhakikisha kwamba wakulima wa eneo la Itilima wanalima kwa kutumia zana bora za kilimo ikiwemo matrekta ili kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ulitengewa shilingi 216.67 kwa ajili ya ujenzi; Kamati ilifahamishwa kuwa mkandarasi alikuwa amewasilisha cheti cha maombi ya malipo ya awali ya jumla ya shilingi 35.6 sawa na 16% ambapo utekelezaji ulikuwa umefikia 48%. Hata hivyo, Kamati ilipata mashaka juu ya ukubwa

wa eneo ulipojengwa mradi kwa kuwa eneo linaonekana kuwa dogo kuliko mahitaji ya mradi na hasa mahitaji ya baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi huu ukikamilika utamuwezesha mkulima kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo pamoja na kuhamasisha vijana kujiunga na kilimo kutokana na uwepo wa zana bora za kilimo. Aidha, kwa kuwa mpango wa Serikali ni kuanzisha vituo kama hivi nchi nzima, Kamati inaishauri Serikali kuongeza umakini katika kuchagua mahali pa kujenga miradi ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa miradi ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Namba 4486 – Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Nyida; Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji uliopo katika Kijiji cha Nyida, Mkoa wa Shinyanga. Lengo la kuanzishwa kwa mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga na kuwawezesha wakulima kulima angalau kwa misimu miwili.

Mheshimiwa Naibu Spika, bwawa hili linalotarajiwa kuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita za ujazo bilioni 7.8 lenye uwezo wa kumwagilia hekta 800 za mashamba ya wakulima 1500, ulitengewa jumla ya shilingi 13.6. Hadi Kamati inatembelea mradi huu, shughuli za ujenzi zilikuwa zimefikia 75% na jumla ya malipo yaliyofanyika ni shilingi 8.48 sawa na 61.28% ya fedha yote ya mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati iliridhika na kazi iliyofanyika na kuitaka Serikali kuhakikisha kuwa inakamilisha mradi huu kwa wakati ili kuwawezesha wakulima kiuchumi na kuongeza kipato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi Namba 4486 – Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Tumbaku – Tabora; Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Bodi ya Tumbaku uliopo katika Kata ya Kanyenye Manispaa ya Tabora unaotekelezwa kwa fedha za ndani. Kamati ilifahamishwa kuwa mradi huu unatekelezwa kwa jumla ya shilingi bilioni 1.2.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Kamati ilitembelea mradi huu Serikali ilikuwa imelipa jumla ya shilingi 984.7 sawa na 78.9% ya fedha za mradi. Aidha, utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umefikia 98%. Katika ukaguzi huo, Kamati iliridhika na utekelezaji wa mradi isipokuwa marekebisho madogo ambayo Kamati inaamini kuwa yamekwishafanyiwa kazi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuimarisha usimamizi ili kuharakisha ukamilishaji wa jengo hilo ili wananchi hasa wakulima wa tumbaku, waanze kupata huduma bora kutoka katika ofisi hiyo na hasa huduma ya Tawi la Benki ya Ushirika ambayo ni moja ya sehemu ya wapangaji katika jengo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida; katika mwaka wa fedha 2024/2025, Fungu 43 – Wizara ya Kilimo iliidhinishiwa na Bunge bajeti ya shilingi 123.75 sawa na 9.9% ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilipokea jumla ya shilingi 53.89 kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na 44% ya bajeti iliyotengwa. Jedwali Namba 03 linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 43 kwa mwaka 2024/2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni asilimia 44 ya fedha iliyotengwa; na

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida hairidhishi na hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango iliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu – 05 iliidhinishiwa jumla ya shilingi 71.88 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025, fedha iliyopokelewa ni shilingi 13.42, sawa na asilimia 18 ya fedha iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika jedwali namba nne.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla ni asilimia 18 ya fedha iliyotengwa; na

(b) Upatikanaji huu wa fedha hauridhishi na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2024/2025 Fungu 24 – Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliidhinishiwa jumla ya shilingi 20.30 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Hadi kufikia Februari, 2025 Tume ilikuwa imepokea jumla ya shilingi 11.3 sawa na 55.6% ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida si wa kuridhisha na hivyo kuathiri ufikiwaji wa lengo yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uzingatiaji wa ushauri wa Kamati; wakati wa kupitia na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Fungu 43, Fungu 24 na Fungu 05 kwa mwaka wa fedha 2024/2025 Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Programu ya Jenga Kesho Iliyobora, Serikali imeendelea kufanya kazi kwa karibu na halmashauri mbalimbali kwa kuainisha maeneo ya mashamba, kuanzisha vituo vya zana za kilimo ikiwemo matrekta na viambata vyake, *power tillers* katika halmashauri. Vilevile katika kuhakikisha kuwa programu ya *BBT* inakuwa endelevu Serikali imeendelea kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake pamoja na mafunzo ya kilimo biashara. Kamati inasisitiza Serikali kuendelea na usimamizi wa programu hii ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuongeza ajira na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

(b) Serikali imeanza kuweka nguvu katika uzalishaji wa pembejeo hapa nchini. Serikali imeongeza bajeti ya uzalishaji wa mbegu bora kufikia bilioni 44.42 na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu nchini unafikia tani 47.07. Aidha, Serikali imeongeza bajeti ya mbolea hadi kufikia bilioni 300 na upatikanaji wa mbolea umefikia tani milioni 1.2. Kamati pia ilifahamishwa kuwa, Mkandarasi wa kusimika mitambo ya kiwanda chenye uwezo wa kuchanganya mbolea tani 120 kwa mwaka amepatikana.

Pia Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imewezesha ujenzi wa kiwanda cha viuatilifu cha *Plant Biodefenders Limited* kilichopo Mkoani Kilimanjaro chenye uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa mwezi.

(c) Kamati iliarifiwa kuwa utekelezaji wa ushauri wa kuanzisha Wakala wa Kilimo utakaosimamia shughuli za ugani ikiwemo miundombinu na rasilimali za kilimo umefikia hatua nzuri. Pia Kamati ilifahamishwa kuwa utekelezaji wa majukumu ya wakala huo utaanza mara taratibu husika zitakapokamilika ili kuongeza tija katika sekta ya kilimo. Pamoja na hatua hiyo iliyofikiwa Kamati inasisitiza kuwa utekelezaji wa ushauri huu ukamilishwe mapema iwezekanavyo.

(d) Katika kuhakikisha kuwa yanakuwepo mazingira ya kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu, Serikali kupitia *ASA* imeingia mikataba na wazalishaji wa mbegu 110 watakaolima eneo lenye ukubwa wa hekta 6,753 kwa mazao mbalimbali ikiwemo mahindi, mpunga, ngano, alizeti na ufuta. Mikataba hiyo itahusu kukodisha ardhi yenye ukubwa wa hekta 1,893 kwa kampuni binafsi saba za uzalishaji wa mbegu katika Shamba la Mbegu la Mbozi.

(e) Katika kuendeleza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini, Serikali imeendelea na utekelezaji kwa kujenga Maabara Kuu ya Kilimo Dodoma iliyofikia wastani wa 96%, Ujenzi wa Ofisi za *TARI* Makao Makuu 65%, ujenzi wa ghala

tano katika vituo vya *TARI* Tumbi, *TARI* Selian, *TARI* Hombolo, *TARI* Dakawa na *TARI* Naliendele, uliofikia wastani wa 40.4%.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla Kamati imeridhika kuona ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume zake katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa Wizara na hivyo kushindwa kuzingatia ipasavyo baadhi ya ushauri uliotolewa na Kamati. Hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha ya kutosha kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya maduhuli na matumizi kwa mwaka wa fedha 2025/2026; kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo – Fungu 43 inategemea kukusanya jumla ya shilingi bilioni 8.67. Fedha inayotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la 19% ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mchanganuo wa fedha na makusanyo kwa fungu unaonekana katika Jedwali Namba 05.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yameongezeka kwa 19% ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha uliopita, na
(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kufikia 80% ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, upo uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Fungu 05 – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya shilingi 3.6 ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Jedwali Namba 06 linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi unaonesha kwamba kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 ni sawa na lengo la maduhuli ya mwaka 2024/2025. Kamati inaona kuwa bado ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu uchambuzi wa matumizi ya kawaida; mwaka wa fedha 2025/2026 Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiria kutumia shilingi 231,280,005,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Fedha hizi ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa asilimia sita ikilinganishwa na bajeti kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mchanganuo wa makadirio hayo unaonekana katika Jedwali Namba 07.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ongezeko la asilimia sita kwenye bajeti ya matumizi ya kawaida, ongezeko hili linaonesha mwelekeo mzuri kwani fedha hizi zitaongeza msukumo wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo. Ongezeko hili la bajeti linategemewa kwenda sambamba na upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufanisi wa utakelezaji wa miradi ya umwagiliaji, usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo unategemea upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati; kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 37 ya Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo imeahidi kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira, sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoendeshwa kiuchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na ongezeko hilo la bajeti ya matumizi ya kawaida, Kamati inaona kuwa kuna haja ya kuongeza bajeti ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya sekta hii na kuhakikisha kuwa tija inaongezeka katika kilimo. Kuongezeka kwa bajeti kutaboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za

ugani pamoja na kuimarisha usimamizi na ukaguzi wa vyama vya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makadirio ya matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya shilingi trilioni 1.01 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa mwaka wa fedha 2025/2026. Makadirio hayo ni pungufu kwa 0.5% ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2024/2025 kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 08.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba: -

(a) Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imepungua kwa 0.5% ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2024/2025;

(b) Punguzo la bajeti kwa 0.5% inaweza kuathiri kufikia malengo yaliyowekwa katika mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo;

(c) Ukamilishaji wa miradi ya maendeleo unaweza kuleta tija kama Serikali itazingatia utoaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu maoni na ushauri wa Kamati**;** baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa bajeti pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ninaomba kuwasilisha maoni na ushauri wa Kamati kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika Wizara ya Kilimo – Fungu 43: -

(a) Bajeti ya kilimo, bado haikidhi mahitaji halisi ya sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014), yanayozitaka nchi wanachama kutenga 10% ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya

sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, fedha hizo zitolewe kwa wakati ili kuwezesha kufikia malengo na mikakati iliyokusudiwa;

(b) Pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali za kuendelea kuajiri wagani, bado mahitaji ya huduma za ugani ni makubwa katika maeneo mengi nchini. Hali hii imesababisha baadhi ya maeneo makubwa kuhudumiwa na mgani mmoja na hivyo kukosekana kwa tija iliyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutenga bajeti na kuajiri maafisa ugani wa kutosha ili kusogeza huduma kwa wakulima wengi zaidi na kuleta tija katika kilimo kama ilivyokusudiwa;

(c) Hali ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa imeendelea kuwa kwenye tarakimu mbili (35%) ikilinganishwa na shabaha ya kupunguza upotevu huo hadi asilimia tano ifikapo mwaka 2030. Hali hii inaweza kuathiri usalama na upatikanaji wa chakula cha uhakika wakati wote nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu na kukamilisha ujenzi wa maghala ya kutosha katika ngazi za vijiji, kata na wilaya, hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula. Aidha, Serikali iendelee kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha kuwa maghala yanajengwa ya kutosha karibu na wananchi katika maeneo yote kulingana na mahitaji;

(d) Ukosefu wa masoko ya uhakika kwa baadhi ya mazao ya kilimo katika maeneo mengi ya wakulima nchini na nje ya nchi, umeinyima sekta ya kilimo fursa ya kuchangia ipasavyo katika uchumi, ikiwa ni pamoja na kuwakatisha tamaa baadhi ya wakulima. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua zaidi na za makusudi, ikiwa ni pamoja na kuendelea kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo hapa nchini na nje ya nchi unakuwa wa uhakika. Aidha, Serikali iweke mikakati mahsusi ya

kuhakikisha kuwa mazao yanaendelea kuwekewa mnyororo wa thamani ili kuwanufaisha wakulima;

(e) Maendeleo ya sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inahitaji kuziwezesha taasisi zake za utafiti ili kuongeza tija katika kilimo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali: -

(i) Kuendelea kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuwaongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa ajili ya utafiti na kuendelea kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kukuza sekta ya kilimo nchini; na

(ii) Kuongeza kasi katika kufufua uzalishaji wa mbegu za kutosha za asili (mbegu za wakulima). Kuendeleza na kutunza mbegu hizi kutasaidia kulinda chanzo cha nasaba za mimea ambacho ni msingi wa tafiti zote. Aidha, uzalishaji wa mazao ya asili upewe kipaumbele ili kusaidia upatikanaji wa lishe bora katika chakula na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa uhitaji wa virutubisho vya viwandani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05; kuhusu utekelezaji wa mipango ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji unaipotezea Serikali mapato. Kamati inaishauri Tume kuweka utaratibu utakaowezesha watumiaji wa maji kulipa tozo za maji ili kuiwezesha Tume kufikia malengo iliyojiwekea;

(b) Serikali ifanye uchambuzi wa kina kuainisha miradi ya mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji ambayo yamefikia zaidi ya 60% ya utekelezaji na kuyakamilisha kwa haraka ili tija kwa sekta hii muhimu ya kilimo ianze kuonekana; na

(c) Serikali iendelee kuongeza na kutoa fedha kwa wakati katika miradi ya miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza kasi ya kukamilisha miradi. Aidha, usimamizi wa miradi uimarishwe ili fedha zilizotengwa zilete tija iliyokusudiwa kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Tume ya Ushirika Fungu 24:-

(a) Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kutoa mtaji uliowezesha uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ambayo itasaidia wakulima kupata huduma za kifedha kwa karibu zaidi. Pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha Benki ya hiyo Kamati inaishauri Serikali:-

(i) Kuendelea kuimarisha benki hii kwa kuhakikisha inapata mtaji wa kutosha kuhudumia wakulima katika maeneo mbalimbali nchini; na

(ii) Serikali ihakikishe Benki hii inaendeshwa kibiashara na kuleta ushindani kwenye sekta ya benki nchini.

(b) Mgawanyo wa majukumu na uwajibikaji katika Tume umepunguza ufanisi na kusababisha changamoto hasa za usimamizi na uwajibikaji wa Maafisa Ushirika. Kamati inaendelea kuitaka Serikali kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ushirika haraka ili kutatua changamoto zinazotokana na usimamizi hafifu na kukosa uwajibikaji katika sekta ya ushirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho; Wizara ya Kilimo ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia hususani lengo namba moja linalohusu kupunguza umaskini uliokithiri na lengo namba mbili linalohusu kutokomeza tatizo la utapiamlo kwa kuimarisha lishe bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kwa ushirikiano walionipa na waliouonesha katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina, lakini ninaomba majina yao yote yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge *(Hansard)*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa ninaomba kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Njombe Mjini kwa kuniamini na kunipa ushirikiano mkubwa katika kipindi chote cha uongozi wangu, ninaomba tuendelee kushirikiana kwa pamoja ili neema ziendelee kutufikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ninapenda sana kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa kipekee wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya uongezaji wa bajeti ya Wizara kwa lengo la kuongeza tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, maamuzi ya Mheshimiwa Rais yameonesha utashi mkubwa wa kisiasa na uthubutu alionao katika kubadilisha maisha ya wakulima wadogo wadogo na Watanzania kwa ujumla. Sisi tunampongeza na tunamtakia afya njema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho lakini siyo kwa umuhimu ninapenda kutumia nafasi hii kumshukuru sana Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe - Waziri wa Kilimo na Mheshimiwa David Ernest Silinde - Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu - Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu Dkt. Hussein Mohamed Omary na Dkt. Stephen Justice Nindi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Baraka Leonard kwa kuwaongoza vyema watumishi wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kufikia kukamilisha kwa taarifa hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo Fungu 43, 24 na 05, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, ninaomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA KILIMO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**SEHEMU YA KWANZA**

**1.0 MAELEZO YA JUMLA**

**1.1 Utangulizi**

**Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, napenda kutoa shukrani kwa niaba ya Kamati kwa kunipa nafasi ili niweze kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023.

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 118 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025, pamoja na Maoni na Ushauri wa Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/ 2026.

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii ina sehemu tatu. Sehemu ya Kwanza ni utangulizi; Sehemu ya Pili inabainisha uchambuzi wa namna bajeti ya Wizara ya Kilimo kwa mwaka wa fedha 2024/2025 ilivyotekelezwa na makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara kwa mwaka wa Fedha 2025/2026; na Sehemu ya Tatu inahusu maoni na mapendekezo ya Kamati; pamoja na Hitimisho.

## 1.2 Msingi wa Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kifungu cha 6(1)(b) kikisomwa pamoja na kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Februari, 2023, kimeipa Kamati ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo jukumu la kushughulikia Bajeti ya Wizara ya Kilimo. Katika kutekeleza jukumu hili tarehe 21 na 24 Machi, 2025 Kamati ilichambua Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na kufanya ulinganisho kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya **Fungu 43** – Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na **Fungu 05** – Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Aidha, Kanuni ya 117(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge imeweka masharti yanayotaka Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Wizara hii kuchambuliwa na Kamati kabla ya kujadiliwa Bungeni. Naomba Bunge lijadili hoja ya Waziri wa Kilimo kwa pamoja na Taarifa hii.

## 1.3 Mawanda ya Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Katika kusimamia masuala ya kibajeti, Kamati imechambua **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na **Fungu 05** - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji. Uchambuzi huu ulifanyika baada ya Kamati kutembelea ili kujiridhisha kuhusu hali halisi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika mafungu yaliyotajwa hapo juu.

# SEHEMU YA PILI

## 2.0 MATOKEO YA UCHAMBUZI NA TATHMINI

## 2.1 Ufafanuzi wa Jumla

**Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya Uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi yanaweka msingi wa ushauri wa Kamati kuhusu hoja ya Waziri wa

Kilimo. Uchambuzi ulijielekeza katika maeneo mawili ambayo ni Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026.

### 2.2 Uchambuzi wa Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (2), baada ya ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, Kamati ilifanya uchambuzi wa Taarifa za Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ili kuliwezesha Bunge kushauri ipasavyo kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo inajumuisha mafungu matatu, Wizara ya Kilimo - **Fungu 43**, Tume ya Maendeleo ya Ushirika - **Fungu 24** na Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu 05**.

Masuala yaliyochambuliwa ni pamoja na Ukusanyaji wa Maduhuli, Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya kugharamia Miradi ya Maendeleo na Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya kugharamia Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

#### 2.2.1 Makusanyo ya Maduhuli kwa Wizara ya Kilimo – Fungu 43

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2024/2025 Wizara ya Kilimo ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi 7,000,254,000.00**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 5,471,857,612.22** sawa na **asilimia 78.17** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika **Jedwali Na.01.**

**Jedwali Na. 1 Fungu 43 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika mwaka wa fedha 2024/2025**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| **7,000,254,000.00**. | **5,471,857,612.22** | **78.17** |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2024/2025 fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa makusanyo ya maduhuli unaonesha kwamba: -

(a) Kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ukusanyaji wa maduhuli ulikuwa wa kuridhisha kwani hadi kufikia mwezi Februari, 2025, Wizara na Taasisi zake zilifikisha wastani wa **asilimia 78** ya lengo;

(b) Ukusanyaji huu pia unaweza kumaanisha kuwa makadirio ya maduhuli siyo halisia; na

(c) Mwenendo huu wa makusanyo unaonesha kuwa lengo linaweza kufikiwa ifikapo mwisho wa mwaka wa fedha.

**2.2.2 Makusanyo ya Maduhuli kwa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2024/2025, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji ilijiwekea lengo la kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000**. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025 Wizara ilikuwa imekusanya **Shilingi 1,043,512,015** sawa na **asilimia 28** ya lengo lililokusudiwa. Mchanganuo wa makusanyo hayo unaonekana katika Jedwali namba 2.

**Jedwali Na. 2 Fungu 05 - Makadirio na Makusanyo Halisi katika Mwaka wa Fedha 2024/ 2025**

| UKUSANYAJI WA MADUHULI HADI KUFIKIA FEBRUARI, 2025 | | |
|---|---|---|
| **MAKADIRIO (Tsh.)** | **MAKUSANYO (TSh.)** | **ASILIMIA** |
| 3,600,000,000 | 1,043,512,015 | 28.99 |

**Chanzo:** Randama ya bajeti ya 2024/2025 Fungu 05

**Mheshimiwa Spika**, makusanyo ya maduhuli kwa fungu 05 yanaonesha kwamba: -

(a) Tume ya Taifa ya Umwagiliaji imefika **asilimia 28** tu ya lengo kwa kukusanya jumla ya **Shilingi 1,043,512,015** kati ya **Shilingi 3,600,000,000** zilizokusudiwa. Makusanyo haya hayaridhishi kwa kuwa hayaendani na matarajio na lengo la Wizara.

(b) Mwenendo huu wa makusanyo unaashiria kutokuwepo kwa mfumo madhubuti wa ukusanyaji wa maduhuli na usimamizi wake.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, mwenendo wa makusanyo ya maduhuli ya Wizara unatoa mwelekeo wa kufikia lengo lililokusudiwa. Changamoto zipo katika ukusanyaji wa maduhuli ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kutokufikia lengo lililotarajiwa.

**2.2.3 Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, kwa madhumuni ya kuzingatia masharti ya Kanuni ya 117 (1) ya Kanuni za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo: -

**i. Mradi Namba 4486 – Mradi wa Ujenzi wa Mechanization Center Itilima – Simiyu.**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kutoa Huduma ya Zana Bora za Kilimo (*Mechanization Center*) uliopo Itilima mkoani Simiyu. Lengo la

mradi huu ni kuhakikisha wakulima wa eneo la Itilima wanalima kwa kutumia zana bora za kilimo ikiwemo trekta ili kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulitengewa **Shilingi 216,666,544** kwa ajili ya ujenzi**.** Kamati ilifahamishwa kuwa Mkandarasi alikuwa amewasilisha cheti cha maombi ya malipo ya awali ya jumla ya **Shilingi 35,627,435.90** sawa na **asilimia 16** ambapo utekelezaji ulikuwa umefikia **asilimia 48**. Hata hivyo, Kamati ilipata mashaka juu ya ukubwa wa eneo ulipojengwa mradi kwa kuwa eneo linaonekana kuwa dogo kuliko mahitaji ya mradi.

**Mheshimiwa Spika**, Mradi huu ukikamilika utamuwezesha mkulima kuongeza uzalishaji na tija katika mazao ya kilimo pamoja na kuhamasisha vijana kujiunga na kilimo kutokana na uwepo wa zana bora za kilimo.
Aidha, kwa kuwa mpango wa Serikali ni kuanzisha vituo kama hivi nchi nzima, Kamati inaishauri Serikali kuongeza umakini katika kuchagua mahali pa kujenga mradi ikiwa ni pamoja na kuimarisha usimamizi wa miradi ili tija iliyokusudiwa ipatikane.

**ii. Mradi Na. 4486 - Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji Nyida**
**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Umwagiliaji uliopo katika Kijiji cha Nyida mkoani Shinyanga. Lengo la kuanzishwa kwa mradi huu ni kuongeza upatikanaji wa maji kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji wa zao la mpunga na kuwawezesha wakulima kulima angalau kwa misimu miwili.

**Mheshimiwa Spika**, Bwawa hili linalotarajiwa kuwa na uwezo wa kuhifadhi maji lita za ujazo **bilioni 7.8** lenye uwezo wa kumwagilia **hekta 800** za mashamba ya **wakulima 1500**, ulitengewa jumla ya **Shilingi 13,618,680,790**. Hadi Kamati inatembelea mradi huu, shughuli za ujenzi zilikuwa zimefikia **asilimia 75** na jumla ya malipo yaliyofanyika ni **Shilingi 8,484,395,620.40** sawa na **asilimia 61.23** ya fedha yote ya mradi.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa ujumla Kamati iliridhika na kazi iliyofanyika na kuitaka Serikali kuhakikisha inakamilisha mradi huu kwa wakati ili kuwawezesha wakulima kiuchumi na kuongeza kipato.

**iii. Mradi Na. 4486 - Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Makao Makuu ya Bodi ya Tumbaku- Tabora**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kukagua Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Bodi ya Tumbaku Tanzania uliopo katika Kata ya Kanyenye Manispaa ya Tabora unaotekelezwa kwa fedha za ndani. Kamati ilifahamishwa kuwa, mradi huu unatekelezwa kwa jumla ya **Shilingi 1,237,454,670.13.**

**Mheshimiwa Spika**, hadi Kamati inatembelea mradi huu,
Serikali ilikuwa imelipa jumla ya **Shilingi 984,720,742.96** sawa na **asilimia 78.9** ya fedha za mradi. Aidha, utekelezaji wa mradi ulikuwa umefikia **asilimia 95**.
Katika ukaguzi huo, Kamati iliridhika na utekelezaji wa mradi isipokuwa marekebisho madogo ambayo Kamati inaamini yamefanyiwa kazi. Aidha, Kamati inaitaka Serikali kuimarisha usimamizi ili kuharakisha ukamilishaji wa jengo hilo ili wananchi hasa wakulima wa tumbaku waanze kupata huduma bora kutoka katika Benki ya
Ushirika.

**2.2.4 Upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, **Fungu 43 -** Wizara ya Kilimo, iliidhinishiwa na Bunge Bajeti ya **Shilingi 123,750,689,000** sawa na **asilimia 9.9** ya bajeti yote kwa ajili ya matumizi ya kawaida.

Hadi kufikia Februari, 2025 Wizara ilipokea jumla ya **Shilingi 53,892,899,072.26** kwa ajili ya Matumizi ya kawaida sawa na **asilimia 44** ya bajeti iliyotengwa. Jedwali namba 3 linaonesha mwenendo wa upatikanaji wa fedha wa Fungu 43 kwa Mwaka 2024/2025.

**Jedwali Na. 3: Hali ya upatikanaji wa fedha hadi kufikia Februari, 2025- Fungu 43**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 43 MWAKA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA.** | **KILICHOPOKELEWA** | **ONGEZEKO/ PUNGUFU ASILIMIA** |
| MISHAHARA | 69,894,933,000 | 41,715,806,172.27 | 60 |
| OC | 53,855,756,000 | 12,177,092,899.99 | 33 |
| **JUMLA** | **123,750,689,000** | **53,892,899,072.26** | **44** |

**Chanzo**: Randama ya Wizara Fungu 43

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida ni **asilimia 44** ya fedha iliyotengwa; na

(b) Hali ya upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida hairidhishi na hivyo kuathiri utekelezaji wa mipango iliyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji - **Fungu – 05** iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 71,884,610,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Februari, 2025, fedha iliyopokelewa ni **Shilingi 13,420,633,136.63** sawa na **asilimia 18** ya fedha iliyoidhinishwa. Mchanganuo wa upokeaji wa fedha unaonekana katika **Jedwali Na. 4**.

**Jedwali Na. 4: Hali ya upatikanaji wa Fedha za Matumizi ya Kawaida - Fungu 05**

| UPATIKANAJI WA FEDHA FUNGU 05 MWAKA 2024/2025 | | | |
|---|---|---|---|
| **MATUMIZI** | **KILICHOIDHINISHWA PAMOJA NA NYONGEZA** | **KILICHOPOKELEWA** | **ONGEZEKO/PUNGUFU ASILIMIA** |
| MISHAHARA | 7,506,830,000 | 4,635,603,376 | 54 |
| OC | 64,377,780,000 | 8,785,029,760.63 | 13 |
| **JUMLA** | **71,884,610,000** | **13,420,633,136.63** | **18.67** |

Chanzo: **Randama ya Wizara Fungu - 05**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Upatikanaji wa fedha za matumizi ya kawaida kwa ujumla ni **asilimia 18** ya fedha iliyotengwa; na

(b) Upatikanaji huu wa fedha hauridhishi na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo yaliyotarajiwa.

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2024/2025, Fungu 24 - Tume ya Maendeleo ya Ushirika iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 20,280,063,000.00** kwa ajili ya matumizi ya kawaida**.** Hadi kufikia Februari, 2025, Tume ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 11,251,479,985.06** sawa na **asilimia 55.6** ya bajeti ya matumizi ya kawaida iliyoidhinishwa**.**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, mwenendo wa jumla wa upatikanaji wa fedha kwa ajili ya matumizi ya kawaida siyo wa kuridhisha na hivyo kuathiri utekelezaji wa lengo lililokusudiwa.

### 2.2.5 Uzingatiaji wa Ushauri wa Kamati

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu 43 - Wizara ya Kilimo, **Fungu 24** - Tume ya Maendeleo ya Ushirika na **Fungu 05** - Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Kamati ilishauri masuala mbalimbali ambayo Serikali iliyazingatia.

**Mheshimiwa Spika,** baadhi ya ushauri wa Kamati uliozingatiwa ni kama ifuatavyo: -

(a) Katika programu ya BBT, Serikali imeendelea kufanya kazi kwa karibu na Halmashauri mbalimbali kwa kuainisha maeneo ya mashamba, kuanzisha vituo vya zana za kilimo ikiwemo matrekta 500 na viambata vyake katika ngazi ya halmashauri. Vilevile, katika kuhakikisha programu ya BBT inakuwa endelevu, Serikali imeendelea kutoa mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake pamoja na mafunzo ya kilimo biashara. Kamati inasisitiza Serikali kuongeza usimamizi wa Programu Hii ili kufikia malengo yaliyokusudiwa ya kuongeza ajira.

(b) Serikali imeanza kuweka nguvu katika uzalishaji wa pembejeo hapa nchini. Serikali imeongeza bajeti ya uzalishaji wa mbegu bora kufikia bilioni 44.42 na kuhakikisha kuwa upatikanaji wa mbegu nchini umefikia tani 47,057.08. Aidha,Serikali imeongeza bajeti ya mbolea hadi kufikia bilioni 300 na upatikanaji wa mbolea umefikia tani 1,213,729. Kamati pia ilifahamishwa kuwa, Mkandarasi wa kusimika mitambo ya kiwanda chenye uwezo wa kuchanganya mbolea tani 120 amepatikana.

Pia Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imewezesha ujenzi wa kiwanda cha viuatilifu cha Plant Biodefenders Limited Kilichopo Mkoani Kilimanjaro, chenye uwezo wa kuzalisha lita 20,000 kwa mwezi.

Kamati iliarifiwa kuwa utekelezaji wa ushauri wa kuanzisha Wakala wa Kilimo utakaosimamia shughuli za ugani ikiwemo miundombinu na rasilimali za kilimo umefikia hatua nzuri. Pia Kamati ilifahamishwa kuwa utekelezaji wa majukumu ya Wakala huo utaanza mara taratibu husika zitakapokamilika ili kuongeza tija katika Sekta ya Kilimo. Pamoja na hatua hiyo iliyofikiwa Kamati inasisitiza kuwa utekelezaji wa ushauri huu ukamilishwe mapema iwezekanavyo.

Katika kuhakikisha kuwa yanakuwepo mazingira ya kushirikisha sekta binafsi katika uzalishaji wa mbegu, Serikali kupitia ASA

imeingia mikataba na wazalishaji wa mbegu 110 watakaolima eneo lenye ukubwa wa hekta 6,753 kwa mazao mbalimbali ikiwemo mahindi, mpunga, ngano, alizeti na ufuta. Mikataba hiyo pia itahusu kukodisha ardhi yenye ukubwa wa hekta 1,893 kwa kampuni binafsi saba za uzalishaji wa mbegu katika shamba la mbegu la Mbozi.

Katika kuendeleza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini, Serikali imeendelea na utekelezaji kwa kujenga maabara kuu ya kilimo Dodoma iliyofikia wastani wa asilimia 96, Ujenzi wa Ofisi za TARI Makao Makuu asilimia 65, ujenzi wa ghala tano katika vituo vya TARI Tumbi, TARI Selian, TARI Hombolo, TARI Dakawa na TARI Naliendele, uliofikia wastani wa asilimia 40.4.

**Mheshimiwa Spika**, kwa ujumla, Kamati imeridhika kuona ushauri wake unaendelea kuzingatiwa na Wizara pamoja na Tume zake katika utekelezaji wa majukumu yake. Aidha, upatikanaji wa fedha usioridhisha umeendelea kuwa kikwazo kwa Wizara na hivyo kushindwa kuzingatia ipasavyo baadhi ya ushauri wa Kamati. Hivyo, Kamati inaisisitiza Serikali kutoa fedha ya kutosha kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

### 2.3 Makadirio ya Maduhuli na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

#### 2.3.1 Makadirio ya Maduhuli

**Mheshimiwa Spika**, kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo - Fungu 43 inategemea kukusanya jumla ya **Shilingi 8,665,370,000**. Fedha inayotarajiwa kukusanywa ni ongezeko la **asilimia 19** ikilinganishwa na makadirio ya makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025. Mchanganuo wa lengo la makusanyo kwa fungu unaonekana katika **Jedwali Na.5.**

**Jedwali Na. 5 : Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli - Fungu 43**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2023/2024 NA 2025/2026 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2024/2025** | **2025/2026** | **Nyongeza/ Pungufu** | **Asilimia** |
| | 7,000,254,000 | 8,665,370,000 | 1,665,116,000 | **19** |

**Chanzo: Randama ya Wizara Fungu -43**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kuwa: -

(a) Kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka wa fedha 2025/2026 yameongezeka kwa **asilimia 19** ikilinganishwa na lengo la makusanyo kwa mwaka wa fedha 2024/2025; na

(b) Kutokana na mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025 kufikia **asilimia 80** ndani ya robo tatu ya muda wa lengo, upo uwezekano wa kufikia lengo la makusanyo lililowekwa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa kuzingatia uzoefu wa makusanyo ya mwaka uliotangulia.

**Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa **Fungu 05 -** Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inakadiriwa kukusanya jumla ya **Shilingi 3,600,000,000** ambayo ni sawa na lengo la maduhuli kwa mwaka wa fedha 2024/2025. **Jedwali Na. 6** linaonesha mchanganuo wa makadirio hayo.

**Jedwali Na. 6: Ulinganisho katika Makusanyo ya Maduhuli - Fungu 05**

| ULINGANISHO WA MAKUSANYO YA MADUHULI KWA MWAKA 2022/2023 NA 2023/2024 | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **2024/2025** | **2025/2026** | **Nyongeza/ Pungufu** | **Nyongeza/ Pungufu%** |
| Mfuko (NIDF) | 3,600,000,000 | 3,600,000,000 | - | - |

**Chanzo: Randama Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi unaonesha kwamba, kwa ujumla makadirio ya maduhuli kwa mwaka 2025/2026 ni sawa na lengo

la maduhuli ya mwaka wa fedha 2024/2025. Kamati inaona bado ni muhimu Tume ikajiwekea mikakati itakayoiwezesha kuongeza makusanyo ya maduhuli kwa mwaka huu wa fedha ili kuleta tija iliyokusudiwa.

**2.3.2 Uchambuzi wa Matumizi ya Kawaida**

**Mheshimiwa Spika**, Mwaka wa Fedha 2025/2026, Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika wanakadiria kutumia **Shilingi 231,280,005,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Fedha hizi ni ongezeko la matumizi ya kawaida kwa **asilimia 6** ikilinganishwa na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

Mchanganuo wa Makadirio hayo unaonekana katika **Jedwali Na. 7.**

**Jedwali Na. 7: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2024/2025**

| Na. | FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 43 | WIZARA YA KILIMO | 123,750,689,000 | **135,983,889,000** | 9 |
| 2. | 05 | TUME YA UMWAGILIAJI | 71,884,610,000 | **73,416,447,000** | 2 |
| 3. | 24 | TUME YA USHIRIKA | 20,280,063,000 | **21,879,669,000** | 7 |
| | | **JUMLA** | **215,915,362,000** | **231,280,005,000** | **6** |

**Chanzo: Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24**

**Mheshimiwa Spika**, kufuatia ongezeko la **asilimia 6** kwenye bajeti ya Matumizi ya Kawaida, ongezeko hili linaonesha mwelekeo mzuri kwani fedha hizi zitaongeza msukumo wa kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya miradi ya maendeleo. Ongezeko hili la bajeti linategemewa kwenda sambamba na upatikanaji wa fedha hizo kwa wakati ili kutekeleza majukumu yaliyokusudiwa.

Ufanisi wa utakelezaji wa miradi ya Umwagiliaji, usambazaji wa mbolea pamoja na pembejeo za kilimo, unategemea upatikanaji wa fedha za kutosha na kwa wakati. Kama inavyoelekezwa katika Ibara ya 37 ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM), imeahidi kusimamia kikamilifu hifadhi na matumizi endelevu ya maji, ardhi ya kilimo na mazingira, sambamba na kuongeza miundombinu ya umwagiliaji itakayoendeshwa kiuchumi.

**Mheshimiwa Spika**, pamoja na ongezeko hilo la bajeti ya Matumizi ya Kawaida, Kamati inaona kuwa, kuna haja ya kuongeza bajeti ya kilimo ili kukidhi mahitaji ya sekta hii na kuhakikisha tija inaongezeka katika kilimo. Kuongezeka kwa bajeti kutaboresha miundombinu ya umwagiliaji, ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya hifadhi ya mazao, kuimarisha vituo vya utafiti, upatikanaji wa pembejeo, kuimarisha huduma za ugani pamoja na kuimarisha Usimamizi na Ukaguzi wa Vyama vya Ushirika.

**2.3.3 Makadirio ya Matumizi kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilichambua makadirio ya jumla ya **Shilingi 1,011,695,070,000** kwa ajili ya kugharamia Miradi ya Maendeleo inayopangwa kutekelezwa na Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026. Makadirio hayo ni pungufu kwa **asilimia 0.5** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 kama inavyoonekana katika **Jedwali Na. 8**

**Jedwali Na. 8 Makadirio ya Bajeti ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2025/2026**

| NA. | FUNGU | TAASISI | MAKADIRIO KWA MWAKA 2024/2025 | MAKADIRIO KWA MWAKA 2025/2026 | ASILIMIA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 43 | WIZARA YA KILIMO | 683,286,032,000 | 702,275,933,000 | 2.8 |
| 2. | 05 | TUME YA UMWAGILIAJI | 331,899,223,000 | 308,721,961,000 | -6.9 |
| 3. | 24 | TUME YA USHIRIKA | 828,626,000 | 697,176,845,000 | -15.9 |
| | | **JUMLA** | **1,016,013,881,000** | **1,011,695,070,000** | **-0.5** |

***Chanzo:* Randama za Fungu 43, Fungu 05 na Fungu 24**

**Mheshimiwa Spika,** uchambuzi wa jumla unaonesha kwamba: -

(a) Bajeti ya Maendeleo kwa Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika imepungua kwa **asilimia 0.5** ikilinganishwa na Mwaka wa Fedha 2024/2025;

(b) Punguzo la bajeti kwa **asilimia 0.5** inaweza kuathiri kufikia malengo yaliyowekwa katika mpango wa kuendelea kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo; na

(c) Ukamilishaji wa miradi ya maendeleo unaweza kuleta tija kama Serikali itazingatia utoaji wa fedha za kutosha na kwa wakati kama ilivyotarajiwa.

## SEHEMU YA TATU

### 3.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya uchambuzi wa kina kuhusu utekelezaji wa Bajeti pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Tume ya Taifa ya Umwagiliaji na Tume ya Maendeleo ya Ushirika, ninaomba kuwasilisha Maoni na Ushauri wa Kamati kama ifuatavyo:-

### 3.1 Wizara ya Kilimo – Fungu 43

(a) Bajeti ya kilimo, bado haikidhi mahitaji halisi ya sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya utekelezaji wa Azimio la Maputo (2003) na Malabo (2014) yanayozitaka nchi wanachama kutenga **asilimia 10** ya bajeti ya Taifa kwa ajili ya sekta ya kilimo. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuongeza bajeti ya kilimo ili kufikia malengo yaliyokusudiwa. Aidha, fedha hizo zitolewe kwa wakati ili kuwezesha kufikia malengo na mikakati iliyokusudiwa;

(b) Pamoja na juhudi zilizofanywa na Serikali za kuendelea kuajiri Wagani, bado mahitaji ya huduma za ugani ni makubwa katika maeneo mengi nchini. Hali hii imesababisha baadhi ya maeneo makubwa kuhudumiwa na Mgani mmoja na hivyo kukosekana kwa tija iliyokusudiwa. Kamati inaishauri Serikali kuona umuhimu wa kuendelea kutenga bajeti na

kuajiri Maafisa Ugani wa kutosha ili kusogeza huduma kwa wakulima wengi zaidi na kuleta tija katika kilimo kama ilivyokusudiwa;

(c) Hali ya upotevu wa mazao baada ya kuvunwa imeendelea kuwa kwenye tarakimu mbili (**asilimia 35**) ikilinganishwa na shabaha ya kupunguza upotevu huo hadi **asilimia 5** ifikapo mwaka 2030. Hali hii inaweza kuathiri usalama na upatikanaji wa chakula cha uhakika wakati wote nchini. Kamati inaishauri Serikali kuendelea kuimarisha miundombinu na kukamilisha ujenzi wa maghala ya kutosha katika ngazi za Vijiji, Kata na Wilaya hasa kwenye maeneo yenye uzalishaji mkubwa wa mazao ya chakula. Aidha, Serikali iendelee kushirikiana na sekta binafsi katika kuhakikisha kuwa maghala yanajengwa ya kutosha karibu na wananchi katika maeneo yote kulingana na mahitaji;

(d) Ukosefu wa masoko ya uhakika kwa baadhi ya mazao ya kilimo katika maeneo mengi ya wakulima nchini na nje ya nchi, umeinyima sekta ya kilimo fursa ya kuchangia ipasavyo katika uchumi ikiwa ni pamoja na kuwakatisha tamaa wakulima. Ili kukabiliana na changamoto hii, Kamati inaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi ikiwa ni pamoja na kuendelea kuhakikisha upatikanaji wa masoko ya mazao ya kilimo hapa nchini na nje ya nchi unakuwa wa uhakika. Aidha, Serikali iweke mikakati mahsusi ya kuhakikisha kuwa mazao yanaendelea kuwekewa mnyororo wa thamani ili kuwanufaisha wakulima;

(e) Maendeleo ya Sekta yoyote yanatokana na tafiti za kutosha kuhusu sekta husika. Sekta ya kilimo inahitaji kuziwezesha taasisi zake za utafiti ili kuongeza tija katika kilimo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali: -

i. Kuendelea kuwekeza na kuimarisha taasisi za utafiti wa kilimo nchini ikiwa ni pamoja na kuwaongezea rasilimali watu na rasilimali fedha kwa ajili ya utafiti na kuendelea kuwajengea uwezo watafiti wa kilimo ili waweze kufanya kazi zao kwa ufanisi na kukuza sekta ya kilimo nchini; na

ii. Kuongeza kasi katika kufufua uzalishaji wa mbegu za kutosha za asili (mbegu za Wakulima). Kuendeleza na kutunza mbegu hizi kutasaidia kulinda chanzo cha nasaba za mimea ambacho ni msingi wa tafiti zote. Aidha, uzalishaji wa mazao ya asili upewe kipaumbele ili kusaidia upatikanaji wa lishe bora katika chakula na kuchangia kujitosheleza kwa virutubisho na kupunguza ulazima wa uhitaji wa virutubisho vya viwandani.

**3.2 Tume ya Taifa ya Umwagiliaji – Fungu 05**

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu Utekelezaji wa Mipango ya Tume ya Taifa ya Umwagiliaji kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati inashauri yafuatayo: -

(a) Ukusanyaji hafifu wa maduhuli ya Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji unaipotezea Serikali mapato. Kamati inaishauri Tume kuweka utaratibu utakaowezesha watumiaji wa maji kulipa tozo za maji ili kuiwezesha Tume kufikia malengo iliyojiwekea;

(b) Serikali ifanye uchambuzi wa kina kuainisha miradi ya mabwawa ya kilimo cha umwagiliaji ambayo yamefikia zaidi ya asilimia 60 ya utekelezaji na kuyakamilisha kwa haraka ili tija kwa sekta hii muhimu ya kilimo ianze kuonekana; na

(c) Serikali iendelee kuongeza na kutoa fedha kwa wakati katika miradi ya miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza kasi ya kukamilisha miradi. Aidha, usimamizi wa miradi uimarishwe ili fedha zilizotengwa zilete tija iliyokusudiwa.

**3.3 Tume ya Maendeleo ya Ushirika – Fungu 24**

(a) Kamati inaipongeza Serikali ya Awamu ya Sita, inayoongozwa na Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kukubali kutoa mtaji uliowezesha uanzishwaji wa Benki ya Ushirika ambayo itasaidia wakulima kupata huduma za kifedha kwa karibu zaidi. Pamoja na nia njema ya Serikali kuanzisha Benki ya hiyo Kamati inaishauri Serikali:-

i. Kuendelea kuimarisha benki hii kwa kuhakikisha inapata mtaji wa kutosha kuhudumia wakulima katika maeneo mbalimbali nchini; na ii. Serikali ihakikishe Benki hii inaendeshwa kibiashara na kuleta ushindani kwenye Sekta ya Benki nchini.

(b) Mgawanyo wa majukumu na uwajibikaji katika Tume umepunguza ufanisi na kusababisha changamoto hasa za kiusimamizi na uwajibikaji wa Maafisa Ushirika. Kamati inaendelea kuitaka Serikali kukamilisha mapitio ya Sheria ya Ushirika haraka ili kutatua changamoto zinazotokana na usimamizi hafifu na kukosa uwajibikaji katika Sekta ya Ushirika.

## SEHEMU YA NNE

### 4.0 HITIMISHO

### 4.1 Maelezo ya Kuhitimisha

**Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Kilimo ni mwezeshaji na mratibu muhimu wa kufanikisha utekelezaji wa mipango mbalimbali ikiwemo Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili na utekelezaji wa Malengo Endelevu ya Milenia (SGDs) hususani lengo namba 1 linalohusu kupunguza umaskini uliokithiri na lengo namba 2 linalohusu kutokomeza tatizo la utapiamlo kwa kuimarisha lishe bora.

### 4.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutumia fursa hii kuwashukuru kwa dhati Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara, Kilimo na Mifugo, kwa ushirikiano waliouonesha katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya Wizara ya Kilimo. Kutokana na ufinyu wa muda sitaweza kuwataja kwa majina lakini naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Deodatus Philip Mwanyika, Mb | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mariam Ditopile Mzuzuri, Mb | M/Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Job Yustino Ndugai, Mb | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Salma Rashid Kikwete, Mb | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Prof. Sospeter Mwijarubi Muhongo, Mb | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mb | Mjumbe |

| | | |
|---|---|---|
| 7. | Mhe. Khadija Hassan Aboud, Mb, | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Kunti Yusuph Majala, Mb | Mjumbe |
| 9. | Mhe. Tauhida Cassian Galos, Mb | Mjumbe |
| 10. | Mhe. Dkt. Medard Matogolo Kalemani, Mb | Mjumbe |
| 11. | Mhe. Antipas Zeno Mgungusi, Mb | Mjumbe |
| 12. | Mhe. Daud Silanga Njalu, Mb | Mjumbe |
| 13. | Mhe. Eng. Ezra John Chiwelesa, Mb | Mjumbe |
| 14. | Mhe. Francis Isack Mtinga, Mb | Mjumbe |
| 15. | Mhe. Lucy John Sabu, Mb | Mjumbe |
| 16. | Mhe. Ng'wasi Damas Kamani, Mb | Mjumbe |
| 17. | Mhe. Prof. Patrick Alois Ndakidemi | Mjumbe |
| 18. | Mhe. Janejelly James Ntate Mb | Mjumbe |
| 19. | Mhe. Yustina Arcadius Rahhi, Mb | Mjumbe |
| 20. | Mhe. Pauline Philip Gekul, Mb | Mjumbe |
| 21. | Mhe. Abdulaziz Mohamed Abood. Mb | Mjumbe |
| 22. | Mhe. Atupele Fred Mwakibete, Mb | Mjumbe |
| 23. | Mhe. Salim Turky Toufiq, Mb | Mjumbe |
| 24. | Mhe. Mohammed Said Issa, Mb | Mjumbe |

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuona umuhimu wa sekta ya kilimo. Kwa kipindi kifupi cha uongozi wake tumeshuhudia kasi kubwa ya uongezaji wa bajeti ya wizara kwa lengo la kuongeza tija kwenye kilimo.

**Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini siyo kwa umuhimu napenda kutumia nafasi hii kumshukuru Mhe. Hussein Mohamed Bashe (Mb) - Waziri wa Kilimo na Mhe. David Ernest Silinde (Mb) – Naibu Waziri wa Kilimo, kwa ushirikiano mkubwa wanaoipatia Kamati ambao kwa sehemu kubwa umechangia kuiwezesha Kamati kutekeleza shughuli zake kikamilifu.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Wizara ya Kilimo na Taasisi zilizo chini ya Wizara wakiongozwa na Katibu Mkuu Bwana Gerald Geofrey Mweli, akisaidiwa na Naibu Makatibu Dkt. Hussein Mohamed Omary na Dkt. Stephen Justice Nindi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge - Ndg. Baraka I. Leonard kwa kuwangoza vyema watumishi

wa Ofisi ya Bunge katika uratibu na usimamizi wa shughuli za Kamati kwa ujumla hadi kukamilika kwa taarifa hii.

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo (Fungu 43, 24 na 05), kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Deodatus Philip Mwanyika (Mb)
**MWENYEKITI KAMATI YA BUNGE YA VIWANDA, BIASHARA, KILIMO NA MIFUGO**

21 Mei, 2025

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kusoma vizuri.

Waheshimiwa Wabunge sasa tunaanza kuchangia, tunaanza na Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, ajiandae Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, ajiandae Mheshimiwa Katani Ahmad Katani.

**MHE. SALMA R. KIKWETE:** Mheshimiwa Naibu Spika wa Bunge letu Tukufu awali ya yote ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kupata hii fursa ya kuchangia hii Wizara ya Kilimo ambayo ni Wizara nyeti sana kwa ustawi wa Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya katika Taifa letu la Tanzania, Afrika na Duniani kwa ujumla. Pia, nimpongeze yeye Mheshimiwa Rais wetu kwa kuwa mgombea pekee wa Chama chetu Cha Mapinduzi. Tanzania inamwamini, Watanzania wanamwamini na wanamwamini kwa kazi nzuri ambazo anazifanya katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni imani yangu na ni imani ya Watanzania wote kwa ujumla kwamba kama tunavyojua mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi. Kwa kuwa ni mwaka wa uchaguzi kutokana na kazi kubwa na ni nzuri ambayo ameifanya katika nyanja mbalimbali na hasa katika hii Wizara yetu ya kilimo, hatuna mashaka hata kidogo kwamba Watanzania watamchagua kwa kura nyingi na kwa kura za kihistoria kwa mabadiliko au kwa mapinduzi makubwa aliyoyafanya ndani ya Wizara yetu hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo nimpongeze Dkt. Emmanuel Nchimbi; nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango; nimpongeze Rais Mwinyi wa Zanzibar; na nimpongeze msimamizi wa Shughuli za Serikali Bungeni, Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Kassim Majaliwa Majaliwa; pamoja na Naibu Waziri Mkuu, Mhesimiwa Dkt. Doto Biteko bila kusahau Watendaji wa Wizara ambao wanaongozwa na Mheshimiwa Hussein Bashe. Mheshimiwa Hussein Bashe ni jemedari aliyeshika makali. Hatuna mashaka na ndugu huyu, Ndugu Hussein Bashe kwa kazi kubwa na nzuri ambayo anaifanya katika hii Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo ninaamini Hotuba hii ambayo leo Mheshimiwa Bashe ameitoa imesikilizwa na wWtanzania wote. Watanzania wameona kazi nzuri iliyofanyika katika hii Wizara, hongera sana Mheshimiwa Waziri wetu wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa hii Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema imesikilizwa na Watanzania wote, Mheshimiwa Bashe haukuacha kipengele hata kimoja, umeeleza kwa mapana yake. Haya yote uliyoeleza ni kutokana na maagizo ambayo tarehe 22 Aprili, 2021 Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa ndani ya Bunge hili ametoa maelekezo jinsi gani ya kufanya, jinsi gani ya kuleta mapinduzi ya kilimo katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ameeleza hali ilivyokuwa mwaka 2021 wakati Mheshimiwa Rais anasema na baadhi ya mambo hayo ni mikopo midogo, uhaba wa maafisa ugani, ushiriki mdogo

wa wanawake na vijana, mfumo dhaifu na mambo mengine yote Watanzania wameyasikia. Ulipokabidhiwa wewe Wizara hii, umeifanyia haki. Maeneo ya umwagiliaji yalikuwa ni machache, sasa hivi maeneo ya umwagiliaji yameongezeka. Ukitaka uwe na chakula cha uhakika ni lazima uongeze tija kwenye umwagiliaji. Maeneo ya umwagiliaji yameongezeka kwa kiasi kikubwa, hongera sana. Mama Samia umetizima ndoto zako kwa kufanya Tanzania iwe ni eneo la pekee katika Taifa letu hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na suala la ongezeko la chakula tulikuwa tunazalisha mahindi kidogo, leo hii kwenye chakula tunajitosheleza. Ukitaka uondokane na umaskini na suala zima la usalama wa chakula ni lazima uwe na uhakika wa chakula. Leo chakula tunazalisha kwa 100% na tunajitosheleza, hongera Mheshimiwa Waziri Bashe, hongera Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, chakula ni jambo la msingi, kulikuwa na suala la chakula, kulikuwa na suala la mafuta hapa na ikifika wakati na hasa katika mwezi ule ambao sisi kama waislamu tunaamini ilikuwa ni changamoto, sukari hakuna. Leo hii hatuzungumzii tena, tunazungumzia changamoto kwa kiasi kidogo sana, hongera sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo tunataka tuzungumzie suala la mbegu. Kuhusiana na suala zima la mbegu sasa kama nchi, kama Taifa tunazalisha wenyewe mbegu zaidi ya 80%, asilimia iliyobaki ni kidogo tu ambayo tunaomba kutoka nje. Mbegu ndiyo kila kitu katika usalama mzima wa chakula, hongera sana kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuhusiana na suala la uzalishaji wa mbegu, lakini mbegu hizi ambazo tunazalisha kama tunavyosema tunazalisha wenyewe na nyingine zinatoka nje. Kuna suala zima la mbegu zetu za asili.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbegu za asili ni kitu muhimu kwa nchi na ni kitu muhimu kwa Taifa lolote lile. Kila mtu lazima awe na kitu chake, wakoloni walipokuja kututawala walitugawa katika

mataifa na walipotugawa katika mataifa walisema vitu vyote sisi havina maana, vitu vyote ni vya kishenzi. Sasa kutokana na hili hata kwenye suala la mbegu wametutengenezea mikakati tusiwe na vyetu. Kwa hiyo, leo tukiwa na mbegu zetu itatusaidia sana kuondokana na ule utumwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunisikiliza, ninaunga mkono hoja kwa 100%. Ninaipongeza sana Serikali, ninampongeza sana Mama Samia Suluhu Hassan. Tunaingia kwenye uchaguzi, tunakuombea urudi tena, tunawaombea Wabunge wote warudi tena ili tuendelee kuchapa kazi kwa maendeleo ya Taifa letu la Tanzania. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsanteni sana. Mheshimiwa Anne Kilango, ajiandae Mheshimiwa Katani na ajiandae Mheshimiwa Ditopile.

**MHE. ANNE K. MALECELA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi kubwa ya afya na uhai.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninamshukuru sana Waziri, Mheshimiwa Bashe, kila Mbunge atakayesimama hapa atakupongeza na ambaye hatofanya hivyo anakunyima haki yako, unastahili kupongezwa. Mtu akikuangalia haraka haraka anaweza asikufahamu, lakini wewe ni Waziri mzuri sana. Waziri ambaye ni msikivu sana, anayesikiliza Wabunge, anayeshirikiana na wenzie, kubwa kuliko yote yeye ni mchapakazi sana, hongera. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niongee kwa nguvu kubwa, ninaomba na Watanzania wanisikilize vizuri. Watanzania wenzangu nchi isiyokuwa na chakula inapoteza usalama, nchi ikikosa chakula inapoteza utulivu, sasa mimi ninaomba nitumie nafasi yangu na Watanzania wanielewe kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ya Awamu ya Sita imefanya jambo kubwa sana, kwa sababu gani ninasema hivyo? Rais - Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021 alikuta bajeti ya kilimo ya mwaka 2021/2022 ilikuwa shilingi bilioni 294. Ninaomba

Watanzania mpasikilize hapa, alikuta bajeti ya kilimo mwaka 2021 na mwaka 2022 shilingi bilioni 294. Leo hii bajeti ya kilimo yam waka 2025/2026 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu ameipandisha mpaka imefika shilingi 1,242,000,000,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tafsiri ya hilo jambo lililofanywa na Serikali ya Awamu Sita ni pana mno. Siwezi kusimama nikaliongea wala hakuna mtu anaweza akaliongea. Uitoe nchi kwenye shilingi bilioni 294 bajeti ya kilimo uipeleke kwenye shilingi trilioni 1.242. Kwanza ni kwamba amehakikisha kuna utoshelevu wa chakula *(food security)* kwenye nchi yake, hilo ni la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, amesimama imara kuhakikisha nchi yake inakuwa na usalama kwa sababu wananchi wakiwa na njaa ndugu zangu ndipo kelele zinapokuwa nyingi. Kwa hiyo, ninaomba Watanzania waelewe kwamba alilolifanya Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na Serikali yake, halijawahi kufanywa, ni kubwa mno. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi mimi niseme ukweli mimi ni Mbunge wa Same Mashariki, Jimbo la Same Mashariki 100% liko vijijini. Jimbo la Same Mashariki 100% wanalima, ni kilimo, sasa ukishafanya hivi kwa Jimbo la Same Mashariki hivi mnategemea kweli Samia akapate kura 60% Same Mashariki? Haiwezekani. Wananchi wamemkubali sana, jinsi ambavyo Rais ameamua kukishika kilimo cha nchi hii, hakuna nchi yoyote Afrika Mashariki imefanya hivyo, hakuna. Sisi sasa hivi utoshelevu wa kilimo ni asilimia ngapi? Ni 128%. Nikiwa na maana kwamba sisi tunawauzia majirani zetu hapa, nchi haina kelele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mimi ningeomba kuzungumzia jimbo langu kidogo. Ninaomba niongelee jimbo langu; kwanza niipongeze Serikali sana kwamba imejitahidi sana kuhakikisha miundombinu ya kilimo kwenye Jimbo la Same Mashariki inakuwa vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na Skimu ya Ndungu, mimi kwenye jimbo langu nina skimu ya kisasa moja kubwa ambayo ni ya Serikali inaitwa Skimu ya Ndungu. Ndungu ni kata ambayo ina wakulima zaidi ya 3,000 lakini ile skimu inategemewa na wananchi

zaidi ya 16,000. Ninaishukuru Serikali, imekuwa inaingalia ile skimu vizuri sana, ninawapongeza sana. Mheshimiwa Waziri sasa ombi langu kwako, ninaomba Skimu ya Ndungu iangaliwe vizuri zaidi, ninaomba muongeze pesa ili kupeleka kwenye skimu ile kwa sababu wanaoitegemea ni zaidi ya wananchi 16,000. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali, ninaomba nikubali kwamba Serikali iliniletea shilingi bilioni 1.7 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya kilimo katika Kata ya Myamba. Mheshimiwa Waziri lakini nikuombe sasa kazi imefikia 99% lakini bado kuna mifereji mingi ya Kata ya Myamba haijaboreshwa na Kata ya Mpinji hamjaanza kabisa na ndiyo nimeongea na umwagiliaji mkoa wameniambia wameleta *request* kwako kuomba fedha kwa ajili ya Kata ya Myamba na Mpinji. Ninakuomba ulitekeleze hilo katika mahesabu yako ya hii bajeti ya sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niende kwenye Kata ya Kihurio, haa! Ninaunga mkono hoja. Nimepotezea wapi muda? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Katani, Ajiandae Mheshimiwa Ditopile na ajiandae Mheshimiwa Silanga.

**MHE. KATANI A. KATANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nichukue fursa hii kumshukuru *Allahu Tabāraka wa Taʻālā*. Pia nimpongeze sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni mkulima, kwa hiyo ninapochangia kilimo, ninachangia kitu ninachokifahamu sana kwa sababu ninaishi nacho. *Transformation* aliyoifanya Rais Samia kupitia Waziri Mheshimiwa Bashe, ninadhani ni ya kuigwa Afrika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mambo matatu kwa sababu ninatoka kwenye korosho na nikukumbushe kwa sababu tulikuwa wote. Kuna wakati tuliua hapa *export levy,* tukaifuta, lakini kwa utashi wa Mheshimiwa Rais mwaka jana tumerejesha *export levy* yote na irudi kwenye korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kubwa lililofanywa na Mheshimiwa Rais kupitia Waziri Mheshimiwa Bashe ni suala la ruzuku ya pembejeo ya kilimo. Tangu ninazaliwa kwenye korosho hakukuwahi kupatikana ruzuku ya kilimo, lakini tangu Rais Dkt. Samia amechanguliwa wakulima wa korosho wa Taifa hili wanapata pembejeo bure. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kifedha, kwa mara ya kwanza Rais Dkt. Samia tarehe 28 Aprili amezindua Benki ya Ushirika ambayo inakwenda kutoa mikopo kwa wakulima chini ya 10%. Haya ni mambo ambayo yanamchanganua Mheshimiwa Rais na dhamira yake ya dhati kwa wakulima wa Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kwenye korosho kuanzia mwaka 2021/2022 Serikali ya Mama Dkt. Samia imetupatia fedha shilingi bilioni 59.4; mwaka 2022/2023 ikatupatia fedha shilingi bilioni 96.8; mwaka 2023/2024 ikatupatia shilingi bilioni 189 ya ruzuku ya pembejeo; na mwaka 2024/2025 tukapata shilingi bilioni 281. Hii ruzuku tunayoisema ni utashi wa Mheshimiwa Rais na akaamua kurejesha *export levy* ili fedha yake yote iende ikahudumie wakulima wa korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha; pamoja na jitihada za Mheshimiwa Rais anazozifaya kwa Taifa hili kwa wakulima, pamoja na jitihada za Mheshimiwa Waziri na wasaidizi wake kuona wakulima wanapata pembejeo bure, leo fedha zimekusanywa na *TRA* zimeenda Hazina. Mpaka leo tunapozungumza zaidi ya shilingi bilioni 194 hawajarejeshewa Bodi ya Korosho kulipa wazabuni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nina mashaka kwa kazi kubwa inayofanywa na Waziri Mheshimiwa Bashe na tunakwenda kuvunja Bunge tarehe 27 Juni, Mungu si Athuman kwa kazi anazofanya anaweza akatolewa pale akapewa nafasi kubwa zaidi. Je, atakuja Waziri mwenye maono kama Waziri Mheshimiwa Bashe? Je, hawa wanaodai fedha, maana Waziri Mheshimiwa Bashe anakesha usiku na watu wa benki kuona namna gani wazabuni zote wa kilimo walikuwa hawakopesheki. Kwa utashi wa

Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Bashe alikuwa anakutana na wa benki mpaka usiku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ikitokea leo Mheshimiwa Bashe amepewa nafasi kubwa, hizi fedha atakuja Waziri mwenye maono ya wakulima? Hawa waliosambaza pembejeo kwa miaka minne hawajapewa fedha, watalipwa na nani? Niombe sana kama uwezekano wa fedha kukusanywa na *TRA* imekuwa ni shida, mlete sheria hapa fedha zikusanywe na Bodi ya Korosho yenyewe kwa sababu ndio inatoa *export permit* ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni rahisi sana anayekwenda kuchukua *export permit* analipa na *export levy* na fedha zitakwenda kutumika kwa ajili ya korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wazabuni wa pembejeo wengi wanadaiwa na benki, lakini tuna shilingi bilioni 194, hivyo kwa hesabu ya mwezi Machi ninaamini kwa korosho zilizosafirishwa mpaka sasa maana yake *TRA* kwa maana ya Hazina wamekusanya zaidi ya shilingi bilioni 200 ya korosho. Tunadaiwa na wazabuni zaidi ya shilingi bilioni 356. Wazabuni hawa ni Watanzania wenzetu, wameipatia Serikali pembejeo za zaidi ya shilingi bilioni 626. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuombe sana kwa hekima zako uone jambo hili ni namna gani Serikali inaweza kufanya *intervention* ili fedha zipelekwe Bodi ya Korosho, wazabuni walipwe pembejeo. Tunaposema leo tumezalisha tani 528,000 maana yake tangu tumepata uhuru wa Taifa hili hatujawahi kuzalisha korosho tani 528,000. Hizi ni jitihada za Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muunganio wa Tanzania kwa kutoa pembejeo bure. Kama wazabuni hawakupewa fedha, nani ataendelea kuleta pembejeo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wa mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma wanaolima korosho sana na mikoa ya Pwani, Tanga tuna matumaini makubwa na kazi inayofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan. Sasa hizi fedha ambazo tumekubaliana na tumepitisha sheria hapa na zimeshakusanywa...

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe sana Serikali na Mheshimiwa Rais, ninadhani wasaidizi wake wanasikia, aone namna ya kuingilia kati jambo hili ili fedha wapewe Bodi ya Korosho, wazabuni walipwe fedha na wakulima waendelee kupewa pembejeo bure kama dhamira ya Mheshimiwa Rais inavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukija Mtwara kazi inayofanywa na Waziri Bashe, leo tuna kongani ya viwanda inajengwa pale Malanje. Katika fedha zinazokusanywa ni pamoja na hizo fedha ambazo zinakusanywa kwenye korosho. Niombe sana Mheshimiwa Rais kama Waziri Bashe haendi mbele umuache kwenye kilimo hapa awasaidie Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii mikakati mlioanza akija mtu mwingine isije sisi watu wa korosho tukaja tukalia tena hapa. Sisi tulishakombolewa, hatuna habari ya kulia tena hapa. Sisi hapa ni kupongeza na kusubiri bei bora ya korosho kama ilivyotokea mwaka jana, shilingi 4200 na zaidi, hii ni heshima kubwa kwa wakulima wa zao la korosho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, wageni waliopo Bungeni asubuhi hii:

Wageni waliokaa Jukwaa la Spika, wapo wageni wa Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe - Waziri wa Kilimo ambao ni Mheshimiwa Dkt. Anthony Diallo - Mwenyekiti wa Bodi ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania; Ndugu Benson Ndiege - Mrajisi Tume ya Maendeleo ya Ushirika; Ndugu Naitapwaki Tukai - Mkuu wa Wilaya ya Nzega; na Mheshimiwa Shomary Mndolwa - Mkurugenzi wa Halmasahuri ya Mji wa Nzega. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge; wapo wageni wengine wa Mheshimiwa Bashe - Waziri wa Kilimo ambao ni Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Wakuu wa Taasisi, Wakuu wa Vitengo, Idara na Maafisa kutoka Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Wapo pia Wakuu wa Taasisi za Sekta Binafsi zinazojishughulisha na kilimo na wadau kutoka Mashirika ya Kimataifa, karibuni. *(Makofi)*

Pia wapo wadau kutoka taasisi za fedha za *NMB, CRDB, TADB, Azania Bank* na *Stanbic*. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Madiwani na Halmashauri ya Mji wa Nzega wakiongozwa na Mwenyekiti wa Halmahsauri Ndugu Barbara Makono, karibuni, mmemuona Waziri wenu anavyosifiwa, sasa mkienda huko tena. *(Makofi)*

Wapo pia Viongozi wa Mji wa Nzega, Viongozi wa Madhehebu ya Dini kutoka Wilaya ya Nzega, karibuni. *(Makofi)*

Wageni wengine ni Wenyeviti na Mameneja wa Vyama Vikuu vya Ushirika, Viongozi wa CCM Mkoa wa Tabora pamoja na Viongozi wa CCM Wilaya ya Nzega na watumishi kutoka Ofisi ya Mbunge Jimbo la Nzega Mjini. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Regina Ndege Qwaray, wakiongozwa na Mbunge Mstaafu Mheshimiwa Jitu Vrajlal Soni kutoka Babati. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Soni ni Mbunge wa zamani na vilevile ni mkulima mzuri sana. Hongera sana. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Priscus Tarimo ambaye ni mpigakura wake kutoka Moshi Mjini, Mkoa wa Kilimanjaro Ndugu Ahmed Karia. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Neema Mwandabila ambaye ni Ndugu Neliwike Mwambepo, Mtumishi kutoka Kampuni ya *Benz Agro Dodoma. (Makofi)*

Wageni waliolitembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo; wageni 10 wa Kikundi cha Sala kutoka Parokia ya Kiwanja cha Ndege cha Jijini Dodoma. *(Makofi)*

Namuita sasa Mheshimiwa Ditopile, ajiandae Mheshimiwa Silanga.

**MHE. MARIAM D. MZUZURI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitangulie kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujaalia uzima na afya kuweza kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu hili kuweza kuchangia kwenye bajeti ya Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nikushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii. Kipekee ninaomba niungane na wenzangu waliotangulia kuchangia kuunga mkono bajeti ya Wizara ya Kilimo kwani tumejionea sisi. Miaka minne ya uongozi shupavu wa Dkt. Samia Suluhu Hassan, umewatendea haki wakulima wa nchi hii. Ongezeko la bajeti tangu bajeti yake ya kwanza mpaka leo ni kweli inaakisi mahitaji ya wana kilimo wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nimesimama hapa unajua ndio tunaelekea ukingoni mwa Bunge hili la Kumi na Mbili. Siku siyo nyingi tutarudi kwa wananchi kwenda kuwaelezea ni nini tuliyoyaahidi mwaka 2020, yapi tumeweza kufanya na wapi tunaenda kuyaendeleza iwapo watatupatia tena ridhaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Bunge hili siyo sana la kushauri shauri pamoja na kazi ya kupitisha bajeti, lakini tunatumia fursa hii kuelezea yale mema na makubwa yaliyofanywa na Serikali yetu wa Awamu ya Sita, lakini kwa ushauri, usimamizi na utekelezaji wa Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninao ujumbe kutoka kwa wakulima wa nchi hii na wanasema hivi; wanatambua Chama Cha Mapinduzi kimeshampitisha rasmi Dkt. Samia Suluhu Hassan kuwa mgombea wa nafasi ya Urais kwa uchaguzi utakaofanyika mwezi Oktoba, 2025. Wanasema hivi; wao Tanzania hii wapo zaidi ya milioni nane na tena wamesajiliwa na wamejiandikisha kupiga kura. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo atoe mashaka kura zote za wakulima ndani ya nchi hii zitaenda kwa Dkt. Samia Suluhu

Hassan. Wanasema nia wanayo, uwezo wanao na sababu za kwenda kumuunga mkono wanazo. Kwa uchache kutokana na ufinyu wa muda nitazielezea kwa uchache sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja utashi wake wa kisiasa kama kiongozi wa nchi yetu, lakini binafsi yeye mwenyewe Dkt. Samia Suluhu Hassan ni mtu ambaye ameonesha imani kubwa kwenye kilimo kwa sababu anayo mapenzi ya dhati kwenye sekta yake ya kilimo. Kwanza yeye mwenyewe ni mkulima kwa vitendo, anayo mashamba hapa Dodoma na kule Morogoro. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunasema hivi, tumegundua kumbe mume wa Rais wetu kipenzi Mzee Ameir Hafidhi kwa utaalamu wake ni mtaalam wa mambo ya kilimo. Ukiachilia mbali yeye mwenyewe ni kilimo. Kwa hiyo, sisi wakulima wa nchi hii pamoja na kumtambua Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kama Rais wetu kipenzi, lakini sisi tunamtambua kama shemeji yetu, wifi yetu na mkwe wetu. Kwa hiyo, ni sababu kubwa ya sisi kumuunga mkono itakapofika mwezi Oktoba, 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, imekuwa ni kilio cha wakulima tangu Uhuru wa nchi yetu tunasikitika, tunalia kwamba mbona Serikali haituungi mkono? Keki hii ya Taifa mbona haifiki kwetu? Kwa kweli utashi wake Dkt. Samia Suluhu Hassan tangu aingie madarakani tumeona namna anavyohangaika kuhakikisha keki ya Taifa hili inawagusa wakulima, inawafuta machozi na inaenda kuwainua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Rais tunakushukuru sisi wakulima, leo siyo tu kwamba umesikia kilio chetu, lakini tukuhakikishie leo tunatabasamu na kucheka sisi wakulima. Leo hoja za wakulima zinajadiliwa na sekta binafsi, Serikali na kila mtu katika nchi hii. Ongezeko la bajeti limekuwa kubwa na hiyo ndio sababu kubwa ya sisi kumuunga mkono. Tukienda kupiga kura tunaenda kupiga kura kwa ajili ya ruzuku kwenye maeneo mbalimbali na mazao mbalimbali ndani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kuna ruzuku kwenye korosho zaidi ya shilingi bilioni 200. Leo kuna ruzuku kwenye pamba ambayo mkulima wa pamba kwenye msimu huu wa kilimo

ameenda kulimiwa kwa ruzuku ekari moja kwa shilingi 35,000, huko nyuma alikuwa analimiwa kwa shilingi 70,000 mpaka shilingi 100,000. Nani kama Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wakulima? Lakini hakuishia hapo, kapeleka ruzuku kwenye tumbaku zaidi ya shilingi bilioni 21, leo hii tunasimama kidete kusema Tanzania nchi ya pili Afrika kwa kuzalisha tumbaku. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaenda kupiga kura kwa ajili ya uimarishaji, tulifika hatua tukakata tamaa kwenye ushirika, lakini leo siyo tu kwamba ushirika umekuwa imara, leo hii tuna Benki ya Ushirika. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? Leo tukienda kupiga kura tunapiga kura kwa ajili ya mashamba makubwa ya pamoja ambayo yanaajiri vijana na akina mama. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kupiga kura tunapiga kura kwa ajili ya miradi mikubwa ya umwagiliaji, mabwawa pamoja na miundombinu. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kilimo? *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii siyo ruzuku tu kwenye mbegu na kadhalika, ruzuku mpaka kwenye kununua mazao yetu. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? Tunashuhudia wenyewe tukipiga kura tunaenda kupiga kura kwa ajili ya kukua kwa kilimo chetu kutoka 2.7% mpaka 4.2%. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan kwenye kilimo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kupiga kura, tunaenda kupiga kura kwa sababu Dkt. Samia Suluhu Hassan ametujali wakulima wadogo ndani ya nchi hii na wakati anaingia madarakani kuna mkulima alikuwa anavuna magunia mawili tu, lakini leo kutokana na uwekezaji wake tunavuna zaidi ya gunia 30 kwa ekari moja. Nani kama Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo machache, lakini nipende kumshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na Wizara yake na taasisi zote zilizo chini ya Wizara ya Kilimo hawajatusahau Dodoma, pia hawajatusahau Halmashauri ya Kondoa Mji kwa miradi mikubwa ya umwagiliaji ya *BBT,* pamoja

na kutuchimbia visima kwa wakulima wadogo ndani ya Halmashauri ya Kondoa Mji, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Njalu Daudi Silanga, ajiandae Mheshimiwa Munde na Mheshimiwa Cherehani. Muda ninafikiri utatosha…

**MHE. NJALU D. SILANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru kwa kunipatia nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya KIlimo. Hotuba ambayo kwa kweli inatia matumaini makubwa ndani ya Taifa letu. Pia nampongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na nzuri anayoifanya kwa kuthubutu na kusimamia haki na biashara za kilimo. Hongera sana Mheshimiwa na timu yako kwa kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri ametaja mikakati yake katika hotuba yake, lakini amezungumzia Mkoa wetu wa Simiyu. Simiyu ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa pamba, ametaja kiwanda cha vifaatiba, lakini ametaja na kuwa na mpango mzuri wa kujenga kiwanda cha kuongeza thamani ya zao la pamba. Sisi Wana-Simiyu na wananchi wa Mkoa wa Simiyu tunakusubiria kwa hamu sana na tuko tayari kuupokea na kufanya kazi hiyo kwa vitendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ikumbukwe kuwa kwa haya mazuri yote Mheshimiwa Rais akiwa Makamu wa Rais alikuja Simiyu akielekeza kuwa na kiwanda cha vifaatiba na sasa hivi upele una mkunaji na mkunaji ni Mheshimiwa Rais na wewe msaidizi wake ambaye sasa umeonesha nia na matumaini makubwa. Tunaamini tutafanya kazi vizuri na tutawabadilisha Watanzania wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana Mheshimiwa Bashe kwa mikakati mizuri hasa kwenye suala zima la vijana wa *BBT*. Nchi hii kuna Maafisa Ugani wapo vijijini, lakini wamezidiwa kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi Wabunge wote tuliomo humu ndani tunatoka kwenye Mabaraza yetu tunajua changamoto

zilizopo kwenye halmashauri zetu. Ushauri wangu maafisa vijana hawa wanaotokana na *BBT* tuwapeleke katika mazao yote ya kimkakati. Kila taasisi ambayo inashughulika tumbaku, korosho, kahawa, mazao yote ambayo umetuorodheshea zaidi ya tisa, tuwapeleke hawa vijana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukishawapeleka hawa vijana, Serikali kupitia halmashauri na Serikali za mkoa waunganishe iwe *chain* moja ya kufanya kazi kwa sababu lengo ni moja, ili tusikinzane na *D by D* ambayo ni ya kisheria zaidi ili wewe Waziri ukitoa maelekezo yashuke mpaka huku chini, wasaidiane taasisi na taasisi binafsi ili kusukuma uzalishaji wa mazao haya ya kimkakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia tu kwenye mfano wa tumbaku na mfano wa pamba, mwaka 2023 tulishuka uzalishaji mpaka tani 142. Mwaka jana tukavuka baada ya kuingiza mpango wa Mheshimiwa Bashe ambao aliuanzishia Dodoma, lakini akachukua mawazo yetu, ameshusha mpaka kule chini. Tunakupongeza kwa kuendelea kutusikiliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, imetoka kwenye 140 tumekwenda kwenye 282. Mwaka huu tuna matarajio ya kupata 500 hili ni jambo ambalo linatia matumaini. Nini kifanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, vijana hawa ambao umewaleta kupitia *BBT* tuendelee kuwajali na kuwaajiri, tuwaingize kwenye mifumo kadri bajeti ya ajira inavyopatikana ili kutia moyo na kuongeza tija katika uzalishaji wa zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili, umenunua matrekta zaidi ya 500 na ya karibu 70% yamekuja katika mkoa wetu wa Simiyu. Matrekta haya yatafanya kazi vizuri yakirasimishwa kwenye vikundi ambavyo wakulima wako tayari kununua ili kusudi Serikali iendelee na jukumu lingine la kuendelea kuongeza matreka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, linguine ni kuwa matrekta haya kwa mazingira ambayo kule kijijini kwenye utaratibu ambao mmeshauanzisha kule Serikalini kwamba itoke *control number*

ndiyo aende akalime, kwa hiyo kalenda yetu itakuwa inatupita, lakini ni mpango mzuri, mimi ninakuomba sana, ziko *AMCOS* ambazo ziko imara, ziuziwe yale matrekta, wakulima wale waendelee kulima, waendelee kushindana, hasa kule Usukumani tuna tabia ya kushindana. Nikiona trekta yangu na mwingine na mwingine mwaka unaofuata atanunua. Ndiyo kazi kubwa ya Serikali kuhakikisha kwamba mnawainua kiuchumi na kuweza kuongeza Pato la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni suala la pembejeo; pembejeo zetu zinapatikana katika kipindi cha awamu kama tatu/nne hivi, wakati mwingine inaathiri mazao yetu ya pamba na mazao mengine. Ninaomba kama ilivyo kwenye hotuba yake ameelezea kuwa na malori, magari ya kubebea na vitu vingine, ninamuomba sana Mheshimiwa Waziri, pembejeo hizi ziwe zinaingia nchini kuanzia mwezi wa sita na mwezi wa saba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mkulima anapochukua mbegu aondoke na pembejeo yake, pale ndiko mtakapofahamu kwamba mkulima yupi anayelima na mkulima gani ambaye Halimi, lakini sasa hivi kwa ugawaji wa pembejeo zinakuja mpaka mwezi wa 12 ama mwezi wa kwanza, tayari watakuwa wameshamaliza hiyo kazi. Ninakuomba sana Mheshimiwa Waziri jambo hili ni muhimu uweze kutusaidia sana katika maeneo haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuwa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi ilituelekeza kuimarisha ushirika na kazi hii imefanyika vizuri sana, ninakuomba Mheshimiwa Waziri na timu yako, hebu tuendelee wafanye kama inavyofanya *KACU*, wafanye kama inavyofanya *SIMCU*, wafanye kama inavyofanya ile ya Chato ili kusudi ushindani uwepo katika maeneo. Tuondokane na dhana ya kuwa na chombo ambacho chenyewe kinasubiria kuletewa vikamisheni vidogo vidogo ambavyo havina maana, waingie sokoni kama hawa watu wengine na italeta tija kubwa sana kwenye mfumo mzima wa soko huria ambao utakuwa umefanyika. Kwa hiyo, ninaendelea kushauri jambo hili ni muhimu likafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri, mazao yetu haya ambayo umebinafsisha kwenye *COPRA* tunakushukuru, tumeyaona kabisa mabadiliko yanavyokwenda, lakini elimu iendelee kutolewa katika maeneo yetu tunakotoka hususan kwa viongozi ngazi za wilaya na ngazi za kimkoa. Tunaamini Wizara mnakuwa na masikio mengi, mnashiriki katika makongamano mbalimbali ya kidunia, lakini waliopo kule chini hawajapata hii elimu, kwa hiyo, unapokuja na majukumu ya moja kwa moja, unakuwa ni ukinzani kati ya Serikali kwa Serikali, lakini kama watu wote mnaimba wimbo unaofanana, ninaamini kabisa *COPRA* na wengine watakuwa ni sehemu ya kutafuta masoko na kueneza jitihada nzima za Wizara yako ili kufanya kubwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa zaidi ninaungana na mchangiaji aliyemaliza Mheshimiwa Ditopile kwamba yote haya tunayafanya ni kwa sababu msimamizi wetu Amiri Jeshi Mkuu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amedhamiria kuhakikisha mazao yote ya kimkakati na kilimo na ukizingatia 60% ya Watanzania ni wakulima na wafugaji, jambo hili Mheshimiwa Rais tunampongeza sana, lakini tunakupongeza wewe kwa uthubutu.

Mheshimiwa Naibu Spika, maneno ni mengi, ninakuhakikishia Mheshimiwa Waziri na timu yako chapa kazi, maneno yatakuwepo na tutakusifu muda wote, tunaamini ukianzisha jambo wapo maadui wengine wasiotaka maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Njalu. Mheshimiwa Munde, Mheshimiwa Cherehani na ajiandae Mheshimiwa Sabu.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kuchangia.

Awali ya yote na mimi ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha siku ya leo kuchangia katika Bunge letu Tukufu ambalo ndiyo tunaendea ukingoni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niungane na Wabunge wenzangu kumpongeza sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kwenye nchi yetu nzima hususan kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wenzangu wametangulia wamesema bajeti iliyokuwepo ya kilimo katika nchi hii, lakini leo tunaenda kwenye shilingi trilioni 1.2. Hili ni jambo kubwa na ni jambo la kihistoria na jambo hili haliwezi kusahaulika kabisa. Inaenda kuinua wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninampongeza Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe, ninampongeza Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo pamoja na Wakurugenzi wao wote wa taasisi hii ya Kilimo ambao wameweza kuweka historia ya Wizara ya Kilimo. Wizara hii zamani ilikuwa kama ni *bench* fulani, lakini leo wamefanya kazi kwa ushirikiano na kuiona Wizara ya Kilimo ilivyokwenda kuinua Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wametimiza *slogan* yao ya kilimo ni biashara, walikuwa wanasema kilimo ni biashara lakini leo tumeona Watanzania wote wanakwenda kwenye kulima. Zamani ulikuwa ukilima unaonekana kama ni mtu maskini, hauna uwezo, lakini leo kila mtu anatamani kulima kwa kazi kubwa ilivyofanywa na Wizara ya Kilimo. Kwa kweli, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba nijikite sasa kwenye kilimo chetu cha tumbaku. Toka tumepata uhuru hatujawahi kuona mabadiliko makubwa kwenye kilimo cha tumbaku kama kipindi hiki. Ninaipongeza sana Wizara ya Kilimo hasa Mheshimiwa Waziri na timu yake yote. Tulikuwa tunalima kilo 39,000 kabla Rais Samia hajaingia madarakani, sasa hivi mwaka jana tumepata kilo 122 na tunakwenda kwenye kilo 160,000. Hili ni jambo kubwa sana halijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia katika suala zima la bei, tulikuwa na dola 1.65 sasa hivi tunakwenda kwenye wastani wa dola 2.4 mpaka dola 2.8. Wakulima wameanza kuuza tumbaku yao na wanafanya sherehe kuona wanauza kwa bei kubwa

ambayo hawajawahi kuitarajia. Nani kama Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, tulikuwa na kiwanda kimoja cha tumbaku tu cha *Alliance One*, tulikuwa na *TLTC,* lakini walivyojitoa Mheshimiwa Waziri amefanya jitihada za makusudi tumepata mwekezaji mzawa ambaye ni Mkwawa. Amejenga kiwanda kikubwa cha tumbaku, anachakata kilo 60,000 mpaka kilo 120,000. Hicho ni kitu kikubwa sana kwenye wakulima wa tumbaku, tunampongeza sana huyu mwekezaji Mkwawa kwa kazi nzuri anayoendelea kutufanyia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji Mkwawa amejenga kiwanda kikubwa cha tumbaku ambacho hakipo Afrika Mashariki nzima ambacho sasa tumbaku yetu itapata soko kubwa na itahitajika zaidi. Tunaendelea kupongeza Serikali kwa jitihada zao za kuinua zao hili la tumbaku. *(Makofi)i*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisiwaache *TFC*, hii taasisi ilikuwa imekufa lakini Rais amefanya maamuzi magumu ameifufua, leo *TFC* imegawa mbolea kwa wakati, siyo tu kugawa mbolea kwa wakati pia imeshusha bei kutoka dola 72.45 mpaka dola 63. Tunampongeza sana kaka yetu Mshote na watumishi wake wote wa taasisi yake kwa kazi nzuri waliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatujawahi kupata ruzuku ya mbolea, ndiyo mara ya kwanza, tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa ruzuku ya mbolea. Pia wale wote waliokuwa wanadai ruzuku za nyuma zimeanza sasa kulipwa, changamoto ni ndogo, wapo wanaolipwa mara mbili na wapo ambao hawajalipwa kabisa, kwa hiyo, ninaiomba Wizara izikague hizi changamoto na kuzimaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mwizi wa fadhila nisipomsifia Mkurugenzi wa Benki ya Kilimo *(TADB)* kaka yetu Nyabundege kwa kazi nzuri aliyoifanya. Wakati wanaanza kufufua vyama hivi vya ushirika ambavyo kama vilikuwa vimekufa, ali-*risk* na kuvikumbatia vyama vya ushirika akatoa shilingi bilioni 36 kwa

ajili ya kuvifufua vyama hivi vya ushirika na hatimaye leo ushirika unaendelea mpaka kufikia kufungua benki yao ya ushirika.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa muda wetu ni mfupi sana.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, muda wangu.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa nimesema kaa chini muda wetu ni mfupi sana. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika,....

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbunge sijakuruhusu.

Mheshimiwa Munde, endelea.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, ninampongeza sana Mkurugenzi wa *TADB* kwa kuvishikilia Vyama vya Ushirika, kuviinua na kuvikumbatia, ku-*risk*, leo hii mpaka wamefikia hatua ya kufungua benki yao. Ninaiomba Serikali, imefanya jambo zuri la kufungua Benki ya Ushirika, imetoa mtaji wa shilingi bilioni tano, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu, lakini wasiiache Benki ya Kilimo, waendelee kuiboresha iendelee kushirikiana na Benki ya Ushirika hatimaye wakulima waweze kufanikiwa zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, benki hii ya ushirika nimuombe Mheshimiwa Waziri iwe kimbilio la wakulima. Wakulima hawajawahi kuwa na kiinua mgongo. Niiombe Wizara ya Kilimo itoe elimu kwa wakulima, wanunue hisa nyingi kwenye benki yao ya ushirika, hatimaye waje wapate gawio iwe kiinua mgongo cha mkulima pale atakapozeeka atashindwa kulima, lakini awe na gawio lake linatoka kwenye Benki ya Ushirika.

Kwa hiyo, tuiombe benki hii ya ushirika iwe ndiyo kimbilio la wakulima na iwe ndiyo wanaweza kupata kiinua mgongo chao pale wakizeeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, taasisi zote Serikali, Wabunge tunapata kiinua mgongo, wakulima huwa hawapati kiinua mgongo. Benki hii ya Ushirika ije ifanye jambo hilo kwa wakulima wetu na kuendelea kuacha *legacy* ya Mama yetu Samia Suluhu Hassan kwa wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaipongeza sana *NFRA,* safari hii wakulima walilima sana hasa mazao ya mahindi na *NFRA* ilinunua mazao yote kwa bei nzuri na kuhakikisha wakulima wetu wanaendelea kunufaika. Hili ni jambo kubwa sana, tunampongeza sana Rais wetu Samia Suluhu Hassan na tunasema kwa umoja wetu, Samia Suluhu Hassan anastahili kupita bila kupingwa hata Oktoba, acha ndani ya Chama Cha Mapinduzi tumempitisha bila kupingwa, lakini tunawaomba wapinzani ambao ni watani wetu wa jadi waache nafasi ya Urais, agombee Samia peke yake kwa kazi kubwa aliyoifanya ndani ya nchi hii, anastahili kupewa hiyo heshima kwa kazi kubwa aliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie tu wenzetu wa upande wa pili, *reforms* zetu ziko vizuri, tunasubiri uchaguzi tuje tufanye uchaguzi wa kweli na haki. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshajiandaa, tuna *reform* nzuri na za kutosha. Kwa hiyo, wale wanaosema *no reform* sisi hatuelewi kwa sababu sisi tayari tuna *reform* nzuri na za uhakika. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, kengele ya pili tayari Mheshimiwa Munde.

**MHE. MUNDE T. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Maneno uliyosema ni murua, kwa hiyo ahsante. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wabunge, muda wetu ni mfupi, Mheshimiwa Cherehani ulikuwa unafuata sasa ulikuwa unataka utoe taarifa uchangie, uchukue muda wa mwenzio halafu na wewe unapewa nafasi uchangie tena. *This is not fair*.

Mheshimiwa Cherehani, ajiandae Mheshimiwa Sabu.

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mimi nikushukuru wewe na pia nimshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mheshimiwa Rais leo imetuchukua miaka 61 hatukuwa na Benki ya Ushirika, lakini kipindi cha Dkt. Samia Suluhu Hassan leo kazindua Benki ya Wana-Ushirika. Ni benki ya wakulima, ni benki ambayo ilikuwa ni ndoto za Mwalimu Nyerere, Mheshimiwa Rais amezitimiza na leo wakulima wanaenda kwenye dirisha lao la kuchukua fedha/mikopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba tu, benki hii ya ushirika ambayo Mheshimiwa Rais ameizindua ambayo Mheshimiwa Rais ametimiza ndoto yake, tunaomba isambae nchini kote kwa wakulima wote. Ninakupongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Bashe na timu yako yote, pia nimpongeze sana Mrajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, Dkt. Benson Ndiege, ninawapongeza sana viongozi wote wa Vyama vya Ushirika nchini, Vyama Vikuu kwa umoja na mshikamano waliouonesha kuhakikisha kwamba benki hii inatimiza malengo yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia ninawapongeza sana Warajisi wa Vyama vya Ushirika nchini, wao walikuwa pia washauri wazuri wa vyama vyetu vya ushirika kwa ajili ya kupeleka hisa kwenye

benki hii ambayo leo ina zaidi ya shilingi bilioni 55. Pia niendelee kukupongeza Mheshimiwa Waziri, umetengeneza kura za Mheshimiwa Rais kwa wakulima wote nchi hii kwa heshima kubwa, kwa kiwango ambacho ni cha kimataifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nenda popote kwa wakulima wa chai wanamsifia Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakulima wa tumbaku wanamsifia Dkt. Samia Suluhu Hassan, wakulima wa mpunga, mahindi, chai, kahawa na maeneo yote ambako wakulima wanalima nchi hii wote wanafurahia ruzuku ya pembejeo, wote wanafurahia ruzuku ambayo ilikuwa ni kama ndoto kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakumbuka Mheshimiwa Waziri tulipokuwa Mbeya wakati Mheshimiwa Rais anazindua, watu wengi hawakuamini, maneno mengi yamesemwa, lakini leo waliosema maneno ndiyo wanaotumia *NPK* ya shilingi 60,000, ndiyo wanaotumia *CAN* ya shilingi 60,000, ndiyo wanaotumia *urea* ya shilingi 70,000 na leo wameamini kwa macho. Nami niendelee kukutia moyo Mheshimiwa Waziri, chapa kazi, songa mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kukuomba Mheshimiwa Waziri, benki yetu ya kilimo imefanya mema sana kwa wakulima. Kwa upande wa pamba pamoja na kahawa ni zaidi ya shilingi bilioni 132 zimeenda. Ni hawa ambao toka mwaka 2018 Mheshimiwa Waziri mwaka 2019, wewe mwenyewe ukiwa Naibu Waziri ulikuja Kahama kuungana na wananchi wa Kahama na wakulima wote na ukaanza wewe kwa sauti yako kupeleka fedha zaidi ya shilingi 4,500,000,000 kwa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama *(KACU)* ambacho kilikuja kufanya kazi nzuri sana. Leo ni zaidi ya miaka saba kinaendelea kununua pamba kwa wakulima kwa ushindani mkubwa na leo kimepewa Kiwanda cha Wilimili, kimeyajenga, kinasimika pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kuipongeza Bodi ya *KACU* ikiongozwa na Mwenyekiti wake Ndugu yangu Emmanuel Nyambi Masanja pamoja na menejimenti yake. Wameonesha utulivu mkubwa wa kusimamia fedha za benki. Niendelee kupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Vyama vya Ushirika tukivisimamia vizuri, Vyama vya Ushirika na vile Vyama Vikuu tunaenda kuonesha mapinduzi makubwa sana kwenye ushirika. Tuendelee kuwatia moyo, tuendelee kuwashika mkono ili wasimamie mazao yetu kwa sababu ndiyo wanaosimamia wakulima wetu. Mheshimiwa Waziri mimi niendele kutoa ombi, umefanya vizuri sana kwenye mazao yote, umefanya vizuri sana kwenye tumbaku kama walivyoongea Wabunge wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii ukiangalia *trend* ya masoko inavyoenda na masoko yaliyoishia jana, wastani wa bei unaocheza ni dola 2.8. Pia wanunuzi wa tumbaku leo wakati Mheshimiwa Waziri Bashe ukiwa Naibu Waziri, wewe mwenyewe ulikuwa unatembea Ofisi za Wizara ya Fedha kwenda kuondoa kodi na kufuta tozo, kitu ambacho ilikuwa ngumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipindi cha Mheshimiwa Rais leo miaka minne, tozo zaidi ya 26 zote zimeondolewa kwenye tumbaku. Leo wastani wa bei ambao wakulima wanafurahia ni dola 2.8. *L10F* ambayo ilikuwa inauzwa dola mbili leo *L10F* ina dola 3.320. *L1O* ina dola 3.3, *L1L* ina dola 3, *L20F* ina dola tatu, madaraja yamebadilika wakulima wanafurahia sana. Hawa wakulima Mheshimiwa Waziri wanaenda kanisani, hawa wakulima wana ibada, wanakuombea sana wanamwombea sana Mheshimiwa Rais. Nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri, chapa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi letu moja ambalo tunakuomba Mheshimiwa Waziri, tuondolee tozo ya mionzi. Tozo hii inawaumiza wanunuzi. 0.2 ya kila tumbaku inayouzwa kusafirishwa nje wanatozwa hawa wakulima thamani yake, ina maana wanunuzi wakisafirisha dola milioni mbili, asilimia mbili lazima watozwe. Wanunuzi wanachofanya Mheshimiwa Waziri, hawaendi kulipia fedha yao, wanachofanya kazi yao ni kumpunguzia bei mkulima na mimi ombi langu Mheshimiwa Waziri, *export leavy* hii dola 0.2 ikifutwa kwenye mionzi wanunuzi wanaenda kumpelekea bei mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunaenda kutoka kwenye dola tatu tunaenda kwenda kwenye *L10F* ambayo ni tumbaku

bora, tunaenda kwenye dola nne. Tutaenda kukimbizana na mataifa ya wenzetu Malawi na Zimbabwe ambao wenzetu wameenda kwenye dola nne mpaka dola tano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaendelea kushauri kwa sababu tumepiga hatua, uzalishaji sasa umeongozeka, basi tuwe na mnada wa masoko ya tumbaku. Tuwe na mkataba, lakini pia tuwe na minada ili tupige hatua tuende kama mataifa wenzetu wanavyofurahia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo wakulima wenye uwezo wa kufanya kwa mnada na wapo wakulima ambao hawana uwezo wataingia kwenye mikataba. Hili inawezekana likakuvusha sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri kuna zao ambalo tumelisahau sana, nalo ni zao la maembe. Maembe ningekuomba ingiza na lenyewe kwenye ushirika. Ongea na Vyama vya Ushirika hivi wafanye tathmini ya maembe ambayo yanavunwa kiholela kule kijijini, yavunwe kwa utaratibu mzuri kama ulivyofanya mazao mengine, yavunwe kwa utaratibu mzuri. Ni eneo ambalo yatachangia mapato makubwa kwenye Serikali zetu, halmashauri zetu zitapata fedha nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu leo mti mzima wa embe unauzwa shilingi 2,000, mtu anaokota maembe yote, tena kwa utaratibu wa kutikisa na yale machanga nayo yanapotea, lakini tukiwaingiza kwenye utaratibu mzuri, tukawapa dawa wakayapulizia vizuri, tutawapa utaratibu mzuri wa kuvuna yale maembe yetu. Tayari kwenye halmashauri zetu tutapata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Mheshimiwa Waziri niendelee kukuomba, tayari benki ya *TADB* inahudumia *KACU*, inahudumia *MBCU*, inahudumia, *ACCU*, inapeleka fedha *SIMCO,* ombi langu usimkatie tamaa *SHIRECU* na Nyanza.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Cherehani kwa mchango mzuri. *(Makofi)*

**MHE. EMMANUEL P. CHEREHANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ninashukuru na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sabu.

**MHE. LUCY J. SABU:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya bajeti ya Wizara ya Kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa fursa hii, lakini kiupekee kabisa nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya katika Wizara hii ya Kilimo, tunampongeza kwa dhati kabisa Waziri wa Kilimo - Mheshimiwa Hussein Bashe, Naibu Waziri - Mheshimiwa David Silinde na watendaji wote wa Wizara kwa kazi kubwa na nzuri waliyoifanya katika Wizara hii. Mmedhihirisha kwamba wakulima wa nchi hii mmewatendea haki kweli kweli kwa namna ambavyo mmeweza kuwapa kipaumbele na tunajionea. Bajeti ilikuwa shilingi bilioni 294 na sasa tunaenda kwenye shilingi trilioni 1.2, ama kweli ongezeko la bajeti hili tuna imani linaenda kuwa na matokeo chanya kwa wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Simiyu ni mkoa kinara katika uzalishaji wa zao la pamba, tunashukuru Serikali kwa kuwekeza katika zao la pamba na kwa namna ya kipekee tunampongea Balozi Mwanri kwa namna ambavyo ameendelea kuhamasisha wakulima wa zao la pamba. Pia kiupekee ninampongeza Mkuu wa Mkoa - Mheshimiwa Kenani Kihongosi kwa usimamizi mzuri pamoja na Mkuu wa Wilaya Mheshimiwa Simon Simalenga, wameendelea kuwasimamia wakulima vizuri, na kwa kweli uwekezaji mkubwa ambao umefanywa na Serikali ambapo tunaona pembejeo za pamba za kutosha pamoja na dawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji huu wote unakadiriwa kuwa na thamani ya shilingi bilioni 5.5. Kwa kweli wakulima wa Mkoa wa Simiyu wa zao la pamba tunaishukuru sana Serikali kwa kututhamini, lakini pia kwa kuwekeza katika zao la pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye bajeti tumeona Mheshimiwa Waziri kuna mpango wa ujenzi wa kiwanda cha vifaatiba. Kwa kweli kiwanda hiki kitakuwa na manufaa makubwa sana kwa wakulima wa pamba na itawapunguzia mzigo Serikali kuagiza vifaatiba nje ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi nzuri iliyofanywa katika Wilaya ya Bariadi, Halmashauri ya Mji wa Bariadi, tunaipongeza Serikali kwa kuleta matrekta 13 ambayo kama tulivyoambiwa Serikali imeweka bei elekezi ya shilingi 35,000 ambayo imewapunguzia gharama wakulima kuweza kulima katika mazingira ambayo hayatawapa vikwazo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tumepokea vijana wa *BBT* 15 katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi, ambapo vijana hawa wanafanya kazi nzuri sana ya kuelimisha wakulima na kutoa mafunzo. Tunaishukuru Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumepokea viuadudu *acre pack* 145,000 tunaishukuru Serikali, mbegu tani 555, *pump* 1,500, ndege nyuki sita. Kwa kweli tunaishukuru sana Serikali kwa uwekezaji mkubwa huu ambao unaenda kuwanufaisha wakulima wa Wilaya ya Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa Mfumo wa Stakabadhi Ghalani. Kwa mara ya kwanza Serikali imeruhusu mfumo huu wa wa stakabadhi ghalani katika Mkoa wa Simiyu na tunaishukuru ambapo wameanza na zao la choroko na msimu huu unaofuata tutaenda kwenye mazao ya mbaazi na dengu. Tunaiomba sasa Serikali kwa sababu kuna changamoto ya maghala, iweze kutuongezea ghala ambapo itaruhusu minada ya mazao mchanganyiko kuweza kuendelea katika Wilaya yetu ya Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Wizara ijenge ghala katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi ambapo ndipo tunao wakulima wengi, iweze kuwafikia na waweze kupata uhakika wa masoko. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru Serikali kwa kuwekeza katika miradi ya umwagiliaji, pale Wilaya ya Bariadi tunao Mradi wa Kasoli ambapo mradi huu kwa kweli umekua ukisuasua sana na tunaomba Mheshimiwa Waziri aweze kutupia jicho, na ikiwezekana aweze kuufuatilia kwa karibu sana kuweza kuhakikisha kwamba, kwa sababu wananchi hawa wanausubiri sana mradi huu, na wanaamini kwamba utaenda kuwasaidia kuwa na uhakika wa kulima mwaka mzima bila changamoto ya aina yoyote. Tunaomba utusaidie Mheshimiwa Waziri utakapokuwa unahitimisha hoja yako basi uweze kutoa tamko ambalo litawasaidia kuweza kuona wananchi wa Bariadi katika mradi huu umetupia jicho la karibu zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, tunao mradi ambao uko katika Kata ya Mhango ambapo mradi huu ni mahsusi kwa ajili ya mabadiliko ya tabianchi, ni mradi wa umwagiliaji. Tunaomba pia utusaidie Mheshimiwa Waziri, muweze kuusukuma mradi huu na uweze kukamilika kwa wakati na wananchi waweze kunufaika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya kipekee ninashukuru sana kwa namna ambavyo Serikali imeweza kuwatumia vijana wa *BBT* na katika Mkoa wa Simiyu kama nilivyosema, Halmashauri ya Mji wa Bariadi tunao vijana 15 ambao kwa namna ya kipekee wameonesha ushirikiano na sekta binafsi kupitia makampuni ya pamba kuweza kuwaajiri. Tunaomba muendelee kutuongezea vijana wengine ili kilimo kiendelee kuwa na tija zaidi na waweze kunufaika kupitia elimu ya mafunzo na kilimo cha kisasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kujenga visima virefu vya umwagiliaji katika Mkoa wa Simiyu na ninaomba Wizara iweze kutuongezea kujenga visima vingine katika Halmashauri ya Mji wa Bariadi ambavyo vitawasaidia wakulima kuwa na uhakika wa maji ama kwa kuweza kulima kwa kilimo cha umwagiliaji kwa mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kwa kumalizia ninaiomba Wizara katika mpango wa ununuzi wa magari, ikumbuke pia Halmashauri ya Mji wa Bariadi kuweza kuiongezea gari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan tunamhakikishia Mkoa wa Simiyu ana kura za kishindo ifikapo Oktoba, 2025. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ninawashukuru kwa michango yenu. Jioni tutaanza na Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, atafuatia Mheshimiwa Agnes Hokororo, Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, Mheshimiwa *Engineer* Ezra Chiwelesa na Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

Waheshimiwa Wabunge, ninasitisha shughuli za Bunge mpaka saa 11.00 jioni.

*(Saa 7.05 Mchana Bunge Lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11:00 Jioni Bunge Lilirejea)*

*Mwenyekiti (Mhe. Joseph K. Mhagama) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, tuketi.

Katibu.

**NDG. AZIZA WAZIRI KHEIR – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**MWENYEKITI:** Majadiliano yanaendelea, alishatamkwa Mheshimiwa Ng'wasi Kamani, atafuatiwa na Mheshimiwa Kunti Majala, Mheshimiwa Agnes Hokororo ajiandae.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia katika Wizara hii muhimu sana ya Wizara ya Kilimo kwa ustawi wa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu kwa miaka minne nchi yetu imeshuhudia mapinduzi makubwa sana katika sekta ya kilimo. Sensa pekee tuliyofanya kwa kipindi hiki imetuonesha kwamba Watanzania wengi zaidi ya 70% wanategemea shughuli za kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bajeti hii ni bajeti ya Watanzania walio wengi na Mheshimiwa Rais ameendelea kutuheshimisha kwa kuweka ongezeko kubwa sana la bajeti na mpaka sasa tunavyozungumza, tunazungumza bajeti ya shilingi trilioni 1.2; haijawahi kutokea katika historia ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia niendelee kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote wa Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ambayo inasimamia Wizara hii. Wizara hii imekuwa ni Wizara sikivu kila tunapoishauri, tunabadilishana mawazo na mwisho wa siku wanakwenda kutekeleza yale tunayoshauriana kwa mustakabali mzima wa Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa mfano, tulikuwa na mtikisiko mkubwa sana mwaka jana katika bajeti ya mwaka 2023/2024 katika suala zima la sukari. Wote tunajua namna gani tulitikisika humu ndani, tunajua namna gani Watanzania walitikisika, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisimama imara, Waziri alisimama imara, Kamati ilisimama imara, Bunge hili lilisimama imara na mpaka sasa tunavyozungumza, sisi Wanakamati tumekwenda kutembelea kiwanda ambacho kimefanya *extension* na *extension* hiyo ikikamilika suala la sisi kuagiza sukari litakuwa ni historia kwenye nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninaamini kwamba mapinduzi makubwa yanayofanyika katika kilimo katika Serikali hii ya Awamu ya Sita yanakwenda kupunguza ikiwezekana kuondoa kabisa changamoto ya umaskini kwa Watanzania wote. Kati ya vitu ambavyo pia sisi vijana wa Kitanzania tutaendelea kumpenda, kumuombea na kumshikia bango Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia

Suluhu Hassan ni katika kutushirikisha sisi au kuona haja ya kushirikisha vijana na wanawake katika kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alisimama mbele ya Afrika nzima katika kikao kilichofanyika pale Dar es Salaam cha Usalama wa Chakula, akaahidi Afrika nzima kwamba nchi hii inakwenda kuhakikisha inashirikisha vijana na wanawake katika kilimo na kuhakikisha tunakwenda kuondoa kabisa changamoto ya usalama wa chakula; kwanza, kwa nchi yetu, kwa Afrika na ikiwezekana tutailisha dunia nzima na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, amesimamia msimamo huo na mimi kama mwanakamati nipo hapa kushuhudia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, programu ya *BBT* tulianza rasmi Machi, 2023. Tulianza kwa kuhakikisha tunaweka vijana na wanawake katika kilimo. Kwanza, kuhakikisha tunawawezesha lakini tunawavutia na kuhakikisha tunawawekea miundombinu bora ili pale wanapoingia katika kilimo, kilimo hicho kiwakomboe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa tuna miaka miwili tangu tuanze programu hii na programu hii watu wengi walishikilia bango katika kitu kimoja tu, lakini programu hii ya *BBT* ina vitu vitano; moja, ina mashamba makubwa ambayo ndio *block farming;* lakini mbili kuna *BBT financing* ambayo ni suala la kuwawezesha kiuchumi wanawake na vijana katika kushiriki kwenye shughuli za kilimo. Pia tuna suala la uchimbaji wa visima kwa wakulima wadogo kwenye *BBT,* lakini tuna suala la *BBT* ugani na pia tuna suala la *value addition* kwenye *BBT*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la mashamba makubwa tulianza na ku-*recruit* vijana kama 812. Vijana wale walipewa mafunzo na mwisho wa siku walihitimu kupitia mafunzo ya JKT vijana kama 600 na kitu. Tunavyozungumza sasa *pilot phase* imefanyika katika mashamba makubwa mawili; Chinangali na Ndogoe na mpaka tunavyozungumza sasa sisi Wanakamati tumetembelea zaidi ya mara moja, mara mbili kwenda kuangalia nini kinaendelea pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vijana wale wamejengewa nyumba. Zaidi ya 80% ya vijana wale waliopo katika kambi zile za mashamba wanaishi kwenye nyumba ambazo waliahidiwa. Pia vijana wale wa Chinangali wamepewa kila kijana ekari tano, lakini kwenye Shamba la Ndogoe kila kijana ekari moja. Vijana wale wametengenezewa miundombinu kwa ajili ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingine ambako utaratibu unaendelea kuweka *central pivot system* ya umwagiliaji, lakini kuna kwingine *drip system* zimekwisha kamilishwa. Pia kuna bwawa linaloweza kubeba maji takribani lita milioni 27 limekwishajengwa katika Shamba la Chinangali, wale vijana wanaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi wote tunajua nchi hii ina miaka 60 ya uhuru, lakini dunia hii imetokea mbali. Maendeleo ni hatua, hatuwezi kuwa tumeanzisha *BBT* mwaka 2023 leo hii mwaka 2025 tukataka tuwe tumekamilisha ila sisi tuliokwenda kuona na tunasimamia tunakiri kwamba hatua zilizofikiwa ni kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaamini na tulishauri kwamba ile *system* iliyotumika ku-*recruit* wale vijana imeacha vijana wengi wakiamini kwamba na wao wangefaa kuingia mle. Mheshimiwa Waziri, tunakushukuru ulikuwa msikivu ukasema hapana tushushe katika ngazi za halmashauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunavyozungumza sasa zaidi ya halmashauri 20 kwa maana ya halmashauri 21 katika mikoa tisa, zimekwishaanzisha *system* za *BBT,* lakini tunavyozungumza sasa halmashauri zipo katika mazungumzo na Wizara yetu kuhakikisha zinatenga maeneo. Maeneo haya yanapatikana na Wizara inaingia kuanzisha haya mashamba makubwa ili kijana asilazimike kuomba katika ngazi ya Taifa, kila mmoja katika halmashauri yake apate kufikiwa na neema hii na hiki ndicho tunachosema kwamba Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ameridhia kwamba vijana wajikomboe katika umaskini na wajiajiri kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la visima juzi tu hapa tumeona Mheshimiwa Waziri, ametutangazia kwamba kuna

magari 12 yameshakuja ya kuchimba visima. Visima zaidi ya 62,000 vitachimbwa kwenye mashamba ya wakulima wadogo wadogo. Wote tunajua kilimo hakihitaji mvua, kilimo kinahitaji maji na maji ndio haya Waziri leo kupitia visima hivi tunakwenda kuondoa changamoto hii na wakulima watalima mwaka mzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala zima la *BBT financing*, kwenye hili kwa kweli tumshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. Wakati anaingia alituahidi kwamba atahakikisha mikopo katika kilimo inapata riba ya *single digit*. Tunavyozungumza sasa benki ya kilimo na benki za kibiashara zinatoa mikopo kwa wakulima kwa asilimia tisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, si hivyo tu, Mheshimiwa Waziri na Wabunge wote hapa mtakuwa mashahidi, mkulima alikuwa hakopesheki katika benki za kibiashara, lakini kupitia programu mbalimbali zinazoendelea, mkulima sasa ameaminiwa na anakopesheka katika benki za kibiashara. Leo hii tunazungumzia programu kupitia *AGITF* kuna mikopo inatoka kwa vijana kwa 4.5%. Tunachotakiwa kufanya ni kuchangamkia fursa hizi, lakini Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, ametufungulia milango ya kuhakikisha vijana na wanawake wanawezeshwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kwenye suala zima la *BBT* Ugani, wameanza katika mazao ya korosho na pamba ambako vijana kwa kushirikiana na Chuo cha *SUA,* vijana waliosoma elimu ya kilimo wanapelekwa kwenda kusaidia wakulima kwenye uzalishaji. Leo hii tunapozungumzia katika zao la pamba peke yake, vijana maafisa ugani zaidi ya 730 wamepelekwa katika mikoa inayolima pamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hili, samahani dakika chache, nimpongeze sana Mwenyekiti wa Bodi ya Pamba, kwa sababu vijana hawa kwa kazi waliyofanya kwa msimu mmoja haijawahi kutokea katika historia ya nchi hii. Wakulima wa pamba, mikoa inayolima pamba watatuambia hapa, ilikuwa ni kwa ekari moja hazizidi kilo 200 miaka yote, lakini kwa mwaka huu wakulima wamevuna kuanzia kilo 1,000, 1,500 na kuna wengine

wanazungumzia kilo 2,000 kwa ekari moja ya pamba kupitia vijana hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vivyo hivyo kwenye korosho tunategemea kwamba kupitia programu hii, vijana hawa waende katika...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako ulishaisha.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mazao yote ili tuweze kukuza uzalishaji, tunavyozungumzia suala la kulisha Afrika na kulisha dunia hiki ndicho tunachozungumzia. Mimi nishauri mambo machache, samahani kwa..... *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako ulishaisha, tuna wachangiaji wengi.

**MHE. NG'WASI D. KAMANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Baada ya kusema hayo ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa Kunti Majala, tafadhali una dakika tano. Kambi ya Walio Wachache mna dakika 10 watu wawili.

Una dakika tano, ninaomba uanze tafadhali.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa muda na mimi ili niweze kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii ya mwisho ya mwaka 2025. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia afya na uzima na hatimaye leo tupo hapa tena tunawazungumzia wakulima wa Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nianze na suala zima la uwepo wa Watanzania ambao walikuwa wapo tayari kulitumikia Taifa hili ili tuweze kusonga mbele. Nimeingia Bunge hili mwaka

2015. Wakati ninaingia humu ndani kwenye sekta ya kilimo tulikuwa tunaimba na ikifika Wizara ya Kilimo ilikuwa ni tafrani humu ndani hususan kwenye suala zima la pembejeo za kilimo likiongozwa na suala la mbolea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Tanzania tunaenda kuandika historia kwamba migogoro na mahitaji ya mbolea inaenda kuwa historia ndani ya Taifa letu. Mwaka huu hatujasikia kelele tena za mbolea, wakulima wetu wamepata mbolea kwa wakati na wameweza kuzitumia na wamepata tija.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nini ombi langu kwa Mheshimiwa Waziri? Mheshimiwa Waziri, wakulima wetu sasa wamefanikiwa kupata hiyo mbolea, lakini bado tuna changamoto chache. Changamoto ya kwanza ni ufikishaji ama ufikishaji kwa mbolea kwa mkulima yule wa kule chini. Kwa hiyo, ninachokiomba Mheshimiwa Waziri, tutengeneze mfumo wa kuhakikisha wale mawakala wetu wanaosambaza mbolea tuone ni namna gani tunawasukuma watupelekee mbolea kule kwa wakulima wetu chini ili wakulima wetu wapunguze gharama kubwa wanazozitumia kwa ajili ya kuitafuta ama kuifuata hiyo mbolea pale makao makuu ya wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi la pili ambalo ninatamani kulisema kwenye hiyo hiyo mbolea kwamba tuna watu ambao leo wameanzisha viwanda vya mbolea hapa nchini na kuna wengine ambao wanaingiza. Nia na dhamira ya Serikali yetu na Taifa letu ni kuhakikisha tunawalinda Watanzania ambao wamewekeza ndani ya nchi yetu na hata hao wageni ambao wamekuja wakawekeza ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna viwanda vipo hapa Mheshimiwa Waziri, vimewekeza na vimesaidia kusukuma uwepo ama ongezeko la mbolea nchini lakini bado wana malalamiko yao; malipo yao hawajalipwa mpaka leo.

Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Waziri, utakapokuja watu hawa wanatamani kusikia kauli ya Serikali. Wamewapa wakulima wetu mbolea, je, ili tusiwakatishe tamaa na wakulima wetu msimu

unaokuja wakakosa mbolea kwa ajili ya kilimo, wanatamani kusikia ni lini mafao yao, ni lini madeni yao yanakwenda kulipwa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiachana na suala zima la mbolea, ninaomba sasa niende kwenye mambo mengine; uwepo wa mbegu ndani ya Taifa letu. Mheshimiwa Waziri, umeelezea vizuri sana kwa mapana yake na jitihada kubwa ambazo mnaendelea nazo kwenye Wizara. Nikuombe Mheshimiwa Waziri, bado tuna changamoto kubwa sana ya mbegu, hususan mbegu ya mahindi na sio mbegu ilimradi mbegu, ni mbegu iliyo bora yenye tija kwa wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, bado tuna changamoto ya mbegu ya mahindi, lakini pia na mbegu ya alizeti; bado tuna shida. Kwenye mbegu za miche na nini angalau mmesimama mko vizuri, lakini kwa wakulima wa mahindi na alizeti bado wana changamoto kubwa sana ya mbegu za mahindi. Mheshimiwa Waziri, mbegu nyingi za mahindi na alizeti bado si salama, si mbegu bora kwa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo wengi wao wanaochukua mbegu hizi wanaenda wanapanda, lakini tija yake ni ndogo sana. Kwa hiyo, badala ya kupiga hatua tunaendelea kumrudisha huyu mkulima nyuma. Kwa hiyo, niombe jitihada kubwa muendelee kuziwekeza ili tuhakikishe sasa kwenye hawa watu ama mashamba yetu yale ya mbegu ambayo mmeshayaanzisha, twendeni tukasimamie sisi wenyewe tuzalishe mbegu zenye tija ili wakulima wetu wanapokwenda kuzitumia mbegu hizo ziweze kuwapatia tija kwenye kilimo chao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara pia imesema vizuri kwenye suala zima la ongezeko la mbegu za mafuta nchini. Mheshimiwa Waziri, umetuambia sasa hivi kwenye suala zima la mbegu za alizeti ama ongezeko la nafaka za mbegu za mafuta ni za kutosha ni zaidi ya 100%. Sasa nikuombe Mheshimiwa Waziri, mkishirikiana na Wizara ya Fedha ile tozo ambayo mliiondoa, niombe irudi ili mbegu hizi ziweze kutumika kuzalisha mafuta ya kutosha na mazao yao wanayoyalima wakulima wetu yapate soko na hatimaye tuweze kujitegemea kwenye zao la mafuta ili

tuepuke gharama kubwa tunazozitumia za kuagiza mafuta kutoka nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana Mheshimiwa Waziri, viwanda vipo vya kutosha, wakulima wamezalisha alizeti ya kutosha. Kwa hiyo, tunakuomba na wakulima wa alizeti wanasema wameona mazao mengine mmekuwa mkitoa bei elekezi, ni kwa nini zao za alizeti kila mwaka linakuwa halina bei elekezi? *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, ninaomba hitimisha tafadhali.

**MHE. KUNTI Y. MAJALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimuombe sana Mheshimiwa Waziri na sisi zao la alizeti na hususan kwenye Mikoa ya Dodoma, Simiyu na Singida zao hili ambalo ndio tunaamini litatuondolea changamoto ya mafuta liweze kupewa kipaumbele ili wakulima wetu waweze kupata tija, lakini pia tuondokane na adha kubwa ya upatikanaji wa mafuta kutoka nje na kupunguza hizo gharama na hizo fedha ziweze kufanya kazi nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Agnes Hokororo, atafuatiwa na Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, na Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei ajiandae.

**MHE. AGNES E. HOKORORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja iliyopo mezani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kuunga mkono hoja, lakini pili nitumie fursa hii kumshukuru sana na kumpongeza Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa namna ambavyo ameifanya sekta ya kilimo kuwa na mageuzi makubwa sana na hasa ukianza kuangalia mafanikio yale yaliyoorodheshwa katika kitabu cha hotuba ya Mheshimiwa

Waziri. Mimi pia ninaona hayo ni mafanikio makubwa katika Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na daktari bingwa, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Waziri Bashe pamoja na Naibu Waziri na kwa kweli kwenye hii Wizara kama hii dhima ilikuwepo miaka mingi, lakini hii dhima iliyokuwepo kwenye Wizara yenu ya kujenga sekta ya kilimo endelevu na yenye ushindani ili kukuza uchumi shirikishi, kuboresha maisha ya mkulima kwa mara hii mmeipatia kuliko mara nyingine yoyote. Hongera sana Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hayo mafanikio kuna eneo kubwa ambalo tunaona kabisa kwamba upatikanaji wa pembejeo na viuatilifu ni jambo ambalo limeongeza uzalishaji kwa kiasi kikubwa sana. Nikiangalia baadhi ya mafanikio, kwanza unakuta bei ya mazao hasa sisi watu wa Mkoa wa Mtwara kama mashuhuda, ni mashuhuda wazuri kwa sababu kwa msimu uliopita korosho iliuzwa kwa wastani kwa bei ya shilingi 3,500 mpaka 4,195 kwa lile soko la *TMX*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mliona picha kwenye mitandao ya kijamii watu walikuwa wanatutania kule. Sitaki kwenda kwenye huo utani, lakini mbaazi pia iliuzwa kwa shilingi 1,800 mpaka 2,200. Ninataka nimwambie Mheshimiwa Bashe, kazi aliyoifanya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa wakulima wa Mkoa wa Mtwara haijapata kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kwetu mbaazi ilikuwa ni mboga Mheshimiwa Bashe. Ulikuwa unavuna tenga mbili unaiweka tena ukianza kula na familia yako mpaka wakati mwingine ina-*pukuswa,* nikwambie kwa kikwetu. Ukitaka kubadilisha mboga unaitoa kwenye zile punje unasaga inaitwa *barahoa,* lakini kwa mara ya kwanza mbaazi imekuwa ni zao la biashara, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ufuta umeuzwa kwa wastani wa shilingi 4,000 haijapata kutokea. Sisi tunaishukuru Serikali inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan na pia

tunakushukuru wewe Mheshimiwa Bashe, wewe huna baya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kazi hiyo nzuri na kwa kweli leo baada ya mafanikio makubwa uliyoorodhesha kwenye kitabu chako, ninaomba nishauri maeneo mawili kwa ufupi sana. Eneo la kwanza, hii kazi nzuri inayofanywa na Wizara, maafisa huduma za ugani kubaki kwenye halmashauri sio sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakurugenzi wa Halmashauri wana vipaumbele vingi, wana mambo mengi, kwa hiyo, hata bajeti inapowekwa kwenye Idara za Kilimo kwa Maafisa Ugani haitoki, lakini hata inapotoka inawekwa kutekeleza majukumu mengine, si rahisi sana. Kwa hiyo, huduma za ugani, na mmewapatia maafisa ugani pikipiki kwa mfano, tunatarajia sasa hao wakaweke mafuta kwa mishahara yao halafu wakulima watembelewe? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninadhani kutokana na vipaumbele vingi walivyonavyo wakurugenzi si rahisi huduma za ugani wakatekeleza miradi yote ama kazi zile kwa 100%, kama watakuwa wanasimamiwa na Wakurugenzi wa Halmashauri. Ni muhimu kurejesha huduma za ugani Wizarani, inawezekana, lakini tukiacha hivi watakuwa bado wananing'inia tu kwa sababu, hata wakipangiwa, kwa mfano fedha kidogo; unataka kuniambia atapewa Afisa Ugani akashughulikie? Aka-*check* shamba darasa? Badala ya hiyo fedha ikalipe deni ambalo kwa siku hiyo, ama kwa wiki hiyo, mkurugenzi anatakiwa alilipe?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninadhani umefika wakati kwa kweli, huduma za ugani zirudishwe Wizarani ili kuona tija. Pia kuwa na mtiririko sahihi kutoka Wizarani mpaka kule chini kwa wanaowasimamia wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo la pili, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mwaka jana hapa katika hili Bunge tulikurudishia, tulikupa tena kisheria, fedha za *export levy* na ni za kisheria kabisa. Sasa mimi nilikuwa ninatamani kujua tangu tulipokurudishia hapa Bungeni fedha za *export levy,* umepata kiasi gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizi fedha kwa mujibu wa sheria zinatakiwa zirudishwe bodi. Zikifika Bodi ya Korosho zikatekeleze majukumu ama wajibu uliopangwa kisheria, pamoja na kuendeleza zao la korosho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa hizi fedha kama zinaenda zinatoka huko, asubuhi hapa Mheshimiwa Katani alichangia, zikaenda huko zinakokwenda, halafu tena Waziri sijui kwa taratibu zako, sijui kwa namna utakazozipata, lakini mimi nina uhakika kwa sababu ukiacha kuwatetea wakulima, lakini pia mimi ni mkulima, hatujaiona tija ya hizo fedha tulizokurudishia. Pengine wanaohusika watuambie, ni kwa kiasi gani fedha za *export levy* zimekuja kwako, kama Waziri wa Kilimo ama Bodi ya Korosho, kwenda kuendeleza zao la korosho? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nirudie tena kuwashukuru sana, nikushukuru sana Waziri, Mheshimiwa Bashe, kwa kazi nzuri. Mungu abariki kazi ya mikono yenu, nina imani kura zote za Mkoa wa Mtwara, kwa mafanikio mazuri tuliyoyapata katika kilimo, tunampelekea Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana.

Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Kimei.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Kilimo. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa *commitment* hii kubwa anayozidi kuifanya, maana mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kilimo. Tumeona ongezeko la fedha kutoka shilingi bilioni 297, leo ninaongelea shilingi trilioni 1.242; ni hela nyingi sana ambazo zimewekezwa. Kwa hiyo, tuzidi kupongeza na kushukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi hizi kipekee zimuendee Waziri - Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Silinde - Naibu Waziri, Katibu Mkuu – Ndugu Gerald na wasaidizi wengine. Ninasema mpewe pongezi kwa sababu unapoona Mheshimiwa Rais anaruhusu fedha hizi ziende kwa wingi huko maana yake ni ana *confidence* na ninyi. Wizara zipo nyingi na kila Wizara ni muhimu, lakini kwa haya ambayo mnayafanya, mipango mizuri na usimamizi mzuri, ndio maana mnaona pesa zinatiririka, na hasa Wanakamati pia tumekuwa tunapambana kujua kama kuna mkwamo wowote tupige kelele, lakini Mheshimiwa Bashe, mara nyingi umetuhakikishia upo mstari wa mbele hata ku-*push* kutoka Wizara ya Fedha na mambo yanaenda. Kwa hiyo, tuwapongeze sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikirejea sasa katika hotuba ukurasa wa 128 wa hotuba yake Mheshimiwa Waziri, ametaja vipaumbele sita ambavyo atavitekeleza kwa kutumia mikakati 30. Sasa mimi nilikuwa ninatafuta yale yanayonihusu kwa sababu unajua mambo yapo mengi. Hii Wizara tunatamani hata *sometimes* iwe na siku tano au sita, maana ni Wizara ya wakulima, ni Wizara ya nchi nzima, lakini kwa sababu tunakimbia na hizi dakika saba, nane, *sometimes* huwezi kufika sehemu unapotaka kuongea na ndio maana watu wetu huko watashangaa mbona hukusema hili! Muda hautoshi tupo *limited. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiangalia ukurasa wa 132 kwenye kipaumbele chako namba tatu, umesema kuimarisha usalama wa chakula na lishe. Sasa mkakati ambao nilikuwa nimeuona ni uwekezaji kwenye miundombinu ya uhifadhi wa chakula mpaka kufikia tani 3,000,000 kwa mwaka 2030. Mheshimiwa Bashe na kipaumbele namba nne pia, kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji, mauzo ya nje ya nchi na mkakati ambao ninaurejea ni kujenga miundombinu ya masoko ya mazao ya kilimo, kwa ajili ya wakulima katika halmashauri mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nimshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa maelekezo ambayo umeyapokea, kipekee nikushuru wewe mwenyewe binafsi Mheshimiwa, ulini-*assure* kwamba tulete maandiko, kwa ajili ya ujenzi wa soko la mazao ya kilimo katika Wilaya ya Biharamulo, eneo la Lusahunga. Pia

ukanihakikishia ujenzi wa maghala ya chakula katika eneo la Lusahunga pale kwa sababu ni *junction* inayo-*serve* Kigoma, Rwanda na Burundi na inayo-*serve* watu wanaoenda Uganda. Kwa hiyo, nikushukuru sana na salamu hizi za shukrani ninaahidi, kwa niaba ya Wana-Biharamulo, mtazipokea mwezi Oktoba mwaka huu wa 2025. Sisi hatuna maneno mengi, tunaenda kwa vitendo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kitu kingine pia Mheshimiwa Waziri *for the first time,* hata sisi leo watu wa Kagera na hasa sisi wa Biharamulo, nimeona kwenye bajeti yako, ukurasa wa 203 umeongelea ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji, huko una mabwawa 114. Tuna Bwawa letu la Mwiruzi pale limetajwa, linalojengwa kwa *meter cubic* 13,000,000 za ujazo au lita za ujazo 13,000,000,000. Ni bwawa kubwa sana na linaenda kuwangilia kwenye skimu ya umwagiliaji, ile skimu 42 umetuweka tena Wilaya ya Biharamulo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna skimu ya umwagiliaji ya hekta 13,000 eneo la Mwiruzi, kwa hiyo, tuzidi kushukuru na ndio maana tunasema mambo ni mengi, lakini tungeweza kuyasambaza yote hapa yasingetosha, yote hii ni shukrani kwa sababu hata sisi *for the first time* tunaenda kupata mradi wa umwagiliaji, skimu kubwa katika Wilaya ya Biharamulo na licha ya skimu tunapata bwawa kubwa lenye ujazo wa lita 13,000,000,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo suala nilitaka niliongelee pia hapa suala la kahawa, sisi tunaotoka Mkoa wa Kagera tunaelewa. Mheshimiwa Rais alivyoingia mwaka 2021 kahawa kwa Mkoa wa Kagera ilikuwa na tozo 49, kupitia juhudi za Mheshimiwa Waziri na maelekezo ya Mheshimiwa Rais, tozo zimefutwa kutoka 49 zikabaki saba. Ndio maana kwa Mkoa wa Kagera *by 2021,* mimi ninaongelea kwangu Biharamulo bei ya kahawa ilikuwa inauzwa kati ya shilingi 1,200 mpaka shilingi 1,400. Kwa mwaka jana ambao tumemaliza tumeuza kahawa kilo moja kwa shilingi 5,400 robusta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, siyo kitu kidogo, unaweza ukaona kazi kubwa iliyofanyika. Tuzidi kupongeza bidiii kubwa

sana iliyofanywa na Serikali, kwa ajili ya kuwainua wakulima wa kahawa kwa Mkoa wa Kagera na hususani Biharamulo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumekuwa tunapokea miche ya ruzuku ila Mheshimiwa Waziri, Biharamulo tumeenda mbali zaidi, maana Wilaya ile ni kubwa. Kwa hiyo, tumetengeneza vitalu vinne sasa hivi katika kanda tofauti tofauti ili wananchi waweze kupata hii ruzuku ya miche ya kawaha kulekule waliko. Ninapoongea sasa tuna vitalu vya miche 1,150,000 ambayo tutaigawa katika mwaka huu 2025, lakini ikiwa katika maeneo manne tofauti ili huduma tuweze kuisogeza karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee Mheshimiwa Waziri nikushukuru kwa habari ya wakulima wa tumbaku. Ninakumbuka kipindi kile ulinihakikishia kwamba unapambana, kwa ajili ya ruzuku ya watu wa tumbaku. Haikuwa rahisi, maana uliwekewa vikwazo kwamba ni zao la biashara, tukapata vikwazo vikubwa sana, lakini kwa bidii yako umepambana mpaka sasa hata sisi wakulima wa tumbaku tumeanza kupata ruzuku ya tumbaku. Yote hii ni kwamba mnapigana msiwasahau wakulima wa zao lolote lile kwa sababu bado wanaingiza fedha za kigeni, wanazidi kutuletea heshima katika nchi. Kwa hiyo, nikushukuru sana kwa hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikushukuru kwa ahadi ya ujenzi wa ghala la kuuzia tumbaku katika Kata ya Kalenge, maana tumehangaika sana kwa muda mrefu. Tulikuwa tunaenda kuuzia tumbaku Kahama, unatoa tumbaku Biharamulo, lakini wewe mwenyewe umetoa maelekezo kwa watu wa Bodi ya Tumbaku na wameshaniona, tunatafuta eneo ili waje wajenge ghala lile kwa ajili ya kuuzia tumbaku katika Wilaya ya Biharamulo na hususani Mkoa wa Kagera, tumbaku yetu isitoke nje. Yote haya ninashukuru na ninazidi ku-*appreciate*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu nikutie moyo kwa kitu kimoja; kilimo siyo *betting,* unajua ukienda kwenye *betting* ukiwa na shilingi 1,000 unaweza ukaingia na ukatoka na shilingi 1,000,000. Ndugu zangu kilimo ni mchakato, ndio maana tumekuwa tunaambiwa kuna upembuzi yakinifu, kuna usanifu hapo, uanze kulima, ukimaliza uvune, upeleke sokoni. Kuna

maneno mengi sana yanasemwa hususani kwenye miradi hii ya *BBT*. Mimi nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri, wewe fanya kazi, wananchi wanaona matokeo, kamati imeona matokeo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, anayeenda kulima kwenye mashamba, wengi tunaona mazao yakiwa yametoka, lakini tungekuwa tunaona misitu kabla ya kukatwa ndio tungejua kilimo ni *process*. Kwa hiyo, tukutie moyo, ufanye kazi tupo nyuma yako, tunachohitaji ni matokeo haya tutayaona baada ya muda. Huwezi kwenda kulima ukaona matokeo leo, matokeo tutayaona baada ya muda kwa sababu kilimo ni *process*. Tulianza na shilingi bilioni 297 leo tupo shilingi trilioni 1.2.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa muda wako umeisha. Tafadhali hitimisha.

**MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamalizia, dakika moja; leo tupo shilingi trilioni 1.2 kwa hiyo, haya ndio tunayoyasema, ulianza taratibu, sasa unazidi kupanda, unavyozidi kupanda ndipo tutakapokuja kuona matokeo mazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana kwa nafasi. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Ezra.

Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei, atafuatiwa na Mheshimiwa Janejelly James Ntate, halafu Mheshimiwa Kavejuru, ajiandae.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa fursa hii. Nianze tu kwa kujiunga na wenzangu kumshukuru na kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa mkakati anaousimamia kwenye sekta hii ya kilimo ambao sasa umeanza kuonesha matumaini na neema kwa wakulima na kuonesha kwamba kujenga uchumi shirikishi ambao unashirikisha watu wengi wakiwemo wakulima wetu inawezekana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwamba maono yake haya yalianza pale alipoweza kumuona Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Silinde pamoja na Katibu Mkuu wa Wizara akawapa jukumu la kuendeleza sekta hii ambayo wamekuja na ubunifu mkubwa. Kwenye sekta hii siyo rahisi kubuni sana kwa sababu miaka mingi tumesema kilimo ni siasa, lakini nani aliweza kufikisha hiyo siasa mahala pake, kama siyo Rais Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, timu yake kwenye Wizara pamoja na taasisi wanazozisimamia ambazo kusema kweli tumeanza kusikia mambo ya kutoa mbegu, kwenda usambazaji wa mbolea na kadhalika na *reform* kwenye ushirika unaanza kuonekana. Kwa hiyo, ninasema kwamba sisi Watanzania ambao tunajumuika kwenye sekta hii, kwa pamoja lazima tumsifu na tumshukuru sana kwa kazi anazochapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika bajeti hii *the whole thing* ambacho mimi kinanisikitisha kidogo ni kwamba *release* ya *funds,* fedha zilizotolewa mpaka mwezi Aprili kama kweli nimesikia vizuri kwenye hii hotuba ni 53%. Haitoshelezi kwa kazi inayofanyika na ndio ninaamini kwamba bado kuna miradi imezubaa zubaa huko kwa sababu hela haijaenda mahali pake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sababu moja inaweza ikawa pengine tume-*over stretch* kwamba *implementation capacity* kwenye Wizara haiwezi kwenda na fedha nyingi kiasi hicho na hautatarajia kwa sababu shilingi trilioni 1.2 mahali ambapo kulikuwa na shilingi bilioni 294 inawezekana ikawa kwamba ni lazima wajipange vizuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nilikimbilia kusema kwamba kwenye Wizara hii tatizo kubwa ni mifumo na taasisi, *institution building* ndani ya Wizara na sekta kwa ujumla kwamba nitamfikishiaje mkulima mdogo pale kijijini mbolea, *efficiently?* Nitamfikishiaje pembejeo? Nitamfikishiaje, kama ni huduma, hata ya trekta ili aweze ku-*expand?* Mtamfikishiaje mbegu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiki kitu kilikuwa kipo, hii *institution building*. Huu mfumo ulikuwepo, lakini huu mfumo ulikufa baada ya *cooperatives* kufifia. Hii *movement* ya ushirika ilidhoofika na baada ya kudhoofika, basi ikawa imeua ile *chain* ambayo ilikuwepo. Tulikuwa tumeunda, miaka ya nyuma huko na tulivyokuwa wadogo tulikuwa tunaona jinsi ambavyo mabwana shamba, huduma ya ugani, ilikuwa inakwenda kupitia ushirika na inasimamiwa kupitia ushirika. Sasa hakuna hicho kitu, kimekufa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kusema kwamba kitu kinachoua ushirika siyo sheria, siyo kanuni, ni watu. Sasa kama watu wanakamatwa wamefanya uzembe huko halafu hawaadhibiwi inavyostahili, wanaendeleza kuua ushirika na mimi ninakuomba Mheshimiwa Bashe ninaamini kwamba Mheshimiwa Rais ataku-*back up* kwamba mtu akifanya kosa kwenye kuendesha ushirika, kama wale kule kwetu Vunjo, walishindwa kulipa fedha za wakulima wa kahawa wakakaa nazo, kwanza walizimeza halafu hawakuwalipa na wakawa hawako hata wawazi kwamba hiyo hela imeenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu kama wale wafungwe. Ni kuwafunga, hata hamna mambo ya faini kwa sababu mpaka leo hii Mheshimiwa Waziri ulisema.

Hee, ni dakika tano tano! Basi, kama ni tano tano, ninaona mambo mabaya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba ninafikiri takwimu ambazo ametoa Mheshimiwa Bashe kuhusiana na uzalishaji ulivyoongezeka, ukiangalia na jinsi ambavyo kweli kwenye *NBS* Mtakwimu Mkuu wa Serikali anavyosema *agriculture* ina-*grow* kwa *4.1 percent,* siamini kama ni kweli. Naamini lazima tuoanishe mahali fulani, kuna mahali ambapo watu wa takwimu hawajapata mambo haya yanayoendelea kwenye sekta hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme kwamba pamoja na hivyo, ukiangalia jinsi fedha ilivyotiririka, mabwawa yanayojengwa ni mengi mno kwa wakati mmoja, huwezi kujenga yote kwa wakati

mmoja, inakuwa kwamba lazima utakuwa unalaza damu mahali. Kwa hiyo, hela inalala pale, halafu humalizi, chukua machache maliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna bwawa moja ambalo nilizungumza juzi, Mheshimiwa Silinde akalijibu vizuri sana kwenye swali langu, Bwawa la Urenga. Bwawa la Urenga pale ni *natural,* hata halihitaji kuchimba, maji yanakuja yanasimama pale, yanachotwa, halafu linanywesha. Lile bwawa linasaidia watu zaidi ya 27,000 na eka zinazoweza kunyweshwa kwa kupitia bwawa hilo ni eka 15,000 *is a low hanging fruit. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru kwamba Mheshimiwa Silinde alivyotembelea kwa kutumwa na Mheshimiwa Waziri, aliona, akashangaa, akasema kuna *potential.* Sasa yeye hakuona ile *potential* kwa sababu hajajua watu wanaoitegemea; watu wa Kata ya Kirua Vunjo Mashariki, Kirua Vunjo Kusini, Kata ya Kahe Mashariki yaani ni watu wengi. Sasa hivi mazao yao yamedumaa kwa sababu lile bwawa halipo, liliharibika kidogo na linahitajika kurekebishwa na alituahidi kwamba limeingia kwenye bajeti. Ninakuomba sana Mheshimiwa Bashe, usiliache hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru pia kwamba Mkurugenzi wa Tume ya Umwagiliaji naye ameanza kukarabati mifereji, mingine inatoka kwenye bwawa hilo hilo. Kwa hiyo, ameanza ukarabati, ni kitu ambacho kusema kweli kinaleta matumaini na neema kwa Wana-Vunjo. Ninaomba muendelee na kazi hiyo, ninaamini kwamba tutafika vizuri. Pia tujue kwamba kwa Wana-Vunjo…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa. Muda wako umeisha, hitimisha hoja yako Mheshimiwa, tafadhali.

**MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema *BBT* tu kwamba mnyororo wa thamani wa mazao, kama ndizi na nini, aendelee kutusaidia pale. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Stephen Kimei.

Mheshimiwa Janejelly James Ntate, atafuatiwa na Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix na Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, ajiandae.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru Mwenyezi Mungu na mimi kupata wasaa wa kuchangia, kama Mjumbe wa Kamati ndani ya Wizara hii. Ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ninampongeza nikiwa na sababu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilivyoanza Bunge nilianzia Kamati ya Kilimo, tulikuta bajeti ni shilingi bilioni 294, wakati huo Mheshimiwa Bashe alikuwa ni Naibu Waziri. Sasa tunawauliza mtafanya nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ukiniuliza sifa za Mheshimiwa Bashe, nitakuambia ni usikivu, uthubutu na ujasiri na ukiniuliza tena, nitakuambia ni uthubutu, usikivu na ujasiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, alitupa moyo akasema haitachukua muda bajeti yetu itakuwa imeongezeka na ndio zilikuwa kelele zetu na leo tunaongelea bajeti ya shilingi trilioni 1.2. Haya ni maono ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini amempata kijana, Mheshimiwa Bashe ambaye ameweza kuyashikilia akiwa na msaidizi wake, Mheshimiwa Silinde na wana timu yao inayoongozwa na Ndugu Gerald Mweli, imejipanga na wamejipanga sawasawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niwaambie, Mheshimiwa Bashe inawezekana unachofanya kwa vijana wa Tanzania hawajakielewa. Kamati ni mashahidi, tulivyoenda kwenye semina ya tamthilia ya mbegu, vijana walitoa ushuhuda, ukiwa kanisani unaweza ukasema ushuhuda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakasema vijana tuingie kwenye kilimo kwa sababu ni wakati ambao Mungu ametupatia Mheshimiwa Hussein Bashe kutusaidia sisi vijana kwenye kilimo;

sasa tusisubiri ameshatoka ndipo tunamsifia, leo anatakiwa apate sifa zake. Maono ya Mheshimiwa Rais ameyatekeleza kwa kusaidiwa na wasaidizi wake. Ukimwangalia Mheshimiwa Silinde yeye yupo kimya kimya, lakini akikwambia anakwenda mahali atatekeleza na anatekeleza kweli. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niongelee umwagiliaji na uchimbaji wa *scheme*. Ameongea Mheshimiwa Kimei, kama hatukupeleka hela kwa usahihi na inavyotakiwa kwenye umwagiliaji tutawaonea wataalam walio kwenye umwagiliaji. *Scheme* ile ukishaianzisha unatakiwa uimalize, ukiiacha katikati kama ikija mvua ile *scheme* itaondoa halafu utaona kama mtaalam amekula fedha, kumbe hajala fedha, ni sisi hatupeleki fedha za kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe Wizara ya Fedha wapeleke fedha kama zilivyopangwa kilimo. *Passion* ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan ni kilimo. Ili kilimo kiende hizi *scheme* zijengwe zimalizike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilichogundua kwenye umwagiliaji ni ushirikishwaji wa wananchi mahali ambapo hizo *scheme* zipo. Nitatoa mfano wa *scheme* ya Ilanyinda ambayo ipo Mkoa wa Shinyanga. Tulifika kwa Mkuu wa Mkoa taarifa aliyotupatia ndiyo ambayo Mkurugenzi anayotupatia na ndiyo ambayo Mheshimiwa Waziri aliyokuja nayo kwenye Kamati. Uhakika huu ninaupata wapi? Tulipofika kwenye *scheme* wanamfahamu Mkuu wa Mkoa utadhani ndiye Waziri wa Kilimo, ni kwa sababu kila wakati anakwenda kukagua mradi huo, lakini tuliyekuta anasimamia ule mradi ni Mwenyekiti wa Kitongoji, ndiye anawasimamia wale vibarua wa kila siku.

Kwa hiyo, wale watakuwa na uchungu wa kuutunza ule mradi kwa sababu wameshirikishwa. Hii tuombe na Wizara nyingine zenye miradi ziige mfano huu wa kushirikisha wananchi walio eneo hili ili kuweza kulinda kilichopo pale. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niongelee mikoa *potential* ambayo tunatakiwa tuiangalie kwa macho mawili kwenye kilimo. Kuna Mkoa wa Morogoro, kiti chako kilitupa ruhusa kama Kamati ya

Kilimo tukaweka kambi kama siku tano Mkoa wa Morogoro. Mkoa wa Morogoro kila zao linaota. Kuna Mkuu wa Mkoa tusipompa maua yake ni kumwonea, Mheshimiwa Adam Malima, amekuja na *formula* kwa vijana. Kama tukiifanya Tanzania na Mheshimiwa Bashe ukiichukua hii vijana wote hakuna atakayelia lia na ajira zilizopo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulishuhudia kugawa miche ya karafuu kwa vijana walio darasa la kwanza kila kijana miche 10, na Mheshimiwa Naibu Waziri tulikuwa wote. Sasa mimi kwa hesabu yangu ndogo, sikusoma *PCM,* nikapiga hesabu kwa miche hiyo 10 kwa kijana ambaye amepewa yupo darasa la kwanza, mkarafuu unaanza kutoa maua na mazao ukiwa na miaka minne, mkarafuu mmoja unatoa kilo 15 na bei ya karafuu sasa hivi ni shilingi 30,000. Sasa kijana huyu wakati anafika darasa la sita atakuwa na uwezo wa kutengeneza shilingi 4,500,000. Anapofika *form six* atakuwa anatengeneza shilingi milioni 22 kwa mche mmoja. Sasa tuchukulie *form six* naye ameanza kupanda huku, alipokuwa *form one* akaanza kupanda mwenyewe, mpaka anafika chuo kikuu ana miche 100. Miche 100 kwa kilo 15 atakuwa anatengeneza milioni 45 ni kijana gani atataka umuajiri? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo waliosema kwamba mali ipo shambani, ipo shambani kweli. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Waziri alichukuwe hili, tuanze huu utaratibu kwa vijana walio shule za msingi kuwapa mazao ambayo yanaota sehemu ile, itakuwa ni *BBT* nyingine, huku anasoma huku anatengeneza hiki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nitumie muda huu kumwomba Mheshimiwa Waziri, mimi nimeanza, nimechukua vijana wa Mkoa wa Dar es Salaam wapo 20, na amenisaidia Mheshimiwa Mbunge wa Mvomero, nimepitia kwa *RAS*, pale Mvomero kuna ekari tano za kupanda kakao. Sasa mimi nitamfuata kabla Bunge halijaahirishwa ili anisaidie vijana hao wapate fedha waende kulima kakao. Baada ya miaka minne wale vijana watakuwa wanavuna na bei ya kakao kilo moja ni shilingi 29,000. Hao vijana baada ya muda watakuwa ni wasemaji wakubwa wa kilimo, tutakuwa tumepunguza vibaka Dar es

Salaam. Wapo tayari kuweka kambi Mvomero kwenda kulima. Mimi nimwombe alichukuwe hilo. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa kusema hayo ndiyo narudia kumpa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu awe na amani, hawa vijana wote ndio wanaokwenda kumpiga kura, akina mama wote ndio wanaokwenda kumpigia kura. Kwa suala alilokumbuka la wakulima wa Tanzania ambayo ni 70%, sisi tuliokuwa maskini wakulima wa Tanzania leo tunakuwa matajiri kwa ajili yake. Yeye Mheshimiwa Bashe anaendelea kutekeleza maono hayo. Tumeona kila mikoa tunayotembea, tumeona hizo *scheme* za umwagiliaji na tumeona sasa anakuja kuvumbua zile mbegu za asili ambazo amesema kwamba kabla Bunge halijavujwa zitakuwa zimesajiliwa *TARI* ili sasa mtu aamue, akienda sokoni akute mbegu ya asili, akute hizi za kisasa aamue analima nini. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale akina mama wa Karatu walimpa ushuhuda siku ile kwamba mbegu ya asili ya mahindi kwenye hekta moja unaweza ukavuna magunia 45; mbegu ya asili ambayo inavumilia ukame, haihitaji mbolea sana, ni mbolea ya asili ya samadi. Hebu turudi kwenye vitu vyetu vya asili, hebu twende tukatumie mbegu za asili. Aliziona zilikuwa pale, aliona mahindi yalivyokuwa pale, unga wake tumenunua, ni mtamu kuliko unga unaotoka kwenye mahindi ya kawaida haya ya sembe. Sasa twende tufanye hivyo, kilimo kibadilike lakini kwa kukumbuka na mbegu zetu za asili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niendelee kuwapongeza kwa vifaa walivyoleta…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umekwisha tafadhali.

**MHE. JANEJELLY J. NTATE:** Oooh, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, Mheshimiwa Kavejuru Eliadory Felix, atafuata Mheshimiwa Aloyce Andrew Kwezi, na Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda ajiandae.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru na mimi kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kwenye hoja hii ya Wizara ya Kilimo. Mimi pia niungane na wasemaji walionitangulia kuwapa pongezi sana sana Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Naibu wake Mheshimiwa David Ernest Silinde, Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu. Nimpe pongezi kubwa sana Mheshimiwa Rais kwa dhamira yake ya dhati ya kuamua kufanya mapinduzi ya kilimo hapa nchini kwetu. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu unakwenda kujikita kwenye hotuba, ukurasa ule wa 152 na nilikuwa ninajaribu kuulinganisha na ukurasa wa 129, hasa nikizingatia bajeti ya mwaka 2025 ambayo hasa imelenga kwenye ukuaji wa sekta ya kilimo kwa upande wa mazao ya kilimo kufikia asilimia tano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeliangalia jedwali lile namba tano la ukurasa 152, kwanza nitoe pongezi kubwa sana kwa wakulima wa mazao ya biashara, hawa wamekuwa na mchango mkubwa sana wa kutuingizia fedha nyingi za kigeni, niwapongeze wakulima wa korosho, pamba, pareto, kahawa, tumbaku, chai, mkonge, sukari na kakao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizo bado kuna jitihada inayohitajika kwenye mazao haya ya biashara. Yapo mazao matatu ambayo nimeyaangalia kwenye jedwali hilo, nikiangalia malengo yake ni madogo sana. Zao la kwanza nimeangalia zao la kahawa, lengo la bajeti ya mwaka 2025/2026 ni kutoka sasa kwenye uvunaji wa kahawa ambao tulipata tani 86,366; kwa kakao kutoka tani 13,652 kufikia tani 15,000, na zao la pareto kutoka tani 3,327 kufikia tani 5,000. Ninaomba nitolee mfano tu kwenye zao la kahawa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo nchi ambazo uchumi wake umebebwa na kahawa, kidunia nchi ya kwanza ni Brazil, ya pili ni

Vietnam na ya tatu ni Colombia. Ukija kwenye Bara la Afrika, pamoja na kwamba sisi Tanzania ni nchi ya tatu, lakini nchi inayoongoza katika uzalishaji wa kahawa ni Ethiopia. Ethiopia sasa hivi kwa mwaka inazalisha tani 472,000. Nchi ya pili ni Uganda ambao wamefanya mapinduzi makubwa sana. Kwa mwaka 2021 Uganda walikuwa wanazalisha kahawa tani 242,000 lakini kwa msimu uliopita wameweza kupata uzalishaji wa tani 384,000. Sisi tumepiga hatua, tumetoka kwenye 51 tumefika 81. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mimi ninashangaa, sasa tunataka 81 tunataka kuongeza tu tofauti hiyo ya 85,000 ni kama 4,000. Mbona ni kidogo ilihali hili ni zao muhimu linalotuingizia fedha za kigeni? Isitoshe linalimwa katika mikoa 16 hapa nchini. Ukilinganisha eneo ambalo linafaa kwa ajili ya kilimo hapa kwetu Tanzania ni kubwa mara tatu zaidi ya eneo ambalo linalimwa zao la kahawa nchini Colombia. Hata eneo ambalo linazalishwa kwa kahawa nchini Ethiopia ambayo ndiyo nchi namba moja katika Bara la Afrika ni dogo ukilinganisha na ardhi yetu ambayo inafaa kwa ajili ya kilimo cha kahawa. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ninaomba Serikali iangalie kwa dhati kwa sababu hili ni zao ambalo linatuingizia fedha nyingi. Sasa hivi soko lake limeendelea kupanuka na bei yake ipo juu, linatuingizia fedha za kigeni. Kunahitajika mkakati mahsusi sasa wa kutoka kwenye hizi tani ambazo zipo chini ya 100,000 twende angalau hata kwenye 200,000. Majirani zetu ambao ni wanne wa Kenya kwa kipindi kile cha mwaka 2021/2022 walikuwa na uzalishaji wa tani 34,000; lakini sasa hivi wapo wanatukaribia, na wana malengo ya kuvuka zaidi ya hii 85 ambayo sisi tumepanga.

Kwa hiyo, ninaomba jitihada mahsusi iwekwe kwenye mazao haya ya biashara hususan biashara ambayo tayari inalimwa kwenye mikoa 16. Itatoa ajira nyingi sana na itawanyanyua maskini wengi na kupunguza umaskini uliokithiri katika jamii zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo ningeomba kwamba pamoja na jitihada na ruzuku ambayo imekwishaendelea

kutolewa basi ruzuku kubwa ya Serikali ilenge na jitihada kubwa ziende kutolewa ikiwa ni pamoja na pembejeo na kilimo kwenye mazao haya ya biashara ili tuendelee kupata fedha za kigeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho niishukuru Wizara, nimeona kwenye bajeti hii inayokwenda kujengewa nyumba nne kwenye Kituo cha *TACRI* cha Mayaya. Ninawapongeza watumishi wote wa *TACRI* katika Kituo cha Mayaya, wanafanya kazi kubwa sana. Msimu uliopita wamezalisha miche mingi ya kahawa na yote ilichukuliwa na wakulima kwa muda mfupi. Ninaomba waongezewe bajeti yao ili wazalishe miche mingi ya kahawa na iliyo bora. Sasa hivi wakulima wa kilimo cha kahawa nchini kote wamehamasika kulima kilimo hiki. Kwa hiyo, tunaomba jitihada ziongezeke kwa ajili ya kuongeza miche bora, ikiwa ni pamoja na pembejeo za kilimo zije kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa ambapo ni kukumbushia tu, ni kilimo cha tangawizi. Katika Jimbo langu la Buhigwe kwenye bajeti mbili zilizopita Wizara iliahidi kutujengea miundombinu ya…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa, muda wako umeisha tafadhali.

**MHE. KAVEJURU E. FELIX:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Aloyce, atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda na Mheshimiwa Ndaisaba ajiandae.

**MHE ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Ninaomba nichukuwe nafasi hii kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya na uhai leo hii tumeweza kusimama hapa kuchangia Wizara yetu ya Kilimo.

Pili, nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi nzuri na kubwa anayoifanya ya kuhakikisha Watanzania ambao sehemu kubwa ya maisha yetu yanategemea kwenye kilimo.

Tatu, nichukue nafasi hii kupongeza Wizara, ndugu yangu Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Silinde pamoja na Katibu Mkuu na timu nzima. Kwa kweli ninataka niwathibitishie kwamba wamefanya kazi kubwa sana. Kazi waliyoifanya kwenye sekta ya kilimo; hii Wizara ndiyo tulikuwa tunaona kuwa ni ile Wizara ambayo tunaona kwetu kwamba ilishindikana. Sasa tangu mwaka 2021 mpaka sasa mapinduzi yaliyofanyika kwenye hii Wizara ni mapinduzi ambayo hatukuyatarajia. *(Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nitawatolea mifano michache tu na ninachukua *sample* ya jimbo langu na wilaya yangu ya Kaliua. Hadi mwaka 2021 sisi ni wakulima wakubwa wa tumbaku, na Wilaya ya Kaliua ndiyo inayoongoza kwa uzalishaji wa tumbaku katika nchi yetu ya Tanzania, tunazalisha takriban kilo milioni 30.2. Tumbaku hii nyingi na ndiyo tunayoitegemea wananchi wa Tabora, wananchi wa Kaliua na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini ambacho tumefanya? Kabla ya mwaka 2021 tulikuwa tunapewa ukomo wa kulima kwamba wewe mkulima wa tumbaku mwisho wako wa kuzalisha ni kilo 1,000; mwisho wako wa kuzalisha ni kilo 2,000 na mwisho wako wa kulima ni kiasi fulani. Unakuwa na maeneo makubwa lakini umepewa ukomo kwamba huwezi uka-*access* kulima kadri ya mtaji wako, huwezi uka-*access* kulima kadri ya uwezo ulio nao. Sasa haya yote yamekwenda kuwa historia na ndiyo maana ninasimama kifua mbele kama Mbunge, kama mwakilishi wa Jimbo la Kaliua kuwaambia Watanzania kwamba mapinduzi yaliyofanyika kwenye sekta ya kilimo hususani kwenye zao la tumbaku ni makubwa sana ambapo Mheshimiwa Waziri anatakiwa kupewa makofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ukiachana na ukomo, upatikanaji wa mbolea, huko nyuma ilikuwa inafikia msimu unaanza tayari tumetoka kwenye mabedi, tumekwenda kwenye

masuala ya tumbaku imeshapanda ndipo mbolea inakuja huku tumbaku ikiwa imekwishaanza kuharibika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, jambo hilo sasa limekuwa ni historia, kwa sababu mpaka sasa mbolea inayoendelea kuanzia msimu wa mwaka huu mwezi wa nane, wa tisa na kuendelea tumeambiwa mbolea ipo. Hivyo niwathibitishie wakulima kwamba wakae mkao wa kutulia, mbolea ipo, walime tani yao. Kile kizuizi cha kulima kwamba watalima na nini biashara hiyo imeshakwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni kuhusu bei ya tumbaku; hapa kwenye bei ya tumbaku ilikuwa historia. Sasa ninakuthibitishia kwamba jana nilikuwa ninapokea simu za wananchi wa Usinge, Kazaroho, Igwisi na Zugimlole wameuza tumbaku, wameuza hadi dola tatu. Dola tatu tunaongelea takribani shilingi 7,000. Hii kitu imekuwa ni *common* kwao, kwa nini? Ni kwa sababu Mheshimiwa Bashe, Waziri wetu mchapakazi ameweza kufungua *channel* za kuhakikisha kwamba kampuni za kutosha za tumbaku zinafanya kazi nzuri sana kule Kaliua, zinafanya kazi nzuri sana kwenye nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimwombe Mheshimiwa Waziri aendelee kushirikiana nao kuhakikisha kwamba masoko yanayoendelea sasa hivi wauze katika bei ambazo ni nzuri kama walivyoanza ili kuhakikisha sisi tunapokwenda kule, Mama Samia anapozunguka ni makofi, ni kura za kutosha, CCM inasonga mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili ambalo ningetaka kupongeza kwenye kilimo cha tumbaku *reference* ambayo mimi Kaliua nimesimama kum-*support* Mheshimiwa Waziri na kumpongeza ni hapa, wakati Mheshimiwa Rais anaingia mwaka 2021 tulikuta bajeti kwa mfano ya Kaliua ilikuwa ni shilingi bilioni 3.2. Sasa ninaongea bajeti ya mapato ya ndani ya Kaliua imekwenda hadi shilingi bilioni 8.9, hebu mpigieni makofi Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu, ukipandisha *own source* ikapanda kwa kiwango hiki cha shilingi bilioni 8.9 tafsiri

yake ni kwamba ndiyo maana mnaona sisi Kaliua tunao hata uwezo wa kujenga vituo vya afya kwa fedha ya ndani. Kwenye jimbo langu vinajengwa vituo vya afya viwili, kwenye jimbo la mwenzangu Ulyankulu kule vinajengwa, haya ni mapato ya ndani. Hii yote ni faida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, zipo kampuni zimefanya vizuri zaidi, zimeweza hata zenyewe kutoa *CSR* na kujenga vituo vya afya na ndiyo maana tunawaambia kwamba kwa kweli sekta ya kilimo imepata mwenyewe. Kama ni upele, Kaka Bashe yeye ndiye mkunaji wa upele anayestahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninasimama hapa, leo watashangaa Kwezi mbona anapongeza sana, ndugu zangu ninataka niwathibitishie kwamba hii *BBT* sio kitu cha mchezo, hii ni sehemu kubwa sana ya ajira. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri, *DC* wangu Ndugu Gerald Mongela amepokea matrekta ya kutosha Kaliua. Tulitenga hekari 16,000; kwa kilimo tuna hekari 6,500 na 10,000 ni kwa ajili ya mifugo. Vijana kule wapo tayari, wapo tayari kwa maelekezo na pia wapo tayari kufanya kazi. Sisi kama mnavyotujua, mzigo mzito tunao na tunapiga kazi, hatuna cha kuchelewa nacho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ambalo nilitaka niliongelee; hili jambo ni ombi; ombi langu kubwa ni kwamba kuna kitu hapa zile *AMCOS*. Mimi kule kwangu anajua kabisa jimbo lile lina watu takribani 400,000 na wengi ni wakulima 90% wameniomba *AMCOS* takribani 14; na hii ni kwa sababu gani! Unakuta kwamba vijana wetu wamemaliza darasa la saba, wengine wamemaliza *form four* na wengine wamemaliza *form six*. Kwa hiyo, nilikuwa ninaomba unaweza ukaangalia ili kutusaidia *AMCOS* Kaliua. Hiyo ni *special request* ya kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ningeweza kukupongeza ni suala la Benki ya Ushirika. Kwa kweli hapa umevunja *record*. Ninakuomba hata wakija wale wakulima binafsi wenye uwezo hakikisheni mmeweka programu nzuri sana kuhakikisha hawa wakulima tayari wana uwezo wa kukopa kupitia vyama vyao vya ushirika, kupitia vikundi mbalimbali, lakini hata

mmoja mmoja kwa sababu ni wanaushirika wanaotambulika na wana uwezo huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo ninaweza kumalizia hapa ni jambo kubwa sana ambalo nitapenda kuliongelea. Ninaziomba sasa kampuni za tumbaku, kwa kweli Mheshimiwa Bashe ninaomba zaidi wajikite na wenyewe kuwekeza katika maeneo yetu. Maana yake kama maghala yanavyojengwa sasa hivi, wanaendelea kukuza uchumi wa maeneo mbalimbali. Mheshimiwa *Engineer* Ezra pale ameomba akasema liko moja. Mimi kwangu yako mengi, lakini ninatamani sana hata twende kwenye kujenga kiwanda cha tumbaku ili tuwapunguzie gharama za kusafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwalimu Nyerere alikuwa na *idea* nzuri sana, tunajua Morogoro mambo ni mazuri, lakini *in future* hebu jaribu kuangalia kwenye Mkoa wetu wa Tabora tunaweza tukaenda kiasi gani kwa sababu tumbaku ndiyo iko pale na mambo mazuri yako pale. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho kabisa ambalo nilitaka kusisitiza ni ruzuku. Ninakushukuru kwa ruzuku, wananchi wanaendelea kulipwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. ALOYCE A. KWEZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimalizie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja kwa 100%. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro atafuatiwa na Mheshimiwa Sophia.

Samahani Mheshimiwa Sophia Hebron Mwakagenda, atafuatiwa na Mheshimiwa Ndaisaba na Mheshimiwa Anna Richard Lupembe ajiandae.

Mheshimiwa Sophia, dakika tano. *(Makofi)*

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia. Kwa mara ya kwanza ninampongeza Mheshimiwa Waziri kwa sababu ameweza kusaidia zao la parachichi kwa kutuletea wataalam, lakini pia kufanya *pilot project* katika Jimbo la Rungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ameleta ndugu zetu wa *COPRA* na Dada Irene amekuwa mwaminifu, amefanya kazi kwa nguvu sana kuhakikisha kwamba yale machungu ya kuuza parachichi kwenye viroba msimu ujao mtasimamia vizuri, kwa hilo ninakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka kuzungumzia suala la chai. Ninajua kama umeweza parachichi, leo hii viwanda vyetu viwili; Kiwanda cha Katumba kimefungwa na Kiwanda cha Busokelo kimefunga. Mheshimiwa Bashe, watu wamekusifia hapa na mimi nimekwishakusifia, unashindwaje kwenye chai? Tunaomba usimamie suala la viwanda vya chai. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninatambua viwanda vinaenda kwenye Wizara ya Viwanda pia, lakini mimi ninaamini mashamba yale yasipochumwa chai, mkulima hana taarifa yoyote wala hajui anafanyaje. Kuna wafanyakazi ziadi ya 200 ambao hawajalipwa. Ninaomba Mheshimiwa Bashe, hushindwi kusimamia suala la chai katika Wilaya ya Rungwe. Ninaomba sana tuma watu kama ulivyotusaidia kutuma watu kwa ajili ya parachichi. Nina uhakika unaenda kulimaliza hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wazee wetu wanalia na sisi tunaowawakilisha pia tunakueleza pia Mheshimiwa Bashe. Haujawahi kushindwa, basi fanya na hili. Umefanya kwenye tumbaku wamekusifia na umefanya kwenye ufuta. Kule nyumbani kwetu chai inaharibika. Karibu uje usimamie, wananchi wanasubiri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunakushukuru pia pamoja na Mheshimiwa Rais kwa ajili ya hii Benki ya Ushirika. Ninaamini tukiwa na benki kama hizi basi hata uwekezaji kule nyumbani na hata hii

chai tunayoizungumzia, tunahitaji Serikali iwe na viwanda vyake yenyewe. Kwa kuwa tukiwatumainia hawa watu wanatuacha katikati. Tunaomba hii benki iende Mbeya, ukaipeleke Rungwe na ukaipeleke Njombe kwa sababu tunaamini huko ndiko kwenye wakulima Mheshimiwa Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, ninaomba nizungumzie suala la mbegu za asili. Ninakushukuru kwamba tulikuwa tunazalisha takribani tani 800,000 lakini sasa hivi umevuka umefikia tani 1,400,000. Hili ni suala bora sana kwa sababu kuwa na mazao ambayo tunaziacha zile mbegu zetu za asili, sisi kama Waafrika na sisi kama Watanzania tusije tukapoteza ile asili tuliyokuwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, watu wa Kamati wamesema hapa kwamba hata kwenye ugali, kwa mfano mbegu ya mahindi, ugali wake ni bora zaidi. Basi tunaomba tuendelee kutunza mbegu zetu za zamani. Tuna maparachichi ya kisasa kweli, lakini tuwahimize wakulima wachanganye na maparachichi yale ya zamani na kwenye mahindi hivyo hivyo, tuhakikishe tunasimamia yale mambo yetu ya zamani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunashukuru sana kwa suala la mbolea na ulizungumza wakati wa wadau wa parachichi ukasema utawatumia ndugu zetu wa *ITRACOM* kwa ajili ya kupata mbolea *specific* kwa ajili ya parachichi. Ninaomba hawa ndugu zetu wa *ITRACOM* kama kuna mbolea zaidi basi muwape hiyo *order* kwa sababu ulisema bajeti unayo. Pia kama wana madeni ninaamini utafanya nao kazi vizuri ili waweze kutusaidia, kwa sababu mwisho wa siku wameweza kusaidia kuweza kuleta mbolea na mbolea zimefika kwa wakati. Tumeona Wabunge hapa wanakusifia na kweli msimu ukifika mbolea ipo. Tunashukuru kwa ajili ya viuatilifu ambavyo umesema utatupatia, kwa kweli tunakuunga mkono. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tunafahamu kabisa na wenzangu wamesema, wakati unaanza bajeti ilikuwa shilingi bilioni 290; leo hii tunazungumzia shilingi trilioni 1.2. Mimi nina uhakika hayo magari ambayo umeshanunua tayari na

tumeshakwisha kuyaona kwamba yatafika na kugawanywa sawasawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaendelea kukumbusha, mimi kwa kweli ninaendelea kuitwa Mama Parachichi kwa sababu tuna mikoa sita inayolima parachichi. Kwa hiyo, tunaamini kule kwetu Mbeya hautatuacha kwa sababu ndiko parachichi zilikoanzia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo visima hivi pamoja na kwamba tuna miezi nane ya mvua katika Mkoa wa Mbeya, lakini bado ikifika mwezi wa tisa, kumi, kumi na moja na wa kumi na mbili, kunakuwa kuna ukame. Hivyo basi, tunahitaji sana kuwa na maji, ninaamini hautatuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza Mheshimiwa Bashe pia katika suala la magari 500 ambayo amekwisha kuyaeleza katika bajeti yake. Basi katika mgawanyo wa magari, tunaomba usiiache Wilaya ya Rungwe na wilaya zinazotuzunguka kwa kuwa na sisi pia ni wakulima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, kwa kuwa sisi kambi ya tulio wachache umetupa muda kidogo, ninaunga mkono bajeti yako kwa mara ya kwanza kwa kuwa ninawatetea wakulima. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Sophia kwa kuzingatia muda, ninakushukuru sana. Mheshimiwa Ndaisaba George Ruhoro, atafuatia Mheshimiwa Anna Richard Lupembe na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, ajiandae.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ya Wizara ya Kilimo. Kwanza, ninampongeza sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais mwenye upendo na mama wa kipekee ambaye ameonesha nia yake ya dhati kabisa kumkomboa mkulima wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulipoona kwa mara ya kwanza tu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan amepandisha bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 297 kwenda shilingi trilioni 1.2, tuligundua Mheshimiwa Rais Samia ameamua. Maamuzi ya Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kuongeza bajeti kwenye kilimo yamepeleka tabasamu kubwa kwa Watanzania na kwa wakulima wa nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais Samia alitufurahisha wakulima alipopeleka askari wawili wa mwamvuli ambao ni Mheshimiwa Hussein Bashe na Ndugu yangu Mheshimiwa Silinde. Mlipotumwa kwenda kama *frontline foot soldiers* kwenda kutatua *obstacles* zilizoko kwenye kilimo na hakika mmejua kuwafurahisha Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani, wananchi wangu wa Ngara na wale wa Mkoa wa Kagera, mmegusa penyewe. Mheshimiwa Bashe na Mheshimiwa Silinde, tunawashukuru sana kwa kuongeza bei ya kahawa. Mwaka 2021 kahawa ya maganda kwa kilo moja ya Robusta iliuzwa shilingi 1,200. Msimu huu ulioisha, kilo moja tumeuza shilingi 6,700. Haya ni mapinduzi makubwa kabisa kwenye kilimo. Tunawapongeza sana Mheshimiwa Bashe na mwenzako na watumishi wote wa Wizara ya Kilimo kwa kazi nzuri mliyoifanya. Aidha, tunawapongeza kwa mageuzi makubwa mliyoyafanya kwenye zao hili la kahawa. Kwanza, kubadilisha mfumo wa kuuza kahawa kutoka kununua kiholela holela kupitia Vyama vya Ushirika na kahawa kuanza kuuzwa minadani. Hapa mliupiga mwingi. Mwenye kisu kikali ndiye anayekula nyama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, minada mliyotuletea baada ya kuwa tulileta maombi imemwezesha mkulima kuuza kahawa yake kwa mtu mwenye pesa nyingi ambaye anakuwa ameleta *bid* kubwa. Mheshimiwa Bashe hongereni sana kwa kazi nzuri mnayoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunawashukuru kwa kuondoa tozo zaidi 49 ambazo zilikuwa zinamuumiza mkulima na kubakisha tozo saba ambazo tozo hizo sasa anatozwa mfanyabiashara wa kahawa na siyo mkulima. Hii imetoa nafuu kubwa sana kwa

wakulima wa kahawa. Ahsanteni sana kwa kazi nzuri mliyoifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nielekeze mchango wangu kwenye baadhi ya vitu muhimu ambavyo Wizara imewahi kuahidi na inatakiwa ivifanye. Hapo nyuma nimekuwa nikiomba Wizara itusaidie kuileta *NFRA*, ifanye *price stabilization* kwenye zao la mahindi ndani ya Wilaya ya Ngara na Mkoa wa Kagera. Mmetuahidi kwamba mwezi wa tano, wa sita huu *NFRA* walitakiwa kuwa Ngara, *unfortunately* hatujawaona. Ni ombi langu kwako Mheshimiwa Hussein Bashe na wenzako mtusaidie jambo hili liweze kutimia, *price stabilization* ifanyike, wakulima waache kuuza mahindi kwa bei ndogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona mpango mzuri sana wa Wizara ya Kilimo kuhakikisha inaanzisha *irrigation scheme* kubwa. *Scheme* hizi zitaweza ku-*serve* mashamba makubwa ya kahawa na mazao mengine maeneo mbalimbali nchini, lakini kumbukeni changamoto kubwa ya wakulima ipo kwa wakulima wadogo wadogo na wakulima wa kati wanaovuna kuanzia tani 10 mpaka tani 100. Ninaomba nilete ombi kwako Mheshimiwa Bashe. Njoo na ubunifu wa ruzuku ya kuwezesha kutengeneza miundombinu ya umwagiliaji kwa wakulima wa kahawa wanaozalisha tani 10 mpaka tani 100 kwa msimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, changamoto ya wakulima wa kahawa kwa sasa ni sisimizi wanaokula mizizi ya kahawa nyakati za kiangazi wakitafuta maji na ndicho chanzo cha kahawa nchini kukauka na kupunguza uzalishaji. Bila kuwapa *irrigation, mini-irrigation scheme*, mashamba yataendelea kukauka. Ninaomba sambamba na kugawa mbegu ya ruzuku, wakulima wanaozalisha vizuri waweze kusaidiwa katika eneo hili. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ya kwanza ililia)*

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua hiyo ni kengele ya kwanza na ninajitahidi kwenda na muda wangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mathalani kwenye upande wa miche ya kahawa. Ninaipongeza Wizara kupanga kugawa miche milioni 20 ya kahawa katika msimu huu. Mahitaji ya Wana-Ngara ni miche milioni 10 ndani ya kipindi cha miaka mitano. Wananchi wa Ngara wanaomba pale tulipoweka vitalu vya miche ya kahawa pembeni yake tuweke na vitalu miche ya parachichi. Wanapochukua miche ya kahawa, wachukue na ya parachichi. Anapomaliza kuuza kahawa, anapotumia fedha kabla haijaisha parachichi iwe imekomaa na aanze kuuza na aendelee kupata pesa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba utusaidie miundombinu iliyowekwa kwa ajili ya kuotesha miche ya kahawa kwenye viriba au vitalu, hiyo hiyo itumike kuotesha miche ya parachichi pembeni kandokando ya vitalu vya miche ya kahawa. Tutapiga njiwa wawili kwa jiwe moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna masoko ya kimkakati ambayo Wizara iko inayajenga maeneo mbalimbali nchini ikiwepo Ngara. Nimeona ukurasa wa 107 wa Hotuba ya Mheshimiwa Bashe iliyojaa matumaini wa Watanzania imeonesha kwamba lile Soko la Kabanga limefika 50%. Sitaki kubishana na zile takwimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Wilaya ya Ngara amekwenda kutembelea pale amekuta mambo siyo mazuri sana, ninajaribu kutumia lugha nzuri. Kamati ya Siasa imeenda wiki iliyopita imekuta kazi siyo nzuri sana. Mheshimiwa Bashe nimeanza kusema wewe ni *frontline foot soldier* ambaye umeondoa *obstacles* nyingi kwenye Wizara ya Kilimo, hili haliwezi kukushinda. Ninaomba utusaidie kufuatilia masoko haya kwa sababu Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa wanashindwa kufuatilia vizuri kutokana na *setup* na usimamizi unaotoka Wizarani moja kwa moja kwenda kule. Ninaomba utusaidie eneo hili ili masoko haya yaweze kukamilika kabisa. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. NDAISABA G. RUHORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kumpongeza Mheshimiwa Bashe kwa kazi nzuri. Hotuba yake imejaa matumaini makubwa kwa Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante! Muda wako umeisha Mheshimiwa. Mheshimiwa Anna Richard Lupembe atafuatiwa na Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke. Mheshimiwa Suma Ikenda na Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma wajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia bajeti ya Kilimo. Kwanza, kabisa ninaomba nimshukuru Mungu ambaye ametupa uzima na uhai hatimaye tuko hapa tunachangia maendeleo ya kilimo katika Taifa letu la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa ambayo ameifanya kupitia kilimo. Amefanya kazi kubwa sana, lakini ninaomba nimpongeze Waziri Bashe pamoja na Naibu Waziri. Ninaomba nimpongeze Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na ninaomba niwapongeze watendaji wote wa Wizara ya Kilimo pamoja na taasisi zote zinazohusika na Wizara ya Kilimo kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya katika nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nimpongeze Mheshimiwa Waziri Bashe kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kupitia Wizara ya Kilimo; ameonesha taswira mpya kabisa katika Wizara ya Kilimo. Vilevile amefanya kazi kubwa na nzuri ambayo hata leo wakulima wa Tanzania wamebadilisha maisha yao kupitia majukumu mazito, kuona matatizo yao na kuyabeba kama ya kwake yeye binafsi. Ninaomba nikupongeze sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya kwanza tulikuwa tunakusumbua sana kupitia mazao yetu ya kibiashara kama tumbaku na pamba, lakini ulitazama kwa mtazamo chanya.

Ukahakikisha, ukaanza kufuatilia zao moja baada ya lingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka Mheshimiwa Bashe hakuna zao lililokuwa linasumbua kama tumbaku. Wakulima wa tumbaku walikuwa duni. Waliokuwa wanalima zao la tumbaku walikuwa maskini, lakini toka ulivyoingia Mheshimiwa Bashe umebadilisha taswira ya wakulima wa tumbaku. Leo hii wakulima wa tumbaku nao wako katika historia ya kilimo chao ambacho wanacho katika maendeleo ya nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu umwagiliaji; Mheshimiwa Bashe ninaomba nikupongeze na nikushukuru sana. Ulikuja kwenye Jimbo langu na uliniahidi katika umwagiliaji kwenye Jimbo la Nsimbo utaweka mabadiliko makubwa sana na uliahidi kuwa utatoa shilingi bilioni 50, ninakushukuru. Ninaomba nikupongeze na mkandarasi Mchina alianza kazi katika Skimu ya Umwagiliaji ya Usense. Vilevile, ulisema utajenga nyumba kwa ajili ya yule ambaye ataisimamia skimu ile, ambaye ni afisa kilimo na kumletea gari. Hata hivyo, kwa bahati mbaya mpaka sasa hivi ule mradi umesimama kabisa. Sasa sielewi matokeo yake yakoje, lakini ninaomba nikushukuru sana kwa sababu ulifika lakini una nia njema na wakulima wa nchi yetu ya Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba nishukuru Mheshimiwa Rais ameleta ruzuku kwa wakulima. Ruzuku ile wakulima wa pamba na wakulima wa tumbaku walikuwa hawana ruzuku kabisa, lakini sasa hivi wakulima wa tumbaku wamepata ruzuku na wenyewe sasa hivi wananeemeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ninaomba nikupongeze Mheshimiwa Waziri kwa kuwarejeshea wakulima ruzuku ile ya mwaka jana. Ile bakshishi yao umeanza kuwalipa, lakini mpaka sasa hivi kuna watu ambao wameanza kulipwa, lakini mpaka sasa hivi kuna wengine hawajaanza kulipwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niipongeze Benki ya *NBC,* wao wameanza kulipa zile *AMCOS* zao ambazo wako nazo, lakini bado *CRDB* hawajaanza kuwalipa wale wakulima katika *AMCOS* zile nyingine. Ninaomba Mheshimiwa Bashe sasa hivi

wakulima wana matumaini makubwa sana na wewe, wanakupenda kwa sababu umebadilisha maisha yao. Wakulima wa Tanzania wanakupenda, umebadilisha maisha yao kwa kiwango kikubwa sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba hawa ambao bado (Benki ya *CRDB)*, basi iongeze *speed* iwalipe ili na wenyewe *AMCOS* nyingine ziweze kupata manufaa yale yanayotakiwa na kupata stahili yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu stakabadhi ghalani; ndani ya Mkoa wetu wa Katavi hususan Jimbo la Nsimbo tunalima ufuta na wananchi wa Halmashauri ya Nsimbo walikuwa bado hawajazoea kuingia kwenye stakabadhi ghalani. Hata hivyo, ninaomba niishukuru Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wanaendelea kuifanya. Tunaona kupitia mikoa mingine ya Mtwara, Lindi na sehemu mbalimbali kupitia stakabadhi ghalani manufaa makubwa ambayo wanayapata. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba mwaka huu Mkoa wa Katavi tuingie kwenye stakabadhi ghalani na wananchi bado hawajazoea, hili jambo ni geni kwao. Nilikuwa ninaomba sana twende kwenye elimu kwa mwaka huu. Tuwape elimu ya stakabadhi ghalani kwa sababu walikuwa hawajawahi kufanya kupitia zao la ufuta. Ninaomba tuwafundishe kwanza, tuwaelekeze mwaka huu halafu mwakani sasa tuingie kwenye stakabadhi ghalani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake sasa hivi imekuwa ni mgongano kwa sababu hawajui, hawajazoea, wameshazoea kuuza kiholela na sisi tunapenda kwa sababu unaona sasa hivi hapa kuna Waheshimiwa Wabunge wamesema waliongia kwenye stakabadhi ghalani kupitia ufuta wameuza kwa bei nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa ninaomba, tunatamani na wananchi wa Mkoa wa Katavi waweze kupata mafanikio ya ufuta na mwaka huu 2025 wamelima sana ufuta, lakini jambo hili la stakabadhi ghalani limewakuta tayari wameshazoea mtazamo mwingine na wanatakiwa waingie kwenye mtazamo mwingine. Nilikuwa ninaomba sana tuingie kwenye elimu...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru. Mheshimiwa Bashe ninaomba nikupongeze sana kwa kazi kubwa uliyofanya kupitia sekta ya kilimo, hongera sana. Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan katika Mkoa wetu wa Katavi atapata kura 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana, ninaomba kuunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Josephine Genzabuke.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipa nafasi. Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema, aliyenijalia afya na kunipa kibali cha kusimama ndani ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nianze kwa kuunga mkono hoja na ninaunga mkono hoja hii kwa 100%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninampongeza sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kazi kubwa anayoifanya ya kuwatumikia Watanzania. Hakika wote ni mashahidi, tumeona ni jinsi gani anavyojitaabisha usiku na mchana kwa ajili ya kututumikia sisi Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Bashe kwa moyo wa dhati kabisa, Mheshimiwa Bashe hongera sana, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara yako. Kwa kweli Mheshimiwa Bashe, sote ni mashahidi wewe ni mnyenyekevu kwa kila mtu na unamsikiliza kila mtu, pengine ni kipaji ulichopewa na Mwenyezi Mungu, Mungu aendelee kukujalia hekima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba niendelee kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa namna ilivyoamua kwa dhati kabisa kukipandisha kilimo na kukipa kipaumbele, kwa sababu ni ukweli

usiofichika, kilimo kimeajiri watu wengi sana, kimeajiri watu wengi sana wanawake kwa vijana na ukiangalia sasa hivi watu wengi wamejielekeza kwenye kilimo na hata Wabunge mliopo humu ndani wengi mna mashamba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ninaendelea kuipongeza Serikali kwa namna ilivyoona kilimo kiweze kupewa kipaumbele kwa sababu kimeajiri watu wengi na bado wapo watu wanaomaliza vyuo wanarudi vijijini kwenda kujiajiri. Hivyo basi nipongeze kwa kazi kubwa ambayo Serikali imeifanya chini yako Mheshimiwa Bashe, kwa kupeleka mbolea ya ruzuku kwa wingi. Niombe tu mbolea iendelee kufika kwa wakati kwa sababu mvua za kwanza ni za kupandia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile niendelee kuiomba Serikali ipeleke ruzuku kwenye mahindi, alizeti, mpunga na kwenye mbegu za muhogo, maeneo hayo nayo wanahitaji sana mbegu kwa sababu ukiangalia kwa mfano mahindi yanapatikana, lakini wakati mwingine bei inakuwa ni kubwa, kuna watu wengine hawawezi kuhimili bei hiyo. Kwa hiyo, tunaomba muendelee kupeleka ruzuku kwa wingi kwenye mbegu za mahindi, mpunga, mbegu za alizeti na mbegu za muhogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo, Mkoa wa Kigoma sisi zao letu la biashara ni pamoja na muhogo. Mheshimiwa Bashe nikuombe, mwaka juzi 2023, mwaka jana 2024 zao la muhogo limeporomoka sana kutoka kilo moja shilingi 800 kuja mpaka shilingi 200 wakati mwingine shilingi 300. Kwa hiyo, wakulima wanakata tamaa sana, tunaomba kama unavyofanya mambo mengine, uendelee kujitaabisha kutusaidia kututafutia soko la muhogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado mchikichi Kigoma unahitajika, tunaomba michikichi iendelee kupelekwa Kigoma ili wananchi waweze kupata mbegu zilizo bora waendelee kuzalisha zao hilo la mchikichi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niipongeze Serikali chini ya Mheshimiwa Rais na wewe mshauri kwa kuanzisha Benki ya Ushirika, benki hii itawasaidia sana wakulima, lakini mpeleke elimu

ili watu waendelee kuelimishwa, wafahamu maana ya ushirika, waweze kuupenda ushirika na kuweka pesa zao kwenye ushirika na wakati mwingine sasa waanze kukopa kupitia kwenye benki yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa, Mheshimiwa Waziri kule Kasulu kuna kampuni moja inaitwa Vod Sell, ilinunua tumbaku kwa wakulima, bado wakulima wale wanadai dola 208,503. Mheshimiwa Waziri, pesa hizo ni nyingi sana, tunaomba hao wakulima walipwe pesa zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu mmoja anadai kuanzia shilingi milioni 18, mwingine shilingi milioni 20 wengine mpaka shilingi milioni 15. Fikiria wanavyoshinda wanalima, wananyeshewa na mvua, wanajenga mabanda, lakini wameshindwa kulipwa. Tunaomba hao wenye Kampuni ya Vod Sell walipe pesa za wakulima mara moja. Mheshimiwa Waziri, nami kabla ya kuondoka kurudi Kigoma nitakuja ofisini kwako, ninaomba hiyo kampuni ilipe hizo pesa za wakulima mara moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, dola 208,503 ndizo wanazodai hawa wakulima. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninarudia tena dola 208,503.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo ninarudia kuunga mkono hoja, lakini kwa kuleta kilio cha wakulima hao wanaodai pesa zao, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Suma Ikenda.

**MHE. SUMA I. FYANDOMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nami nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. Ninamshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uzima na afya

njema ambapo nimefanikiwa kupata nafasi ya kuchangia kwenye Wizara hii ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Waziri wa Wizara hii ya Kilimo Mheshimiwa Hussein Bashe pamoja na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Silinde pamoja na Wizara yote kwa ujumla, wakiongozwa na Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu na watendaji wote kwa ujumla mnafanya kazi nzuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilimpongeza sana Mheshimiwa Hussein Bashe na ninarudia tena kumpongeza, kwa namna ambavyo anafanya vizuri sana kwenye Wizara hii. Wizara hii ya Kilimo kiukweli kabisa umeitendea haki Mheshimiwa Hussein Bashe, mwaka jana ndiyo umetia fora moja kwa moja. Kwa sababu Siku ya Wakulima Tanzania Nanenane hapa Dodoma mambo uliyoyafanya ni makubwa sana, haijawahi kutokea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, magari 40, matrekta 500, *power tiller* 800, pikipiki 6,444, vishikwambi 6,426, sare za wakulima yaani sijui niseme nini Mheshimiwa Hussein Bashe kwa kazi kubwa na nzuri unayoifanya, kwa kweli umeitendea haki Wizara hii. *(Makofi)*

Ndugu zangu Wana-Nzega Mjini hongereni sana kwa kumchagua Mheshimiwa Hussein Bashe kuwa Mbunge wenu, hamkufanya makosa na ninawaomba sana msikosee mwaka huu mumchangue kwa kishindo, mumpe kura za kutosha Mheshimiwa Hussein Bashe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nami kwa sababu ni Mbunge wa Viti Maalum, nitafika huko ili niweze kumuombea kura kwa kumpigia magoti Mheshimiwa Hussein Bashe, ili aweze kurudi tena kwenye Bunge hili la Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa namna ambavyo ameendelea kuwajali wakulima. Mheshimiwa Rais wetu alisikia kilio cha wakulima, mbolea ilikuwa ikiuzwa shilingi 150,000 akatoa ruzuku

kwenye mbolea mpaka sasa hivi ni shilingi 75,000. Wakulima wanakushukuru sana Mheshimiwa Rais na shukrani yao utaiona tarehe 29 Oktoba, 2025 pale ambapo utapewa kura nyingi za heshima, za kishindo hasa kwenye Mkoa wangu wa Mbeya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kaka yangu Mheshimiwa Hussein Bashe anafanya kazi nzuri na njema sana, lakini Mkoani kwetu Mbeya Wilaya ya Rungwe kuna kilio kikubwa sana kaka, kuna kilio kikubwa mno, wakulima wa chai wamepata tatizo kubwa sana. Wakulima wa chai wa Kayuki, Chivanjee, Msekela na Masukuru kulikuwa kuna Kiwanda cha Chivanjee alipewa mwekezaji, mwekezaji huyo alikuwa akifanya vizuri sana Mo Dewji, alikuwa akifanya vizuri, lakini mwisho wa siku hatujui kulitokea nini. Kiwanda kilifungwa tangu tarehe 26 Machi, 2024; wakulima wale wanapata shida sana kwa sababu hilo zao limebeba watu wengi sana wa Wilaya ya Rungwe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Waziri Bashe, ninakuomba sana useme neno utakapokuwa unakuja ku-*windup* hapo, useme neno kwa ajili ya wakulima wa chai wa Wilaya ya Rungwe hasa wanawake wamekuwa wakipata shida mno. Walikuwa wakiamka saa 11 alfajiri wanajiandaa kwenda kuchuma chai pamoja na akina baba, lakini sasa hivi hawana kazi za kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimwia Waziri Bashe, kulikuwa na kiwanda kile cha Katumba pale cha *WATCO*, kimefungwa rasmi tarehe 9 Mei, 2025, hawa wakulima wafanye nini? Na hao wakulima wa *WATCO* hapo wao tangu mwezi wa pili hawajalipwa fedha zao mpaka sasa, kiwanda kimefungwa na wao kwa kujidunduliza tu walinunua mbolea na hiyo mbolea hawana hata fedha za kulipa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamuomba Mheshimiwa Waziri Hussein Bashe, kwa huruma yako wewe kaka una hekima, una busara ninakuomba utakapokuja kusema hapa useme neno kwa ajili ya wakulima wa chai wa Wilaya ya Rungwe. Mungu aendelee kukubariki na kukuongoza kama vile ambavyo tunaliombea Taifa hili la Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nafasi hii uliyonipa acha nimpongeze sana Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan anavyolipenda Taifa hili la Tanzania kwamba liendelee kupata sifa kubwa. Ni juzi tu amefanya jambo kubwa ambalo limekwenda kumpitisha kiongozi wetu wa upande wa afya ndugu yetu Profesa Janabi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, kwa sababu anasimamia, anakuwa kipaumbele namna ya kuongea na mataifa mengine ili Watanzania tuweze kusikika kwa nafasi mbalimbali kwa kuwa ameendelea kuwa hapo, alianza na Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson ambaye alimpa nafasi kubwa kwa sababu alimuombea kule kwenye Mabunge ya Dunia akawa Rais wa *IPU*. Mungu akubariki sana Mheshimiwa Rais wetu Dkt. Samia Suluhu Hassan. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajivunia sana na tunajisikia furaha na amani. Kwetu sisi ni dua kwako, Mwenyezi Mungu aendelee kukupa uzima na afya njema ili tufike salama Oktoba, 2025 mambo yote yaweze kwenda sawasawa kwenye kapu la kura ambazo utakuwa unazihesabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru sana kwa nafasi uliyonipa, Mwenyezi Mungu akubariki sana. Ninaunga mkono hoja Wizara hii na bajeti hii iende kupita sawasawa na Mheshimiwa Bashe alivyoomba, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud na Mheshimiwa Riziki Said Lulida ajiandae.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza kabisa ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipatia uhai na afya niweze kuongea kwenye Bunge hili. *(Makofi)*

Pili, ninapenda kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuipa kipaumbele sekta na Wizara ya Kilimo na tatu, ninampa hongera na pongezi nyingi Waziri Mheshimiwa Hussein Bashe, kweli

amefanya kazi kubwa, tumekuwa wote pamoja kwa muda mrefu, lakini amefaya kazi kubwa kwenye Wizara hii ya Kilimo akisaidiwa pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Silinde; pamoja na Katibu Mkuu Ndugu Gerald Mweli, kwa kweli na Wizara nzima, wafanyakazi wote, sekta ya kilimo sasa hivi imekuwa juu inapaa. Tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa sababu amekipa kipaumbele kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, utafiti; ninashukuru sana kuona bajeti ya utafiti imeongezeka, sasa hivi watafiti wanafanya utafiti wao kwa kufurahi kwa sababu angalau wanaona kitu walicho nacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikisema utafiti ninaungnisha hiyo hiyo inasema *TARI* ambayo wanatafiti mbegu na vitu vingine, *ASA* ambao wenyewe wanazalisha mbegu na *TOSCI* ambao wenyewe wanaona ubora wa mbegu, hivi vyote ukiviweka kwa pamoja unapata mbegu bora ambayo inakwenda kwa mkulima. Kwa hiyo, tunashukuru sana kwa jitihada kubwa ambazo mmeongezea bajeti kwenye taasisi hizi zote tatu ambazo zimeungana kwa pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, tatu, nne, ninashukuru sana Serikali kwa ruzuku inayotoa. Tunampongeza Mheshimiwa Rais, kwani ametoa ruzuku kwenye mbolea, ametoa ruzuku kwenye mbegu hasa alizeti, mahindi, pamoja na viuatilifu. Tunashukuru sana wakulima wote hata wadogo, wadogo wanashukuru sana wanafurahia kupata ruzuku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri, haya yote ni mawazo hasa mengine amebuni yeye na Mheshimiwa Rais yeye kwa pamoja tunawapongeza wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya zana za kilimo; vituo vya zana za kilimo ambavyo umesema kuwa matrekta yanaletwa pale na watu wanakuja kukodi ekari moja kwa shilingi 35,000, Mungu awape nini. Tunamshukuru sana Mheshimiwa Rais hata mkulima mdogo mdogo ataweza kuchukua shilingi 35,000 na ataweza kulima angalau ekari yake akiweka mbolea, akafanya

kanuni bora za kilimo anaweza akapata kwa ekari moja magunia zaidi ya 40 ya mahindi. Mungu awabariki kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mazao mbalimbali; nikisema mazao mbalimbali yamepanda bei nianze na zao la kokoa ambalo tunalima katika Mkoa wetu wa Morogoro. Kilo moja imefikia shilingi ngapi mnajua? Imefikia shilingi 28,000 kilo moja ya kokoa, sasa kwa nini uende kulima mazao mengine. Kahawa na yenyewe imepanda mpaka shilingi 8,000, shiingi 6,000. Wakulima sasa hivi huwaambii nenda kulima, wanajituma wenyewe kwenda kulima kwa sababu soko lipo na bei ni nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunamshukuru sana Mkuu wetu wa Mkoa Mheshimiwa Adam Malima ambaye anasukuma pamoja na Wakuu wao wa Wilaya, pamoja na Maafisa Ugani kwa kazi nzuri wanayoifanya kwa upande wa kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasema, kilimo Morogoro ni ghala la chakula. Morogoro ni ghala la chakula kwa sababu tunazalisha mpunga, sisi Mkoa wetu wa Morogoro ndiyo wa kwanza Tanzania. Tunashukuru sana Waziri Mheshimiwa Bashe, sekta ya umwagiliaji tumepewa skimu mbalimbali ambapo kwa kweli na wakulima wanajituma kwenye wilaya zote kwa wastani wanazalisha mpunga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, afisa ugani; maafisa ugani walikuwa wamesahaulika jamani, tunakushukuru sana Mheshimiwa Rais kwa kuwakumbuka. Tunashukuru sana Waziri Mheshimiwa Bashe, kwa kuwakumbuka na kuwapa vitendea kazi. Sasa hivi angalau wana vitendea kazi, mnawajengea nyumba mmesema ninyi wenyewe, wana vishikwambi, wana pikipiki, wana *soil scanners* ambazo zinaangalia afya ya udongo. Kwa hiyo, tunashukuru sana wafanye kazi, wafanye kazi kwa hivi vifaa wamevipata, kwa hiyo wamfikie hata mkulima mdogo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija kwenye bajeti; bajeti imepanda imetoka kwenye shilingi bilioni 294 mpaka shilingi trilioni 1.2, kwa kweli haijawahi kutokea tunamshukuru sana na kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jambo hili kwa kuipa

kipaumbele sekta ya kilimo na kuipandisha kuona kufikia hapo ilipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Tume ya Umwagiliaji, tumezunguka Tanzania nzima kuona umwagiliaji, mimi mwenyewe ninasema Tume ya Umwaguliaji inafanya vizuri, kuna *scheme* mbalimbali, kuna *scheme* kubwa ambazo Mheshimiwa Waziri umezitaja kwenye hotuba yako zinaendelea vizuri, Ndugu yangu Mndolwa ahsante kwa kazi unayoifanya pamoja na watu wako wa Tume ya Umwagiliaji, mnafanya vizuri sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushirika ulikuwa umekufa tunashukuru sasa hivi unafanya vizuri chini ya Mheshimiwa Waziri Bashe, hongera sana umefanya kazi kubwa Mheshimiwa Rais apewe maua yake kwa kuisimamia sekta ya kilimo na kutoa mchango mkubwa kwenye Benki ya Ushirika ambayo hii benki ya ushirika wataitumia wakulima wote wadogo na wakubwa, wanaweza kuitumia kwa sababu ni benki yao ambapo kuna vikundi mbalimbali vya wakulima tunashukuru sana kuona inakwenda vizuri ili mradi wachague viongozi wazuri, wawaongoze vizuri waende vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu viwanda vya sukari, kuna viwanda vya sukari vinaenda vizuri...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana, naunga mkono hoja na Mwenyezi Mungu akubariki, abariki Wizara ya Kilimo na ambariki Mheshimiwa Rais na Waziri wa Kilimo Mheshimiwa Bashe ubarikiwe na Mungu. *(Makofi*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.*(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud atafuatiwa na Mheshimiwa Riziki Said Lulida na

Mheshimiwa Neema Gelard Mwandabila pamoja na Mheshimiwa Venant Daud Protas wajiandae.

**MHE. KHADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa fursa jioni hii ya leo. Kwanza kabisa nichukue fursa hii adhimu kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa maono yake na kiu yake katika kuhakikisha kilimo cha Watanzania kinakua na wakulima wa Tanzania wanapata tija katika mazao yao na kuinua uchumi wa nchi kupitia sekta hii ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninawapongeza viongozi wa Wizara hii nikianza na Waziri wa Kilimo, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu wote pamoja na watendaji wote wa Wizara hii katika kuhakikisha wanalisaidia Taifa na wanawasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri wa Kilimo mdogo wangu Mheshimiwa Bashe ni zawadi kwa wakulima wadogo wa nchi hii, nasema hivyo kwa sababu anajitoa maisha yake na usalama wa maisha yake kukabiliana na kuwasaidia wakulima hawa wadogo wanaodhulumiwa kwenye viuatilifu, kwenye kununua mbegu *fake* na mambo mengine yanayohusu sekta ya kilimo ambao anapambana na wahalifu hao, Mwenyezi Mungu ndiye atayekupa ulinzi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea napenda pia kuwapongeza eneo ninaloliwakilisha, Taasisi Zisizo za Kiserikari kwa juhudi kubwa anayofanya kushirikiana na Serikali katika kuinua sekta ya kilimo, kuwasaidia wakulima kwenye elimu, kwenye mafunzo pia kuwajengea uwezo na kusimamia kilimo na hasa kilimo ikolojia, mbegu za asili, viuatilifu vya asili na mambo mengine yanayohusu kilimo pamoja na kuwatafutia masoko, wanafanya kazi kubwa sana kushirikiana na Serikali, wana haki ya kupongezwa na wao kwa mchango wao mkubwa kwa wakulima wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu kuhusu huduma za ugani Serikali imejitahidi sana kuwawezesha, kuwajengea uwezo, kuwapa vifaa watu wetu hawa, wafanyakazi

wetu hawa Maafisa Ugani, naomba tuendelee kuwajengea uwezo kuwapa elimu na mafunzo mbalimbali ili kukabiliana na changamoto mpya zinazojitokeza kila siku kwenye sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa ujenzi wa viwanda vya mbolea, lakini pia naendelea kushauri tuendelee kuwekeza zaidi kwenye viwanda vya mbolea tuwajengee uwezo wananchi wetu wa ndani ya nchi waweze kuwekeza kwenye viwanda vya mbolea pamoja na mbolea hizi za asili viwanda vidogo vidogo huko vijijini kwenye mashamba yetu sekta hii ipewe kipaumbele, kwa sababu kuimarisha sekta ya mbolea, kuimarisha sekta ya mbegu, kuimarisha sekta hii ya viuatilifu ni usalama wa chakula, lakini pia ni usalama wa nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye mbegu za asili naomba sera, sheria zitambue urithi huu wa mbegu za asili na kuwe na benki maalum ya mbegu za asili pamoja na mabenki hayo ya mbegu za asili, tuone na mpango kazi wa muda mrefu wa kuwa na mabenki haya kwenye maeneo, kwenye Wilaya hata kufikia kwenye eneo la kata. Kuwe na utafiti, uongezwe utafiti kwenye mbegu hizi za asili kuona virutubisho vyake na viini lishe vyake ili mtakapopata sasa uhakika mbegu hizi ziendelee kuzalishwa kwa wingi, zisambazwe kwa wananchi na zipewe ithibati kwa muda muafaka ili ziweze kutumika badala ya kufanyiwa utafiti zikabaki tu kwenye *store* na kwenye maghala, zipewe ithibati, wakulima weweze kutumia pamoja na kutoa mafunzo zaidi kwenye kilimo ikolojia kwa maana kilimo hai na kilimo hifadhi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu upotevu wa mazao; Serikali imejitahidi sana kujenga maghala na vihenge kwa ajili ya kuhifadhi mazao, naipongeza Serikali, lakini pia nashauri Serikali kwa wale wakulima wadogo wadogo wanaoweza kuhifadhi magunia 10 mpaka 100, kuna mifuko hii ambayo inaitwa *hermetic* haitumii kemikali, inahifadhi kwa kutumia viuatilifu vya asili hakuna kemikali kwenye hii mifuko, lakini bei yake ni kubwa sana ni shilingi 5,000. Tuone sasa namna ya kufanya kupunguza kodi ili mifuko hii iwe na bei nafuu wakulima waweze kuitumia na kuhifadhi mazao yao na kuepukana na ile adha ya kuharibu mazao yao bila ya muda muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nampongeza Mheshimiwa Makamu wa Rais nampongeza na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maana hawa ni wasaidizi wakuu wa Mheshimiwa Rais, wanavyomtia moyo na wanavyompa *support* katika kuhakikisha kilimo cha nchi hii kinafanikiwa. Tunapoomba kwamba Wizara hii iongezewe bajeti, tunaipongeza Serikali kwa kuwa kila mwaka sasa hivi tunaongeza bajeti kwenye sekta hii ya kilimo na tuna kila sababu ya kuendelea kuiombea bajeti Wizara hii iongezeke ili kufikia mafanikio tunayoyatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema baadhi tu ya mafanikio ambayo tunapoomba bajeti yanafanyiwa kazi, kwa maana sasa kuna ongezeko kubwa la ujenzi wa mabwawa ya umwagiliaji na uchimbaji wa visima, ongezeko kubwa la ruzuku ya mbolea, mbegu na viuatilifu, ongezeko kubwa la maghala na vihenge, ongezeko kubwa la bei ya mazao ya wakulima, ongezeko kubwa ya matumizi ya dhana bora za kilimo, ongezeko kubwa la kuwapatia vitendea kazi maafisa ugani wetu, kuanzisha kilimo cha hanga, kuongeza ajira kwa wanawake na vijana, kuanzishwa kwa Benki ya Ushirika ili kuwasaidia wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache tu niliyoyasema kuna haja ya kuendelea kumuunga mkono Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mama yetu Mheshimiwa Rais, Dkt. Samia Suluhu Hassan na kuhakikisha mwezi Oktoba tunampitisha kwa kura nyingi za kishindo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, ahsante muda wako umeisha...

Ahsante. Mheshimiwa Riziki Said Lulida.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru kwa kunipatia nafasi na mimi kuchangia katika hoja ya bajeti ya Wizara ya Kilimo, kilimo ni uti wa mgongo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema aliyetujalia kupata afya njema na kuwepo hapa na sisi ni wawakilishi wa wakulima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa hekima, utulivu na amani aliyoijenga katika nchi hii na kuleta kuheshimiana ndiyo tumefika hapa, nchi ambayo haina utulivu hata kilimo hakiwezi kufanya kazi, lakini kwa hekima yake ameifanya hii nchi imekuwa na hekima na kuwachagua vijana hawa, mimi nilikuwa nao Kamati ya Bajeti nawajua vizuri sana, namjua Mheshimiwa Bashe, namjua Mheshimiwa Silinde tulikuwa wote Kamati ya Bajeti, kwa kweli walikuwa wanafanya kazi kubwa sana na mimi napongeza sana, kazi zenu zinaonyesha sasa hivi kwamba ninyi ni vijana mnakwenda na *4G,* ni vijana wa digitali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninamshukuru Katibu Mkuu Ndugu Gerald Mweli na watendaji wenzake wengine. Mimi kwa heshima ya Mkoa wangu wa Lindi na Mtwara na Ruvuma ambao ni wakulima wa korosho tunasema ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli korosho ilichezewa kwa muda mrefu, kwetu korosho ilikuwa ni vita ya kiuchumi, watu walikuwa wanahakikisha wananunua korosho kwa bei ya kutupa, kilo moja shilingi 600 wakapandisha mpaka shilingi 2,000, lakini hata hiyo unapata kwa bei nusu nusu hauipati yote. Sisi ndiyo wa kwanza kuanza na stakabadhi ghalani, lakini tuseme kweli ya Mwenyezi Mungu leo korosho tumefikia zaidi ya shilingi 4,050 kutoka shilingi 1,200 zao ambalo lilikuwa linachezewa mpaka kufikia hapo tunasema ahsanteni, wakulima wanaheshimika huko nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili tumepewa ruzuku ya pembejeo za viuatilifu bure, tuseme nini sisi wakulima zaidi ya kuongeza kilimo tu. Zao la ufuta lilishakufa, leo kila mtu/watu wanahama huko Sikonge, wanahama Tabora, Mwanza wapi watu wote wanakimbilia Lindi kwenda kulima ufuta, kwa vile kule kwanza tunapata ufuta ambao ni bora, hii yote ni kwa ajili ya kuwa kuna utulivu, kuna amani, kuna kuheshimiana na hata hivyo

mazingira bora yamewafanya watu waweze kulima kule Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeona katika hii bajeti mahindi yameongezeka, mchele umeongezeka, korosho imeongezeka, kahawa imeongezeka, miwa imeongezeka, tunataka nini zaidi ya kumuomba Mwenyezi Mungu na kumshukuru! Usiposhukuru kwa kidogo basi hata kwa kikubwa huwezi kukishukuru, maana yake leo wale wakulima, mimi ni mtoto wa mkulima, lakini mimi mwenyewe ni mkulima, ninalima alizeti na ninalima mahindi, nasema Mwenyezi Mungu haya tunayoyaona yazidi kuongezeka, tuna nafasi kubwa ya kuongeza ili kilimo hiki tutakachofikia 4.1% kiweze kuongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la matrekta; nimeangalia matrekta yamegawiwa gawia Tanzania nzima Mkoa wa Lindi na Mtwara haipo. Hakuna haja ya kugawa sungura nusu nusu, kama ni maendeleo yasiwe ya kibaguzi baguzi, Mkoa wa Lindi pia tunataka matrekta. Nimeongea na baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wenzangu, Kilwa walishaomba *BBT* lakini hawakupewa trekta hata moja, sasa tunataka vijana wa Kusini ambao walikuwa ni wazururaji wa hovyo hovyo nao wafikiriwe kupelekewa matrekta ili na wao waweze kuendeleza suala la kilimo kwa ubora wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitazungumzia heshima kubwa anayotupa Mheshimiwa Rais ni kubwa lazima tuseme ahsante Watanzania. Leo unaona vurugu za kiuchumi hizi, *economic crisis* ambazo tunaziona *economic interference, business interference, colonialisation interference* hizi zote ni kwa ajili ya uchumi tu. Sasa hivi tunasema tumepata vijana mahiri ambao wameweza kusimama na ma-*tycoon,* ma-*tycoon* hawa wametajirika sana na nchi yetu lakini hawajatujengea hata shule, hawajatujengea hata hospitali, hawajatupatia hata ile hela wanayoipata wakawa matajiri kusema watatunufaisha Watanzania, wao ni kuchuma na kwenda mbele hatukubali!

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania tumefikia mahali ambapo tunampa mzigo mzito huyu kijana kuwa wale kwanza hawatakubali kumuona mtu anakuwa *strong* kama vile. Kijana

yeyote wa Kiafrika, Kitanzania akiwa *strong* lazima akutane na *crisis!* Nawaombeeni Mwenyezi Mungu atawapa ulinzi na wale wanaojifanya nchi hii wanaichezea wanavyotaka tumefika mahali tunasema *enough is enough*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wajiulize wanafanya biashara kubwa kwa kutumia uchumi wa Tanzania tumenufaika nini na wao zaidi ya wao kututaka wanunua vitu kwa bei ya chini na kwenda kunufaika huko nje? Leo tunataka ulimwengu wa viwanda vya korosho viwepo Mtwara. Mheshimiwa Bashe ukae na Mheshimiwa Waziri wako wa Viwanda una uwezo wa kufufua viwanda vyetu. Lindi hakuna kiwanda hata kimoja, lakini viwanda vile ni ajira tosha kwa watu wa Kusini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaizungumzia Nachingwea; wakati wa ukoloni walipima lile eneo wakakuta ardhi ya Nachingwea ni kwa ajili ya kilimo cha soya, ardhi ya Nachingwea ilikuwa ni ardhi mojawapo *fertile* mpaka ilitolewa treni kutoka Mtwara mpaka Nachingwea, maana yake nini? Ni kuhakikisha Nachingwea yenye maendeleo ya kilimo, inawezekana mkakae chini mjiulize tunafanya nini kuisaidia Nachingwea kuna *farm one* mpaka *farm 17* ambayo waliacha wakoloni, yako pale mpaka sasa hivi. Tunaomba yale mashamba sawa suala la zao la soya ndiyo linastawi sana Nachingwea. Soya, karanga, mahindi ni matumaini yangu haya mazao ambayo tunayazungumzia sasa hivi tutazidi kuboresha na kuweza kuwapa kipaumbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu biashara ya soko, Mheshimiwa Bashe wewe ni mwanangu, ni marafiki zangu, naomba tutengeneze ujirani mwema kati ya Tanzania na Comoro. Comoro ni nchi ya jirani, tukitegemea masoko ya nje yakitukatalia sisi tutakuwa tumekwama na mazao yetu. Comoro ni watu ambao wana asili ya Kusini, chakula chetu ni kimoja, mazao yetu yanafanana, kaa chini na Mabalozi, Balozi Yakubu na nchi ya Comoro tuone tunafanya nini ujirani mwema kwa kuwapelekea chakula, maana yake Comoro yote unayoiona wanategemea chakula kutoka Tanzania Bara, hivyo tukifanya mradi ule wa Mtwara na Lindi kupeleka bidhaa zetu Comoro utatujengea uchumi bora katika Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeangalia katika miradi ya umwagiliaji nimesoma toka mwanzo mpaka mwisho kwa muda mfupi bado tunahitaji umwagiliaji Kusini. Kuanzia Mto Rufiji, Mto Mwenkuru, Mto Matandu, Mto Ruvuma ni maeneo yenye mito tunahitaji umwagiliaji wa kutosha.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Mbunge.

**MHE. RIZIKI S. LULIDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru sana Mwenyezi Mungu awabariki, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Neema Mwandabila.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii ili nami niweze kuchangia katika Wizara hii muhimu kwa maendeleo ya Taifa letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe mchoyo wa fadhila nami niungane na wenzangu ambao wamekuwa wakiendelea kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Bashe, Mheshimiwa Silinde pamoja na Katibu Mkuu na timu nzima ya Wizara ya Kilimo. Kikubwa kinachonifurahisha kwenye Wizara hii ni namna ninavyowaona Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri na Katibu wanavyokuwa na ushirikiano mzuri na mafanikio yoyote panapokuwa na ushirikiano lazima muweze kufanikiwa kwa hiyo kwa hilo nawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina yangu jioni hii, ninafahamu muda nilionao ni mchache, lakini kuna vitu ambavyo ninatamani kuongelea. Kwanza ningependa kuanzia kwenye zao la parachichi, niseme tu kwamba tunapongeza Wizara kwa hatua ambayo imeendelea kuchukua ya kuzalisha miche ya parachichi, lakini pia kuwezesha sekta binafsi kuanzisha uchakataji wa *rejects* yale maparachichi ambayo yalikuwa yanaonekana *reject,* kwetu tuna mwekezaji ambaye ni Lima anatusaidia sana kupunguza hiyo *burden* ya maparachichi ambayo yanakuwa hayajafikia viwango vya ubora wa kusafirisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati nilifanikiwa kumtembelea na alinipa uhitaji wake akaniomba niwasilishe kwa Wizara, nilijaribu kufikisha ujumbe, lakini kupitia *forum* hii ningependa pia kuomba kwamba Mheshimiwa Bashe na timu yako nzima tazameni namna ya kumsaidia Lima katika kutumia ile fursa vizuri kwa sababu kuna *production* ya mafuta sawa, lakini kuna bidhaa zingine ambazo zingeweza kuzalishwa ikiwemo mbolea baada ya ule mchakato wa kutoa mafuta kwa ile takataka inayokuwa imebaki. Kwa hiyo hilo pia naomba alinituma niwaombe, kwa hiyo, nawasilisha ombi lake kama lilivyo naomba mlipokee Mheshimiwa Bashe na timu yako nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nilikuwa na wazo dogo kwenye eneo la ufuta kwa maana ya kwamba tukiwekeza kwenye *private sector* kama ambavyo tumefanya kwenye kuwanusuru wakulima na hizo *rejects* za parachichi tufanye *processing* ya ufuta, tumekuwa tunaisafirisha kama ilivyo, tunafahamu kama ingefanyiwa mchakato wa uchakataji nchini ufuta ungeweza kuongeza ajira kwa watu wetu kwa eneo kubwa. Kwa hiyo, tujaribu ku-*shift* kutoka kwenye eneo la kusafirisha malighafi hii ya ufuta kama ilivyo, tui-process iwe angalau kwenye *final product or semi final product* ili iweze kwenda ikiwa imewasaidia wananchi wetu. Pia tunafahamu hata zile pumba tu zinazokuwa zinabaki zinaweza zikawa tija kwa uzalishaji kwenye eneo la mifugo, kwa hiyo hilo pia nilitamani niwasilishe hilo ombi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niendelee kuwapongeza tena kwenye eneo la *BBT*. Kitendo tu cha kuwa na maono ya uanzishaji wa *BBT* mimi kwangu niseme tunafarijika kuona kwamba kweli Wizara ina dhamira ya kuwakomboa vijana, wanawake na watu wengine ambao wanakuwa na uhitaji. Ninataka tu niseme kwamba nilifanikiwa kupitia taarifa vizuri, nikasikitika tu eneo dogo kuona Mkoa wa Songwe na ukubwa wake hakuna shamba hata moja la kwenye Mradi wa *BBT,* kwa hiyo hili pia ninaiomba Wizara, ninamuomba Mheshimiwa Waziri na timu yake hebu angalieni namna ya kuanzisha shamba hata moja kwenye Mkoa wa Songwe la *BBT,* kwa sababu tunayo maeneo makubwa na sisi ni wakulima wakubwa na kwa kufanya hivyo utakuwa umewanusuru vijana na wanawake wa Mkoa wa Songwe, kwa namna moja au nyingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli kwa kufanya hivi utakuwa umewanusuru vijana na wanawake wa Mkoa wa Songwe kwa namna moja au nyingine. Hili ni ombi langu sasa mimi kama Mbunge, nikuombe Waziri na timu yako mtusaidie hata kuwa na mashamba. Mkiweka hata moja moja kila wilaya au hata moja tu kwenye Mkoa wetu, utakuwa umetusaidia sana Mheshimiwa Waziri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kuwasilisha ombi hilo nirejee kwenye Mfuko wa Pembejeo. Nilipata nafasi ya kutembelea katika Mfuko wa Pembejeo katika dhamira ya kuona kwamba wananchi wa Mkoa wangu wa Songwe wananufaikaje na Mfuko wa Pembejeo *(AGITF)* kwamba kuona ni namna gani wananchi wangu watanufaika. Nikaenda *at least* kuomba watufanyie mafunzo, niwaite kwenye mkoa wangu wafanye mafunzo. Changamoto tuliyokutana nayo ilionekana hawana bajeti kwa ajili ya utoaji wa mafunzo kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mmewapa pesa nyingi ambapo mmeweza kutoa kwa bajeti ya mwaka 2024 mmetoa shilingi bilioni 5.7 *out of ten billion* lakini kwenye takwimu hizo hizo ilionesha kwamba ni wananchi 49 tu ndiyo waliopata mkopo ambao nao una thamani ya shilingi milioni 503.

Sasa Mheshimiwa Waziri kwa sababu wewe ni mtu wa matokeo na ungependa kuona mambo yanakuwa na tija, mmeweka pesa nyingi ambayo haijaenda kwa wananchi. Mnafanya nini kuhakikisha fedha hizi ziende kwa wananchi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu; kama vile tunavyowekeana malengo kwenye maeneo mengine kwamba tunakuomba mwalimu uhakikishe umefikia lengo hili basi na wewe weka malengo kwenye taasisi hii ionekane kwamba kila mkoa *at least* waweze kukopesha hata watu 50. Kwetu sisi kama wananchi tunaona kwamba itakuwa na faida, lakini Mheshimiwa Bashe huwezi ukaniambia nchi hii kwa mwaka mzima wakopeshwe watu 49 tu. Mimi sioni kama tunakuwa na dhamira kweli ya dhati ya kuwakomboa wananchi. Kwa hiyo, nikuombe Mheshimiwa Bashe kwenye hili utusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi tuna shida na hizi fedha, mashamba tunayo, dhamana tunazo na tuna uwezo wa kuonesha tija kwenye maeneo haya. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, ninaomba kwenye eneo la mfuko wa pembejeo muwekeane malengo, kila mkoa ulete watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kibaya zaidi hata maafisa kilimo tukiwauliza kwenye maeneo yetu hawajui kwa habari ya Mfuko wa Pembejeo, wanakuwa wanakushangaa tu unapokuwa unaongelea suala hili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. NEEMA G. MWANDABILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Nilikuwa na mengi ya kuongea lakini niseme tu tuna imani na Wizara hii na tuna imani na waliopewa kusimamia Wizara hii na tunaendelea kuwaombea Mungu aendelee kuwatunza ili wafanye kazi nzuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaunga mkono hoja, ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Venant Daud Protas, atafuatiwa na Mheshimiwa Francis Isack Mtinga, Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate, Mheshimiwa Yahya Ally Mhata na Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea wajiandae.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuwa mmoja wa wachangiaji leo katika bajeti ya Wizara ya Kilimo ambayo bajeti hii inawagusa wananchi wetu moja kwa moja hasa sisi tunaotoka maeneo ya vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze na mimi kuungana na Wabunge wengine wote walioanza kuchangia tangu asubuhi kumpongeza Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili niipongeze Wizara ya Kilimo ikiongozwa na ndugu yetu Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe,

Mbunge wa Nzega Mjini, Mheshimiwa David Silinde, Katibu Mkuu na timu yote ya Wizara. Kwa kweli mwaka 2020 tulikuwa tunaingia hapa sisi Wabunge wapya, miongoni mwa Wizara ambayo ulikuwa ukiingalia iko hoi, ukimuangalia Waziri yuko hoi, watumishi hoi ni Wizara ya Kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa unamkuta Waziri hoi, Wizara hoi, wakulima hoi, ndiyo hii Wizara ilikuwa inaonekana hivyo mwaka 2020, lakini kwa sasa hivi unaweza kwenda hata shamba umevaa suti. Hii Wizara ndiyo imetupa mfano kuona mkulima namba moja anakwenda kukagua wakulima ana *uniform* ndiyo maajabu hayo, ndiyo mabadiliko hayo yameanza kwa kasi. Kwa hiyo, nikupongeze sana Mheshimiwa Waziri kwa kazi kubwa na umeleta *reform* nzuri ambazo wananchi wanaziona moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na bajeti ya shilingi bilioni 200 mwaka 2020, leo tumefika shilingi trilioni 1.2. Hayo ni mapinduzi ya kijani na hapa maana yake ni nini? Mheshimiwa Rais ameona mbali sana, amesema tukiwekeza kwenye kilimo, kwa sababu wanasema kula ni lazima kuoga ni hiyari, ndiyo hii kwa sababu kuoga unaweza ukachagua siku gani nioge au nisioge, lakini kula lazima utakula hakuna siku ambayo utachagua leo nisile. Hata wale ndugu zangu wanaofunga wanakula daku ndiyo wanafunga asubuhi. Kwa hiyo, hii ni Wizara ambayo inakwenda sana kuwagusa wananchi kila siku. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais aliona mbali kwa sababu tukizalisha chakula kingi, tutajilisha wenyewe na tutalisha mataifa mengine. Yale mataifa ambayo ni wavivu kulima wenyewe kila siku wanashinda kwenye *TikTok,* sasa watakuwa wana njaa. Wakati sisi tunalima wenyewe wako kwenye *TikTok,* kwa hiyo wakati wanataka kula sisi tutakuwa na chakula tutakwenda kuwauzia na Serikali yetu na nchi yetu tutapata fedha za kigeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi ninawashukuru na hii bajeti ninaiunga mkono kwa 100% na Mheshimiwa Waziri ukimaliza tu anza kutekeleza majukumu yako bila kusubiri kelele za watu wengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kama nilivyosema, lakini niseme jambo moja ambalo ninataka nishauri. Jambo la kwanza Mheshimiwa Waziri, hebu simamia vizuri, umesimamia kote, hizi mbegu kwa nini zinakuwa kila siku bei haieleweki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuja hapa na swali la msingi, Mheshimiwa Silinde akanijibu majibu ambayo ukienda kwenye uhalisia hayaendani kabisa, akaniambia bei elekezi ya mbegu gani haizidi hata shilingi 14,000 lakini ukienda mtaani inafika mpaka shilingi 30,000.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima kule wanalalamika na sisi tumewaambia mbegu bora ili tupate mazao ya uhakika tulime mbegu za kisasa. Sasa mbegu za kisasa tumewaletea umaskini, unanunua mbegu shilingi 30,000 unaenda kupata gunia 20 sawa, lakini unakuja kumuumiza wakati anaenda kununua mbegu hana fedha yule mkulima. Mimi niombe kwenye Wizara hii, mwaka huu tunakupitishia bajeti, nenda kadhibiti mfumuko wa bei holela kwenye mbegu. Hilo ndilo jambo la msingi, nenda ukalianzie moja kwa moja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna Taasisi ya *ASA;* nilikuwa leo na *DG* pale nimemwambia mzee kama una tatizo sema wakubwa ndio hawa. Sasa mimi niwaambie wekezeni pale huyu mzee apate fedha tuzalishe mbegu za kisasa. Tuna watu wa utafiti kule, *TARI* na nani wapeni fedha tumalize mambo yetu, achaneni na mbegu za kutoka nje anaangalia mwaka huu Tanzania tuwapelekee kwa shilingi ngapi, anakadiria akiwa huko amekaa kwenye *computer.* Hilo ninaomba mkalisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye suala la mbolea ya ruzuku mmefanya kazi nzuri, mwaka huu mmeleta kwenye vijiji. Ninaomba ongeza kasi, peleka mbolea kwenye vijiji na vitongoji ili wananchi waweze kupata vizuri mbolea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake ya bajeti amesema vizuri sana, mwaka huu ana mpango angalau kwenye halmashauri tuwe na mashamba ya pamoja *(BBT).* Kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Uyui tulitenga hekari zaidi

ya 17,000 tangu mwaka 2021 tunataka tulime korosho. Baraza la Madiwani limepitisha, wewe ukaja ziara ukiwa Naibu Waziri ukatuahidi trekta halijaja mpaka leo. Sasa mimi nikuombe ule mradi umekwisha changamka, mimi nikuombe kwenye bajeti hii usitusahau Mradi wa Kalangasi kuhusu korosho ambao tuliupitisha katika halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine kuna mradi wa bwawa ambalo mimi nikushukuru sana. Hili bwawa mimi nimeanza kulisikia tangu niko darasa la nne na sasa nimekuwa Mbunge nimekwenda kulikwamua Bwawa la Goweko na wewe ulinipa heshima ulikuja.

Mimi nikuombe kwenye taarifa leo umeniambia lile bwawa liko 50%, ukienda *physical* kule wanasema 98%, wote mnachanganya taarifa. Mimi nikuombe, mkandarasi amepatikana *advance payment* inahitajika, mzee wa umwagiliaji anasubiri tu fedha umuingizie aende akasimamie kule kwa sababu na yeye mwenyewe ni mtu wa mjini anaweza kwenda kumsimamia mkandarasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, Mheshimiwa Waziri, mimi nikuombe; Serikali ina mpango mzuri wa kuwasaidia wakulima wake katika kilimo cha miwa. Kwenye jimbo langu umeniletea kilimo cha miwa ambacho nilikwenda kuongea na wananchi wa Kata za Loya, Miswaki na kwingineko huko ambako ulipeleka wataalam wako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kule wananchi wamekwisha niambia wenyewe hawahitaji kilimo cha miwa, wanahitaji kilimo cha mpunga kiimarishwe. Sasa mimi niombe wale wataalam ambao wanakwenda kila siku kuweka *beacon* kule, hebu toa maelekezo kwanza. Wale wananchi kama tunahitaji mradi twende tukashirikiane na wananchi tuwaeleweshe kwa utaratibu kuliko sasa hivi inavyokwenda kule nani hajui, wananchi hawajui, Mbunge hajui, Diwani hajui.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Serikali…

**MHE. TABASAM H. MWAGAO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

**MHE. VENANT D. PROTAS:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niombe kwenye kilimo cha miwa kule kwenye maeneo yetu ya Bonde la Loya, wananchi wamenituma na mimi ndiye mwakilishi wa wananchi, wamesema kwa sasa wanahitaji kulima mpunga na siyo miwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe Mheshimiwa Waziri, kwenye hili ninaomba uniunge mkono ili wananchi wasipate taharuki kwa yanayoendelea katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Innocent Sebba Bilakwate.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuchangia Wizara hii muhimu. Awali ya yote kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujalia kuweza kufika wakati huu na kuchangia Wizara hii muhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Rais kwa mapinduzi makubwa ambayo ameyafanya kwenye kilimo. Kipekee nimpongeze sana Mheshimiwa Bashe pamoja na timu yake kwa kazi kubwa, nzuri na ya kipekee ambayo wanaifanya kwenye nchi yetu kupitia kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati mwingine tunapopongeza hapa watu wanasema sijui wengine ni chawa, sijui ni nini lakini tunasema vitu ambavyo vimefanyika. Mimi nianze kusema, Mheshimiwa Bashe wewe ni kijana wa pekee. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakumbuka mwaka 2022 nimezungumzia sana suala la kahawa. Ninakumbuka Mheshimiwa Bashe ulisema sasa tunaamua kupambania kahawa. Mheshimiwa

Bashe mimi ninakosa maneno mazuri ya kusema zaidi ya kusema Mungu akubariki pamoja na timu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa ya Kyerwa na Mkoa wa Kagera, wakulima walikuwa wanapangiwa bei; anayeamua kupanga shilingi 800, anayeamua kupanga shilingi 1,100, lakini tulipoongea Wabunge, Mheshimiwa Bashe ukasikia na ukasikiliza maelekezo ya Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa ikakusanywa kwenye ushirika, kahawa ikaanza kuuzwa kwenye mnada. Mheshimiwa Bashe kwa kweli mimi niseme haya ni maajabu. Kahawa imetoka shilingi 800 mpaka 1,100 tulizokuwa tunapangiwa leo hii kahawa mwaka jana imefika shilingi 6,500; haya ni maajabu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakulima hawa ambao walikuwa wananyonywa, ambao walikuwa wanafanyiwa vitu vya hovyo lakini kupitia kwako na kwa Mheshimiwa Rais leo hii imewezekana. Mheshimiwa Bashe tunakuombea, tunakutakia kila la kheri na haya uliyoyafanya umeyafanya kwa wakulima ambao walikuwa maskini. Mimi nikuhakikishie unapotenda mema hakika Mungu hatakuacha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninajua ilikuwa ni vita kubwa sana. Wakati tunapambana kuhakikisha kahawa inauzwa kwenye minada ilikuwa ni vita, walikushawishi, walileta maneno ya kila namna kuhakikisha unakata tamaa, lakini Mheshimiwa Bashe hukukata tamaa, ulisonga mbele na sisi Wabunge tukaendelea kukuunga mkono, leo hii tunayaona mafanikio makubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa kwa Mkoa wa Kagera ndiyo siasa, ndiyo kila kitu. Unapogusa kahawa unagusa maendeleo, unagusa uhai wa Wana-Kagera na vita hii usifikiri imeisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii mimi niwaambie baada ya mimi kupambana kuhakikisha kahawa inauzwa kwenye mnada na Serikali ya Mama Samia ikasikia, vita inayoendelea Kyerwa siyo ya kawaida. Ninapowaambia leo, siku ya leo, hao waliokuwa

wanawapangia bei wakulima wamezunguka kwenye kata zote kuhakikisha wanakutana na mabalozi na wajumbe wao, viongozi wote kuhakikisha wanawahonga pesa huyu Mbunge ambaye amepambania kahawa asirudi Bungeni. Hata hivyo, mimi ninaye Mungu anayenipigania na ninajua kama Mungu aishivyo ninarudi hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vita hii sitasahau kumpongeza Mkuu wa Wilaya pamoja na Kamati yake ya Ulinzi na Usalama, wamefanya kazi kubwa. Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa Mheshimiwa Fatma Mwasa, mama huyu ni mpambanaji, amehakikisha kahawa ya Wana-Kagera inaendelea kunufaisha na kuleta tija kwenye Taifa letu. Kwa kweli tunampongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kahawa kwenda kwenye minada, sasa kuna mbinu nyingine wamekuja nayo. Bado biashara ya butura inaendelea. Wanachofanya hao wanunuzi wakubwa wanapeleka pesa kwa mawakala wao na wameanza kununua kahawa kupitia hii na hili nithibitishe sitataja, lakini itafika wakati nitasema. Kuna kiongozi mmoja aliyeaminiwa, mwaka jana kahawa imekamatwa magari zaidi ya sita, kahawa ambayo haioneshi imepitia kwenye *AMCOS* yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo wamekuja nalo, wanasema hao wakulima ambao wako karibu na mipakani tupeleke hela *cash* ili wasipeleke kahawa Uganda. Sasa wanachokifanya, mimi nilikwenda kwenye Kata ya Murongo mwaka jana nikakuta wakulima hawa wanapewa *cash* shilingi 3,200 lakini kwenye mnada ilikuwa ni shilingi 4,500. Niliposema nikampigia Mrajisi. Mrajisi akasema tunalifuatilia na nikamwambia kiongozi mmojawapo ambaye huyo ndiye kinara wa kufanya hiyo biashara. Sitamtaja tu, wakati ukifika nitasema tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima ya chama changu na nidhamu sitamtaja, lakini kilipotokea mimi nikasema lazima wananchi wapewe bei ambayo iko kwenye mnada. Baada ya kusema, kiongozi huyo anasema Mbunge anafuatilia biashara yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nimechaguliwa na wananchi kuhakikisha ninawatetea wananchi wangu, kuhakikisha ninaipambania Serikali yangu kahawa isiende Uganda na wananchi hawa wapate bei nzuri, hiyo ndiyo kazi niliyotumwa. Nitahakikisha ninaifanya, sitaogopa wala sitayumbishwa na siko tayari mimi kama Mbunge kuwekwa kwenye mfuko wa mtu mmoja kuona wananchi wangu wanateseka, wananchi wangu wanapewa bei ya hovyo. Kwa hiyo, hili nitapambana nalo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimuombe sana Mheshimiwa Bashe, amefanya mambo makubwa kwenye kahawa. Sasa kahawa yetu, mimi bado ninamini tunaweza kupata bei nzuri zaidi ya hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kahawa tunayoipeleka nje tunapeleka ghafi. Sasa Mheshimiwa Bashe nimeona unasema kuanzisha viwanda vya aina gani, lakini sasa tuombe, tafuta wawekezaji wakubwa wawekeze kwenye viwanda vikubwa vya kahawa. Kahawa yetu ichakatwe hapa ili na sisi twende kuuza nje kahawa ambayo imechakatwa hapa ambapo itakuwa imeongeza bei. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine Mheshimiwa Bashe, kahawa yetu…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa, muda wako umeisha, tafadhali.

**MHE. INNOCENT S. BILAKWATE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinitaja halafu unaniruka.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante nami kupata nafasi hii kutoa mchango wangu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mhata, samahani, kuna mtu amesema kuna jambo hapo.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mimi, ulinitaja, sasa ninaona umeniruka sijui…

**MWENYEKITI:** Pole sana Mheshimiwa Francis. Samahani Mheshimiwa Mhata ninaomba uketi.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Francis, tafadhali.

**MHE. FRANCIS I. MTINGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa nafasi hii ya kuchangia kwenye Wizara ya Kilimo, Wizara ambayo ndiyo tegemeo la nchi yetu kwa maana ya ajira, chakula, usalama na kila kitu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kutengeneza timu nzuri sana kwenye Wizara hii muhimu kwa kumuweka Mheshimiwa Bashe kuwa kinara wa Wizara hii. Mheshimiwa Bashe mimi ninamfahamu vizuri, ndiyo maana hata nilipokuwa Katibu Mkuu wa Vijana nilimuunga mkono awe Makamu Mwenyekiti wa Vijana Taifa, lakini bahati mbaya timu iliyokuwa inaongozwa na Mheshimiwa Ridhiwani wakatuzidi fitina wakatushinda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo nimpongeze pia Mheshimiwa Rais kwa kumpa timu Mheshimiwa Bashe ya watu wenye akili zinazofanana na Mheshimiwa Bashe. Naibu Waziri na Katibu Mkuu wanasababisha Wizara hii iende kwa kasi ambayo leo ushuhuda unaonesha kwa jinsi Wabunge wote ambavyo wanampongeza Bwana Bashe kwa kazi inayoonekana kwa macho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ninataka tu niseme kwenye suala la umwagiliaji. Miradi ya umwagiliaji ni miradi ambayo inataka *full package* ikamilike ndipo uone matunda yake. Huwezi kuona matunda ya mradi wa umwagiliaji hata uwe na pesa

nyingi kiasi gani kama uko nusu ama uko robo tatu ama uko robo. Kama ni maji kufika kwenye skimu lazima yafike, kama ni mifereji kwenda kwenye mashamba lazima iwepo ndipo uweze kuona matokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha zinazotakiwa kwenye umwagiliaji ni takribani kama shilingi trilioni 1.5; umwagiliaji peke yake. Hii ni zaidi hata ya bajeti nzima. Ninajua kwamba haiwezekani hivyo vitu vikafanyika kwa mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi niiombe Serikali, kupitia Waziri wa Fedha, basi kile kinachopangwa kwenye mradi wa umwagiliaji kwenye bajeti husika kiende chote kwa sababu zile *phase* ambazo zimepangwa kwenye miradi hii, kama zitakuwa zinaenda kwa utimilifu baada ya miaka kadhaa tutaona matokeo makubwa sana ya miradi hii ya umwagiliaji. Haya yanayoonekana kwa sasa bado ni cheche tu, kama miradi yote ya umwagiliaji itakwenda kama ilivyopangwa nina hakika kwamba nchi yetu itailisha dunia.

Kwa hiyo, mimi ninaomba sana Wizara ya Fedha katika kutoa zile fedha kwenye Wizara mbalimbali, pesa zinazohusu umwagiliaji ziende zote ili matokeo yaonekane kwa sababu kilimo hiki kwanza kinaongeza mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, ukichukulia tu mazao ya *horticulture* yameongeza pesa nyingi sana za kigeni. Mwaka 2020 tuliuza kama dola za Kimarekani milioni 290, lakini mwaka 2024 zimekwenda mpaka karibu dola za Kimarekani 590, kwenye mazao tu ya *horticulture*. Sasa kama miradi ya umwagiliaji yote itaenda vizuri maana yake ni mazao haya yataongeza fedha kiasi gani. Kwa hiyo, mimi ninataka tu nisisitize na kuiomba Serikali, fedha zote za umwagiliaji zinazopangwa kwenye bajeti ya kila mwaka ziende zote ili haya matokeo ambayo tunategemea yatakuwa ya ajabu sana yaweze kufanyika haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nikushukuru sana Mheshimiwa Bashe kwa jinsi ambavyo umelitendea jimbo langu. Kuna mabonde zaidi ya 900 ambayo yanatakiwa yapate umwagiliaji, lakini kwa upaendeleo maalum umenipatia shilingi bilioni 34

kwenye jimbo langu mradi wa msingi unaendelea vizuri, mifereji karibu yote ya urefu wa kilometa sita tayari na midogo inaendelea, lakini bwawa umeliongeza kutoka maji ya ujazo wa lita bilioni tano sasa linakwenda lita bilioni 12.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ni jambo la pekee, vijiji karibu vinne; Kijiji cha Kibi, Kijiji cha Msingi, Kijiji cha Nduhumo, Kijiji cha Inshinsi, wananchi takribani 12,000 wanakwenda kunufuaika na mradi huu. Nilikuja ofisini kwako nikakuomba uniongeze miradi miwili mikubwa, Bonde la Tatazi na Bonde la Mwangeza, umekubali na leo hii kuna *consultant* wa *continental* anafanya upembuzi yakinifu katika Jimbo la Mkalama. Ubarikiwe sana rafiki yangu, wewe unataka niendelee kuwa Bungeni na wananchi wa Mkalama watanirudisha kwa sababu wanajua unaendelea kunipa miradi ambayo inawanufaisha na kuwaondoa katika umasikini. Wananchi wa Mkalama huko mliko mjue kabisa Mheshimiwa Bashe ananilinda na miradi analeta, ninyi nirudisheni Bungeni ili mbadilishe maisha yenu. Ubarikiwe sana ndugu yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana, jambo la bajeti, kama nilivyosema kwenye *horticulture* msiliache, lakini Mheshimiwa Bashe mazao ya *horticulture* naomba utupie macho kwenye suala la embe. Kama parachichi na mazao mengine yameongeza kiwango cha pesa mpaka kufikia dola milioni 500 ninahakika ukitupia jicho la pekee kwenye embe, tena embe ina upendeleo maalum kwa sababu jimbo lako na mkoa wako wa Tabora watu wanalima embe. Wapo watu wengi sana wameitikia mwito wa kulima embe, naomba uliangalie kwa jicho la pekee zao hili, hakika kwa nguvu ambayo unaipeleka kwenye mazao mengine, ukipeleka robo tu, kidogo, kwenye zao la embe pesa nyingi sana za kigeni zitaongezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nikuombe sana katika mipango yako, Mheshimiwa Bashe zao la embe na mazao ya *horticulture* kwa ujumla ni *high values* ambayo ina thamani kubwa sana. Zao dogo tu, lakini kiasi kidogo tu kinaleta fedha nyingi sana za kigeni kwa hiyo, nikuombe sana hili ulishughulikie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilitaka niseme tu kuhusu hili la bajeti na nikupongeze kwa kazi kubwa na nimpongeze Rais wangu kwa kukupanga. Ninaamini utarudi na kama atapenda atakuacha kwenye Wizara hii kwa sababu ndiyo Wizara yenye roho ya nchi na utaendelea kufanya mambo na Watanzania wataendelea kunufaika. Mungu akupe maisha kijana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa Francis. Mheshimiwa Yahya Ally Mhata.

**MHE. YAHYA A. MHATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kupata nafasi hii jioni ya leo kutoa mchango wangu kwenye Wizara hii ya Kilimo.

Kwanza nami nichukue nafasi hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu, mwingi wa Rehema ambaye ameniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kutoa mchango wangu kwenye bajeti hii.

Pili, kama ilivyo ada, nami nimshukuru sana Waziri mwenye dhamana, ndugu yangu Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe na Naibu wake Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu Bwana Hussein na Bwana Stephen kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kuendelea kumshauri Waziri wetu ili aweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba nitoe mchango wangu katika maeneo yafuatayo; kwanza ni kwenye ushirika. Naishukuru sana Wizara kwa bajeti hii iliyowasilishwa asubuhi, imezungumzia kuhusu uanzishaji wa Benki ya Ushirika katika mikoa minne na moja ya mkoa ni Mkoa wa Mtwara ambako mimi natoka katika mkoa huo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli Mkoa wa Mtwara unahitaji sana benki ambayo ita-*deal* na wakulima moja kwa moja. Ni matarajio yangu Mheshimiwa Bashe benki hii ya ushirika

itatatua changamoto za wakulima wetu. Wakulima wetu, hasa wa zao la korosho, naomba hapa ieleweke benki hii ije Mtwara kutatua changamoto za wakulima wa korosho, siyo wafanyabiashara wa korosho. Wakulima wa zao la korosho wanahitaji sana fedha, ili waweze kuinua mashamba yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe unatoa pembejeo na viuatilifu bure kwa wakulima, lakini hivi peke yake havitoshi kwa sababu ili mkulima wa korosho aweze kufanya vizuri anahitaji fedha, kwa ajili ya palizi, maandalizi ya shamba. Mtu mwenye ekari kumi, mwenye ekari 15, yeye na mke wake hawataweza kulima bila kuwa na msaada wa mkopo. Kwa hiyo, tunategemea benki hii iwajali zaidi wakulima. Mtu mwenye ekari 10 au 15 hataweza kupulizia hivi viuatilifu unavyovitoa bure, kama hatakuwa na usaidizi wa watu wa kumsaidia, naye anahitaji fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye kuokota korosho, Mheshimiwa Bashe umeshazungumza hapa, tunahitaji fedha ile, ndoo moja ya *plastic* ni shilingi 2,000. Kwa hiyo, mtu peke yake hutaweza kufanya bila kuwa na msaada wa wasaidizi. Kwa hiyo, benki hii ije kutatua changamoto zinazowakabili wakulima wetu, vinginevyo tutakuwa tunafanya kazi bure. Kwa hiyo, mimi nakushukuru sana Mheshimiwa Bashe kwa kuliangalia hili jambo kwa makini zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeangalia kwenye ushirika, huku ambapo ndiyo tunaenda kutia nguvu vyama vyetu vya ushirika, *AMCOS*. Kule chini au *SACCOS* zetu zinao watendaji ambao kwa kweli, hatuwatendei haki au hawatendewi haki, wanalipwa malipo madogo sana, Mheshimiwa Bashe. Hebu Wizara ikae iangalie hawa makatibu ambao ndiyo watendaji wakuu wa hizi *AMCOS,* uwezo wao wa malipo unafanana na kazi wanayofanya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Bashe watu hawa wanafanya kazi mwaka mzima, lakini unaweza ukashangaa, mtumishi wa *AMCOS* analipwa shilingi 100,000 kwa mwezi na kazi anayoifanya ni kubwa sana. Kwa hiyo, mimi ningeomba sana

Mheshimiwa Bashe, hebu tukaangalie jinsi gani ya kuboresha mishahara ya hawa watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, hebu twendeni tukaiangalie sheria ya hivi vyama vyetu sasa hivi tubadilishe muda. Muda wao wa uongozi, kukaa madarakani, ni miaka mitatu. Mheshimiwa Bashe miaka mitatu kwa chama kufanya shughuli zake kikamilifu mimi naona hautoshi, anachaguliwa mwaka wa kwanza, akifika mwaka wa pili anawaza uchaguzi mwaka wa tatu. Kwa hiyo, kunakuwa na changamoto sana kwa hivi vyama kufanya shughuli za kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hebu tufikie hatua, tufikirie jinsi ya kubadilisha muda, badala ya miaka mitatu twende miaka mitano, kama ilivyo katika hivi vyama vyetu vya kisiasa. Kwa kufanya hivi tutawezesha watendaji wetu wa ushirika kuweza kufanya kazi kwa uadilifu na kwa maangalizo makubwa zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine Mheshimiwa Bashe kwenye kilimo mimi nakupongeza sana, umeeleza kwenye bajeti yako kwamba kilimo kimeweka ajira kwa maana ya chakula asilimia 100. Tunajitosheleza kwa chakula, ni jambo la kujivunia sana na siyo kwa Tanzania tu, hata Afrika Mashariki wanatutegemea sisi kwa chakula. Mimi nakupa hongera sana kwa hili, linachangia pato kubwa sana la Taifa, 26.3%; umezungumza kwenye bajeti yako kwamba kilimo kinachangia Pato la Taifa, karibu 26.3%, hili jambo ni la kheri, lakini 61.3% ya wananchi wake wanategemea kilimo. Nini matarajio yetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, matarajio yetu ni kwamba sasa nguvu kubwa uliyoielekeza sehemu nyingine, hebu nayo ilete upande wa Kusini. Mheshimiwa Bashe kule jimboni kwangu mimi sina mradi hata mmoja wa umwagiliaji. Ninalo Bonde kubwa la Mto Ruvuma, mwaka 2024 ulinipangia bajeti kule kwa ajili ya umwagiliaji, lakini hakijafanyika kitu. Nakuomba sana katika bajeti hii ya mwaka huu 2025 hebu tia macho kidogo utusaidie wananchi wa jimbo langu, ili waweze kupata mradi wa umwagiliaji, ila nakushukuru sana, umeleta miradi miwili ya umwagiliaji, kwa maana ya vyakula vya bustani, kule katika Kata ya Likokona na Kata ya Nangomba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mkandarasi yuko kazini; jambo hili ni la kheri na wananchi, naamini kabisa kuanzia mwakani wataona manufaa kwa kazi nzuri.

Mwisho kabisa, Mheshimiwa Bashe, mimi nakutakia kheri wewe, Naibu Waziri na watendaji wote kwa kazi kubwa mnayoifanya ya kuboresha zao letu la korosho na uchumi wa nchi yetu, ahsanteni sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Mhata. Mheshimiwa Alfred James Kimea.

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Nina mambo machache, kama matano hivi ya kuchangia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniweka salama na kunipa afya, leo ninawasemea wananchi wa Korogwe na Watanzania kwa ujumla. Namba mbili ninaomba nitumie fursa hii kumshukuru na kumpongeza Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, kwa kuendelea kutekeleza miradi mikubwa kwenye nchi hii, lakini pamoja haiachi sekta ya kilimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepiga mahesabu kwa miaka michache iliyopita, sekta ya kilimo bajeti yake imeongezeka kwa zaidi ya 100%, kutoka kwenye dola 290 mpaka *1.2 billion*. Ni hatua kubwa sana kwa nchi yetu, hivyo nimpongeze Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, lakini pia niwapongeze viongozi wa Wizara hii, Mheshimiwa Bashe, kaka yetu Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu Gerald na Naibu Katibu Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu Mheshimiwa Waziri naomba unisikilize vizuri, watu wa Korogwe wanatamani kusikia hapa vizuri, Mheshimiwa Waziri tangu naingia Bungeni nimekuwa nikifuatilia mabonde yangu mawili ya Korogwe Mji, moja ni Bonde la Mahenge na namba mbili ni Bonde la Kwamsisi. Mheshimiwa Waziri ulilitangaza Bonde la Mahenge, ukapeleka mkandarasi, wananchi wakawa na matumaini makubwa sana, lakini baada

ya miezi sita/saba hakuna kilichofanyika, ukasema tunamtoa mkandarasi Tume ya Umwagiliaji itafanya yenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya mwaka hakuna kilichofanyika, ukasema tunatangaza kupata mkandarasi mwingine. Mheshimiwa Waziri hadi sasa hivi tunavyoongea hakuna kitu kinachoendelea kwenye Bonde lile la Mahenge, Kata ya Kwamndolwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi wananchi wa Kwamndolwa na Mahenge wanahisi sifuatilii juu ya jambo hili na wewe mwenyewe unafahamu namna ninavyohangaika, ninavyokufuata, ninavyokusumbua juu ya jambo hili. Mheshimiwa Waziri ninakuomba, ukiwa unahitimisha, u-*note* kabisa hapo, usemee Bonde la Mahenge. *Otherwise* nakuomba ukipata muda twende ukaseme mwenyewe mbele ya wananchi wa Korogwe, ili wadhihirishe kwamba mimi nimetimiza wajibu wangu, iliyobaki ni upande wenu. Mheshimiwa Waziri naomba hilo niishie hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hilo nina Bonde langu la Kwamsisi. Mheshimiwa Waziri mwaka 2024 kwenye bajeti ilionekana kama linaenda kutangazwa na ukaenda kuwaambia wananchi wa Kwamsisi shilingi bilioni tisa. Mama, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alivyokuja Korogwe nikaongelea Bonde la Kwamsisi kutangazwa na kuanza utekelezaji wake, akatoa maelekezo kwamba litangazwe, mkandarasi apatikane. Mheshimiwa Waziri hadi sasa hivi sijui kinaendelea kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na hili naomba ukiwa unahitimisha ugusie au hiyo safari yetu ya Korogwe uende na mimi Kwamsisi ili uweze kuwaeleza wananchi. Hayo ni ya kwangu mawili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho ninalotaka kutoa ushauri Mheshimiwa Waziri ninaona una malengo mazuri na makubwa juu ya kilimo cha nchi hii. Kimsingi tunazalisha zaidi ya mahitaji yetu na tunaweza kuuza, Mheshimiwa Waziri, nina ushauri mmoja, sijui kama unafahamu wapo wananchi wa nchi hii ambao wanatamani kulima, lakini hawana uwezo wa kununua mbegu. Wapo wanaonunua mbegu ambazo hazina ubora, kutokana na

gharama kubwa ya mbegu, lakini pia wapo wananchi wanaoweza kuona mazao yao ya shamba yakiteketea na wadudu, lakini hawana uwezo wa kununua dawa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu, ninajua inaweza isiwezekane leo, lakini weka kwenye *strategic plans* zako, natamani siku moja kwenye nchi hii wananchi wote wakulima wawe wanagawiwa mbegu bure ili kusiwe ni *option* ya mtu kulima au kutolima, kwa sababu ya kukosa mbegu. Unaweza ukaanzisha utaratibu, wakati wa kulima watu wanapewa mbegu bure, baadaye wanapewa dawa bure, wanapewa mbolea bure na wakati wa kuvuna wanarudisha zile gharama Serikalini na zinatumika kwa kipindi kijacho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii tutaweza kumkomboa mkulima kwa sababu wananchi wa nchi hii wengi ni maskini. Kweli kuna ruzuku, lakini mbolea unaweza ukaishusha ruzuku mpaka 70,000, lakini yuko mtu ambaye analala na njaa, anaamua aidha anunue chakula kwa kuwalisha familia au siku hiyo wakanunue mbolea, ana-*opt* kununua chakula. Kwa hiyo, wananchi wa nchi hii wanatamani sana kuchangia kwenye sekta ya kilimo, lakini maisha magumu yanawarudisha nyuma. Hilo ni ombi langu tuliweke kwenye mpango siku moja nchi hii iweze kutoa mbolea na mbegu bure.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. DKT. ALFRED J. KIMEA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Huo ndiyo ulikuwa mchango wangu na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Alfred James Kimea.

Mchangiaji wetu wa mwisho atakuwa Mheshimiwa Boniphace Getere, kwa dakika tano.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi ya kuchangia hii Wizara. Cha kwanza ni kuwapongeza tu watendaji wa Wizara,

Mheshimiwa Bashe, Naibu wake Mheshimiwa Silinde, Katibu Mkuu Gerald na watendaji wengine wote wa Wizara ya Kilimo. Pia nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Pamba, huyu mzee anafanya kazi sana, Mheshimiwa Bashe wewe usiangalie umri angalia kichwa chake kinafanya kazi kiasi gani tuendelee kuwa naye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunampongeza Rais kwa kazi nzuri aliyofanya kwa kupandisha bajeti ya kilimo kuwa kiasi hicho. Mheshimiwa Bashe unajua kuna watu wanalitazama jambo hili kama la kawaida, wapo watu duniani waliwahi kuuliza tofauti kati ya akili na elimu; mmoja wa watu hao alikuwa ni Albert Einstein, aliuliza elimu ni nini na akili ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wako watu hawajui mambo hayo, wanasema Albert alisema ni bora uwe na akili kuliko kuwa na elimu na akasema wako waliotengeneza hii dunia, akamtaja Isaac Newton, akamtaja Galileo Galilei, akamtaja Archimedes akasema hao ndiyo wanasayansi, *icon* ya dunia ambao hawakuwa na cheti na *diploma* na *degree* na *PhD* na profesa, lakini leo ndiyo watu wanaiga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri wewe Mheshimiwa Bashe Mungu alikupa vyote, una akili na elimu, hongera sana na ndiyo maana watu wengine wanakuona tofauti tofauti wakati ukifanya mambo, ukikasirika asiyekujua anasema huyu bwana hawezi kusogea hapa, ukifurahi wanasema wewe ni mtu laini, lakini Mungu alikupa akili zote, alikupa elimu, akakupa na akili, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa katika maelezo yangu hayo huwa najiuliza umetumia elimu kupandisha bei ya korosho, bei ya kahawa, bei ya ufuta na tumbaku imeongezeka. Hiyo elimu na akili ambayo Mungu anakupa tatizo linakupata wapi kupandisha bei ya pamba? Wapi linakupata hilo tatizo? Yaani maeneo mengine yote unaweza, kwa nini sisi wakulima wa pamba tunalima pamba kwa kutumia milioni mbili, halafu ukiiuza unapata milioni moja? Tatizo ni nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba, akili hizo alizotumia kwa mazao mengine kwa Kanda ya Ziwa aende. Huwa najiuliza hivi Mheshimiwa Bashe akiongea na viwanda vikubwa vya Marekani, vya Canada kule wanakonunua pamba, akawaambia jamani eeh mimi mwaka huu nina pamba, niwauzie bei gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakakwambia bwana pamba kipindi hiki tutakupa kilo shilingi 2,500 ukaja ukamwambia mkulima anayelima eka kumi, bei yake itaanzia shilingi 2,500. Sasa kwa nini mnatuacha sisi tunalima, tunatumia ng'ombe, tunatumia trekta, tunatumia nini, halafu unalima kwa shilingi bilioni 200, unalima kwa shilingi milioni 15, unalima kwa shilingi milioni 20, unapata shilingi milioni 10? Hiyo akili ya maeneo mengine, Bukoba, wapi huko, Songea, hii imeenda wapi huku kwetu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikuombe sana, mwaka huu unaokuja wa 2026 utafute hiyo akili uliyonayo utuwezeshe sisi tupate pamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine, nimpongeze Mheshimiwa Rais. Skimu ya Maliwanda na Kisangwa ni skimu bora sana kwa Mkoa wa Mara na Skimu ya Kisangwa wakulima wa Jimbo la Bunda wanachukua 60% na wa Bunda Mjini 40%, Skimu ya Maliwanda tuna 100% kwa 100%. Umetangaza mkandarasi wa kuikarabati skimu iwe bora kuliko skimu zote Tanzania, lakini mkandarasi hajaja. Tunakuomba huyu mkandarasi, yale matangazo uliyofanya yaje mapema, lakini tunamuomba Mheshimiwa Rais, kama matangazo yatafika, muda wa uchaguzi umefika, akurudishe tena kwenye Wizara hii ili utengeneze skimu hizo. Tunakushukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo mimi ninaliona ni namna pembejeo zinavyowafikia wakulima. Kwa nini pembejeo haiji kwa wakati? nikuombe sasa pembejeo ije kwa wakati, ili watu waweze kulima.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante Mheshimiwa.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, vinginevyo Wizara yako hii ya Kilimo sasa hivi ina rindima. Watu wanajua kwamba Wizara ya Kilimo ina mtu ana akili, mtu ana elimu.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Getere, muda wako umeisha.

**MHE. BONIPHACE M. GETERE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera sana na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge nawashukuru. Namshukuru pia Waziri Mheshimiwa Hussein Bashe, pamoja na Naibu Waziri kwa kuendelea kupokea hoja za Waheshimiwa Wabunge. Nawashukuru Wabunge wote walioweza kuchangia jioni hii.

Baada ya maneno haya niliyoyasema, naahirisha Bunge mpaka kesho saa 3.00 asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.39 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi, Tarehe 22 Mei, 2025 Saa Tatu Asubuhi)*